Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA ISHIRINI

**Kikao cha Ishirini na Tatu – Tarehe 8 Julai, 2005**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Bodi ya Sukari Tanzania kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2004 *(The Annual Report and Accounts of the Sugar Board of Tanzania for the Year ended 30 Th June, 2004)*

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Bodi ya Kahawa Tanzania kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Septemba, 2004 *(The Annual Report and Audited Accounts of the Tanzania Coffee Board for the Year ended 30th September, 2004,)*

*Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Bodi ya Pamba na Mbegu kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2004 (The Annual Report and Accounts of the Tanzania Cotton Lint and Seed Board for the Year ended 30th June, 2004)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA:**

Maoni ya Kamati ya Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2005/2006.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI:**

Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelzaji wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi yaWizara hiyo kwa Mwaka 2005/2006.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 215

### Kasma kwa Ajili ya Halmashari ya Mji wa Korogwe

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU (K.n.y. MHE. JOEL N. BENDERA)** alijibu:-

Kwa, kuwa tangu Bajeti ya mwaka 2004/2005 Mji wa Korogwe ulipata hadhi ya kuwa Halmashauri ya Mji, na kwa maana hiyo ulitakiwa uwe unapata Bajeti yake inayojitegemea ili uweze kujiendesha kwa maana ya kupata kasma yake katika masuala ya huduma za jamii kama Elimu, Maji, Afya, Miundombinu ya Kiuchumi, barabara, Umeme na kadhalika. Pamoja na kupatiwa wataalam mbalimbali kuendesha Halmashauri hiyo. Lakini jambo la kusikitisha ni kuwa hadi leo Halmashauri hiyo haijafanyiwa hivyo, badala yake bado wanaazima wataalam toka kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe jambo linaloleta mgongano katika masuala ya kimaendeleo katika Halmashauri hizo mbili na kukosa ufanisi:-

(a) Je, ni sababu zipi za msingi zinazochelewesha Halmashauri ya Mji wa Korogwe kupatiwa Kasma zake ili iweze kujitegemea badala ya kuendelea kutegemea Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe?

(b) Kupata Halmashauri ya Mji maana yake ni kupatiwa wataalam wa Idara zote. Je, ni lini wataalam hao watapatikana kwa ajili ya Halmashauri hiyo?

(c) Kwa kuwa, zipo stahili muhimu ambazo ni lazima mji uliopata hadhi upatiwe, kama vile magari ya taka, magari ya maji taka, huduma za zimamoto na kadhalika. Je, ni lini huduma hizi zitapelekwa katika Mji huo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joel Nkaya Bendera, Mbunge wa Korogwe Mashariki , lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Ofisi yangu kwa kupitia Tangazo la Serikali Namba 352 la tarehe 17 Septemba, 2004 iliipandisha hadhi Mamlaka ya Mji Mdogo wa Korogwe kuwa Halmashauri ya Mji. Kufuatia kupandishwa hadhi Ofisi yangu imeshafanya maandalizi ya awali ikiwa ni pamoja na kumteua Mkurugenzi wa Mji na tayari watumishi 272 wamepelekwa katika Halmashauri ya Mji wa Korogwe kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Mji) Namba 8 ya mwaka 1982, Halmashauri ya Mji huanza kuwa Halmashauri rasmi baada ya Uchaguzi wa Madiwani. Hivyo, Halmashauri ya Mji wa Korogwe itaanza rasmi baada ya kupatikana Madiwani katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2005. Hii ni kutokana na ukweli kuwa Halmashauri ni muunganiko wa Watendaji na Madiwani na kwamba Watendaji peke yao hawawezi kuunda Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kawaida kasma hutolewa kwa Halmashauri baada ya Halmashauri kuanzishwa rasmi kama nilivyoeleza hapo huu. Hata hivyo Halmashauri ya Mji wa Korogwe imeshapata kasma yake ambayo ni *Vote 86-U6* na tayari Halmashauri hiyo imeshafungua Akaunti ambayo hutumika kupokea fedha kutoka Hazina ambazo hupelekwa katika Halmashauri kwa matumizi ya kawaida.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la sehemu (a) hapo juu, jumla ya wafanyakazi 272 wameshahamishiwa katika Halmashauri ya Mji wa Korogwe, kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe na kwamba mara baada ya Halmashauri kuanzishwa rasmi itapewa kibali cha kuajiri wataalam wake kwa kuzingatia mahitaji na vipaumbele.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Mji wa Korogwe imeshapewa baadhi ya mali na vitendea kazi kama ifuatavyo:-

(i) Magari manne (*Land Cruiser 2*, Samurai 1, Isuzu gari la taka 1, na *tractor 1*.
(ii) Nyumba *(NHC 36, Canteen 1).*
(iii)Stendi na vibanda vya biashara.
(iv)Masoko na machinjio.

Mheshimiwa Naibu Spika, rasilimali za watu na vifaa mbalimbali vya kutolea huduma zitatolewa kwa Halmashauri hiyo baada ya kuanzishwa rasmi na kwa kutegemea uwezo wa Serikali na Halmashauri yenyewe. Kwa ujumla Halmashauri nyingi nchini zinakabiliwa na tatizo la uhaba wa watumishi hata hivyo kwa madhumuni ya kupeleka madaraka kwa wananchi Serikali haitasita kuanzisha Halmashauri mpya pale inapobidi bila kuogopa kwamba uhaba wa watumishi bado unatukabili.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali miwili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa uanzishaji wa Miji mipya au Halmashauri Mpya ni gharama na huwa zinaanzishwa kama alivyosema pengine bila maandalizi kamili. Sasa tunapoanzisha Halmashauri hizi bila maandalizi hamuoni kwamba tunadumaza maendeleo badala ya kuleta maendeleo zaidi?

Halmashauri ya Korogwe bado hela zilizotengwa hata kwa mwaka huu ni kidogo sana, sasa Serikali inatamka nini katika kuiongezea Halmashauri hii maana hata vifaa vya kutendea kazi vilivyotajwa ni vichache sana?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu maswali miwili ya nyongeza ya Mheshimiwa Shekiffu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya sababu ya kutangaza halmashauri mbalimbali mapema kidogo kabla pengine ya wakati ambapo Waheshimiwa Wabunge mngetarajia kwamba ingekuwa imeambatana na mambo mengine ni kutokana na kufanya maandalizi hayo kwa sababu Halmashauri hizi zinahitaji maandalizi ya kutosha kabla ya kuanza rasmi kwa maana ya *take off* na ndiyo maana katika hatua hiyo umeona tumefanya juhudi hizo ili itakapokuwa imekamilika katika uchaguzi basi madiwani hao ndiyo watakaoanza sasa kufanyakazi ya kufanya hatua zile ambazo zinatakiwa kwa sababu bila hao haitawezekana kwa kweli hata kupeleka vifaa vingi au fedha nyingi kwa sababu madiwani hawapo.

Lakini pili, ni kweli kwamba fedha zilizotengwa si nyingi lakini kwa upande mmoja inatokana na ukweli kwamba fedha yenyewe haitoshi katika Bajeti zetu lakini ni matarajio yangu kwamba mara tu baada ya madiwani kupatikana rasmi wao ndiyo watakaoanza kupanga Bajeti na kujaribu kuiomba Serikali sasa ipeleke fedha za kutosha kwa ajili ya matumizi mbalimbali. (*Makofi*)

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwanza niishukuru Serikali kwa kuupatia Mji wa Korogwe kuwa Halmashauri ya Mji na pia niishukuru Serikali kwa kuipandisha Manispaa ya Tanga kuwa sasa Jiji. Naomba niipongeze sana Serikali kwa hilo.

Nina swali dogo la nyongeza, kwa muda huu uliopo sasa kuna mgongano kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe na Halmashauri ya Mji kwa maana fedha kwa mfano ya *Road Toll* zinapelekwa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe. Je, tatizo hilo sasa na matatizo mengine ambayo yapo litakuwa limetatuliwa ili kuufanya sasa Halmashauri ya mji ifanya kazi yake kwa kujitegemea yenyewe badala ya kutegemea Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe maelezo kwa Mheshimiwa Bendera kwa swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba kwa sasa Halmashauri ya Mji wa Korogwe itaendelea kufanya kazi chini ya usimamizi wa jumla na uongozi wa jumla wa Halmashauri ya Wilaya iliyopo hivi sasa na hii ndiyo inayoleta hiki unachokiita

mgongano kwa sababu hakuna namna ambayo tunaweza tukaruhusu fedha zote zikaenda kwenye Halmashauri hiyo wakati Baraza la Madiwani kwa maana ya kuwa na Mwenyekiti wa Halmashauri bado hajapatikana.

Lakini Mheshimiwa Bendera nataka nikuhakikishie kwamba jambo hili ni la mpito tu mara tu baada ya uchaguzi mta *take over* jambo hili na mtalishughulikia ninyi wenyewe. (*Makofi*)

Na. 216

**Viongozi Walioshika Nyadhifa Nchini.**

**MHE. OMAR M. MWENDA (K.n.y. MHE. OMAR S. CHUBI)** aliuliza:

(a) Je, ni viongozi gani (Kwa majina) wameshika nyadhifa za Urais, Makamu wa Kwanza na Pili wa Rais Waziri Mkuu tangu tupate Uhuru hadi 1995?

(b) Je, Serikali inaweza kutoa orodha ya Mabaraza ya Mawaziri katika kipindi hicho hicho (1961 - 1995)?

(c) Je, taarifa hizo zinaweza kupatikana katika vitabu na kupelekwa katika Shule za Msingi, Sekondari, Vyuoni na Vyuo Vikuu ambako elimu ya siasa inatolewa kwa kiwango kidogo sana?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (K.n.y. WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, MENEJIMENT YA UTUMISHI WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma naomba kujibu swali la Mheshimiwa Chubi, Mbunge wa Kilwa Kaskazini lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-
(a)Viongozi waliokwisha kushika nyadhifa za Urais, Makamu wa Rais, Makamu wa Kwanza wa Rais, Makamu wa Pili wa Rais na Waziri Mkuu tangu tupate Uhuru hadi mwaka 1995 ni kama ifuatavyo:-

**Walioshika nafasi za Urais (1961-1995):**

(i) Hayati Mwalimu Julius K. Nyerere (1962-1985);
(ii) Mheshimiwa Alhaji Ally H. Mwinyi (1985-1995);
(iii) Mheshimiwa Benjamin W. Mkapa (1995-2005).

**Makamu wa Kwanza wa Rais:**

(i) Hayati Sheikh Abeid A. (Karume) (1964-1972);

(ii) Alhaj Aboud Jumbe Mwinyi (1972-1978).

**Makamu wa Pili wa Rais (1961-1995):**

(i) Mheshimiwa Rashid Kawawa (1964-1976).

**Makamu wa Rais (1961-1995):**

(i) Mheshimiwa Rashid Kawawa (1962-1963);
(ii) Alhaji Aboud Jumbe Mwinyi (1979-1984);
(iii) Alhaji Ally H. Mwinyi (1984).

**Waziri Mkuu na Makamu wa Rais:**

(i) Mheshimiwa Joseph Sinde Warioba (1985-1990);
(ii) Mheshimiwa John Samwel Malecela (1991-1995).

**Waziri Mkuu (1961-1995):**

(i) Hayati Mwalimu Julius K. Nyerere (1961-1962);
(ii) Bw. Mheshimiwa Rashid M. Kawawa (1962);
(iii) Hayati Edward Sokoine (1978-1979 & 1983-1984);
(iv) Mheshimiwa Cleopa D. Msuya (1980-1982);
(v) Mheshimiwa Salim A. Salim (1984);
(vi) Mheshimiwa John S. Malecela (1991-1995);
(vii) Mheshimiwa Joseph S. Warioba (1985-1990);
(viii) Bw. Frederick T. Sumaye (1995-2005).

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa orodha ya Wajumbe wa Baraza la Mawaziri tangu nchi yetu ipate uhuru hadi mwaka 1995 ni ndefu sana, na kwa kuzingatia kanuni za Bunge lako tukufu kuwa majibu yasichukue muda mrefu naomba kwa ruksa yako Mheshimiwa Mheshimiwa Spika nimpatie Mheshimiwa Mbunge orodha hiyo mara baada ya kujibu swali hili hapa Bungeni. (*Makofi*)

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa ofisi yangu iko wazi kushirikiana na watafiti na waandishi wa vitabu mbalimbali, lakini mpaka sasa hakuna mtafiti au mwandishi aliyefika kuomba taarifa hizi. Kama wapo nawakaribisha kufika kuja kuzitafuta.

**MHE. OMAR. M. MWENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu yake mazuri Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza maswali miwili ya nyongeza.

Kwa kuwa, viongozi aliowataja walishirikiana na wazee katika kuanzisha au kukomboa nchi hii. Je kuna utaratibu gani wa wazee hao ili kuwekwa katika kumbukumbu ya miongoni mwa watu walioikomboa nchi hii? La kwanza.

La Pili, kuna utaratibu gani katika viongozi hawa waliotajwa katika kuwaenzi ili nchi hii hatimaye vizazi vipya vijue kwamba hawa ni wakombozi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENT YA UTUMISHI WA UMMA) :** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali miwili ya Mheshimiwa Mwenda kama ifuatavyo:-

Ni kweli kabisa Waheshimiwa hawa walioshika nyadhifa wakati wa mwanzoni wameshirikiana na wazee wa aina mbalimbali wake kwa waume kutoka kwenye Wilaya zetu na mikoa yetu na huko ndiko tunakotegemea kwamba Wilaya na Mikoa itaweka taarifa hizo sahihi na kujua ni wazee gani walioshiriki na viongozi hao wakubwa. Ni tumaini letu kwamba hasa katika ofisi za Chama cha Mapinduzi kuanzia *TANU* ambapo *record* hizo zipo ndiko huko unaweza kupata taarifa kamili za viongozi hawa.

Ama vilevile ziko taarifa kwenye Kumbukumbu ya Taifa, kule ukienda taarifa za viongozi hawa zipo, watu ambao wameweza kutoa taarifa hizo huko kule utazipata zile ambazo hazikupatikana utazipata kwenye Wilaya na Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jinsi ya Kuwaenzi. Viongozi hawa tunawaenzi kadri tunavyokwenda na juzi juzi tumepitisha sheria hapa jinsi ya kuwahudumia viongozi wetu nafikiri ni kutokana na Sheria hiyo kama kuna haja ya kuiboresha basi taarifa iletwe tu tutaiboresha sheria ile na kuangalia jinsi gani ya kuwaenzi hawa viongozi wetu pamoja na hao wazee wengine ambao pengine mnataka tuwaingize humo ndani, tutaweza kuiboresha hiyo sheria.

Na. 217

**Mikataba ya Huduma kwa Wateja**

**MHE. BERNARD K. MEMBE (K.n.y. MHE. MARIA D. WATONDOHA)** aliuliza:

Kwa kuwa, Serikali imeandaa utaratibu mzuri wa kutoa huduma kwa wananchi kwa kuandaa mkataba wa huduma kwa mteja kwa ajili ya watumishi wa Wizara mbalimbali na kwa kuwa, watoa huduma ni watumishi walio katika Wizara husika:-

(a) Je, ni Wizara zipi zimekamilisha maandalizi ya mikataba ya huduma kwa wateja?

(b) Je, nani anawajibika na kuhakikisha kuwa huduma zinatolewa kama ilivyoainishwa katika jedwali zilizotolewa?

(c) Kama mikataba ipo, je, kwa nini Serikali katika kujibu swali la nyongeza kwa swali Na. 66 la Tarehe 8/2/2005 ilisema "wataonekana wakisimamiwa" ilimaanisha watumishi hawafanyi kazi mpaka wasimamiwe?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma naomba kujibu swali la Mheshimiwa Watondoha, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya Wizara 24, Idara zinazojitegemea 9 na Wakala 5 tayari zina mikataba ya huduma kwa mteja. Aidha, Mikataba 11 ya Wizara, Idara inayojitegemea 1 na Wakala 3 tayari imezinduliwa.

(b) Mheshimiwa Spika, Watendaji Wakuu, Wasimamizi na Watumishi wote wa Wizara na Idara zinazohusika ndio wenye wajibu wa kuhakikisha kuwa huduma zinatolewa kama ilivyoainishwa katika mikataba yao. Aidha, wananchi nao kwa upande mwingine kama wateja wana haki ya kuhoji kwa njia mbalimbali ama huduma walizozitarajia hazitolewi kama ilivyotakiwa.

(c) Mheshimiwa Spika, usimamizi kama sehemu muhimu ya uongozi katika sehemu ya kazi unalenga yafuatayo:-

Moja, Kuhakikisha kuwa kunakuwepo na uwajibikaji;

Mbili, Malengo yanatekelezwa na taarifa inatolewa;

Tatu, Kufahamu mahitaji kwa ajili ya utekelezaji wa Majukumu;

Nne, Kutambua matatizo yanayoathiri ufanisi;

Tano, Kupima ubora na ufanisi wa kazi; na

Sita, Kupima malengo na mafanikio na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikataba ya huduma kwa mteja haichukui nafasi na wajibu wa usimamizi. Hilo linabaki kuwa ni jukumu la viongozi na wasimamizi ambao pamoja na mambo mengine wana wajibu wa kuhakikisha kuwa mikataba hii inatekelezwa na malengo ya Wizara yanafikiwa.

**MHE. BERNARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali miwili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba dhana nzima ya Mkataba kwa wateja inalenga hasa katika kuwajibika kwa viongozi mbalimbali kwenye ngazi za Utumishi pale wanapokosea wanachukuliwa hatua na wanawajibika. Mheshimiwa Waziri analielewa hilo kwamba dhana au *concept* ya mkataba kwa wateja ni uwajibikaji?

La pili, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba moja ya nguzo kuu ya mkataba kwa wateja ni utunzaji wa kumbukumbu kwenye ngazi za Utumishi zinazotoa athari na zinazosumbua wastaafu pamoja na watu wote wanaofariki kuhakikisha kwamba kumbukumbu zao zinawekwa na anayeshindwa kutekeleza hivyo anawajibika, analielewa hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali miwili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bernard Membe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu langu la awali la mwisho nilisema mikataba ya huduma kwa mteja haichukui nafasi ya wajibu wa usimamizi kwa hiyo ni dhahiri kwamba nalielewa kwamba ni nguzo kubwa mojawapo ya mikataba hii ni wajibu ambao lazima uwepo kwa viongozi wanaosimamia. Bila hivyo basi mikataba hii haitafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kuhusu kumbukumbu ni wajibu na hii ni mojawapo kabisa ya nguzo kubwa katika mikataba hii kwamba kama hakuna kumbukumbu sahihi basi hakuna usimamizi sahihi kwa hiyo hakuna uwajibikaji sahihi na ni lazima vitu hivyo vyote vifuatane pamoja na ndiyo maana tumesema lazima viongozi wawajibike kuhakikisha kuwa mikataba hii inatekelezwa ili malengo ya Wizara yaweze kufanikiwa.

Na. 218

**Sera ya Wanyamapori**

**MHE. SEMINDU K. PAWA (K.n.y. MHE. MATHEW TAKI OLE – TIMAN**) aliuliza:-

Kwa kuwa, dhana na sera ya Wanyamapori zinalenga kuwashirikisha wananchi kama uhifadhi endelevu na kuufaidi uhifadhi huo:-

(a) Je, ni kwa nini mpaka sasa uanzishwaji wa *Wildlife Management Authority (WMA)* unalegalega?

(b) Kwa kuwa, miongozo *WMA* iliyotolewa na Serikali zina ukiritimba mkubwa. Je, ni lini Serikali itatathmini – *review* miongozo hiyo ili kurahisisha uanzishwaji wa mamlaka hiyo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimia Mathew Ole – Timani, Mbunge wa Ngorongoro, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya kuanzisha *WMA* ni utekelezaji wa Sera ya Wanyamapori ya 1998 ya ushirikishaji wa jamii hasa wananchi wanaoishi katika maeneo yenye wanyamapori katika uhifadhi wa wanyamapori. Utekelezaji wa kuanzisha *WMA* umechukua muda mrefu kutokana na sababu mbalimbali. Sababu kubwa ni kwamba utekelezaji wa dhana hii unahusisha vyombo na wadau mbalimbali katika kuusimamia. Ingawa kimsingi Sheria ya Wanyamapori Na. 12 ya mwaka 1974 inahusika moja kwa moja katika kutekeleza dhana ya *WMA*, ni budi sheria hii itumike sambasamba na Sheria nyingine zinazohusika kama vile

(i) Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999;

(ii) Sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982; na

(iii) Sheria ya Vyama vya Hiari Sura ya 337.

Hivyo ilikuwa ni lazima kwanza kuoanisha Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori Na. 12 ya mwaka 1974 na sheria nyingine zinazohusika kwa lengo la kuondoa utata wa kisheria. Aidha, ilikuwa lazima wananchi na wadau wengine waelimishwe kiasi cha kutosha kuhusu dhana ya *WMA* pamoja na Kanuni husika ili kusiwepo migongano wakati wa utekelezaji.

Kutokana na sababu hizo, imechukua muda mrefu kwa wahisani na wadau wengine wakiwemo wananchi wa maeneo yaliyoteuliwa kuwa ya majaribio kuelewa umuhimu na manufaa ya mpango huu. Hivi sasa, elimu ya kutosha imetolewa kwa wahisani na wadau ambapo wameelekezwa kuhusu taratibu zinazotakiwa. Hivi sasa utekelezaji unaendelea kwa kasi ya kuridhisha

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni za *WMA* na Miongozo ya kuanzisha *WMA* haina ukiritimba na kama nilivyoeleza kwenye jibu la sehemu (a), tatizo kubwa lilikuwa uelewa kuhusu umuhimu wa Sheria nyingine katika utekelezaji.

Kanuni za Hifadhi yaani Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori 2002 ziliandaliwa na maeneo 16 yaliteuliwa kuzitekeleza kwa majaribio katika kipindi cha miezi 36 kuanzia Januari 2003. Baada ya kipindi cha majaribio, Serikali itafanya tathmini ya Kanuni hizo ili kuona kama zimekidhi matarajio ya Sera katika ushirikishaji wa wananchi.

Matokeo ya tathmini hiyo yatawezesha Serikali kuzifanyia kanuni marekebisho kama itakavyoonekana inafaa kwa ajili ya kuziboresha na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa dhana ya kuanzisha *WMA*.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali miwili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa, zipo sheria karibuni sita zilizotajwa za kuainisha jambo hili na ziko katika sekta Mtambuko na Wizara mbalimbali, hivi Wizara kwa nini isikae pamoja na Wizara nyingine ili kuainisha haya mambo ambayo yana utata na migongano ili kuwa na kitu kimoja?

Pili, kwa kuwa, katika mkutano uliofanyika kule Arusha wa wadau mwaka huu 2005 Mheshimiwa Mama Meghji alikuwa makini kweli kutueleza wadau ambao tulihudhuria mkutano ule na kwamba uchambuzi unaendelea hivi sasa.

Je, kwa nini kuharakisha mambo haya ambayo yanaleta hasara kwa sababu kuna matatizo ya ukiritimba ambao umetajwa na Mheshimiwa Mbunge kwamba baadhi ya watu wanaomba maeneo ya uwindaji lakini bado kuna ukiritimba wa kuweza kupata maeneo hayo likiwemo la kule Morogoro kama maeneo ya Matambwe na maeneo ya kwa Mbunge wa Ngorongoro?

Ahsante nashukuru sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Pawa, kama ifuatavyo:-

Kwanza napenda kusema kwamba Serikali imekuwa makini na Wizara hizi kwa kweli zimekaa lakini kuna utaratibu wa *WMA* kwa mfano kama eneo liko katika hifadhi basi lazima lifanywe kuwa eneo la kijiji na kwa maana hiyo iko katika sheria ya *Local Government* lakini mbali ya hivyo kuna utaratibu pia wa kufikia hizi *WMA*.

Kwa mfano lazima maeneo hayo yakamilishe kwa mfano Mpango wa Usimamizi na Matumizi Bora ya Ardhi yaani kuwepo na *Land Use Plan,* lazima pia kuainisha ukubwa wa maeneo ya uhifadhi wanyamapori jumla yake ni kilomita ngapi na kadhalika na pia kuwepo na kuanzishwa mabaraza ya Wilaya ya ushauri.

Kwa hivyo kuna hizo taratibu ambazo lazima zifuatwe kabla ya kuwa *WMA* kamili.

Na. 219

**Pori la Akiba Liparamba**

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI (K.n.y. MHE. DK. THADEUS M. LUOGA** aliuliza:-

Kwa kuwa, idadi ya wanyama katika Pori la Akiba la Liparamba inaonezeka kwa haraka mno na wengi wao wanaingia kutoka Msumbiji:-

(a) Je, isingekuwa vema kwa sasa zoezi la kuhesabu wanyama likafanyika ili kujua idadi na aina ua wanyamapori waliomo ndani na nje ya pori hilo?

(b) Je, ni lini pori hilo litapandisha hadhi kuwa Hifadhi ya Taifa ndani ya Wilaya ya Mbinga –Ruvuma.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mbunge wa Mbinga Magharibi, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Pori la Akiba la Liparamba lilitangazwa rasmi kuwa Pori la Akiba kwenye Gazeti la Serikali Namba 289 la tarehe 18/8/2000. Tangu kutangazwa kwa pori hili Wizara ya Maliasili na utalii imeendeleza uhifadhi katika pori hilo kwa kuongeza vitendea kazi.

Wizara tayari imekwishapeleka gari moja jipya aina ya *Land Rover* pamoja na mahema ya sare za kazi zinazotumiwa na watumishi watano (5) wanaosimamia pori hilo.

Aidha, Wizara iliendelea kutenga mafungu ya fedha kwa ajili ya kufanya doria na kuboresha miundombinu hasa barabara na madaraja. Juhudi hizi za uhifadhi zimechangia katika ongezeko la wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mbunge wa Mbinga Magharibi lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(b) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, hakuna fungu la fedha lililotengwa kwa ajili ya kuhesabu wanyama katika Pori la Akiba la Liparamba.

Aidha, Wizara imetenga fedha kwa ajili ya kuhesabu wanyama kwenye pori hili ambayo ni sehemu mojawapo katika mchakato wa kukusanya taarifa muhimu katika mwaka wa fedha 2005/2006 kwa kuzingatia kipaumbele na uwezo wa Wizara kugharamia zoezi hilo.

(c) Upandishaji wa hadhi wa pori la Akiba kuwa Hifadhi ya Taifa huzingatia masuala muhimu ambayo ni pamoja na mambo yafuatayo:

- Kuwepo kwa bioanuai ambazo ziko kwenye hatari ya kutoweka ulimwenguni.

- Kuwepo kwa matumizi endelevu ambayo yanaweza kufanyika bila kuleta athari kubwa kwa rasilimali ya maliasili ya na mazingira.

- Kuwepo kwa miundombinu ya kutosha kukidhi mahitaji ya utalii wa picha.

- Kuwepo kwa wanyama wa kutosha (Kwa wingi wa aina) ambao wataweza kuonekana kwa urahisi.

- Eneo kuwa na kiwango cha chini cha Mbung'o ili watalii wasitumie gharama kubwa kujikinga dhidi ya wadudu hao hatari.

Pamoja na hayo, Wizara haioni sababu za msingi za kubadili hadhi na matumzi ya sasa ya pori hilo jipya ambalo bado linaimarishwa kiulinzi na kuendeleza rasilimali ya wanyamapori na mazingira pamoja na kuendelea na kazi ya kukusanya taarifa muhimu kuhusu hali ya bioanuai iliyomo na mazingira yake.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelezo niliyoyatoa, kwa sasa Pori la Liparamba litaendelea kusimamiwa kama pori la akiba kama lilivyotangazwa na Serikali hadi hapo itakapoonekana kuna umuhimu wa kupandishwa hadhi kuwa Hifadhi ya Taifa.

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, napenda kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Pori la Liparamba ingawa ni pori jipya lakini tayari wananchi wanaoishi karibu na pori hilo wanalalamika juu ya wanyamapori kama vile ilivyokuwa *Selou Game Reserve.* Wakati wa masika wanyama wanatoka kwenda kula watu kama vile simba kwa sababu wanyama wako wengi. Je, Wizara ina mpango gani wa kuweka *Game Reserves* nyingi ili kuzuia hali hiyo isitokee?

(b) Pori la Liparamba pamoja na kusema kwamba haliwezi kupandishwa hadhi kuwa Hifadhi ya Taifa, inakadiriwa kwamba kukua kwa wanyama hao kwa kiasi gani mpaka pale ambapo pori hili linaweza kuwa ni Hifadhi ya Taifa?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuhusu wafanyakazi katika maeneo haya ni wachache na mara nyingine wanyama hao huathiri wananchi. Napenda kusema kwamba Wizara imekuwa inawasiliana na Wizara

ya Utumishi ili kuweza kupata wafanyakazi zaidi. Katika kipindi hiki tumeweza kupata wafanyakazi zaidi, lakini japokuwa hawatoshelezi.

Serikali kwa kutambua hilo imefanya utaratibu wa kuwa na *Village Game Scouts*. Kwa hiyo, kuna *Village Game Scouts* ambao wanatoka katika maeneo hayo hayo ya vijiji na ambao kwa kweli wanashirikiana pamoja na wananchi katika suala nzima la kuimarisha *protection* ya wananchi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuwa Hifadhi ya Taifa nafikiri nimeeleza hapa ni mambo gani ambayo lazima yatekelezwe ili eneo lolote liwe Hifadhi ya Taifa. Kwa hiyo, sifikiri kama kuna haja ya kurudia hayo niliyoyaeleza.

Lakini nimeeleza kwa mfano, suala zima la kuwa bioanuai ambayo ipo kwenye hatari ya kutoweka, kuwa matumizi endelevu, kuwepo kwa aina mbalimbali za wanyama na wengi pia. Huwezi ukawa na Hifadhi ya Taifa ukawa na wanyama wachache kwa mfano, wasiwe wa aina mbalimbali kwa sababu hata ukileta watalii hawataweza kuwaona hao wanyama.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza swali kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Mikoa yote ya Kusini haina Hifadhi ya Taifa hata moja; na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri hajapata nafasi ya kutembelea eneo hilo; na kwa kuwa sisi tunafahamu hilo eneo lina wanyama wa kutosha, lina vivutio na ni sehemu ya mto Ruvuma na kuna milima mizuri sana.

Je, haoni sasa ni wakati wa kutoa kipaumbele kulitangaza hilo eneo likawa Hifadhi ya Taifa ili nayo Mikoa ya Kusini ipate heshima kama inavyopata Mikoa mingine? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, unaposema kwamba kuna wanyama lazima kufanya utafiti, huwezi tu ukaenda ukasema unaona wanyama katika eneo ndogo, halafu ukasema kwamba basi kuna wanyama mbalimbali lazima kuwepo na utafiti na ndiyo maana tunafanya utafiti. Pale ambapo pia utafiti unafanywa tunajua wanyama hao kama nilivyokuwa nasema hapa kwamba hawana *passport* wanazunguka. Wanyama hao katika pori hilo wanakwenda sehemu za Msumbiji.

Kwa hiyo, wanapofanya utafiti pia inabidi wakati huo huo utafiti unafanyika Tanzania na utafiti unafanyika Msumbiji ili tusije tukaona kwamba wanyama wale wako

Tanzania kumbe wako Msumbiji. Kwa hiyo, hili napenda kusema kwamba utafiti lazima hufanyike na siyo wanyama ambao tunawaona hivi hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nipende kusema pia hivi sasa kuna pori la Hifadhi ya Taifa ambalo tumepitisha hapa Bungeni la Katavi ambapo kwa kweli Katavi itakuwa ni *National Park* na inaongeza Hifadhi za Taifa katika upande wa Kusini. *(Makofi)*

Na. 220

**Ujenzi wa Uwanja wa Taifa**

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais William Benjamin Mkapa aliahidi kwamba Serikali itajenga na kukamilisha Uwanja wa Taifa wa Dar es Salaam kabla ya kumalizika kwa kipindi chake cha Uongozi. Je, ni lini ujenzi wa uwanja huo utakamilika?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI) (K.n.y. WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Diodorus Buberwa Kamala, Mbunge wa Nkenge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Wizara yangu inaendelea na shughuli za ujenzi wa eneo Changamani la Michezo ya Taifa (*National Sports Complex*) lenye hadhi ya viwango vya Olimpiki ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais William Benjamin Mkapa ya kuwaachia Watanzania uwanja wa kisasa wa michezo. Ujenzi huu utakapokamilika Tanzania itakuwa na eneo bora Changamani la Michezo ambalo litatumika kwa kufundishia na kuchezea michezo katika viwango vya Olimpiki.Utekelezaji wa mradi huu unafanyika kwa awamu mfululizo (*continue phasing*), na katika awamu ya kwanza unajengwa uwanja Mkuu wa michezo wenye hadhi ya Olimpoiki na viiwango vya *FIFA* na *IAAF*. Uwanja huu ukikamilika utakuwa na uwezo wa kubeba watazamaji 60,000 wakiwa wamekaa, na paa lake likiwa limefunikwa kwa asilimia 70. Awamu ya hii inajengwa kwa ushirikiano baina ya Serikali ya Jamhuuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China. Kazi ya ujenzi inafanywa na *MS.Beijing Construction Engineering Group Co. Ltd*. kutoka China. Kulingana na Mkataba, ujenzi ulianza tarehe 2 Novemba, 2004 na utachukua miezi 26, hivyo tarehe ya kukamilika ni tarehe 1 Junuari, 2007.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri.

(a) Kwa kuwa lengo la kuwa na uwanja huo ni kuendeleza michezo, lakini kwa kuwa ni dhahiri uwanja mzuri hautakuwa na manufaa kama hatuna timu nzuri. Je, ni jitihada gani zinazofanywa na Serikali kuhakikisha vilabu vyetu vya mpira vinakuwa tulivu na maamuzi halali ya wanachama yanaheshimiwa na vyombo husika vya Serikali?

(b) Kwa kuwa mwaka 2000 wanachama wa Yanga na mimi nikiwemo kama mwanachama tulikubaliana kwamba tuwe na kampuni, lakini hadi leo msajili wa michezo hajaridhia. Je, hiyo siyo kuingilia uhuru wa vilabu? *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI) (K.n.y. WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwapo kwa uwanja mzuri kama huo bila kuwa na timu nzuri inaweze isiwe na *impact* kubwa au ikawa na heshima kubwa katika nchi hii. Lakini Serikali ijitahidi sana kuviimarisha vyama mbalimbali vya michezo na kila mara imekuwa inasisitiza kwamba suala la uimarishaji wa vyama vya michezo si la Serikali peke yake bali ni la wanachama lakini na vilabu vinavyomiliki michezo hiyo. Kwa hiyo, kwa ushirikiano huo tutaendelea kushirikiana na vilabu, viongozi wa vilabu hivyo na vyama vya michezo mbalimbali kuhakikisha kwamba nchi yetu inakuwa na wanamichezo wazuri wanaofanana na hadhi ya uwanja unaojengwa.

La pili, ni kweli Yanga wameunda kampuni, lakini mimi siyo mwanachama wa Yanga, lakini najua kwamba yanga wameanzisha kampuni na wanao huo utaratibu. Ningependa tu kutoa ushauri kwa Mheshimiwa Mbunge na mwanachama mwaminifu wa Yanga kwamba wiki ijayo tutasoma bajeti yetu hapa na huyo anayekwamisha usajili wa Yanga atakuwa hapa, tukumbushe tu atakapokuwa hapa tulizungumze jambo hili kwa karibu zaidi ili tuone kwa nini hataki kufanya kazi hiyo. *(Makofi)*

**MHE. HADIJA K. KUSAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa suala la kujenga Uwanja wa Taifa ni suala kubwa sana na uamuzi wa kuujenga uwanja huo katika Wilaya ya Temeke hususan Jimbo la Temeke nalo ni suala kubwa sana. Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa yuko tayari kuchukua salamu za wana-Temeke kumpelekea Mheshimiwa Rais pokezi kubwa kwa kukubali uwanja ule hujengwe Temeke? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri uko tayari kupeleka salamu hizo!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI) (K.n.y. WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubali hiyo heshima na nakubali sana pongezi za Mheshimiwa Mbunge wa Chama cha Mapinduzi wa Wilaya ya Temeke, salamu hizo tutamfikishia Mheshimiwa Rais na Watanzania wote wamesikia. *(Makofi)*

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa kilio cha Mheshimiwa Mbunge wa Temeke Mheshimiwa Rais alikisikia na kutoa ahadi. Je, sasa

Serikali haioni kitendo cha kutopunguza kodi za vifaa vya michezo na kuchelewa kuanzisha michezo ya kulipwa kitachelewesha vijana kupata ajira ya uhakika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri swali hili ni jipa lakini unaweza kujibu kama unayo majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI) (K.n.y. WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshauri ndugu yangu Mheshimiwa Venance Mwamoto kwamba hili ni suala la kisera na ni kubwa sana na lina uzito wake. Najua Mheshimiwa Venance Mwamoto ni mwanamichezo na maswali yake huwa yanahusu michezo na yanahitaji kufanyiwa utafiti wa kina. Kwa sababu ni la kisera naomba alilete kwa utaratibu wa kawaida ili tukupe majibu muafaka.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha majibu ya ziada.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuongezea jibu la Mheshimiwa Waziri kwa kusema kwamba jambo la maana tunavyoliona sisi kwa sasa ni kuboresha mapato ya wanamichezo na kwa kuanzia na kama nitakavyotangaza baadaye kabla ya mwisho wa Bunge hili, tutatoa nafuu ya kodi kwa wanamichezo wanaokwenda ng'ambo na kushinda zawadi na kuzileta nchini ambapo zitaingia bila kodi wala ushuru. *(Makofi)*

Na. 221

**Vijana – Nguvu Kazi ya Taifa**

**MHE. LEPHY B. GEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa sote tunaamini kwamba vijana ndio nguvu kazi ya Taifa letu na tunawaona mitaani vijana wengi waliomaliza elimu ya darasa la saba wamekaa tu bila utaratibu maalum:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya makusudi ya kuwasaidia vijana hao ili waweze kutumika ipasavyo katika kulijenga Taifa hili?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI) (K.n.y. WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gembe, Mbunge wa Mpanda Kati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukubaliana na Mheshimiwa Lephy Gembe, Mbunge wa Mpanda Kati , kuwa vijana ndiyo nguvu kazi ya Taifa letu. Vijana vilevile

ni hazina muhimu ya Taifa ambayo inahitaji kuhifadhiwa na kutumika vizuri, ili kuweza kutoa mchango wao na kuongeza tija katika uzalishaji na kuinua pato la Taifa na Maendeleo kwa ujumla. Kwa Tanzania vijana ni takriban asilimia 33 ya idadi ya Watanzania na asilimia 68 ya nguvu kazi. Hii inaonyesha kuwa kundi hili ni kubwa katika jamii na linahitaji kupewa kipaumbele na kuandaliwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi sasa napenda kumjibu Mheshimiwa Gembe, Mbunge wa Mpanda Kati, kama ifuatavyo:-

(a) Serikali imeanzisha Vyuo vya Ufundi Stadi kwa madhumuni ya kuwapatia vijana stadi mbalimbali ili waweze kujiajiri au kuajiriwa Aidha, tunavisaidia vyuo vya watu binafsi na vya taasisi zisizo za Kiserikali vinavyojihusisha na ufundi stadi kwa taaluma na vifaa vya kufundishia.

(b) Wizara yangu inayo Sera ya Maendeleo ya Vijana ambayo Ruya na Mipango yake ya utekelezaji inahamasisha vijana kujiunga katika vikundi vya vijana vya uzalishaji mali (VVKM) ili Serikali iweze kuwafahamu idadi yao, mahali walipo na jinsi ya kuwafikia kwa ufanisi.

(c) Ili kuwaondoa vijana katika umaskini uliokithiri, vijana walio katika vikundi hupewa mafunzo ya stadi za kazi, ujarisimali na ushauri. Aidha, katika mfuko wa vijana kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya vijana huweza kupata mikopo inayowawezesha kuongeza mitaji na shughuli za uzalishaji.

(d) Ongezeko la Bajeti katika sekta mbalimbali hususan za Elimu kuanzia *Primary* mpaka Sekondari hadi Chuo Kikuu, sera na mipango mbalimbali ya Serikali kama vile MMES na MMEM na kadhalika yote inalenga kuwasaidia vijana sambamba na jitihada za *NGO* na mashirika mengine yasiyo ya Kiserikali.

**MHE. LEPHY B. GEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Pamoja na majibu yake mazuri napenda kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa moja ya ajira ya vijana ni pamoja na upigaji wa debe na wapiga debe wapo Mpanda Mjini, Iyonga na Mpimbwe na kote nchi nzima. Inaonaje Serikali kama ingeweka mikakati mahsusi ya kuwawekea mazingira mazuri hao wapiga debe ili kuepukana na matatizo ambayo yamejitokeza kama yaliyojitokeza juzi kule Dar es Salaam baina ya wapiga debe na *Security Group*? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI) (K.n.y. WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ikiratibiwa vizuri ni kweli kazi hii inaweza kuwa ajira ya kutosha kwa vijana. Lakini wanachokifanya Dar se Salaam ni kwa sababu kazi hii imekuwa inafanywa ovyo ovyo na kusababisha vurugu katika Jiji la Dar es Salaam na ndiyo maana wameamua sasa kuifanya vizuri zaidi ili kuondoa kero kwenye vituo na kusalimisha mali ambazo zimekuwa zinaibiwa za wasafiri mbalimbali wanapotumia huduma za mabasi ya Jiji la Dar es Saalam. Kwa hiyo, hiyo ndiyo sababu ambayo Dar es Salaam wameamua kuwaondoa wale wapiga debe ni kwa sababu tu ya

vitendo vilivyokuwa vinaambatana na shughuli zao. Lakini nakubali kwamba kama ikiratibiwa vizuri kazi hii inaweza kuwa sehemu ya ajira ya kuwapa tija vijana.

Na. 222

**Mradi wa wa *Quick Start* kwa Mahakama**

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA (K.n.y. MHE. DR. WILLBROD P. SLAA)** aliuliza:-

Kwa kuwa wafadhili wengi walionyesha nia ya kusaidia kuboresha Mahakama zetu mbalimbali kwa hatua za awali kupitia mradi wa *Quick Start* ambao unahusisha Mikoa ya Arusha na Manyara; na kwa kuwa mradi huo ulizinduliwa rasmi na Waziri Mkuu Mheshimiwa Frederick Tumaye, Mjini Arusha:-

(a) Je, hadi kufikia tarehe 30/5/2005 ni Mahakama ngapi zimejengwa katika maeneo husika ikiwemo Wilaya ya Karatu; na kwamba kwa kuwa Mikoa ya Arusha na Manyara ilikuwa ni *Pilot Area*. Je, ni lini mpango huo utafikishwa katika Mikoa mingine hapa nchini?

(b) Kwa kuwa mradi huo unalenga pia kuwashirikisha wananchi. Je, ni fedha kiasi gani kimechangwa na wananchi wa Wilaya Hanang, Babati, Mbulu na Karatu ikitoa mchanganuo kwa kila Wilaya na kwamba, fedha hizo zimetumika kwa ajili ya shughuli zipi kwa mchanganuo wa matumizi kwa Wilaya ya Karatu; na je, ni nani alihusika kukusanya michango husika katika Wilaya ya Karatu, na kiasi gani kilikusanywa kwa kila kijiji, ziliwekwa kwenye akaunti gani na zinakaguliwa na mamlaka ipi?

(c) Zipo taarifa kuwa kuna vitabu vya michango kwa Wilaya ya Karatu vimepotea na au havijawasilishwa kwenye Ofisi ya Mkuu wa Wilaya inayohusika kupokea michango hiyo; je, hadi kufikia tarehe 30/5/2005 ni vitabu vingapi havijarudishwa au havijatolewa taarifa na wahusika wamechukuliwa hatua gani?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mradi wa *Quick Start* ulifungwa tarehe 31 Desemba, 2004 na shughuli zote zilizokusudiwa kutekelezwa chini ya mradi huo sasa zitatekelezwa kama sehemu ya Mkakati wa Kati wa Mpango wa Kuboresha Sekta ya Sheria uliozinduliwa tarehe 22 Machi, 2005. Hadi Mradi *Quick start* ulipofungwa, katika Mkoa wa Manyara, Wilaya ya Mbulu ilishakamilisha lengo lake la kukarabati na kuweka mipaka ya maeneo ya Mahakama. Katika maeneo mengine, hakuna ujenzi wowote wa Mahakama uliokamilika kwa kuwa Wilaya zilishindwa kukamilisha majukumu yaliyohitajika kwa wakati. Mpango kama huu utafikishwa katika Mikoa mingine baada ya kuukamilisha katika maeneo ya majaribio ili yale tuliyojifunza katika majaribio tuweze kuyazingatia kwa ukamilifu.

(b) Mchanganuo wa fedha zilizochangwa kwa kuwashirikisha wananchi ni kama ifuatavyo:-

Wilaya ya Hanang imekusanya Shs.27,041,075. Wilaya ya Mbulu ilikusanya Shs.47,930,700/= na Wilaya ya Karatu ilikusanya Shs. 13,000,000. Mwenye jukumu la kukusanya na kutunza kumbukumbu za michango ni Halmashauri na ni lazima ionyeshwe katika hesabu za mapato na matumizi na ikaguliwe kama ilivyo kwa mapato na matumizi yoyote ya Halmashauri za Wilaya.

(c) Tofauti na ilivyokuwa katika sehemu nyingine, wakati michango ya wananchi inaanza kukusanywa, ulikuwepo mgogoro uliohusisha Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Karatu na Baraza la Madiwani. Kwa sababu hiyo, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ndiyo ilihusika kupokea michango hiyo. Maelekezo ya Serikali kwa sasa ni kuwa fedha na mali zote zilizokusanywa kukabidhiwa katika Ofisi ya Mkurugenzi. Kwa kuwa zoezi la kukabidhiana likikamilika itatolewa taarifa ya Mhasibu wa Halmashauri, hiyo ndiyo itatuwezesha kuwa na ufahamu wa uhakika kwa suala hilo. Serikali, kupitia Tawala za Mikoa na yenye dhamana kwa watendaji wa Sekretarieti ya Wilaya na ya Halmashauri za Wilaya, itaendelea kulishughulikia kama ilivyoelezwa wakati Wizara hiyo ikihitimisha hoja yake ya Bajeti mwaka huu 2005.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja la nyongeza. Nia ya mradi huu inaonekana ni nzuri na kwa sababu suala hili la majengo ya Mahakama na matatizo mengine ya Kimahakama hayako katika Mkoa wa Manyara na Arusha tu. Je, ni lini Serikali itasambaza mradi huu kwa hiyo njia ambayo wanaitumia katika maeneo mengine ya Tanzania?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba sasa hivi mradi huu umefungwa na tumeuhamishia mradi huu sasa katika *Legal Sector Reform Programme*. Kwa hiyo, baada ya hapo tukishapata uzoefu huo ndiyo tunaweza kufikiria Mikoa mingine.

Na. 223

**Uwezeshaji wa Tume ya Pamoja ya Fedha**

**MHE. ALI AMEIR MOHAMED** aliuliza:-

Kwa kuwa Tume ya Pamoja ya Fedha iliundwa ili kutekeleza matakwa ya Ibara ya 134 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano; na kwa kuwa majukumu ya Tume hiyo ni pamoja na kuchambua mapato na matumizi yanayotokana na au yanayohusu utekelezaji wa mambo ya Muungano na kuchunguza kwa wakati wote mfumo wa shughuli za fedha za Jamhuri ya Muungano na uhusiano katika mambo ya kifedha kati ya pande zote mbili za Muungano:-

(a) Je, Serikali inaweza kulieleza Bunge hili hatua ambazo imechukua kuiwezesha Tume hiyo muhimu kutekeleza majukumu yake?

(b) Kwa kuwa Katiba ya Nchi, katika Ibara ya 134 haionyeshi umri wa Tume hiyo zaidi ya kusema ni ya pamoja. Je, Tume iliyoundwa itadumu kwa muda gani?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Mbunge wa Donge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-
(a) Hatua ambazo Serikali imekwishachukua kwa nia ya kuiwezesha Tume ya Pamoja ya Fedha kuanza kutekeleza majukumu yake ni pamoja na kutoa kiasi cha shilingi milioni 700 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Tume kwa mwaka wa fedha 2003/2005 na pia kutoa kiasi kingine kama hicho mwaka wa fedha 2004/2005. Fedha hizo ziliiwezesha Tume kuwa na uwezo wa:-

(i) Kukodi ofisi zake kwenye Jengo la Sukari lililopo kwenye makutano ya Barabara ya Sokoine na Mtaa wa Ohio Jijini Dar es Salaam na katika jengo la Kitega Uchumi la Shirika la Biashara la Zanzibar *(ZSTC)* lililopo eneo la Gulioni, Zanzibar.

(ii) Kununua vifaa, nyenzo na huduma mbalimbali za ofisi. Aidha katika kipindi hiki cha mpito ambapo Tume bado haijaajiri watumishi wake, Serikali imeiwezesha Tume kuanza kutekeleza majukumu yake kwa kuwapeleka kwenye Tume Watumishi kadhaa ambao wanafanya kazi kwa utaratibu wa kushikiza (*attachment)*. Watumishi hawa wanatoka Wizara ya Fedha, Serikali ya Muungano Tanzania (SMT), Benki Kuu ya Tanzania, Mamlaka ya Mapato Tanzania na Bodi ya Mapato Zanzibar. Katika Mwaka wa fedha wa 2005/2006, Tume imepanga kuajiri watumishi wake mara baada ya taratibu za Kiserikali kukamilika.

(b) Ni kweli kwamba Ibara ya 134 ya Katiba haionyeshi umri wa Tume hiyo. Hata hivyo, Ibara ya Ndogo ya 2(c) inaelekeza kwamba Tume itatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge. Kwa msingi huo, pamoja na Katiba, Tume inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya "*The Joint Finance Commission Act*," ya mwaka 1996. Fungu la 6 la Sheria hiyo linaelekeza kwamba muda wa Tume utakuwa ni miaka mitano. Hivyo basi, kwa vile Wajumbe wa Tume waliopo hivi sasa walioteuliwa mwaka 2003 na hivyo kipindi chao kitamalizika mwaka 2008.

**MHE.ALI AMEIR MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ningependa kumuuliza tu kwamba kwa kuwa suala la kuwa na Tume hii ni suala la Katiba na ni la muda mrefu, hivi kwa nini Serikali inasuasua katika kuifanya Tume hii iwe kamili na kwa hiyo kuondoa miongoni mwa kero za Muungano ambazo zinalalamikiwa sana hasa katika masuala ya mapato na matumizi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano ikihusiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba suala hili limetajwa katika Katiba. Lakini baada ya hapo ilikuja ikatungwa Sheria ya kutekeleza Ibara ile. Kwa hiyo, sasa hivi tuna hiyo "*Joint Finance Commision Act"* ya mwaka 1996 na hivi majuzi tuliifanyia marekebisho sheria ile ili kumwezesha Waziri wa Fedha kuweza kutengeneza *regulations*. Nadhani baada ya *regulations* kutengenezwa matatizo hayo tutakuwa tumeyamaliza. *(Makofi)*

Na. 224

**Wilaya ya Geita Kutofaidi Matunda ya *Geita Gold Mine***

**MHE. ERNEST G. MABINA** aliuliza:-

Kwa kuwa mgodi wa *Geita Goldmine Limited* unaiingizia Serikali fedha nyingi, lakini Serikali hiyo hiyo imeitelekeza Wilaya ya Geita kwa kutoipatia huduma za jamii kama vile Shule za Msingi na Sekondari, ambapo wananchi wanajijengea wenyewe, huduma za afya kama vile Vituo vya Afya vya Kajamwa, Bukoli na Kharumwa ambavyo vimejengwa kwa nguvu za wananchi wenyewe ikilinganishwa na fedha zilizopatikana kutoka kwenye mgodi huo, hivyo wananchi hawaoni faida ya kuwa na mgodi huo katika maeneo yao:-

Je, Serikali itasaidiaje Wilaya hiyo kwa kuhakikisha kuwa inapewa fedha nyingi ili kuboresha huduma za jamii zinazolingana na kiasi cha fedha kinachozalishwa katika Wilaya hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA) (K.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ernest Mabina, Mbunge wa Geita, kama ifuatavyo:-

Serikali ina mpango wa maendeleo ya nchi nzima unaofuata malengo na uwiano ulioamuliwa kwa kuzingatia maslahi ya Taifa zima. Hivyo, kwa kuzingatia misingi ya Kitaifa Wilaya ambazo hazina vitega uchumi vya rasilimali ambazo zingeshindwa kupata fedha za huduma za jamii hufaidika kama Wilaya nyingine zenye rasilimali kama madini.

Makusanyo ya kodi mbalimbali za Serikali yatokanayo na mgodi wa Geita hupelekwa Hazina ili fedha hizo ziweze kutumika kwa shughuli mbalimbali za maendeleo ya Taifa. Hivyo, Wilaya ya Geita, kama zilivyo Wilaya nyingine nchini, hunufaika na mpango wa maendeleo ya nchi nzima.

Hata hivyo, kama ilivyo kwa Wilaya nyingine zenye rasilimali mbalimbali yakiwemo madini, Kampuni ya *Geita Gold Mine,* imefanya na inaendelea kugharamia

huduma za kijamii Wilayani Geita. Kampuni inaendelea kushirikiana na wananchi katika maendeleo na utoaji wa huduma mbalimbali za jamii kama ifuatavyo:-

- Kujenga Vituo vya huduma za afya vya Kasamwa, Bukoli na Karumwa kwa gharama ya Shs.41,700,000/=;
- Kujenga barabara yenye urefu wa kilometa 62 kutoka Geita hadi Ologi na hivyo kuunganisha Mji wa Geita na Isaka;
- Kujenga bomba kubwa la maji urefu wa kilomita 25 toka Ziwa Victoria hadi Mgodini na kuwapa wakazi wa Vijiji jirani, maji kutoka kwenye mabomba 11 yaliyounganishwa kwenye bomba kubwa;
- Kujenga wadi mpya ya Hospitali ya Wilaya ya Geita;
- Kutoa umeme na maji kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya ya Geita;
- Kujenga Shule moja ya Msingi;
- Kujenga na kukarabati barabara ndogo katika Wilaya ya Geita zenye jumla ya kilometa 50;
- Kujenga uwanja wa ndege na nyumba mbili kwa ajili ya Ofisi za Polisi na Uhamiaji;
- Kampuni imeajiri wafanyakazi 1,300 ambao kati yao asilimia 85 ni Watanzania.

**MHE. ERNEST B. MABINA**: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa uzoefu unaonyesha kwamba kila tunapoanzisha migodi kunakuwa na migogoro kati ya wawekezaji na wananchi wanaokaa maeneo ya pale. Kwa mfano Geita, Lusu na Kakola. Hii yote inatokana kwamba wanapokuja wawekezaji wale wananchi wanaokutwa pale huwa hawatengewi maeneo maalum ya kuweza kujiendeleza katika maisha yao.

Je, Serikali inasemaje kuhusu kuwatengea maeneo ya wachimbaji wadogo wadogo ambao wanaweza wakajiletea pato katika Taifa lao?

Je, Serikali ya Tanzania imeiga mfano wa nchi gani ambao wawekezaji wanapokuja kunakuwa na migogoro kama inavyoonyesha katika Tanzania hii? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA) (K.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nikubaliane na wazo la msingi kwamba ni vizuri kuwashirikisha wananchi pale ambapo wawekezaji wanakwenda kufanya shughuli zao ili kuepuka kwanza migogoro mahali panapotekelezwa shughuli za uchumi kama uchimbaji wa

madini. Maana penye migogoro kazi haziendi. Kwa hiyo, naamini katika Tume au Kamati ile iliyoundwa kuangalia namna bora ya kuendesha shughuli zetu za uchimbaji madini kwa kushirikiana na wawekezaji, ninaamini wazo hili la msingi litapata nafasi ya kuona litekelezwe vipi.

Swali la pili kwamba je, Tanzania imeiga mfano gani; sisi Tanzania tusingependa kuiga mfano wa mahali ambako kunatokea migogoro. Tungependa kwanza kama kuna mahali ambapo migogoro inatokea sisi tujifunze kukwepa migogoro mahali zinapofanyika shughuli za uwekezaji. Kwa hiyo, sisi tunapenda kufanya yale ambayo ni ya manufaa kwa nchi yetu. Pale migogoro inapojitokeza tutajifunza kutokana na matatizo yanayojitokeza ili tuyatatue kwa manufaa ya ukuaji wa uchumi wetu.

**MHE. FAUSTINE K. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniruhusu niulize suala la mwisho la nyongeza. Katika jibu la Mheshimiwa Waziri amesema kwamba wamejenga barabara zaidi ya kilometa 50 ambayo barabara hiyo inapita porini haipiti kwa wananchi, ni kwa ajili ya kusomba mizigo ya wawekezaji kupeleka Geita kwenda Kahama. Amesema wamejenga uwanja wa ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uwanja wa Ndege kwanza umejengwa porini na wananchi hawaruhusiwi hata kusogea eneo hilo. Amesema kuna bomba la maji kutoka Ziwa Victoria kuja mgodini. Ni vitundu kama sita mahali pa kupumulia ambapo wananchi wanakwenda kupata maji pale. Je, huoni Mheshimiwa Waziri kwamba ni kudanganya Bunge hili kwamba wananchi wa Geita wanafaidika na mgodi huo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA) (K.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba hii barabara iliyojengwa ya kilometa 50 inapita porini; kwanza kabla ya mgodi huu kufunguliwa ni dhahiri kwamba eneo hilo halikuwa na barabara, kulikuwa na pori ambalo kwa Kiingereza tungesema ni *virgin forest*. Lakini barabara inajengwa kutoka tuseme sehemu “A” kwenda sehemu “B”. Sasa kama inapita porini sidhani kwamba ingekuwa ni sahihi, maana barabara hazipiti hewani.

Swali lingine kwamba uwanja wa ndege huu umejengwa mbali na wananchi hawaruhusiwi kusogea, mimi nina hakika Mheshimiwa Mbunge anajua kwanza hata iwe ni kiwanja cha ndege kama hapa Mjini Dodoma. Tunajua kwamba viwanja vinawekewa uzio kwa usalama wa wananchi wenyewe. Sasa kama kiwanja kimejengwa mahali ambako ni mbali na makazi ya wananchi. Hivyo ndivyo inavyotakiwa.

Mimi juzi nimetoka Kibondo nimepita pale Kahama nimeona pana uwanja mdogo wa ndege umejengwa sambamba na barabara kuu na ile ni hatari. Kwa hiyo, ni vizuri uwanja wa ndege ukawa mbali na mahali wanakoishi wananchi.

Kuhusu Kampuni hii ya *Geita Gold Mine* kwamba ni kweli wamechukua maji Ziwa Victoria, tumesema katika jibu letu kwamba kuna maeneo kama 11 wananchi wameruhusiwa kupata maji kutoka bomba kuu. Yeye anasema ni vitundu vidogo tu na watu wanafuata maji kule. Lakini kabla ya hapo wananchi walikuwa hawapati maji hayo ya Ziwa Victoria. Tukubali hii ni hatua ya maendeleo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kipindi cha maswali tuishie hapo. Nina tangazo moja tu. Kesho Jumamosi kutakuwa na Semina muhimu sana humu ndani ya Bunge. Kama kawaida yetu, Semina hiyo itaendeshwa na Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji, inahusu Mpango Maalum wa Kuharakisha Maendeleo ya Taifa unaoitwa "*Tanzania Mini-Tiger Plan.*" Ni jambo hatujalisikia, kwa hiyo, ni muhimu tukawepo. Kwa hiyo, kesho Semina kama kawaida. Sasa hili ni tangazo tu ambalo nilikuwa nalo. Sasa tunaendelea.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali Kwa Mwaka 2005/2006

### Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kujadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2005/2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuwasilisha hotuba yangu mbele ya Bunge lako Tukufu, napenda nichukue fursa hii kutoa pole kwa wafiwa wote wa Wabunge wenzetu watano waliofariki dunia katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2004/2005. Marehemu hao ni Margareth Bwana (Viti Maalum), Abu Towegale Kiwanga (Kilombero), Balozi Ahmed Hassan Diria (Raha Leo), Kapteni Theodos James Kasapira (Ulanga Mashariki) na Frank Michael Mussati (Kasulu Mashariki). Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu wote hao mahali pema Peponi. Amin.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa Waziri mwenzangu na Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuteuliwa na Chama cha Mapinduzi kuwa Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naungana na mamilioni ya Watanzania na marafiki wengi wa nchi yetu kumwombea kila la kheri na ushindi wa kimbunga cha tsunami katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba mwaka huu wa 2005. Dalili zote zinaonyesha kwamba ushindi huo ni wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwapongeza Viongozi Wakuu wa nchi yetu, Mheshimiwa Dr. Ali Mohammed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuteuliwa na Chama chao cha CCM kutetea

nafasi zao hizo katika Uchaguzi Mkuu ujao. Nchi yetu bado, inauhitaji uongozi wao na ni matarajio yangu, kama yalivyo ya Watanzania kwa ujumla, kwamba watathibitishiwa imani ya Watanzania katika Uchaguzi Mkuu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi zangu haziwezi kukamilika bila ya kuwataja Waheshimiwa Frederick Tluway Sumaye - Mbunge na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba - Mbunge na Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Abdallah Omar Kigoda - Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji. Hotuba zao walizotoa mapema katika Mkutano huu wa Bunge zimeonyesha kiwango cha kujivunia cha maendeleo kilichofikiwa na nchi yetu katika nyanja za kiuchumi, kijamii, miundombinu, utawala bora na kadhalika.

Aidha, hotuba hizo zimetoa mwelekeo wa matumaini wa Bajeti ya Serikali na hali ya uchumi wa nchi yetu kwa jumla. Kutokana na nafasi zao za uratibu wa shughuli hizo Kitaifa, wanastahili pongezi za dhati kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba zote tatu za Viongozi hao zilielezea kwa upeo mpana wa Kitaifa mafanikio makubwa yasiyo kifani ya Serikali ya Awamu ya Tatu na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivi punde, nami nitaelezea mafanikio ya Serikali hiyo katika eneo mahsusi la Wizara yangu. Mafanikio yote hayo ni matunda ya utekelezaji makini wa Ilani za Uchaguzi za CCM za 1995 na 2000 chini ya usimamizi madhubuti wa Mtekelezaji Nambari Wani wa Ilani hizo, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais, wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi.

Mchango wake katika mabadiliko makubwa ya kimaendeleo waliyoyashuhudia Watanzania kwa jumla katika kipindi cha miaka kumi iliyopita unatambuliwa na kila mtu. Mheshimiwa Rais Mkapa anayo kila haki na sababu ya kujivunia mafanikio hayo yaliyomjengea heshima kubwa kitaifa na kimataifa. Zaidi ya yote, anastahili pongezi zetu sote. Pongezi pia zimwendee Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumsaidia vyema Mheshimiwa Rais Mkapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sehemu mbalimbali za hotuba yangu hii, nitatoa shukrani katika mambo mahsusi kwa wastahiki mbalimbali. Hata hivyo, napenda katika hatua hii kutanguliza shukrani maalum za jumla kwa watu waliotoa msukumo maalum uliochangia katika mafanikio ya Wizara yangu. Wa kwanza kabisa katika orodha hiyo fupi ni Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa ambaye hakusita kutoa amri ambazo utekelezaji wake ulitukwamua kila tulipokuwa tumekwama.

Shukrani zangu maalum ziiendee pia Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa John Samwel Malecela, Mbunge wa Mtera. Mimi na wenzangu katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi tumefaidika sana na maoni na maelekezo mbalimbali ya Kamati hiyo ambayo yametusaidia sana katika kuongeza ufanisi wa kazi zetu. Kwa Wajumbe wote wa Kamati hiyo, nasema ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukutambua wewe mwenyewe pamoja na Waheshimiwa, Waziri Mkuu, Waziri wa Fedha na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji katika orodha ya watu wa kushukuriwa maalum kwa ushirikiano wenu ulionisaidia katika utekelezaji wa majukumu yangu. Wengine ni Waheshimiwa Mawaziri na Wabunge wenzangu wote ambao nawaombea baraka za Mwenyezi Mungu warejee tena Bungeni baada ya Uchaguzi Mkuu ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tukielekea Uchaguzi Mkuu wa mwishoni mwa mwaka huu, tunakamilisha enzi itayokumbukwa milele katika historia ya nchi yetu. Enzi hiyo ni ya utawala wa Awamu ya Tatu ya Uongozi wa nchi yetu chini ya Rais Benjamin William Mkapa, toka mwaka 1995 hadi mwaka 2005. Kama nilivyogusia awali, Tanzania imepiga hatua kubwa ya maendeleo katika nyanja zote, katika kipindi hicho. Katika sehemu hii ya hotuba yangu, napenda kutoa kwa muhtasari mafanikio ya uongozi huo katika sekta zilizo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Jukumu la msingi la Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Jeshi la Polisi na Taasisi nyingine za Wizara hii, ni usalama wa raia na mali zao. Katika kipindi cha mwaka 1995 hadi mwaka 2004, uhalifu ulipungua kwa kiwango cha asilimia 20.5 ambapo idadi ya matukio yote yaliyotolewa taarifa katika Vituo vya Polisi ilipungua kutoka 460,578 mwaka 1995 hadi 366,366 mwaka 2004.

Miongoni mwa matukio hayo, yale yenye sura ya ujambazi yalipungua kutoka 9,061 mwaka 1995 hadi 8,693 mwaka 2004, sawa na upungufu wa asilimia 4.1. Makosa hayo yanajumuisha unyang'anyi wa kutumia silaha, unyang'anyi wa kutumia nguvu, wizi wa silaha, kupatikana na silaha na mauaji ya aina zote, kupungua kwa uhalifu katika mazingira ya kuongezeka kwa idadi ya watu kwa wastani wa asilimia 2.9 kwa mwaka si jambo la kawaida; hivyo linastahiki pongezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wizi wa mifugo nao ulipungua kwa asilimia 23.0 ambapo idadi ya matukio ya wizi ilipungua kutoka 5,655 mwaka 1995 hadi 4,354 mwaka 2004. Ajali za barabarani ni uhalifu pekee unaovuta sana hisia za watu ambao dalili za kuudhibiti hazijajitokeza. Idadi ya ajali za barabarani iliongezeka kutoka 13,773 mwaka 1995 hadi 18,031 mwaka 2004, sawa na ongezeko la asilimia 30.9.

Ni jambo la kusikitisha kwamba kadri barabara zetu zinavyokuwa bora ndio ajali nazo zinaongezeka. Kuongezeka sana kwa magari na madereva wazembe kunachangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la ajali za barabarani na hivyo kutoa changamoto kubwa kwa Jeshi la Polisi. Huu ni mfano mzuri wa tatizo la maendeleo, yaani maendeleo ya kuongezeka kwa ubora wa barabara na idadi ya magari yanazaa tatizo la ajali.

Mheshimimiwa Naibu Spika, eneo lingine linalohatarisha usalama wa raia na mali zao ni lile la matukio ya moto. Idadi ya matukio ya moto yaliyoripotiwa nchi nzima upande wa Tanzania Bara ilipungua kutoka 310 mwaka 1995 hadi 269 mwaka 2004 sawa na upungufu wa asilimia 13.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwelekeo wa kuanza kupungua kwa uhalifu ni matunda ya juhudi za makusudi za kuimarisha vyombo vinavyoshughulikia usalama wa raia na mali zao ili kuviongezea ufanisi. Juhudi hizo ambazo zilipewa msukumo binafsi wa Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa, Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, ziliongozwa na Sera ya CCM ya kuwa na Jeshi dogo la usalama wa raia lakini lenye uwezo mkubwa wa kitaaluma na nyenzo za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya utekelezaji wa juhudi hizo ni kama ifuatavyo kwa uchambuzi wa maeneo ya kazi:-

Katika kipindi cha mwaka 1995 hadi 2004, Jeshi la Polisi liliajiri Askari wapya 11,255 ambao waliweza kuboresha uwiano wa Askari na raia kutoka Askari mmoja kwa raia zaidi ya 1,500 mwaka 1995 hadi Askari mmoja kwa raia 1,300 mwaka 2004. Aidha, jumla ya Askari 7,128 walipandishwa vyeo baada ya mafunzo. Ujenzi wa nyumba mpya na ununuzi wa nyumba kutoka baadhi ya Mashirika yaliyobinafsishwa uliliongezea Jeshi la Polisi nyumba za Askari kutoka idadi ya 6,745 mwaka 1995 hadi 7,585 mwaka 2004, likiwa ni ongezeko la nyumba 840 sawa na asilimia 12.5. Idadi ya Vituo vya Polisi iliongezeka kutoka 623 hadi 719 sawa na ongezeko la asilimia 15.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya juhudi hizo za kuimarisha rasilimaliwatu na miundombinu, Jeshi la Polisi pia liliimarishwa kwa upande wa nyenzo za kazi zikiwemo za usafiri. Jitihada za kulifanya Jeshi la Polisi liwe la kisasa zilitafsiriwa kwa vitendo kwa kulipatia mtambo mpya wa mawasiliano na Maabara mpya ya kisasa ya uchunguzi wa vielelezo vya makosa ya jinai.

Mheshimiwa Naibu Spika, yote hayo yaliwezekana kutokana na ongezeko kubwa la Bajeti za Kawaida na Maendeleo za Jeshi la Polisi. Bajeti ya kawaida iliongezeka kutoka Sh.17,303,817,100/= mwaka 1995/1996 hadi Sh. 81,540,491,500/= mwaka 2004/2005, sawa na ongezeko la asilimia 371.2. Bajeti ya Maendeleo nayo iliongezeka kutoka Sh. 891,400,000 mwaka 1995/1996 hadi Sh. 5,300,000,000/= mwaka 2004/2005 sawa na ongezeko la asilimia 494.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka kumi ya Serikali ya Awamu ya Tatu, juhudi kwa upande wa Magereza zilelekezwa katika kuboresha huduma kwa wafungwa kwa kuzingatia haki za binadamu na kusisitiza sera za urekebishaji tabia Magerezani kuliko adhabu za kukomoa. Ingawa matokeo ya juhudi hizo hayajajitafsiri katika kupungua msongamano Magerezani, lakini huduma kama vile za chakula na matibabu, ziliimarishwa kwa kiasi kikubwa.

Aidha, Jeshi la Magereza lilianzisha vazi jipya la heshima kwa wafungwa badala ya kaptura zilizokuwa zinadhalilisha utu wa mfungwa. Pia, Jeshi lilianza kutumia magodoro kwa ajili ya malezi ya wafungwa badala ya virago. Vyoo vya kisasa vilianza kuchukua nafasi ya mitondoo. Zaidi, Magereza yalianza kupatiwa seti za televisheni na redio kwa ajili ya wafungwa kupata habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hicho, mradi wa ujenzi wa Magereza mapya ulifufuliwa ambapo ujenzi uliokuwa umekwama kwa muda mrefu ulikwamuka na mwingine mpya kuanza. Magereza yaliyofaidika na mradi huu wa maendeleo ni Mpwapwa, Kayanga, Muleba, Bunda, Magu, Bariadi, Igunga, Meatu, Kiteto, Makete, Mbarali, Rombo, Ileje, Mbozi, Mbinga, Nachingwea na Segerea. Magereza ya zamani ya Singida, Songwe, King'ang'a, Kibondo na Lushoto yamejengwa upya. Magereza mengine karibu yote yamefanyiwa au yanaendelea kufanyiwa ukarabati mkubwa ikiwa ni pamoja na kupanuliwa, hususan Magereza ya Ngara, Biharamulo, Iringa, Isanga Wanawake, mahabusu Morogoro, Bangwe, Kasulu, Kigongoni na Mugumu. Kwa jumla, uwezo wa kisheria wa Magereza umeongezeka kutoka nafasi 21,188 mwaka 1995 hadi 22,699 mwaka 2004, sawa na ongezeko la asilimia 7.1. Hata hivyo, katika kipindi hicho, idadi halisi ya wafungwa na mahabusu iliongezeka kutoka wastani wa kila mwezi wa 37,917 mwaka 1995 hadi 45,023 mwaka 2004 sawa na ongezeko la asilimia 18.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu hizi zinadhihirisha kuongezeka kwa msongamano Magerezani licha ya jitihada zote hizo za kuongeza nafasi. Sababu ya msingi ya hali hiyo ni wingi wa mahabusu ambao ni karibu nusu ya wote waliomo Magerezani. Sababu hiyo iko nje ya uwezo wa Jeshi la Magereza kwani ucheleweshaji wa kesi Mahakamani unaosababisha mlundikano wa mahabusu, unatokana na utendaji wa Polisi na Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifumo ya maji safi na maji taka iliyokuwa imechakaa kabisa ilifufuliwa kwa kujengwa upya katika Magereza ya Lindi, Bukoba, Singida, Kiomboi, Mahabusu Morogoro, Mtego wa Simba, Wami Vijana, Musoma, Loliondo, Mahabusu Tanga, Korogwe, Urambo, Tabora, Biharamulo, Malya, Ngara, Iringa, Ruanda, Maswa, Shinyanga, Manyoni, Ubena na Kingolwira Wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hicho upatikanaji wa maji safi na salama na ya kutosha uliboreshwa kwa kuchimba visima virefu na mahali pengine kwa kuimarisha vyanzo vya mito. Visima virefu vilichimbwa kwenye maeneo ya Magereza ya Ukonga, Kikosi Maalum Dar es Salaam, Ubena, Segerea, Keko, Same, Kihonda, Kingolwira Wanawake, Mbigiri, Nachingwea, Kibiti na Malya. Vyanzo vya maji vimeimarishwa kwenye Magereza ya Songwe, Matongo, Ilagala, Kitai na Mbarali.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme pia ulipelekwa kwenye maeneo yote yaliyo karibu na mfumo wa Taifa wa umeme kama vile Utete, Geita, Bariadi, Mbulu, Newala, Rombo, Magu, Mpwapwa, Malya, Kwamgumi na Mahenge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwa na mipaka inayotambulika kisheria kwenye maeneo ya Magereza, katika kipindi cha mwaka 1995 – 2004, maeneo ya Magereza yafuatayo yaliingizwa kwenye mpango wa kupimwa ili kupatiwa barua za toleo (*Letter of Offer)*. Magereza hayo ni Songwe, Namajani, Njombe, Makete, Bagamoyo, Rusumo, Arusha, Mkuza, Segerea, Bariadi, Kwitanga, Kiteto, Kihonda, Kambi Mgagao, Butimba, Mtego wa Simba, Kambi Kimbiji, Mbarali, Kalila, Kiabakari, Mang'ola, Urambo, Kilwa, Maweni, Kitengule, Pawaga na Kitai. Upimaji wa maeneo hayo umesaidia sana

kupunguza migogoro ya mipaka na majirani na Magereza husika na pia kuliwezesha Jeshi la Magereza kuwa na mipaka ya maeneo inayotambulika kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa kuimarisha dhana ya urekebishaji wa wafungwa na kupunguza msisitizo juu ya kukiona kifungo Gerezani kuwa ni adhabu ya kukomoa, Jeshi la Magereza katika kipindi cha 1995 - 2004 lilifufua miradi mingi ya uzalishaji mali Magerezani ambayo ilisita kwa muda mrefu. Miradi hiyo hutumika pia kuwapatia wafungwa mafunzo ya amali mbalimbali zinazotarajiwa kuwasaidia katika kuendesha maisha yao warudipo uraiani baada ya kumaliza vifungo vyao.

Katika juhudi hizo, Kiwanda cha Uhunzi cha Ukonga kimefufuliwa, Chuo cha Ufundi cha Mbeya kiliimarishwa na jumla ya vyerehani 66 vimenunuliwa. Katika kufufua mashamba ya kilimo na ufugaji ya Magereza, zilinunuliwa zana, nyenzo na pembejeo mbalimbali kama vile matrekta, malori, mashine za kukamulia mawese (kwa ajili ya shamba la michikichi la Gereza la Kwitanga, Kigoma), madume na mitambo, dawa za mifugo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine, mwelekeo wa kuongeza matumizi ya adhabu mbadala wa kifungo Gerezani ulipewa msukumo katika kipindi hiki. Sheria ya *Parole* ilifanyiwa marekebisho mara mbili katika kipindi cha mwaka 1995 – 2004 ili kupanua wigo wa wafungwa watakaoweza kufaidika nayo. Aidha, Sheria ya Huduma kwa Jamii itakayowezesha wahalifu watakaotiwa hatiani kwa baadhi ya makosa kutumikia adhabu zao za kifungo wakiihudumia jamii nje ya Gereza ilipitishwa na imeanza kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha mazingira ya kazi za Askari, Jeshi la Magereza lilipatiwa vitendea kazi mbalimbali yakiwemo magari, vifaa vya mawasiliano na kadhalika. Jeshi lilipatiwa nyumba mpya 176, nusu yake zikiwa lilizojenga lenyewe na nusu iliyobaki zilinunuliwa kutoka baadhi ya Mashirika ya Umma yaliyobinafsishwa. Pia, lilipatiwa jengo kubwa kwa ajili ya Makao Makuu yake ambalo lilinunuliwa kutoka Kampuni ya Simu 2000.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujiimarisha kirasilimaliwatu, Jeshi la Magereza liliajiri Askari wapya 4,036 katika kipindi cha 1995 hadi 2004. Askari 5,229 walipatiwa mafunzo ndani ya nchi na 491 nje ya nchi. Askari 8,535 walipandishwa vyeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio yote hayo ya Jeshi la Magereza yaliwezekana kutokana na ongezeko kubwa la kibajeti. Bajeti ya Kawaida ya Jeshi la Magereza iliongezeka kutoka Sh. 10,849,429,100/= mwaka 1995/1996 hadi Sh.39,588,514,300/= mwaka 2004/2005 sawa na ongezeko la asilimia 265. Bajeti ya maendeleo nayo iliongezeka kutoka Sh.432,900,000/= hadi Sh. 2,900,000,000/= sawa na ongezeko la asilimia 570 katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka 10 iliyopita Idara ya Uhamiaji iliajiri Maafisa Uhamiaji wapya 647, Vituo vipya vinane vya Uhamiaji vilianzishwa, paliongezwa nyumba 123 za watumishi na Ofisi nne. Yalinunuliwa magari mapya 61, kompyuta mpya 69, pikipiki mpya 31 na redio 26 mpya za mawasiliano. Hivi

karibuni ilifungwa mitambo mipya ya kuandikia *pass* zinazosomeka kwa kompyuta. Mitambo hiyo ipo Dar es Salaan na Zanzibar. Bajeti ya kawaida ya Idara ya Uhamiaji iliboreshwa kwa asilimia zaidi ya 1,100 kutoka Sh. 610,663,900/= mwaka 1995/1996 hadi Sh. 7,342,031,600/= mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Serikali ya Awamu ya Tatu inaingia madarakani, nchi yetu ilikuwa inahifadhi Wakimbizi wapatao 700,000 toka Rwanda katika Mkoa wa Kagera ambao waliingia nchini baada ya kuzuka vita na mauaji ya Kimbari nchini humo mwaka 1994. Wakati huo huo tayari tulikuwa tunahifadhi Wakimbizi wapatao 300,000 kutoka Burundi, Somalia na *DRC*. Wakimbizi hao wa Rwanda walirejeshwa makwao mwaka 1996/1997 na kuwezeshwa kufungwa kwa Makambi ya Benaco, Msuhura, Lumasi, Kitali, Mulonzi, Keza, Kyabalisa, Kagenyi, Rubwera, Mulongo, Omukarilo na Burigi yaliyokuwapo Mkoani Kagera na kupunguza kwa kiasi kikubwa kero kwa wakati wa Mkoa huo ambao walikuwa wameelemewa na mzigo wa Wakimbizi kutoka Rwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hicho, Bajeti ya Idara ya Huduma za Wakimbizi iliongezeka kwa asilimia 317.9 kutoka Sh.86,915,400/= mwaka 1995/1996 hadi Sh.363,194,400/= mwaka 2004/2005. Kuongezeka kwa Bajeti hiyo kumewezesha pamoja na mambo mengine kununuliwa kwa magari mapya kwa ajili ya kuboresha uendeshaji wa Makazi ya Katuba, Mishamo na Ulyankulu ambayo yamekabidhiwa Serikali na pia kuanza ukarabati wa majengo katika Makazi hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tatu, iliwezekana kununuliwa kwa magari 16 mapya ya kuzimia moto kwa ajili ya Halmashauri 15 za Miji na Manispaa, likiwemo gari la ngazi ndefu la kuzimia moto katika maghorofa marefu. Gari hilo ni la kwanza la aina yake nchini. Aidha, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limetoa ushauri mbalimbali zikiwemo za majengo, viwanda, matanki na Vituo vya Mafuta. Pia, ukaguzi umefanyika kwa magari ya aina zote na mitambo. Kwa ujumla Jeshi hilo limeimarisha huduma zake za ushauri na ukaguzi wa tahadhari za moto.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuelezea mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tatu, sasa narudi katika utekelezaji wa shabaha na malengo yaliyopangwa kwa kipindi cha Bajeti ya mwaka wa fedha wa 2004/05. Napenda nianze na hali ya usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imeendeleza kuwa na amani na utulivu katika kipindi cha mwaka wa fedha uliopita wa 2004/2005 licha ya matukio machache yaliyotaka kuhatarisha amani. Wote tumesikia au kusoma kwenye Vyombo vya Habari juu ya matukio ya wizi kwenye Benki za *STANBIC* tarehe 29 Desemba 2004 Jijini Dar es Salaam na *NBC* kule Moshi tarehe 21 Mei, 2004. Kesi kwa matukio yote hayo ziko Mahakamani ingawa ile ya *NBC*, Moshi imekumbwa na tatizo la Mahakama za Kenya na Uganda kuwaachia huru watuhumiwa muhimu. Rufaa zimekatwa kupinga uamuzi wa Mahakama huko Kenya na Uganda. Lakini kesi hapa nchini imebidi ianze kusikilizwa kwa kutumia watuhumiwa waliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwepo pia migogoro ya kidini ndani ya KKKT na baina ya BAKWATA na Waislam wa Msikiti wa Mtoro. Migogoro yote hiyo sasa imekwisha. Matukio mengine yaliyotaka kuhatarisha amani yalitokana na jazba za kisiasa wakati wa uandikishaji katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Unguja na Pemba na wakati wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Jijini Dar es Salaam. Jumla ya watu wanne walipoteza maisha katika rabsha hizo za Zanzibar na Dar es Salaam. Jeshi la Polisi lilisimama kidete katika kudhibiti hali na hivyo kuepusha madhara makubwa zaidi. Napenda kutoa wito kwa wanasiasa kuzingatia umuhimu wa kudumisha amani wakati wakifanya shughuli zao za kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu za mwaka 2004 kwa makosa yote ya kila aina ya uhalifu zinaonyesha kwamba matukio yaliyoripotiwa katika Vituo vya Polisi nchi nzima yalikuwa 366,366. Huu ni upungufu wa asilimia 618,753 yaliyoripotiwa mwaka 2003. Matukio ya uhalifu mkubwa wa jinai yalikuwa 61,376 yakiwa ni pungufu kwa asilimia 19.6 yakilinganishwa na matukio 76,357 ya mwaka 2003. Ajali za barabarani zilikuwa 18,031 ambazo ni nyingi zaidi kwa asilimia 2.4 zikilinganishwa na ajali 17,615 zilizotokea mwaka 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matukio yote makubwa na madogo ya uhalifu yaliyoripotiwa Polisi yalipungua kutoka 510,875 mwaka 2000 hadi 366,366 mwaka 2004 ukiwa ni upungufu wa asilimia 28.3. Matukio ya uhalifu mkubwa wa jinai yalipungua kutoka 86,226 mwaka 2000 hadi 79,619 mwaka 2004 sawa na upungufu wa asilimia 7.7. Hata hivyo, matukio ya unyang'anyi wa kutumia silaha yaliongezeka kwa asilimia 20.3 kutoka matukio 977 mwaka 2000 hadi 1,175 mwaka 2004. Mauaji yaliongezeka kutoka matukio 2,464 mwaka 2000 hadi 2,926 mwaka 2004 sawa na ongezeko la asilimia 18.8.

Ajali za barabarani zilizosababisha vifo na/au majeruhi ziliongezeka kutoka 15,577 mwaka 2000 hadi 18,031 mwaka 2004 sawa na ongezeko la asilimia 15.8. Kwa jumla, mwelekeo unaojitokeza kwa uhakika ni ule wa kupungua sana kwa uhalifu mdogo mdogo, ambapo uhalifu mkubwa ulikuwa ukipanda na kupungua katika kipindi cha miaka mitano cha 2000 – 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuelezea hali ya usalama sasa napenda niingie katika tathmini ya kibajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa mafungu yote manne; yaani Fungu 28 - Polisi, Fungu 29 - Magereza, Fungu 51 - Utawala na Fungu 93 - Uhamiaji, kwa pamoja ilipangiwa kukusanya mapato ya Serikali ya Jumla ya Sh.16,686,040,00/=. Hadi kufikia Aprili, 2005 zilikuwa zimekusanywa jumla ya Sh.12,912,822,191/= sawa na asilimia 77 ya lengo la mwaka mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mafungu yote manne iliidhinishiwa jumla ya Sh. 139, 695,127,500/= kwa matumizi yote ya kawaida na ya maendeleo. Hadi kufikia Aprili, 2005 jumla ya Sh. 110,944,137,905/= zilikuwa zimetumika sawa na asilimia 79 ya lengo la mwaka mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda kutoa tathmini ya shughuli zilizotekelezwa kwa kutumia bajeti ya mwaka uliopita wa 2004/2005 fungu kwa fungu na matarajio kwa kipindi kijacho cha 2005/2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu kubwa ya utekelezaji wa shughuli za Jeshi la Polisi zilielekezwa katika kukabiliana na uhalifu. Miongoni mwa hatua mbalimbali zilizochukuliwa ni pamoja na kuendesha doria za Mitaani na operesheni mbalimbali Mikoani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama inavyofahamika, uhalifu mwingine ni wa Kimataifa. Kwa hivyo, Jeshi la Polisi linaendelea kushirikiana na Majeshi ya Polisi ya nchi jirani na Shirika la Polisi Duniani (*Interpol*) katika kupeana taarifa mbalimbali za uhalifu na kuendesha misako ya pamoja. Mfano wa misako hiyo ni operesheni ya nchi za *SADC* iliyofanyika mwezi Agosti, 2004 kwa madhumuni ya kukamatwa silaha zisizo halali na ile ya mwezi Septemba, 2004 ambayo ilijumuisha nchi za Tanzania, Malawi na Zambia katika operesheni ya kushughulikia makosa ya wizi wa magari, dawa za kulevya, usafirishaji haramu wa silaha na uhamiaji haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na tatizo la silaha ndogondogo katika mwaka 2004, Tanzania ilichoma moto jumla ya silaha 2000 katika maadhimisho ya siku ya silaha ya Umoja wa Mataifa na Siku ya Polisi. Katika hatua nyingine, Serikali imeliwezesha Jeshi la Polisi kuwa na mitambo ya kisasa ya mawasiliano pamoja na Maabara ya kisasa ya uchunguzi wa vielelezo vya upelelezi vinavyohusiana na uhalifu kama vile alama za vidole, nyaraka mbalimbali, bunduki, risasi na milipuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kupambana na rushwa ndani ya Jeshi la Polisi, Semina kadhaa zimefanyika kwa Wapelelezi na Waendesha Mashtaka wa Wilaya ya Kikanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na fedha za Miradi ya Maendeleo, Jeshi la Polisi limeweza kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kukamilisha ujenzi wa nyumba 139 (Kunduchi 92, Dodoma 32, Same 12 na Babati 3);

(b) Kuendeleza ujenzi wa nyumba 68 (Kunduchi 32,Mwanga 16, Katesh 20);

(c) Kukamilisha ujenzi wa Vituo vya Polisi vya Kyela na Kasulu;

(d) Kukamilisha ujenzi wa Ofisi ya Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Iringa na kuendeleza ujenzi wa majengo ya Ofisi za Makamanda wa Polisi wa Mikoa ya Tabora, Mwanza na Ruvuma;

(e) Kuendeleza ujenzi wa Kambi ya *FFU* Finya, Pemba;

(f) Kukarabati Miundombinu ya Chuo cha Polisi Moshi;

(g) Ukarabati na ujenzi wa mabweni ya Chuo cha Polisi Zanzibar;

(h) Taratibu za kumpata Mkandarasi wa kukarabati mashua saba za doria katika maziwa Victoria, Nyasa na Tanganyika zimeshaanza kufanyika;

(i) Kuweka umeme nyumba za Askari Polisi Ziwani, Zanzibar;

(j) Kukarabati jengo la Ofisi ya *RPC* wa Manyara. Jengo hilo sasa linakidhi mahitaji ya Ofisi ya *RPC;*

(k) Maandalizi ya Ujenzi wa Vituo vya Polisi vya Wilaya za Namtumbo na Mpanda yanaendelea. Hivi sasa Bodi za Zabuni za Mikoa husika zinaendelea kushughulikia upatikanaji wa Mkandarasi wa kujenga majengo hayo;

(l) Maandalizi ya awali ya kuanzisha utaratibu wa Polisi Jamii yanaendelea, ambapo Polisi Jamii inatarajiwa kuanza rasmi mwaka ujao wa fedha wa 2005/2006;

(m) Kuanza ujenzi wa Vituo vya Polisi vya Wilaya ya Morogoro na Hanang;

(n) Kukamilisha jengo la upasuaji katika Hospitali Kuu ya Polisi (*Kilwa Road* Dar es Salaam);

(o) Ununuzi wa magari 215 ya Wakuu wa Polisi wa Wilaya na Wakuu wa Upelelezi wa Wilaya pamoja na *FFU*;

(p) Ununuzi wa redio 143 za mawasiliano za aina mbalimbali; na

(q) Kuunga mkono ujenzi wa Vituo vya Polisi vinavyojengwa kwa nguvu za wananchi. Vituo vifuatavyo vilifaidika na utaratibu huo katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2004/2005: Natron, Siha, Mchinga, Ikola, Ipinda, Kisangara, Ugweno, Msangeni, Lang'ata Bora, Namtumbo, Biharamulo, Polisi *Welfare Building* (Biharamulo), Kasumulu, Kyela, Makongolosi, Vianzi Pwani, Boko, Mabatini, Nyakato na Makongolosi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Jeshi la Polisi linatarajia kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na Miradi ya Maendeleo ifuatayo:-

(a) Kukamilisha ujenzi wa nyumba za Askari Kunduchi;

(b) Kukamilisha ujenzi wa majengo ya Ofisi ya Makamanda wa Polisi wa Mikoa ya Tabora, Mwanza na Ruvuma;

(c) Kukamilisha ujenzi wa Vituo vya Polisi vya Morogoro na Hanang;

(d) Kukamilisha ujenzi wa nyumba za *FFU* Finya – Zanzibar;

(e) Ununuzi na ukarabati wa mashua za doria;

(f) Kukamilisha ukarabati wa nyumba za Askari za Tunguu (Unguja) na Chuo cha Polisi Zanzibar;

(g) Kukarabati mabweni ya wanafunzi CCP Moshi na Chuo cha Polisi Dar es Salaam;

(h) Kuanza ujenzi wa Chuo cha *CID* Dodoma;

(i) Kuanza kujenga vyumba vya mahabusu kwa ajili ya watoto, wanawake na walemavu, kwa kuanzia vitajengwa Mkoa wa Dar es Salaam;

(j) Kuimarisha mawasiliano katika Jeshi la Polisi;

(k) Kuendesha mafunzo ya Askari wapya na mafunzo kazini;

(l) Kuendesha operesheni za kupambana na uhalifu wa dawa za kulevya, ugaidi na wizi wa magari;

(m) Kuendeleza vita dhidi ya rushwa na UKIMWI ndani ya Jeshi la Polisi; na

(n) Kuunga mkono juhudi za wananchi za kujenga Vituo vya Polisi na nyumba za Askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Magereza yetu nchini yameendelea kuhifadhi wafungwa na mahabusu zaidi ya uwezo wake kisheria. Magereza yote nchini yana uwezo kisheria wa kuhifadhi wahalifu 22,699 tu. Tarehe 1 Aprili, 2005 kulikuwa na wafungwa 23,968 na mahabusu 21,017 na kufanya jumla ya 44,985. Tarehe kama hiyo mwaka 2004 tulikuwa na wafungwa na mahabusu 46,965. Kwa hiyo, kumekuwa na upungufu wa asilimia 4.4. Lakini hata hivyo, msongamano bado ni mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, hatua mbalimbali za kiutawala na kibajeti zilichukuliwa zenye lengo la kupunguza msongamano wa wafungwa na mahabusu Magerezani kama ifuatavyo:-

Kufuatia Bunge lako Tukufu kurekebisha Sheria ya Bodi za *Parole* kwa lengo la kupanua wigo wa wafungwa wataofaidika, katika kipindi cha Julai, 2004 hadi Juni, 2005 wafungwa 622 waliachiliwa kwa utaratibu wa *Parole.*

Katika hatua nyingine ya Serikali, jumla ya wafungwa 6,130 waliachiliwa huru kwa msamaha uliotolewa na Mheshimiwa Rais katika kelele cha sherehe za miaka 43 ya Uhuru wa Jamhuri wa Tanganyika na Zanzibar tarehe 26 Aprili, 2005.

Aidha, hadi Aprili, 2005 wafungwa wapatao 561 walikuwa wameachiliwa na kupewa vifungo vya nje kwa kutumia Sheria ya *Extra Mural Labour* ya mwaka 1967.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2004/2005, Jeshi la Magereza pia lilitekeleza miradi ya maendeleo ikiwemo ifuatavyo:-

(a) Kuendeleza ukarabati wa jengo litakalokuwa Makao Makuu ya Magereza;

(b) Kuendeleza ukarabati wa Magereza yenye ulinzi mkali ya Butimba, Maweni, Ukonga, Keko na Gereza Maalum Isanga;

(c) Kuendeleza ujenzi wa mabweni ya wafungwa katika Magereza ya Segerea, Iringa Mjini, Muleba, Kayanga, Rombo, Bunda, Bangwe, Biharamulo, Musoma, Mugumu, Songwe, Liwale, Mtego wa Simba, Same, Ubena, Kitai, Lindi, Bariadi, Singida, Makete, Mpwapwa, Nachingwea, Meatu, Tabora, Mng'aro na Kigongoni;

(d) Kuendeleza ujenzi wa Magereza ya mahabusu ya Wilaya ya Mbarali, Igunga na Mbinga;

(e) Kukamilisha ujenzi wa nyumba na kuendeleza ukarabati wa nyumba za Askari katika vituo vya Chuo Ukonga, Chuo Ruanda, Chuo Kiwira, Rombo, Kibondo, Kayanga, Ileje, Muleba, Mbozi, Mbarali, Mpwapwa, Loliondo, Mwanga, Utete, Mugumu, Bunda, Magu, Bangwe, Mkuza, Kiteto, Makete, Mang'ola, King'ang'a, Kambi ya Mgagao, Kambi ya Kimbiji, Wami Vijana na Kingolwira Wanawake. Aidha, nyumba 30 zimenunuliwa kutoka Kampuni ya Ngozi Tanzania eneo la Kihonda, Morogoro;

(f) Uimarishaji wa mfumo wa maji safi umefanyika katika magereza ya Kihonda, Kibiti, Same, Arusha, Kimbji, Urambo, Kitai, Mugumu na Nachingwea na ukarabati wa mfumo wa maji taka umefanyika katika Magereza ya Bukoba, Mtego wa Simba, Pangani, Lindi, Iringa, Kilwa Masoko, Mahabusu Tanga na Mahabusu Musoma;

(g) Fidia imelipwa katika magereza ya Segerea, Kiteto, Rusumo, Kihonda, Kiberege, Butimba, Kibiti, Mbarali na Kambi ya Mgagao;

(h) Maeneo ya Magereza yaliyopimwa ni Mng'aro, Arusha, Kitengule, Kwitanga na Kalilankulunkulu;

(i) Maandalizi ya ununuzi wa magari 34; na

(j) Ununuzi wa mitambo bora 71 na madume bora 50 kwa ajili ya mashamba ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2005/2006, Jeshi la Magereza litaendelea kuboresha huduma zake na kutekeleza miradi ifuatayo ya maendeleo:-

(a) Kukamilisha ukarabati wa jengo litakalokuwa Ofisi ya Makao Makuu ya Magereza;

(b) Kuendelea na ukarabati wa Magereza yenye ulinzi mkali ya Butimba, Maweni, Ukonga na Keko;

(c) Kuendelea kuikamilisha viporo vya nyumba 28 za Askari na mabweni 20 ya wafungwa;

(d) Kuendelea na ujenzi wa Magereza ya mahabusu ya Wilaya za Mbarali, Igunga na Mbinga;

(e) Kuendelea kuimarisha mifumo ya maji safi na maji taka Magerezani katika Vituo 14;

(f) Kuendelea na upimaji wa maeneo ya Magereza sita na ulipaji wa fidia;

(g) Kuimarisha miradi 41 ya kilimo na mifugo na miradi 6 ya viwanda vidogo vidogo;

(h) Kununua magari 49 na pikipiki 14;

(i) Kuimarisha Shirika la Magereza ili Jeshi la Magereza lianze kujitegemea; na

(j) Kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa na janga la UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2004/2005, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeendelea na majukumu yake ya msingi ya kuzimamoto, kuokoa maisha na mali kwenye majanga ya moto na majanga mengine. Utekelezaji huo ulifanywa kwa

ufanisi na Vikosi vya Zimamoto na Uokoaji vya Serikali na vile vya Makampuni binafsi na Umma kwa jumla.

Zoezi la ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto lilifanyika kwenye maeneo mbalimbali kama ifuatavyo:- Malori ya mizigo 40,000, malori ya mafuta 15,000, magari ya abiria 10,000, magari madogo 6,000, maduka 531, Vituo vya Mafuta 291, viwanda 108, Shule 100, hoteli 60, gereji 50, maduka ya dawa 37, *fuel farm tanks* 36, Benki 15, maghala 10, masoko makubwa 25 na Wizara 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya Askari wa Zimamoto na Uokoaji na mafunzo ya tahadhari na kinga ya moto kwa umma nayo yalitolewa. Jumla ya Askari na raia 3,056 walipatiwa mafunzo kwa uchambuzi ufuatao:- mafunzo ya awali kwa Askari 13, mafunzo ya msingi kwa Askari 43 na mafunzo mahali pa kazi kwa watumishi 3,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali ni kuona kuwa kila Halmashauri ya Mji, Manispaa na Jiji inakuwa na huduma za Zimamoto na Uokoaji kwa ajili ya usalama wa watu na mali zao. Ili kuwezesha Halmashauri zetu kuwa na magari ya kuzimia moto, katika mwaka wa fedha 2004/2005, Halmashauri tisa za Wilaya, yaani za Tanga, Kigoma, Mtwara, Mbeya, Iringa, Tabora, Sumbawanga, Musoma na Songea zilipatiwa fedha kwa ajili ya kununulia magari ya kuzimia moto. Utaratibu wa zabuni umekamilika na matarajio ni magari hayo kuwasili na hivyo kuongeza ufanisi wa Vikosi vya Zimamoto katika kupambana na majanga ya moto katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002 inampa Mamlaka Kamishna wa Zimamoto na Uokoaji kuwa "Kamanda Mkuu" wa shughuli/Vikosi vya Zimamoto na uokoaji nchini. Ili kutekeleza sheria hiyo, Tume ya Utumishi wa Umma kwa kushirikiana na maafisa kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Ofisi ya Kamishna wa Zimamoto na Uokoaji wametembelea vikosi vyote vya zimamoto nchini ili kupata takwimu halisi za mahitaji ya wazimamoto, mafunzo, Ofisi vitendea kazi na masuala ya kiutumishi.

Zoezi hilo limebaini mapungufu yaliyopo na kuweka mikakati ya kuyaondoa. Lengo ni kuunganisha shughuli za zimamoto na uokoaji nchini chini ya utawala mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2004/2005 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeajiri jumla ya Askari 51 kama ifuatavyo:- Kidato cha sita 12, Kidato cha Nne 34 na elimu ya Chuo Kikuu watano.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2005/2006, ni matarajio ya Wizara yangu kuona kuwa Sera ya Taifa ya Moto inakamilika na kuanza kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006, Hazina imetenga Sh.2,555,000,000/= sawa na Sh.365,000,000/= kwa kila moja ya Halmashauri za Lindi, Dodoma, Moshi, Singida, Morogoro, Kibaha na Bukoba kwa ajili ya ununuzi wa magari ya zimamoto.

Aidha, mwaka 2005/2006 Wizara yangu itaendelea kutoa mafunzo kwa Askari wa zimamoto, kwa watumishi wa Serikali katika viwanda na Mashirika mbalimbali ya Umma na binafsi juu ya tahadhari na kinga za moto. Aidha, zoezi la ukaguzi wa tahadhari na kinga za moto kwenye maeneo mbalimbali litaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005 Idara ya Kuhudumia Wakimbizi imeendelea kuwahudumia maelfu ya Wakimbizi. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2005 nchi yetu ilikuwa na jumla ya Wakimbizi 599,873. Wakimbizi hao wanaotoka nchi za Burundi Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo na Somalia. Vile vile wapo Wakimbizi wachache toka Rwanda, Kenya, Uganda na Sudan. Wakimbizi hao wako katika makazi ya makambi yaliyopo katika Mikoa ya Kagera, Kigoma Rukwa na Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, msimamo wetu ni kwamba suluhisho la kudumu la tatizo la Wakimbizi ni kwa Wakimbizi hao kurudi kwenye nchi zao za asili pindi hali ya amani na usalama itakaporejea. Nchi yetu imekuwa ikitekeleza zoezi la kuwarejesha makwao Wakimbizi wa Burundi tangu mapema mwaka 2002. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2005 jumla ya Wakimbizi 182,952 wa Burundi toka kwenye makambi yaliyopo katika Mikoa ya Kigoma na Kagera wamesharejea nchini kwao. Ni matarajio yetu kuwa kazi ya zoezi hilo itaongezeka hasa baada ya kufanyika uchaguzi nchini humo na Serikali ya Burundi itakuwa tayari kuwapokea raia wake wote wanaoishi nchini mwetu hivi sasa kama Wakimbizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo na Shirika la *UNHCR* imefufua upya zoezi la kuwarejesha makwao Wakimbizi kutoka Kongo, zoezi lililositishwa mwaka 1998 baada ya kuzuka upya kwa mapigano nchini humo. Ni matarajio yetu kuwa hali ya amani na utulivu katika Jimbo la Kivu Kusini wanakotoka Wakimbizi wengi walioko nchini itaendelea kuboreka na hivyo kuwezesha Wakimbizi wote kutoka Kongo kurejea makwao katika mwaka wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 5 hadi 6 Aprili, 2005 Serikali kwa kushirikiana na *UNHCR* iliandalia Mkutano wa kimataifa kujadili hifadhi ya Wakimbizi hapa nchini na namna ya kukabiliana na athari zinazosababishwa na Wahisani, Mashirika ya Umoja wa Mataifa na Wadau wengine. Kutokana na Mkutano huo na kwa kushirikiana na Wahisani kupitia *UNHCR*, tathmini itafanywa kuona ni maeneo gani yaanze kupewa kipaumbele kwa misaada.

Mheshimiwa Naibu Spika, matarajio 2005/2006, katika jitihada za kukabiliana na athari za Wakimbizi, Serikali ya Denmark imesaidia miradi yenye thamani ya Shilingi bilioni tisa katika Mkoa wa Kigoma na Wilaya ya Ngara Mkoani Kagera. Miradi iliyolengwa ni mafunzo ya ufundi stadi, maji, kilimo, hifadhi ya mazingira, ardhi, misitu, na maliasili. Miradi hiyo ilianza kutekelezwa Januari, 2004 na ni ya muda wa kati ya miaka miwili mpaka mitatu. Serikali ya Denmark pia imeonyesha nia ya kusaidia zaidi miradi hii baada ya kuonyesha mafanikio.

Aidha, Serikali imetenga fedha katika mwaka wa 2005/2006 kwa ajili ya ukarabati wa majengo katika makazi ya Wakimbizi ya Katumba, Mishamo na Ulyankulu ambayo yamechakaa kutokana na kutofanyiwa ukarabati tangu makazi hayo yalipokabidhiwa kwa Serikali miaka ya sabini na themanini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilianzisha Sheria ya Huduma kwa Jamii mwaka 2002 kwa lengo la kuimarisha dhana ya adhabu mbadala na kusaidia kupunguza msongamano wa wafungwa Magerezani. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Sheria hiyo itaanza kutumika mwaka 2005/2006 katika Mikoa sita ya majaribio ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mwanza, Dodoma, Mbeya na Mtwara. Utawala wa Mahakama tayari umekwishawaagiza Majaji na Mahakimu waanze kuitumikia Sheria hiyo kwa kutoa hukumu za kuitumikia jamii badala ya kifungo Gerezani kwa wahalifu watakostahili adhabu hiyo mbadala kwa mujibu wa Sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2004/2005 Idara ya Uhamiaji iliendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kudhibiti uingiaji, utokaji na ukaaji wa wageni na raia hapa nchini. Katika Kipindi cha mwaka 2004, Idara ya Uhamiaji iliwahudumia jumla ya wageni 582,807 ikilinganishwa na wageni 480,937 walitoka nchini mwaka 2004 ikilinganishwa na wageni 385,266 waliotoka mwaka 2003. Idara ya Uhamiaji pia iliendelea kutoa vibali vya kuishi nchini kwa wageni waliostahili. Mwaka 2004 wageni 6,291 walipewa vibali vya kuishi nchini ikilinganishwa na wageni 7,534 waliopewa vibali hivyo mwaka 2003. Aidha, vibali 1,605 viliongezwa muda ikilinganishwa na hati 8,291 zilizoongezewa muda mwaka 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Uhamiaji iliendesha misako na doria mbalimbali. Zoezi hilo kwa kipindi cha mwaka 2004 lilifanikisha kukamatwa kwa wageni 3,088 waliokuwa wakiishi nchini kinyume cha sheria na kuchukuliwa hatua za kisheria ikilinganishwa na wageni 3,569 waliokamatwa mwaka 2003. Katika hatua nyingine vijana watoro 161 wa Kitanzania walirudishwa nchini toka nchi mbalimbali na kuchukuliwa hatua za kisheria ikilinganishwa na vijana 760 waliorudishwa nchini mwaka 2003. Kwa upande wa uraia, mwaka 2004 wageni 474 walipatiwa uraia wa Tanzania ikilinganishwa na wageni 129 waliopatiwa uraia mwaka 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza malengo ya mwaka wa fedha wa 2004/2005, ujenzi wa Kituo cha Tunguu umekamilika, ujenzi wa Kituo cha Uhamiaji mpakani mwa Tanzania na Msumbiji eneo la Kilambo upo katika hatua za mwisho, ukarabati wa Ofisi ya Uhamiaji Kigoma umenza na ukarabati wa majengo ya Ofisi na nyumba za kuishi watumishi umefanyika katika Vituo vya *KIA*, Namanga na Sirari. Ujenzi wa Kituo cha Tunduma umeshaanza na unafanywa na Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekaji wa mtandao wa kompyuta (*Local area network*) kwa ushirikiano na *UNDP* yako katika hatua za awali kwa Makao Makuu ya Uhamiaji Dar es Salaam, Ofisi ya Zanzibar, Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha na Kilimanjaro, viwanja vya ndege vya *DIA, ZIA, KIA* na Vituo vya Namanga na Mwanakwerekwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utoaji wa *passport* mpya zinazosomeka kwa kompyuta umeanza tarehe 23 Machi, 2005. Kutokana na gharama kubwa, mitambo hiyo imefungwa Dar es Salaam na Zanzibar tu. Aidha, kwa waombaji wa *passport* walioko Mikoani wanatakiwa kuwasilisha maombi yao katika Ofisi za Uhamiaji zilizopo katika Mikoa yao ambapo Ofisi hizo zitayapeleka maombi hayo Makao Makuu ya Uhamiaji Dar es Salaam au Zanzibar ili yaweze kushughulikiwa na waombaji watazipata pasipoti hizo katika Ofisi hizo za Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Idara imepata kibali cha kuajiri Maofisa Uhamiaji wapya 370 na watumishi waliopo kazini wanaendelea kupata mafunzo mbalimbali ili kuongeza ujuzi walionao. Kwa upande wa vitendea kazi, Idara ya Uhamiaji imenunua magari nane, pikipiki sita na boti moja.

Kuhusu vitambulisho vya Kitaifa, Serikali ipo katika mchakato rasmi wa kufanya upembuzi yakinifu ili kujua gharama halisi za mradi mzima na njia rahisi ya kutoa vitambulisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2005/2006, Idara ya Uhamiaji inatarajia kutekeleza malengo yafuatayo:

(a) Kukarabati Vituo vya Manyovu, Mabamba, Sirari, Dar es Salaam (Mtoni Kijichi), *Ex-NBC* Kilimanjaro na kuendelea kukarabati Ofisi ya Uhamiaji Kigoma; *(Makofi)*

(b) Kuendelea na uwekaji wa mtandao wa kompyuta katika Vituo mbalimbali na Ofisi za Mikoa; *(Makofi)*

(c) Kuanza ujenzi wa Ofisi za uhamiaji Mikoa ya Manyara na Dar es Salaam na Kituo cha Kagunga, Mkoani Kigoma;

(d) Serikali imetenga Shilingi bilioni 2.3 ka ajili ya matayarisho ya awali ya utoaji wa Vitambulisho vya Kitaifa kwa ujenzi wa Ofisi, Elimu kwa Umma, vitendea kazi na matayarisho ya zabuni mara upembuzi yakinifu utakapomalizika;

(e) Kuajiri Maofisa uhamiaji 322 wapya na kuwapeleka watumishi 137 kwenye kozi mbalimbali za muda mrefu na muda mfupi;

(f) Ununuzi wa magari 30, pikipiki 30 boti mbili, jenereta 10 na kompyuta 28;

(g) Kuendelea kulipia majengo ya Ofisi na makazi ya watumishi yaliyonunuliwa toka *CRDB*;

(h) Kuendesha misako na doria ili kuhakikisha kuwa wageni wote waliopo nchini wanaishi kihalali na wanaendesha shughuli zao chini ya udhibiti wa Sheria Uhamiaji Na.7 ya mwaka 1995 na kanuni zake za mwaka 1997;

(i) Kuanza zoezi la kutoa *Visa Stikers;* na

(j) Kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa najanga la UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kutoa shukrani zangu kwa wafanyakazi wa Wizara yangu wakiongozwa na Katibu Mkuu Bwana Bakari A. Mahiza akisaidiwa na Wakuu wa Idara na wa Majeshi yaliyo chini ya Wizara hii. Kwa ushirikiano wao thabiti wamewezesha bajeti ya Wizara kuandaliwa na hatimaye kusomwa leo hii.

Shukrani za pekee nazitoa kwa Naibu Waziri wangu Mheshimiwa *Capt*. Mstaafu John Chiligati, Mbunge wa Manyoni Mashariki, ambaye kila mara amekuwa hachoki kufuatilia utekelezaji na kunipa ushauri na ushirikiano wenye manufaa kwa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa Wahisani wote ambao misaada yao imeiongezea nguvu Wizara yangu katika kutekeleza baadhi ya majukumu yake. Wahisani hao ni pamoja na nchi za China, Marekani, Japan, Afrika Kusini, Uholanzi, Canada, Denmark na Uingereza.

Napenda pia niyashukuru Mashirika ya Kimataifa ya *UNHCR, INTERPOL, SAFER AFRICA, IOM, WFP, UNDP, EU* pamoja na wote ambao kwa njia moja au nyingine wanaendelea kuisaidia Wizara ya Mambo ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi jumla ya Sh.172,641,816,200/= kwa mwaka wa 2005/2006. Kati ya fedha hizo, Sh.162,986,316,200/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambayo mgawanyo wake ni kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| Fungu 18: | Polisi: | Sh.96,761,080,300/= |
| Fungu 29: | Magereza: | Sh.50,227,707,800/= |
| Fungu 51: | Utawala: | Sh. 4,270,229,300/= |
| Fungu 93: | Uhamiaji: | Sh.11,727,298,800/= |

Mheshimiwa Naibu Spika, Sh. 9,655,500,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo ambapo Jeshi la Polisi limetengewa Sh.5,400,000,000/=; Magereza Sh.3,900,000,000/=; Utawala Sh.255,500,000/= na Uhamiaji Sh.100,000,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru wewe pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA – (K.n.y. MWENYEKITI KAMATI YA ULINZI NA USALAMA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni na ushauri wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kuhusu Makadirio na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2005/2006 kwa mujibu wa Kanuni ya 81(1) ya Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za rambirambi na pole kwa familia, ndugu na jamaa pamoja na Wapigakura wote wa Jimbo la Kilombero kutokana na kifo cha mpendwa wetu Mheshimiwa Abu Towegale Kiwanga na Mheshimiwa Margareth Bwana, Mbunge wa Viti Maalum, kutoka Mkoa wa Rukwa. Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia nafasi pia kushukuru sana Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa ushirikiano mkubwa walionipa kwa kipindi chote cha miaka mitano nikiwa Mwenyekiti wa Kamati hii. Wametumia uzoefu wao kuhusiana na masuala mbalimbali ya Ulinzi na Usalama kujadili kwa kina masuala mbalimbali yaliyoletwa mbele ya Kamati hii na kutoa ushauri mahsusi wa namna ya kuboresha utendaji kazi wa vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama, ikiwa ni pamoja na Bajeti hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2005/2006. Wajumbe wa Kamati hii ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Dr. John S. Malecela, Mbunge -Mwenyekiti;
Mheshimiwa Dr. Lawrence M. Gama, Mbunge -Makamu Mwenyekiti;
Mheshimiwa Maj. Jesse J. Makundi, Mbunge -Mjumbe;
Mheshimiwa Frank G. Maghoba, Mbunge -Mjumbe;
Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mbunge -Mjumbe;
Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, -Mjumbe;
Mheshimiwa Anne K. Malecela, Mbunge -Mjumbe;
Mheshimiwa Col. Feteh S. Mgeni, Mbunge -Mjumbe;
Mheshimiwa Benito W. Malangalila, Mbunge -Mjumbe;
Mheshimiwa Ireneus N. Ngwatura, Mbunge -Mjumbe;
Mheshimiwa Thomas S. Nyimbo, Mbunge -Mjumbe;
Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mbunge -Mjumbe;

Mheshimiwa Getrude I. Mongella, Mbunge -Mjumbe; na
Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mbunge -Mjumbe.

Naishukuru sana Sekretarieti ya Bunge, Ndugu Mathew D. Kitundu na Ndugu Elisa D. Mbise kwa jinsi walivyoihudumia Kamati kwa ufanisi mkubwa na kuifanya Kamati kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, nampongeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri kwa kuwasilisha mbele ya Kamati Taarifa za Utekelezaji wa ahadi za Serikali chini ya Wizara hii zilizotolewa mbele ya Bunge lako Tukufu pamoja na ushauri uliotolewa na Kamati yangu kwa vipindi tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumze neno moja la ziada kwa ruhusa yako juu ya Mheshimiwa John Z. Chiligati, Mbunge na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa Chiligati amekuwa ni kiungo muhimu sana kati ya Kamati na Wizara nyingine zilizo kwenye Sekta ya Ulinzi na Usalama mbali na Wizara yake mwenyewe. Amekuwa akiongozana na Kamati kwenye ziara zote ambazo Kamati imekuwa ikifanya sehemu mbalimbali nchini na kuhudhuria vikao karibu vyote ambavyo Kamati imekuwa ikifanya.

Wakati wa ziara za Kamati katika maeneo mbalimbali ya nchi, Mheshimiwa Chiligati amekuwa akisaidia sana Kamati kwa kutoa ufafanuzi wa mambo mbalimbali yanayotekelezwa na Serikali katika Sekta ya Ulinzi na Usalama. Tunamshukuru sana kwa utendaji wake huo na tunamtakia kila la kheri aendelee na moyo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 1 na 2 Juni, 2005 Kamati ilizijadili na kuzichambua taarifa za utekelezaji wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na kujadili makadirio ya matumizi ya Wizara kwa Mafungu, 28 - Jeshi la Polisi, fungu 29 - Magereza, fungu 51 - Utawala na fungu 93 - Uhamiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati na malengo ya Wizara kwa mwaka 2005/2006, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi aliwasilisha mbele ya Kamati taarifa ya utekelezaji na Bajeti kwa mwaka 2004/2005 pamoja na malengo ya Wizara kwa mwaka 2005/2006 kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri hivi punde. Kamati ilizijadili taarifa hizo kwa kina na pia Kamati ilipata fursa ya kutembelea baadhi ya maeneo na kujionea mambo makubwa yaliyotekelezwa na Wizara. Kamati inaipongeza sana Wizara hii kwa hatua kubwa iliyopigwa katika kuimarisha utendaji kazi na huduma bora kwa wananchi hata katika mazingira magumu ambayo hayana vitendea kazi vya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2005/2006 Kamati ilijadili mipango ya Wizara kwa mwaka 2005/2006 inayotarajia kuendelea kuboresha mazingira ya kazi pamoja na vitendea kazi ili kuweka misingi thabiti ya utoaji huduma bora kama ilivyoelezwa na Waziri katika hotuba yake. Maelezo ya Waziri yanatilia mkazo malengo yafuatayo:-

(1) Kukamilisha ujenzi wa majengo ya Ofisi za Polisi, nyumba za kulala Askari, kukamilisha ukarabati wa jengo la Makao Makuu ya Magereza na kuendelea na ukarabati wa majengo na miundombinu ya Magereza manne yenye ulinzi mkali;

(2) Kukarabati mabweni ya wanafunzi *CCP* Moshi na Chuo cha Polisi Dar es Salaam, kukamilisha ujenzi wa Vituo vya Polisi vya Morogoro, Katesh na Makambako;

(3) Kununua magari ya doria na ya kubeba mahabusu, kukarabati mashua za doria na ujenzi wa Chuo cha *CID* – Dodoma;

(4) Kuendelea na upimaji wa Magereza sita na ulipaji fidia kwa maeneo ya Magereza, kuimarisha miradi 41 ya Kilimo na miradi 6 ya Viwanda vidogo vidogo kwa ajili ya programu za urekebishaji wafungwa;

(5) Kununua magari na pikipiki kwa ajili ya shughuli za Magereza, Uhamiaji na Polisi. Vile vile, Wizara ina mpango wa kutoa mafunzo mbalimbali kwa watumishi ikiwa ni pamoja na kuendesha programu za kudhibiti maambukizi ya Ukimwi, pamoja na kuendelea kupambana na rushwa;

(6) Ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji katika Mikoa ya Manyara, Dar es Salaam na Kigoma pamoja na ukarabati wa Vituo mbalimbali nchini;

(7) Kuajiri Maafisa Uhamiaji wapya 322 na kuwapeleka watumishi 137 kwenye kozi mbalimbali;

(8) Kuanza zoezi la kutoa *Visa stickers* kwa baadhi ya Vituo vya Kuingilia Wageni Nchini;

(9) Kuendelea na zoezi la kurudisha makwao Wakimbizi wa Burundi na Kongo *(DRC);*

(10) Kuwasilisha Bungeni Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ya Wakimbizi Na.9 ya mwaka 1998 na kutunga Kanuni zake;

(11) Kupima na kuweka mipaka iliyo wazi na kutangaza mipaka ya makazi ya Katumba kwa lengo la kuzuia Wakimbizi kuvamia maeneo ya nje ya mipaka ya maeneo yao;

12) Kukamilisha Sera ya Moto na Ukoaji pamoja na kununua magari ya Zimamoto kwa ajili ya Halmashauri saba pamoja na kutoa mafunzo kwa ajili ya Askari wa Zimamoto na Uokoaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza majukumu hayo pamoja na mengine ambayo sikuyataja kwa mwaka ujao wa fedha, Wizara imeomba kwa mafungu kama ifuatavyo:-

Fungu 28 - Jeshi la Polisi; Matumizi ya Kawaida Sh.96,761,080,300/= na Mipango ya Maendeleo Sh. 5,400,000,000/=.

Fungu 29 - Jeshi la Magereza; Matumizi ya Kawaida Sh.50,227,707,800/= na Mipango ya Maendeleo Sh.3,900,000,000/=.

Fungu 51 - Utawala; Matumizi ya Kawaida Sh.4,270,229,300/= na Mipango ya Maendeleo Sh. 255,500,000/=.

Fungu 93 - Uhamiaji; Matumizi ya Kawaida Sh. 11,727,298,800/= na Mipango ya Maendeleo Sh. 100,000,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati, awali ya yote Kamati inalipongeza Jeshi la Polisi kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kukabiliana na hali ya uhalifu nchini ikiwa ni pamoja na ujambazi. Kwa mujibu wa Taarifa za Polisi hali ya uhalifu kwa wastani imekuwa ikipungua ikilinganishwa na siku zilizopita.

Kwa yale matukio ya uhalifu ambayo yameongezeka, Kamati inatoa wito kwa wananchi kutoa ushirikiano zaidi kwa Polisi ili kuendelea kudhibiti vitendo vya uhalifu nchini. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuongeza Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi mwaka hadi mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha utendaji wa kazi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Kamati inashauri kwamba, Jeshi la Polisi kwanza ihakikishe kwamba Vifaa vya mawasiliano vya kisasa vipelekwe pia katika maeneo ya mpakani hasa mipaka ya Magharibi ambapo kuna matukio mengi ya ujambazi yanayosababishwa na wimbi la Wakimbizi toka nchi jirani.

Pili, Jeshi la Polisi liongezewe magari ya doria ili mitambo ya kisasa ya mawasiliano iweze kutumika kwa ufanisi zaidi katika kukabiliana na hali ya uhalifu.

Tatu, Wizara iweke utaratibu wa kuzifanyia matengenezo ya mara kwa mara nyumba za Askari na majengo mengine pale uchakavu unapojitokeza badala ya kuacha majengo hayo mpaka yachakae kabisa na kuhitaji fedha nyingi za ukarabati. Fedha kwa ajili ya matengenezo ya mara kwa mara ziwe zinaombwa kwenye bajeti ya kila mwaka. Aidha, askari watakaopatiwa nyumba mpya zilizojengwa kwenye maeneo mbalimbali nchini wapewe maelekezo maalum juu ya utunzaji wa nyumba hizo na ukaguzi wa mara kwa mara ufanyike.

Nne, Jeshi la Polisi likishirikiana na Jeshi la Magereza watumie miradi inayoendelea ya ujenzi wa nyumba za bei nafuu kwa kuwashirikisha kikamilifu wafungwa ili wajifunze kutumia teknolojia hiyo rahisi kwa manufaa yao mara wamalizapo kutumikia adhabu zao Magerezani. Kwa mfano, wafundishwe kutumia mashine za *Hydroform* katika kutengeneza matofali kwa gharama nafuu.

Tano, ili kupunguza tatizo la ajali za barabarani, Kamati inashauri kwamba magari yote hasa ya abiria yafanyiwe ukaguzi maalum ili kubaini magari machakavu na kuyapiga marufuku kupita barabarani. Kwa kuwa inaonekana utaratibu wa kuweka vidhibiti mwendo umeshindwa kuleta mafanikio yaliyotarajiwa, Kamati inashauri kuwepo na Askari watakaokuwa wanasafiri na mabasi kwa siri na yale mabasi yatakayokuwa yanagundulika yanakimbia kupita kiasi yafutiwe leseni badala ya utaratibu wa sasa wa kutoza faini.

Sita, ili kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam hasa wakati wa mvua, Kamati inashauri Polisi kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji wabuni namna ya kupunguza msongamano. Aidha, maeneo yanayosimamisha maji yatambuliwe na kufanyiwa matengenezo ili kupunguza msongamano wa magari wakati wa mvua. Pia, Halmashauri ya Jiji ifikirie kuwa na barabara za kupita juu yaani *flying overs.*

Saba, katika kupunguza uharibifu wa barabara, Kamati inashauri kwamba magari yanayopimwa kwenye mizani na kukutwa yamezidisha uzito, mizigo iliyozidi iteremshwe badala ya kuwatoza faini na kuacha yanaendelea na safari na hivyo kuendelea kuharibu barabara. Faini inayotozwa mzigo uliozidi hailingani na gharama na hasara inayosababishwa na uzito huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nane, Kamati imeridhika na kazi inayofanyika ya kukarabati jengo litakalotumika kama Makao Makuu ya Jeshi la Magereza. Ili kukamilisha kazi ya ukarabati kwa wakati, Kamati inashauri kwamba fedha zote zilizoidhinishwa kwa kazi hiyo kwa mwaka huu wa fedha zitolewe kwa mkupuo mmoja ili kazi hiyo iweze kukamilika kwa muda uliopangwa ambao ni Septemba, 2005.

Tisa, ili kuondoa msongamano wa wafungwa Magerezani, Kamati inashauri kwamba kuwepo na mpango maalum wa kujenga Magereza mapya hasa kwenye Wilaya zisizo na Magereza. Aidha, Magereza yapanuliwe kwa kuongeza vyumba vya kulala mahabusu. Hoja ya msingi ya kuongeza Magereza ni kutokana na ukweli kwamba Magereza mengi yaliyopo yalijengwa wakati wa Ukoloni ambapo idadi ya watu ilikuwa takribani milioni kumi wakati wa kupata uhuru na hivi sasa imefikia milioni 36.*(Makofi)*

Kumi, hali ya uzalishaji katika Magereza, hasa kilimo hairidhishi. Kamati inashauri kwamba uwepo mpango maalum wa kufufua uzalishaji wa mazao ya kilimo Magerezani kwa kulima kilimo cha kisasa kitakachotoa mazao mengi kwa hekta.

Pia, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa nguo mpya kwa ajili ya wafungwa Magerezani, ikiwa ni pamoja na kuwawezesha wafungwa kuvaa suti. Kwa moyo huo huo wa kujali haki za binadamu, Kamati inashauri kwamba wafungwa waliopo kwenye maeneo yenye baridi kali wapewe nguo ambazo zitawasitiri wakati wa baridi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipotembelea maeneo mengi Mikoani ilikuta Idara ya Uhamiaji haina vifaa vya usafiri. Kamati inashauri kwamba Maafisa Uhamiaji waliopo Mikoani wapatiwe nyenzo za usafiri kama vile magari na pikipiki. Kipaumbele

kitolewe kwa maeneo ya mipakani ili Maafisa wahusika waweze kudhibiti wahamiaji haramu.

Vile vile, Kamati inashauri kwamba Serikali iwe makini sana katika utoaji wa hati mpya za kusafiria ili kuepuka hati hizo kupewa watu wasio raia.*(Makofi)*

Wakati wa kutengeneza vitambulisho vya uraia kumbukumbu muhimu zote za mhusika ziwekwe kama vile tarehe ya kuzaliwa, leseni ya kuendesha gari, taarifa za kodi, bima na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Zimamoto na Uokoaji Katika kuleta ufanisi kwenye utendaji wa Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji, Kamati inashauri kwamba Sheria ya Zimamoto irejeshwe ya kuwepo na utaratibu wa kuwa na mamlaka moja ya kutoa maelekezo ya Uokoaji na Zimamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nachukua tena nafasi hii kwa niaba ya wenzangu kukushukuru wewe kwa kututeua kuwa Wajumbe wa Kamati hii kwa kipindi chote cha miaka mitano. Aidha, tunaishukuru Serikali kwa kuyafanyia kazi maoni na ushauri ambao Kamati imekuwa ikitoa mara kwa mara kwa lengo la kuboresha utendaji wa vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama.

Baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Wajumbe wenzangu na mimi mwenyewe, nasema kuwa naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. FRANK G. MAGHOBA – MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani Bungeni kuhusu Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2005/2006 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu 43(5)(b)(c) na 81(1) Toleo la 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nichukue fursa hii kuwapongeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi - Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, Naibu Waziri - Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Viongozi na Wataalam wote kwa kufanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niwapongeze Viongozi wote wa Vyama walioteuliwa kugombea nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wale wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, nachukua fursa hii kuipongeza Serikali na Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufanya upendeleo maalum katika Wizara hii ambayo kimsingi ndiyo Wizara muhimili kwenye masuala ya Ulinzi wa Wananchi na mali zao. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi miaka ya hivi karibuni imekuwa ikiongezewa asilimia 25 zaidi ya Bajeti ya kawaida ili kufanikisha mambo kadhaa ya kuimarisha ulinzi wa Nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kutokana na Kambi ya Upinzani kutoa ushauri wake mara kadhaa kwamba Polisi nchini wamekuwa wachache sana na ulinzi kuzorota sana kiasi kwamba wananchi walianza kukosa imani na Serikali yao. Hivi sasa angalau Jeshi la Polisi nchini limeimarika zaidi hasa Serikali pale ilipoamua kununua vifaa mbalimbali vya kufanyia kazi yakiwemo magari na *Boat* sehemu za maziwa yaliyo mipakani mwa nchi yetu.

Aidha, Serikali imeboresha na inaendeleza kuboresha sehemu za kuishi askari wetu. Hali hiyo inatia moyo na inatia moyo pia kwa Askari wetu ambao sasa wanapata morali wa kufanya kazi wakijua wazi kuwa Serikali huwathamini sana katika kazi zao. Pia, Serikali imeboresha Jeshi hilo kwa kununua *Radio Calls* sehemu mbalimbali nchini jambo ambalo linafanya mawasiliano kati ya Kituo na Kituo, Mkoa na Mkoa, Wilaya na Wilaya kuwa rahisi zaidi na kiasi fulani kudhibiti uhalifu nchini.

Katika Hotuba yangu ya Bajeti iliyopita ya mwaka 2004/2005 nilishauri Serikali kuanzisha Chuo cha kufundishia Askari wa Upelelezi, ambao wanaweza kusaidia kupunguza msongamano wa kesi mbalimbali ambazo hukwama kuendeshwa kutokana na kukosa Wapelelezi wa kesi hizo karibu nchini kote. Lakini nafurahi kwamba ushauri wa Wabunge wa Kambi ya Upinzani umekubaliwa na sasa Chuo hicho kitaanza kujengwa hivi karibuni baada ya Wabunge kupitisha Bajeti hii.

Aidha, tunaipongeza Serikali kwa kujenga nyumba za Askari sehemu mbalimbali nchini. Serikali imekuwa ikiendelea kuboresha nyumba za Askari wetu zilizokuwa zina hali mbaya na sasa nyumba hizo zimebadilika sana na Askari wetu wanaendelea kupata matumaini ya kuishi katika nyumba bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi hizo za Serikali katika kuboresha mawasiliano muhimu nchini, nashauri kwamba Mtambo uliofunguliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Mtambo ambao umeigharimu Serikali fedha nyingi, Mtambo huo hautakuwa na maana kama mawasiliano ya Askari wa Doria watakosa vifaa muhimu ili kukamata wezi wa magari na majambazi wanaotumia silaha. Mtambo huo wenye Mawasiliano ya kisasa unahitaji kupewa *support* ya *Radio Calls* na magari yawepo mengi sehemu ya katikati ya Jiji la Dar es Salaam na Askari Kanzu wawepo wengi sehemu zenye matukio ya mara kwa mara ya uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mtambo uliopo Makao Makuu ya Wizara, ambao unaweza kutambua kwa urahisi sana, mbinu zinazofanywa na wahalifu wa kughushi maandishi, noti bandia, kutambua vidole vya mhalifu na kutambua kwa urahisi risasi

zitumikazo kufanyia uhalifu nchini. Mitambo hiyo ni hatua nzuri kwa Serikali katika kurahisisha uchunguzi wa kesi mbalimbali nchini. Nashauri kwamba mitambo haitakuwa na maana kama haitatunzwa vyema na mitambo hiyo kutumika vibaya kwa kupotosha ukweli wa jambo linalohusika hasa katika kutambua vidole vya mhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani bado inasisitiza kuwa ni vyema Serikali ikaanzisha Vyuo vingine viwili nchini vitakavyoweza kufundisha Askari Polisi wengi watakaoweza kutosha kulinda maeneo mengi nchini. Lakini pia ingekuwa vyema kuwepo Chuo kitakachofundisha Askari *Traffic* tu ili Sekta hiyo iweze kuwa endelevu na kusaidia kupunguza ajali mbalimbali nchini kote, kwani kwa sasa Askari *Traffic* wengine huchaguliwa tu bila mafunzo na kupewa kazi hiyo ya *Traffic*. Hiyo ni hatari kwa usalama barabarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali irudishe utaratibu wake wa zamani wa kutoa leseni kwa madereva waliohitimu, kwa kufanyiwa majaribio na magari ya Serikali tu, kwani mtindo wa sasa wa kutumia magari ya Vyuo hupunguza umakini wa madereva hao kujua vyema sheria za barabarani.

Aidha, kuwepo na magari makubwa na madogo kwa ajili ya kufanyia majaribio madereva hao, kwa kufanya hivyo tutapata madereva makini watakaofanya kazi zao kwa uangalifu na kuokoa maisha ya Watanzania, ambapo kila kukicha hupoteza maisha kutokana na madereva wasiojali maisha ya watu wanaotegemewa na Taifa hili katika kuinua uchumi wetu. Magari makubwa katika majaribio, madereva waliofaulu vyema kwenye mafunzo yao wataonekana na wale walio bado pia watajulikana pale pale na pia hawatapewa leseni mpaka watakapofaulu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa kikosi cha *F.F.U.* kiendelee kupewa mafunzo ya kutosha. Lakini pia, Askari hao wanatakiwa wafundishwe mbinu za kupambana na wafanyafujo kwa kutowaumiza wala kuvunja viungo vya watu wanaoandamana au wanaotaka kupeleka ujumbe sehemu fulani kutokana na kutokuridhishwa na baadhi ya mambo ambayo wao wanaona yanagusa maisha yao ya kila siku.

Askari Polisi hao wawe wenye kusimamia waandamanaji hao waendao kupeleka ujumbe kwa amani na kupeleka ujumbe wao bila kuwasumbua kwa virungu na mabomu ya machozi, labda kama waandamanaji hao watakwenda kinyume na makubaliano ya kufanya maandamano. Lakini pamoja na hayo, wanatakiwa kuchukua utaratibu na maamuzi ambayo hayatahatarisha maisha ya wahusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iendelee kuboresha Magereza nchini kote, kwani kadri miaka inavyokwenda na wahalifu wanazidi kuwa wengi na matokeo yake msongamano wa wafungwa unazidi kuwa mkubwa zaidi. Tunaishauri Serikali kubuni mbinu nyingine za kupunguza misongomano ndani ya Magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kabisa kwamba, sasa hivi Magereza zetu hazitoshi kuwatunza wafungwa. Sasa kuna kesi nyingine zinakuwa hazina uzito, unamweka mtu labda ameiba kuku au kamshika mtu makalio au mtu kaiba mkufu anafungwa miaka 10. Matokeo yake sasa Magereza sasa zinajaa kwa wafungwa ambao wana kesi ndogo ndogo. (*Makofi*/*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeshauri hapa Serikali iangalie jinsi ya kuondoa hizo adhabu ndogo ndogo ambazo mtu anaweza akafanyia akiwa nje ya Magereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Magereza nchini inatakiwa yawezeshwe ili wazalishe kupitia kilimo, mifugo na mambo kadhaa lakini yapatiwe vifaa vya kufanyia mambo hayo niliyoyataja. Mfano, ili waweze kulima wapatiwe ma-*tractor* ya kutosha, mbolea za kuotesha mazao haya, wapewe ngo'mbe, mbuzi, nguruwe, kuku na kadhalika ili waendeleze Sekta ya Kilimo/Mifugo. Kwa kufanya hivyo, Magereza itaweza kujitegemea na bila kutegemea Serikali kila wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *Passport*, *Passport* ni haki ya kila Raia wa Tanzania kuipata ili aweze kufanya safari wakati wowote anapotaka. Aidha, gharama ya kuipata *Passport* ni kubwa mno. Sidhani kama Watanzania wote wanaweza kumudu gharama za kununua *Passport* au kubadilisha *Passport* hizo. Ni vyema Serikali ingetenga fedha kwa ajili ya kutengeneza Mashine ambazo zinatengeneza *Passport*.

Nadhani pesa wanazotozwa wananchi sasa hivi ni kwa ajili ya kusaidia kuboresha Mtambo wa kutengeneza *Passport*. Ili kupunguza gharama kwa Watanzania, tungeishauri Serikali itenge pesa kwa ajili ya kutengeneza Mtambo huu na wananchi waweze kulipa kiasi kidogo cha pesa katika kuhakikisha kwamba Mtanzania anapata *Passport*.

Kambi ya Upinzani inaona gharama hiyo ni kubwa na inamnyima haki mwananchi kupata *Passport* hiyo. Tunashauri *Passport* hiyo iuzwe angalau Sh.15,000/= au Sh.10,000/= angalau kidogo wanaweza kumudu gharama hiyo. Vile vile, wataalamu waongezwe kwenye Kitengo hicho cha kutoa *Passport* ili kuondoa msongamano uliopo Makao Makuu. Msongamano huo unaweza kuchochea rushwa kwa wenye haraka, kwani *Passport* sasa hutolewa baada ya mwezi au miezi miwili. Hii yote hutokana na uchache wa wataalam kwenye Kitengo hicho.

Aidha, Kambi ya Upinzani inashauri kwamba, ni vizuri wataalam tulionao waendelee kufanya kazi hata usiku kwa maana ya *overtime* na waweze kulipwa hela zao bila kucheleweshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mishahara na posho za Askari, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuongeza mishahara na posho za Askari Polisi, kwani kwa kawaida Polisi hawana nafasi ya kufanya shughuli zao binafsi baada ya saa za kazi ili kujiongezea kipato kama walivyo watumishi wengine wa Serikali.

Ieleweke kuwa Askari Polisi wanalala nje usiku kucha wakiwa kwenye doria ili kulinda wananchi ambao ndio Walipakodi na Viongozi wa Serikali na Mabenki. Kitendo

cha kuwalipa Askari wa kawaida Sh.80,000/- ni kuwanyima haki kutokana na kazi kubwa wanazozifanya.

Pia, Askari wetu wapewe Posho haraka bila usumbufu wowote kwani kwa kuchelewesha haki zao kunawafanya Askari wetu kukosa Morali wa kufanya kazi, Polisi hao ni hasa wale wanaopelekwa kwenye kazi maalumu, na wale wanaohama toka Mkoa fulani na kupelekwa Mkoa mwingine.

Aidha, Askari wetu kwa kawaida wao huwa hawana Chama chochote. Kwa hiyo, basi nawaomba Askari hao wasikubali kushinikizwa kupigia Chama fulani badala yake wapige kura kumchagua Kiongozi wanayemtaka wao. Hili litafanya uchaguzi kuwa huru.

Pia, Serikali iangalie upya utaratibu wa kuwahamisha Askari Polisi kwani tabia ya kumuacha Askari sehemu moja kwa muda mrefu husababisha Askari kuzoea mazingira na kuzoeana na raia, jambo ambalo baadhi ya Askari ambao siyo waaminifu kujiingiza kwenye vitendo viovu na kuleta doa katika Jeshi letu la Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siku za nyuma kulikuwa na matukio mengi ya ujambazi yaliyohusisha baadhi ya Askari Polisi ambao kwa sasa wametimuliwa ndani ya Jeshi hilo. Hiyo ni hatua nzuri kwani kwa kufanya hivyo, kutafanya wenye tabia hiyo waogope, lakini Askari hao wanaotimuliwa wasiishie kutimuliwa tu, bali wapewe adhabu kali isiyo na mfano ili iwe fundisho kwa wenye tabia hiyo chafu.

Suala la ujambazi nchini ni tatizo sugu ndiyo maana tunasisitiza kuwa na vifaa au mtambo uliopo uboreshwe zaidi kwa kupewa *support* ya *Radio Calls*, Magari ya doria na Askari Kanzu wa kutosha hasa sehemu za Miji mikubwa yenye matukio mengi ili kudhibiti uhalifu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijamaliza, napenda nichukue fursa hii kurudia tena kuwapongeza Maafisa wa Polisi ambao wamekuwa wakifanya kazi nzuri mara kwa mara, hasa Omari Mahita aliyekuwa anasimamia vizuri shughuli zote za Polisi, Adadi Rajab, Aden Mwamunyange, Tibasana, Mwansasu, Alfred Tibaigana-*RPC* Dar es salaam, Gumbo wa Dodoma, Kijana wangu ambaye yuko Makao Makuu, Bwana *Tossy* wa *FFU*, *RPC* Kova na wengine kwa kusimamia kazi zao vyema kwenye maeneo yao. Tunawapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nisiwasahau Wapigakura wangu wa Jimbo la Kigamboni. Kwanza ninawashukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuwawakilisha ndani ya Bunge hili na nashukuru kwamba wamekuwa wakinipa ushirikiano wa kutosha siku zote nilipokuwa nafanya kazi za maendeleo bila kujali itikadi zao.

Pia, niishukuru Serikali kwa kutokunibagua. Mara nyingi imekuwa ikinisaidia pale nilipohitaji msaada wao. Hiyo ni hatua nzuri kwa Serikali kwamba sasa inaelekea siasa zetu zinatuingia vichwani na tunakomaa kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, naomba Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, narudia tena; Kwa kumalizia naomba Wabunge wa

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakubali maombi ya fedha zilizoombwa kwa matumizi ya kawaida ili Askari wetu wafanye kazi iliyokusudiwa kuifanyia kazi ya ulinzi nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Bajeti hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hapo ndiyo tumemaliza wale Wasemaji Wakuu. Tunao walioomba wengi, lakini wa mwanzo ni wale ambao kama tunavyosema kila siku, wale ambao hawajachangia kabisa nao ni Mheshimiwa Hamis Awesu Aboud, atafuatiwa na Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa na Mheshimiwa Haji Juma Sereweji. Hawa walikuwa hawajachangia kabisa. Wengine watafuatia baadaye.

Sasa kufika hapo, namwomba Mwenyekiti, Mheshimiwa Anne Makinda, aweze kuja kunisaidia kuendesha Bunge.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti.*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Mheshimiwa Hamis Awesu Aboud.

**MHE. HAMIS AWESU ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa kupata nafasi hii ili na mimi nijumuike na wenzangu nichangie Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabla sijasahau, nataka niunge mkono hoja asilimia mia moja na sina sababu ya kuikataa hii Bajeti ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu mambo chungu nzima ambayo tulikubaliana hasa katika kipindi kilichopita, yameorodheshwa katika kitabu hiki. Lakini sasa ni wajibu wa kila Mbunge kama kuna dukuduku lake mwenyewe aliseme ili hotuba hii au Bajeti hii iwe nzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Maafisa mbalimbali wa Wizara hii pamoja na Askari hasa Askari wa Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri wanazozifanya katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo nitakayoyachangia ni machache tu na nataka nianzie na suala hili la mahabusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu kuna mahabusu wanaofanya matatizo bila kukusudia na kila binadamu anaweza akafanya matatizo na baadaye akaitwa mahabusu. Lakini mahabusu si jambo la kumfanya mtu kuwa ndiyo amefanya kwa makusudi. Sasa nataka niseme kwamba kwenye mahabusu kuna matatizo. Mahabusu wanapokamatwa na Jeshi la Polisi wanapelekwa Mahabusu, lakini sasa wanaweza wakakaa muda mrefu hukumu yao haijapatikana. Ukiwapeleka Mahakamani, baadaye wanarudishwa huko huko, maelezo yanayotolewa unaambiwa uchunguzi haujakamilika.

Sasa mimi ninachotaka kukisema hapa, ni vyema Jeshi la Polisi waangalie ni kesi zipi za muda mrefu na kesi zipi za muda mfupi kwa sababu sasa ukishampeleka mtu Mahakamani unaambiwa ushahidi haujakamilika. Hivi huu ushahidi wa Jeshi la Polisi ukoje? Kwa sababu mtu ukishampelekea jamaa yake Mahabusu hana uhakika kama atafungwa siku ngapi au atafunguliwa. Kwa hiyo, naomba Serikali ituwekee wazi kuhusu suala zima la Mahabusu. Mimi najua kuwa kuna watu chungu nzima sasa hivi wako Mahabusu zaidi ya mwaka mmoja. *(Makofi)*

Ninalojifunza, raia wengi hatujui Sheria za nchi. Kwa hiyo, unaweza ukafanya makosa bila kujijua ukajishtukia uko Mahabusu. Sasa nasema kwamba itabidi hapa tufanye kazi ya kuelimisha watu watakaopata matatizo tuondokane na hili neno la Mahabusu na ikiwezekana mtu aambiwe umefanya kosa hili, utakaa Mahabusu kipindi fulani, kipindi fulani utatoka. Mahakama nayo pia isimamie kuhakikisha kuwa kama watu makosa yao siyo makubwa, basi yale maelezo yao yatolewe mapema ili mtu ajijue kuwa atatoka au vipi, kwa sababu sasa hivi kuna watu wako Mahabusu miaka chungu nzima hawajatoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niache kwenye Mahabusu niingie kwenye Pensheni za Wafanyakazi hasa wa Jeshi la Polisi. Mimi nazungumzia Pensheni za Wafanyakazi hasa katika Jeshi la Polisi kwa sababu nina ushahidi. Nivi ninavyokwambia, wako Askari Polisi waliostaafiu kazi kipindi kirefu sasa hawajapewa haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyojifunza mimi, kuna Mifuko mbalimbali. Kuna *LAPF*, kuna *PPF*, kuna *NSSF* na kadhalika. Mfanyakazi akishamaliza muda wake hajui kuwa mimi nilijiunga na Mfuko wa *PPF* au nilijiunga na Mfuko wa *NSSF* au nilijiunga na Mfuko gani! Kwa hiyo, nataka niseme kwa wafanyakazi hasa Jeshi la Polisi, ni vizuri muwaambie mapema. Mukiwaajiri muwaambie; mfanyakazi wewe umeingia katika mfuko fulani ili wakati wa kufuatilia mafao yake ajue anafuatilia Mfuko gani, kwa sababu wengine unaweza ukafuatailia Pensheni yako kwenye Mfuko wa *PPF* lakini kumbe hukujiunga na Mfuko wa *PPF* ulijiunga na Mfuko mwingine. Kwa hiyo, tatizo hili ndilo linalowakumba wafanyakazi wetu.

Lakini lingine ninalotaka kulisema, hata kama amejiunga na huo Mfuko unaotakiwa, Askari Polisi au Askari mwingine akishastaafu anatakiwa afuatilie mafao yake Dar es salaam. Hebu niambie wewe mtu anayetoka Jimboni kwangu Mkanyageni, anatoka Kisiwapanza, Chokocho na Mkanyageni pale, umwambie aende akafuatilie fedha zake Dar es salaam, wewe unafikiri atazipata saa ngapi? Akifika kule hana mama, hana mjomba, hana shangazi, itabidi alale *Guest*. Akishalala *Guest,* wiki ijayo arudi tena Mkanyageni, mwezi ujao aende Dar es salaam. Hivi mtamlipa Shilingi ngapi?

Kwa hiyo, ninachoomba, hizi pesa za Pensheni kama itawezekana, *RPCs* wafanye hii kazi. Makamanda wa Polisi wa Wilaya na Mikoa wasimamie fedha za wafanyakazi badala ya kumfanya mfanyakazi peke yake aje Dar es salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naomba kwa hili Makamanda wa Polisi wa Wilaya na Mikoa wasimamie fedha za wafanyakazi wao. Wasiwaachie

wafanyakazi wakishastaafu baadaye wanafuatilia pesa zao Dar es salaam. Kwa hiyo, naomba sana kwa hili, Serikali ifanye kazi ya kusimamia hizi fedha. Lakini lingine nililojifunza, inawezekana kuwa wafanyakazi wengi hawana Akaunti Benki. Tungewafundisha kila mfanyakazi akafungue Akaunti yake Benki. Akimaliza kazi tu, *cheque* yake inaingia katika Akaunti yake badala ya kwenda Dar es salaam, sijui waende wapi, tutafika mahali wafanyakazi watapata matatizo! Hilo moja katika Pensheni.

Lakini la pili hapo hapo, kuna wafanyakazi waliofariki muda mrefu hawajalipwa mafao yao. Ina maana wale warithi wa Marehemu mpaka hivi ninavyokwambia hawajapata pesa zao. Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa warithi wa Marehemu wanapata fedha zao?

Mtu amefariki ana watoto, kaacha mke, kaacha mama, ana pesa zake anahangaika kuja Dar es Salaam akiuliza huko anapigwa chenga ya mwili, akirudi huku anapelekwa huku na kwa sababu wafanyakazi wetu wa Jeshi la Polisi na wafanyakazi wengine, unafikiri ukishakuwa mfanyakazi kumwendela Kiongozi wako wa juu lazima utamwogopa tu. Kwa hiyo, sisi Waheshimiwa Wabunge ndiyo tunaopata hili tatizo sasa. Ukikutwa tu Mbunge, basi Mheshimiwa Bwana mimi tatizo langu nimeachishwa kazi huu mwaka wa pili sijalipwa pesa zangu za *PPF* na kadhalika. Kwa hiyo, kuna watu chungu mzima wamefariki lakini hawajapata pesa zao za urithi. Sasa hilo nalo naomba Serikali isimamie vizuri ili tuondokane na hili tatizo la kufuatilia hizi Pensheni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ninataka nizungumzie ni suala la nyumba za Polisi hasa katika Kituo cha Mkoani Pemba, Mtambile na Kengeja.

Bunge lililopita, nilichangia nyumba hizi hizi na nikatoa rai nikasema hivi, kila Bajeti kama Serikali ingejenga nyumba mbili kila Kituo, nyumba mbili Mkoani, Nyumba mbili Kengeja, nyumba mbili Mtambile kwa muda wa miaka mitano tutakaokaa Bungeni wangekuwa na nyumba nyingi tu. Hivi ninavyokwambia mtu anaweza akatoka Mwambe anafuatilia kazi Mtambile. Pale hakuna nyumba, basi kila alilonalo bovu, wewe unafikiri atafanya kazi kiasi gani? Akifika pale anapangiwa kazi. Kwa hiyo, naomba nyumba za Polisi zijengwe ili wafanyakazi wetu waondokane na hili tatizo la kuzunguka zunguka.

Lakini mbali na nyumba za Polisi za kazi, pia, unajua mfanyakazi raha yake ni pale kazini tu, lakini akishatoka kazini huku alikuwa akipanga nyumba kazini, huku alikuwa akipanga nyumba uraiani, akishatoka pale atakuwa na hali mbaya sana.

Kwa hiyo, ninachokiomba, Askari Polisi na Askari wengine katika Wizara hii wakopeshwe fedha wajengewe nyumba tu au wajenge nyumba katika maeneo yao hata vyumba viwili, maana ukiwemo kazini ukisema kuwa utakodi nyumba, utakodi kweli. Hata mimi Mbunge nikimaliza Bunge sina uwezo hata wa kukodi nyumba. Sikwambii Askari Polisi wa kawaida, hata mimi nikimaliza kazi tu, basi nimeishamaliza Bunge, nyumba ya kukodi uwezo sina. Kwa hiyo, Askari Polisi naye anatakiwa mfanye maarifa yenu wote basi muwasaidie angalau wawe na vijumba vyao katika Mitaa wanayokaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, tangu hapo sikuwa na mengi lakini kulikuwa na mambo fulani, nataka kuyaboresha. Naomba niunge mkono hoja hii na nawashawishi wenzangu kuwa tukubali kuipitisha hii Bajeti ili waweze kupata fedha na fedha hizi zitumike kama ilivyokubaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami kwa sababu ni mara yangu ya kwanza katika Mkutano huu wa Bunge kutoa maoni yangu hapa, napenda nitumie fursa hii kwa niaba ya Wapigakura wangu wa Jimbo la Gando kutoa mkono wa rambirambi kwa wale wote wenzetu waliotangulia mbele ya haki. Mimi nina hakika Mwenyezi Mungu ni mbora wa kuwalipa watu kwa kadri walivyofanya katika maisha yao ya kidunia na naamini atafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, napenda na mimi kidogo nichangie machache katika Wizara hii. Kimsingi sina tatizo na makadirio haya yaliyowasilishwa kwa sababu na mimi lazima niseme kuwa napongeza sana kazi zinazofanywa na Viongozi wote wa Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa kaka yangu Waziri Omar Ramadhan Mapuri, Mheshimiwa *Capt*. John Z. Chiligati na wenzake wote, kwa kweli wanafanya kazi kubwa ambayo sisi kama Watanzania tunapaswa kuithamini.

Lakini ningependa nitahadharishe kitu kimoja. Unajua sisi tuna tabia ya kufikiri mambo kinyume na ukweli wenyewe. Haya ni makosa makubwa. Niseme tu kuwa katika nchi yetu kwa mfano labda tuna Vyama Vingi vya Siasa. Hivi Vyama vimeundwa na wafuasi wake ni watu, sio wanyama. Si Vyama vya Nyani kabisa wala si vya Simba, ni vya watu na kwa msingi huo watu wote walioko katika nchi hii wengi wao watakuwa wanaunga mkono hivi Vyama, ama kwa siri au kwa dhahiri.

Nasema hili nikiamini kabisa katika nafsi yangu kuwa hata hawa Askari ambao tunasema sisi hawana Chama, sio kweli wanaamini juu ya Vyama fulani vya Siasa. Lakini hilo, linatakiwa liwe ndani ya nyoyo zao na lisionekane katika matendo yao. Kwa msingi huo basi, napenda niseme kuwa sisi wanasiasa tuwe waangalifu sana katika kuwaingiza vijana wetu hawa ambao wanafanya kazi nzuri katika mambo ambayo yanaweza yakawaletea matatizo na wakatuhumiwa kuwa wanafanya mambo kinyume na maadili yao ya kazi. *(Makofi)*

Kule Pemba, katika uandikishaji wa kura, bahati nzuri siye ndiyo tulianza kule Pemba katika sehemu ya Zanzibar. Tulianza Kusini Pemba. Kazi nzuri kabisa ilikuwa inafanywa na Askari na napenda nitumie fursa hii kumpongeza sana Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kusini Pemba, *SSP* Faraji Kayuga ambaye ndiye *RPC* kule.

Alifanya kazi nzuri tu ya kusimamia mambo haya na kwa kweli Mheshimiwa Waziri mwenyewe baada ya kutokea matatizo machache ya kibinadamu au ya kikazi, Waziri mwenyewe alikuja pale na sisi tulipokutana naye tulimwambia shukrani zetu juu ya kazi nzuri iliyofanywa na Kamanda yule. Mimi siamini kama yule Kamanda na yeye

haamini juu ya Chama cha Siasa. Siamini! Lakini kazi yake ilikuwa haithibitiki. Hivyo, nasema kwa sababu sisi wanasiasa mara nyingine tunakuwa tuna matatizo.

Kule Pemba kabla ya uandikishaji ulifanywa Mkutano wa kuwahamasisha watu waende wakajiandikishe. Bahati mbaya lugha zilizotumika pale, walizozitumia wanasiasa, zilisaidia kwa kiasi fulani kuharibu uandikishaji ule na kama ingelikuwa si umadhubuti wa Makamanda wale wa Polisi waliokuwepo pale, pengine tungekuwa na hali mbaya. Sasa hapa nasema, tusifanye vitendo sisi wanasiasa vya kuwaingiza Askari katika matatizo. Tuwaache kama wanaamini wawe wanaamini wenyewe tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo ningependa niseme ni suala zima la maslahi ya Askari. Askari Polisi mimi naamini ni miongoni mwa Watumishi wenye kufanya kazi nzito kuliko angeweza kufanya mtu mwingine yoyote. Moja katika kitu muhimu sana katika maisha ya binadamu yeyote ni usingizi. Askari Polisi anaweza kuripoti kazini saa 12.00 ya jioni akatakiwa aondoke ama saa 6.00 ya usiku au pengine saa 12.00 ya asubuhi. Hakulala kijana huyu!

Akirudi nyumbani kuna masuala ya maisha na kijiwe yanamsubiri, hatolala! Jioni atakwenda tena kazini. Sasa kazi zao hawa watu ni nzito! Kwa hiyo, lazima maslahi yao tuyatizame ili kuhakikisha kuwa wanaweza kuishi bila ya manung'uniko. Vinginevyo, tutawaingiza katika mtego mbaya tu. Mtego ama wa kuomba, mtego ama wa kuchukua rushwa, mtego ama wa kufanya vitu visivyokuwa vya maadili kwa sababu hatuwalipi malipo yanayofanya waweze kuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msemaji Mkuu wa Upinzani hapa ametaja Sh.80,000/=. *Yes!* ukizitaja, kwa sababu kuna mtu analipwa Sh.50,000/= ni pesa nyingi, lakini katika suala zima la maisha ya kila siku ya Askari, hii pesa ni kidogo na ningeomba sana Serikali itupie sana macho jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda nizungumzie suala la Askari wanaostaafu na wanaofariki dunia, imekuwa ni balaa. Mfano, mwanamke amepoteza mumewe kaachiwa watoto sita, pia kuna mama wa Marehemu anamtazama, pengine kuna baba wa Marehemu ni mnyonge alikuwa akipelekewa angalau *kivunge* cha sukari na mwanawe sasa ameondoka ghafla, basi hata kile kidogo kinachopatikana ni kwa nini kinakuwa na usumbufu wa namna hiyo? Nenda rudi, nenda rudi, chukua *cheque*, *cheque* haijawa *endorsed! Just a very, very long process* ambayo ina usumbufu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Waziri pamoja na Naibu wake, pamoja na kuwa hii kazi ndiyo tunaimaliza hivi, kwa sababu huu ni Mkutano wetu wa mwisho wa Bunge hili, Mungu ajaalie turudi. Lakini watumie fursa hii kuwaeleza au kuwasimamia

wale Watendaji ambao mie naamini wataendelea kubakia ndani ya Jeshi la Polisi, *unless* patokee mambo mengine makubwa. Hili jambo walirahisishe, vinginevyo kutakuwa na manung'uniko yasiyokuwa ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini tunatoa fursa kwa watu kunung'unika kwa jambo ambalo tunaweza kulifanya? Kama mtu amekufa una-*compute* mafao yake, unayapeleka kwa *cheque*, unai-*endorse,* unamwambia tu Meneja wa Benki: "Ikija *cheque* hiyo katika Mkoa wa Kaskazini Pemba mlipe huyo."

Kuna tatizo gani jamani mpaka watu waende huku, warudi kule au wapewe hati za mahakama? Hizo hati za mahakama zenyewe zipate *endorsement* kubwa kubwa. *Endorsement* kubwa ilikuwa ni kile kifo, kilishatokea na sidhani kama mie Khalifa ninaweza kuja kusema ni mrithi wa Juma Kombo wakati hanihusu, sidhani kama hilo linawezekana! Tujitahidi juu ya jambo hili, tunasababisha malalamiko ambayo si ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu nizungumze kuhusu *passport.* Ninatumia fursa hii kumwomba kaka yangu Mheshimiwa Mapuri, jambo alilolifanya ni zuri, lakini watu hawajalielewa na Mheshimiwa Mapuri ana bahati mbaya akifanya vitu mara nyingine watu wanasema: "Kwa sababu ni Mapuri na ni Katibu Mwenezi wa CCM." Nimepata dhana kwa nini amefanya hivyo…

**MWENYEKITI:** Ungetumia Waziri wa Mambo ya Ndani, siyo Katibu Mwenezi wa CCM.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najua. Ninalisema hilo kwa nia safi kabisa, si kwa maana nyingine yoyote, lakini ninakusudia ile *perception* ya watu waliyonayo ambayo sio nzuri mara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikwenda kumpeleka mtoto wangu kutayarisha *passport* pale Dar es Salaam anataka kwenda kusoma. Mambo yote yakafanywa, taratibu za kujaza fomu, picha na nini na nini, lakini katika dakika ya mwisho sasa tunakwenda kumchukulia ile *passport*, Mkurugenzi wa *Passport* akasema: "Hapa kuna tatizo." Nikauliza: "Tatizo gani tena jamani?" Mkurugenzi akaniambia: "Mheshimiwa, hapa tumepata agizo la Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani kuwa wale wanaotoka Zanzibar wakaombe *passport* Zanzibar."

Najua ni kwa nini imefanywa hivyo. Ni kwa sababu siku hizi katika kuomba *passport* ni lazima watu wathibitishe kuwa wewe kweli ni Mtanzania na Mzanzibari kwa sababu umezaliwa pale, umeandikishiwa cheti pale na mambo mengine yote ni rahisi

kupata hiyo *documentation* ika-*substantiate* kuwa wewe unastahili kupewa *passport*. Naamini dhana ilikuwa ni hiyo, sidhani kama kulikuwa na dhana nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini watu hawajui hivyo, wanaona hii ni *maginalisation*, watu wa Zanzibar hawatakiwi kupewa *passport* Bara. Mimi nimepewa *passport*, mimi ni Mbunge na nimezaliwa Pemba, lakini nina *passport* iliyoandikwa hapa hapa Bara. Mke wangu mie mwenyewe nimemchukulia *passport* hapa Bara, lakini pengine ni kwa sababu ya hiyo *umbrella* ya Ubunge wangu. Mtu wa kawaida atapata taabu. Ni vizuri basi *publicity* juu ya jambo hili ikafanywa ili watu wakaelewa kuwa dhana ni nzuri, sio mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika suala la *passport* zenyewe. *Passport* ni ghali. Ni lazima tukubali, pamoja na kuwa kuna *computerization* imefanywa, kuna mambo mengi , lakini *passport* ni ghali. Ni lazima Serikali i-*subsidize* katika suala hili ili Watanzania kwa sababu hii ni haki yao waweze kulipa fedha kidogo wapate *passport*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, nizungumzie suala la Magereza. Tumepitisha sheria hapa kuwa makosa madogo madogo watu watafungwa huko Mitaani, watafungwa wakiwa nje, lakini bado kuna msongamano Magerezani. Ni lazima hili jambo Viongozi wa Wizara hii waongeze juhudi. Ninaamini wamepiga hatua fulani, lakini waongeze juhudi ili kuhakikisha kuwa tunafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapa pia napenda nishauri. Katika Magereza ya wenzetu wale wafungwa pamoja na kuwa wamefungwa, lakini wanapomaliza vifungo vyao wanakuwa na faida. Kwa nini hatuwezi kubadilisha huu mtindo? Sasa hivi kuna Makampuni mengi tu yanahitaji nguvukazi. Ni kwa nini wafungwa hawapelekwi kwenda kufanya kazi za nje chini ya usimamizi wa Magereza yao ili kile kinachozalishwa na wao asilimia fulani wakawekewa Benki? Mtu anafungwa miaka 10 anakwenda kuanza maisha mapya!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anaonaje kama mfungwa huyu akitoka kuwe kuna kitu kidogo alichowekewa? *At least* anaweza kuona kuwa pamoja na kuwa mie nimekosa uhuru baada ya kuiba kuku nikafungwa muda wa miaka mitano, lakini sasa hizi pesa nilizopata naweza kununua kuku 20 na mie nikafuga wangu nisiibe.

Lakini sasa inakuwa ni kufungwa, ni kulima, ni kulala chini, ni kuvaa hizo nguo zinazoitwa sare, dongo tupu, balaa! Nafikiri tungebadilika tukawa na ubinadamu kidogo na tukawaona hawa watu kuwa tunawafunga kwa sababu imelazimika kufungwa, lakini wasitulaumu kila mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niseme tu kwamba, naanza kushtuka ninapomwona Kamanda mkubwa tu wa Jeshi la Polisi anasimamia Uchaguzi wa Chama fulani cha Siasa, tena Uchaguzi wa Chama ndani ya Chama. Naanza kupata mashaka ya *impartiality* ya Kamanda huyu kwa watu wa Vyama vingine kuwa siyo kuwa wa kile Chama alichokisimamia. Hata kama unafanya, *does it need any publicity that everyone in Tanzania should know that! It's embarrassing.* Tujiweke kando kidogo na vitu kama hivi hata kama tunavipenda. Ni kwa nini tuvipende mpaka tuonekane tunavipenda? Unaweza kupenda kwa siri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, napenda niwashukuru Makamanda wa Polisi Makao Makuu. Makamanda hawa wamekuwa hawana ubaguzi wa namna yoyote kwa mtu yoyote anapokwenda Ofisini kwao. Pongezi maalum napenda nimpe Kamanda Mwansasu ambaye mara nyingi ndiyo anapokea watu kwa niaba ya *IGP*.

Kwa kweli amekuwa akitupokea, akitusikiliza, akitusaidia, akituelekeza na ninaomba Makamanda hawa waendelee na mtindo huu ili nchi yetu ionekane ina Vyama vingi vya Siasa, lakini Watanzania wote ni wamoja ambapo kila mmoja anajali matatizo ya mwenzake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naomba pesa hizi wapewe na ninawashauri Wabunge wenzangu wawaruhusu wapewe hizi pesa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniruhusu ili niwe mmojawapo wa kuchangia hoja hii. Lakini kabla sijachangia hoja hii nitoe pole kwa wafiwa wote wa Wabunge wenzetu na Mwenyezi Mungu aziweke mahali pema roho za Marehemu hao. Amin.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Jakaya Kikwete pamoja na Dr. Ali Shein kwa kuchaguliwa kugombea nafasi ya Urais kwa tiketi ya CCM na watapata ushindi wa kishindo. Vile vile, nimpongeze Rais wa Zanzibar kwa kuteuliwa tena kuwa Mgombea wa Urais huko Zanzibar na *inshallah* atapata ushindi mkubwa tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijachangia, nitoe pongezi kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Naibu wake, Katibu Mkuu pamoja na wataalam wote kwa jinsi walivyoleta hoja hizi na hotuba nzuri hapa ambapo sina shaka kwamba kwa kila atakayesimama atakuwa anaboresha tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza kuzungumzia *passport* ambayo inasemekana kwamba ni ghali sana kwa Sh.50,000/=. Mimi niko kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge na sisi tuliwahi kuhoji na tukataka *passport* angalau iwe ni

Sh.20,000/=, lakini baada ya kufika kule tu na kuona vyombo vinavyofanya kazi kwamba ni vya kisasa kabisa tukawa hatuna hoja.

Hoja ilimalizika pale tulipoambiwa kwamba kuna *passport* ambazo wananchi wanaofanya biashara kwa kwenda Uganda, Kenya na wao kuja hapa Tanzania wamepunguziwa kuwa Sh.10,000=. Ukitazama hivi sasa kwa ujirani wetu na Muungano wetu wa Afrika Mashariki, utakuta wananchi wa kawaida wengi wanakwenda Kenya na Uganda na wao ndiyo wamewekewa *passport* za hali ya chini ya Sh.10,000/=. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama suala hili, wengi wanaokwenda nje ni wale raia ambao wana uwezo mkubwa, kuanzia Wabunge na kuendelea na wale wanaofanya biashara za juu. Kwa hiyo, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge tukawa hatuna hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, nichangie kuhusu ndugu yetu wa Kambi ya Upinzani alivyotoa hoja yake kusema kwamba Askari wasijiegeshe upande wa Vyama. Lakini akumbuke kwamba kuna kiapo cha utii. Ukishaapa kiapo cha utii, yule aliye madarakani ni lazima umfuate na ulinde Serikali iliyopo. Hivi ndivyo ninavyojua.

Hata sisi Wabunge tunaapishwa, kwa hiyo, tunayoyasema yote tunahakikisha ni kweli. Hivyo, ninaamini kwamba, Maaskari hawapo kwenye Vyama na kama wako kwenye Vyama wana upenzi wa ndani kwa ndani, lakini wanakumbuka kwamba kuna kiapo cha utii. Ni lazima waitii Serikali iliyopo madarakani pamoja na Chama chake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kwamba, kwanza ninamshukuru ndugu yangu aliyeondoka sasa hivi, Mheshimiwa Khalifa kwa kusema kwamba Viongozi *wasishadidie* kutoa lugha chafu wakati wa uchaguzi. Nilimwona kidogo kabanabana, ni kwamba hakutaja Viongozi wa aina gani wala wa Chama gani. Kwa hiyo, ninaamini kwamba kavitaka Vyama vyote visitoe kauli mbaya na mie natoa wito vile vile Vyama vyote visitoe kauli mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Khalifa alisema kwamba, kuna Viongozi wanasimamia Uchaguzi wa Vyama. Hakuainisha Uchaguzi wa Vyama gani, aidha *CUF* au vipi, lakini katika uchaguzi wa Chama tuliomaliza juzi sisi wana-CCM na tukawateua wale waliogombea kama Mheshimiwa Jakaya Kikwete, sikuwaona Makamanda kuja pale. Hakusema uchaguzi gani, kabana, ilikuwa atueleze ili tujue namna ya kujibu na huyo anayekuja kujibu Waziri ajue namna ya kuchambua. Kwa hiyo, hapa alivyotubania hatuwezi kusema mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda kuzungumzia kuhusu Jeshi letu la Polisi au Jeshi la aina yoyote. Kwanza, napenda kuongelea kuhusu Askari wetu wanaokwenda

kuchukua mafunzo. Wengine wanachukua mafunzo bado miezi sita tu kustaafu Jeshi la Polisi. Lakini wakishastaafu wanakaa kwa muda mrefu sana hawapati fedha zao, wanapata kwa ile *rank* ambayo wameendea mafunzo na wengine mafao yao yanapotea kabisa. Lakini wengine wanakwenda mafunzo halafu wakirudi wanakaa zaidi ya mwaka mmoja hawajapata mafao yao. Kwa hiyo, ninaomba tu Wizara ijiweke tayari kwa mambo haya ili Askari wetu, vijana wetu kama wanavyotufurahisha na kazi zao nzuri nao wafurahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, napenda kuzungumzia upande wa makambi. Ninavyofahamu, Askari yeyote Kambi ni jambo la lazima na Kambi ni jambo ambalo linaweka ukakamavu wa Uaskari. Kambi ina faida tatu. Faida ya kwanza kabisa ni kwamba, dhana ile inayosema kuwa Askari saa 24, 48, 96 au muda wote yuko kazini inakamilika kwa sababu ukiwa kwenye Kambi tu, moja kwa moja wewe unajihesabu uko kazini. Likitokea lolote pale, kikipulizwa kipenga unafika haraka panapohusika na wakati huo familia yako yote iko Kambini na ukifanya lolote unajua mimi niko Kambini na familia yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala lingine ni kwamba, anakuwa *standby*. Akiwa *standby* na nyumba yake iko mbali anapata mashaka makubwa sana, lakini ikiwa nyumba yake iko pale pale na yuko *standby* pale pale hana matatizo. Kuna *standby* za aina mbili. *Standby* moja kubwa ni kama Serikali ina jambo fulani, aidha, uandikishaji au Uchaguzi Mkuu inabidi Askari saa 24 awe pale pale, lakini Askari yule kama hana nyumba pale Kambini nyumba yake ipo maili tatu au sita utakuta ile dhana ya Askari kwamba saa 24 yuko kazini inapotea. Kwa hiyo, kwa makusudi Wabunge tusimamie suala hili ili tuhakikishe Askari wetu wote wako Kambini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni *discipline*. Askari akiwa Kambini nidhamu yake inakamilika kabisa. Leo ndugu zetu wote wanaoandikisha Jeshi la aina yoyote lile wanaandikisha kuanzia miaka 18 mpaka 22. Lakini wanakaa mafunzo kwa muda wa miezi sita tu. Wakitoka, hawako Kambini wanaingia kwenye nyumba za kiraia aidha, miaka 12 au 18 anakwenda uraiani na anakuwa na fikra za kiraia.

Lakini kutokana na hali ya nchi yetu inavyokwenda au ulimwengu mzima unavyokwenda, Askari ni lazima wawe mahali pamoja. Tumesikia jana tu yaliyotokea Uingereza, Mungu pishia mbali kama yakitokea, hapa hata tukiwakusanya Askari tutakuwa tumechelewa, ni lazima Askari wetu wakae sehemu moja ili tuwapate kirahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa Askari. Siku aliyouawa Mheshimiwa Karume nilikuwa nje. Wakati najiandaa kwenda Kambini, mama watoto akaniambia: “Aaah usiende, ndani nitakuwa peke yangu, utakwenda kufa.” Nikamwambia: “Leo ndiyo siku ya kufa kama nimeandikiwa.” Lakini mwenye nyumba anasema: “Baba nenda katulinde.”

Kwa hiyo, Askari aliye mwoga hatoki kabisa kwenda Kambini na kwa kusema kweli Askari kadhaa kwa siku ile hawakufika mpaka siku ya tatu walivyoona kwamba

kuna hali ya usalama ndiyo wakaanza kujipenyeza. Kwa hiyo, hili suala la Kambi sina shaka nimelichambua vizuri tu. Kwa yule ambaye hajui faida za Kambi ataijua sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa wahamiaji pamoja na wakimbizi ni kwamba tumefanya ziara mbalimbali, lakini la kusikitisha ni kuwa sehemu za mipakani kuna baadhi ya sehemu hata pikipiki za kufanyia kazi hakuna. Haya si makosa ya Maofisa wetu au Mawaziri wetu wa Wizara hii, isipokuwa ni makosa yetu sisi pamoja na Serikali yetu. Kuna haja ya kufanya juhudi za makusudi ili zile sehemu nyeti zipate vifaa vya kutumia ili wakati ukifika watumie kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, kutokana na hotuba hii safi ambayo inatia moyo, kila mmoja atakayesimama atakuwa anaiboresha tu. Lakini nisiwe mwizi wa fadhila, ni lazima nizidi kuipongeza na hasa kwa vile vifaa ambavyo vimepatikana Tuliona sehemu ya *passport*, tukatembelea sehemu za alama za vidole, tukaona ni namna gani utaalam wa sasa unavyofanyika, lakini hapo hapo tukaondoka tukatembea tukaenda sehemu moja ambayo kuna mambo ya teknolojia.

Mfano wewe umekaa chumbani, lakini yanayofanyika huko nje yanaonekana. Kwa hiyo, kama alivyosema Msemaji wetu wa Kambi ya Upinzani, tuboreshe magari ambayo yanaweza kutoa misaada mbalimbali kufanikisha dhamira zilizokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tunaloomba zaidi ni kwamba Askari wetu wa usalama barabarani *(traffic)* wapatiwe *vipando*. Wawe na *nine, nine* zao, wawe na mapikipiki yao na tuhakikishe kwamba masaa 24 mafuta yamo ya kutosha. Askari wetu wakiwa na nyenzo na wakawa wanazitumia kama inavyotakiwa hata hao wananchi na watoto wadogo huwa wana-*admire* sana uaskari.

Lakini sasa hivi imefika wakati Askari anaadhirika, anasimamisha gari inapita kwa juu anaitazama tu hivi hivi! Enzi zetu sisi tunachukua pikipiki, tunasimama na pikipiki yetu tunaiweka pembeni, nilikuwa *traffic* mimi, hatui-*off*, pikipiki inaunguruma *tam tam tam!*. Sasa kama kuna wananchi pale, wanasema hii ndiyo kazi! Tunataka Jeshi la Polisi liende hivyo kwa sababu ndiyo uti wa mgongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi hivi sasa likitokea lolote pawe na Askari kumi tu *wallahi* tutakwenda kukaa foleni nyuma yao ili watulinde na hawana chochote, lakini tunaamini watatulinda. Ni lazima tuwatunze Askari wetu, tuwatunze vijana wetu na jambo moja la kuwatunza ni kuwapatia nyenzo, wakiingia mahali waji-*proud,* mtu anajitambua kwamba mimi ni Askari. Anaweka pikipiki inafanya kazi, anaicheki gari, gari kama haisimami anaifukuza, jeuri zake akiishaifukuza anaipita kiasi maguzo matatu halafu anarudia tena, akirudia anapiga msererekо aaaaaa, ndiyo uaskari unavyofanyika. *(Kicheko/Makofi)*

Lakini leo imefika wakati Askari anaisimamisha gari ana-*off* mafuta yasiishe, *what is that!* Kwa hiyo, ni lazima twende kileo, ni lazima twende na wakati, tutake tusikate. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jakaya Kikwete akikaa madarakani tunamwomba kwamba jambo la kwanza kabisa iwe ni kuvitazama vyombo vya Jeshi la Ulinzi ili viende vizuri na sisi tulale usingizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nizungumze kwa ufupi juu ya Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwanza nianze kwa kuwapongeza Waziri na timu yake yote na Watendaji wa Polisi kwa kazi nzuri wanayoifanya ingawa kuna kasoro hapa na pale ambazo hapo mbeleni nitazisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli sasa hivi kazi inaonekana na tunapata taarifa na tunajionea kwamba sasa hivi Jeshi letu la Polisi kutokana na Serikali kulipatia fedha limeanza kuonyesha jitihada kubwa na hata majambazi wameanza kuogopa na kurudi nyuma. Tunaomba waendelee hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na ujenzi wa nyumba za Polisi. Kwa kweli tunashukuru, tumeona maeneo mengi wamejenga nyumba pamoja na kwamba hazitoshelezi, tunaiomba Serikali iendelee kuongeza fedha ili Askari wote wapate nyumba za kuishi. Pamoja na kujenga nyumba mpya, kinachosikitisha zaidi ni zile nyumba za zamani, hazitengenezwi! Nyingi ziko kwenye hali mbaya! Kwa hiyo, nawaomba sana pamoja na kujenga nyumba mpya, waendelee kutengeneza na zile za zamani ili Askari wanaokaa mle nao wajisikie kwamba wanaguswa na fedha inayotolewa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, tunaomba hizi fedha zinazotolewa, basi zisambae, zisiwe zinajenga mahali fulani fulani tu. Hizi fedha ziende na kule Wilayani zijenge nyumba, maana Askari anayekaa Dar es Salaam, Dodoma au hata kule kwangu Matongo wana hadhi moja na wao wakumbukwe kujengewa hizo nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia vitendea kazi iwe ni hivyo hivyo, visambazwe kwa wote na Askari walio na kazi kubwa zaidi ni pamoja na wale wanaokaa Vijijini, lakini vitendea kazi havitoshi kabisa. Vituo vingi havina *radio calls,* Vituo vingi havina vitendea kazi vingine vya lazima. Kwa hiyo, ninawaomba tu wasambaze ili mawasiliano na utendaji wa kazi uende vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nakumbuka nilizungumza na nikaomba kwamba kwa kuwa Jimbo la Iramba Mashariki liko mbali na Makao Makuu ya Wilaya na kuna Kituo cha Polisi Nduguti ambacho wamepanga kwenye nyumba za wenyeji na hicho Kituo ndiyo kikubwa na kiko katikati ya Jimbo la Iramba Mashariki, niliomba pale pajengwe Kituo cha kudumu na nyumba za Askari zijengwe.

Vile vile, naomba wapate usafiri kwa sababu watu wa Iramba Mashariki wanapata taabu sana kwa sababu Makao Makuu ya Polisi yaliyoko Kiomboi yako mbali na usafiri

huwa siyo mzuri.  Bado narudia kuwaomba, basi na Iramba Mashariki tujengewe hicho Kituo kwa faida ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie matatizo kama nilivyosema ya Polisi wachache ambao hawaendani na taratibu za kiaskari.  Kwanza nimpongeze sana Mkuu wa Polisi wa Mkoa wa Singida, kwa kweli toka aingie Singida, Singida imegeuka imekuwa ya amani na utulivu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna kikundi kidogo cha pale pale Mkoani ambacho chenyewe hakifuati mipaka ya kazi yao, wao ndiyo wamekuwa mabwana wakubwa.  Kuna matukio ambayo yametokea, nikaenda kumwuliza *RPC* akasema: "Silijui hili."  Lakini anachukua hatua.  Wao wanatoka Mkoani wanakwenda Wilaya ya Iramba.  Kuna tukio moja walitoka Mkoani bila Wilaya kujua, bila *OCD* kujua, wakaenda kumkamata Mtendaji wa Kijiji cha Dominick.  Hayo ni makosa makubwa na wamemkamata kwa kosa ambalo halikuwepo.

Tajiri mmoja alikuwa analima kule kwenye shamba alilopewa na kile Kijiji, lakini alikuwa halimi muda mrefu, Serikali ya Kijiji ikalichukua lile shamba na kuwagawia Wanakijiji.  Tajiri huyo alizunguka akaenda Mkoani kumweleza Afisa Upelelezi wa Mkoa.  Bila kuulizia tatizo, akaenda kumkamata kijana wa watu bila sababu.

Kwa hiyo, inaumiza sana na bado kikundi kile kile cha Afisa Upelelezi wa Mkoa huyu ambaye nasikia amehamishwa kwenda Wilayani kukamata Watendaji wa Wilaya akiwemo Mkurugenzi wa Wilaya, bila viongozi wake kujua. Hii inachafua sana sifa nzuri ya polisi.

Mimi naomba hili likomeshwe, acha hivyo wateremke maeneo wanayokaa wenzetu Wasukuma, maeneo ya Mtekende, Ndaho, matukio mengi tu yapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba Uongozi wa Polisi Taifa uafuatilie hilo. Sisi tulikuwa na imani, tuna ushirikiano mzuri sana na polisi, tuna ushirikiano mzuri sana na Mkuu wa Polisi. Sasa hawa wachache wanaochafua, sisi tunaomba wachukuliwe hatua. Inakuwaje polisi wanatoka Mkoani wanakwenda Wilayani bila *OCD* kujua, wanakwenda kufanya nini? Hizi kesi zote ukiangalia hakuna kesi, wananchi wanabambikiwa tu ili watolewe upepo. Sisi tunaomba sana hili liishe, hatutaki Jeshi letu la Polisi lichafuliwe.

Mimi nimetoa mfano wa Dominic na mkifuatilia upo na kwa sababu niliandika barua mpaka kwa Naibu Waziri. Huu mfano wa Wilayani upo na hiyo kesi haipo. Kwa hiyo, tunaomba mjitahidi kuwabaini hao watu wachache wanawachafua, muwaondoe na kuwachukulia hatua siyo kuwahamisha. Kumhamisha siyo sababu kwa sababu yale mabaya aliyokuwa anafanya sehemu hiyo, atayapeleka na sehemu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongee kidogo juu hawa askari wetu wa *traffic.* Ni Askari ambao tunawategemea wafanye kazi nzuri na wengi wamekuwa wanafanyakazi nzuri, lakini kuna wachache hawafanyi kazi nzuri. Bado ukienda na basi wanasimama,

wanazunguka na kondakta nyuma, sijui huwa wanaongea nini. Halafu kuna mtindo unaofanyika ule wa kung'oa karatasi za bima na kuchukua leseni ya dereva. Sasa mimi nataka kujua hizi bima zina nini, bima kama imekwisha si mhusika ashitakiwe, kuzing'oa ndiyo sababu? Sisi tunaomba itafute njia nyingine na hawa watu wa Mashirika ya Bima ndiyo wafanye hizo kazi, ni kazi yao. Kwa hiyo, mimi naomba sana haya mambo madogo madogo yaangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije upande wa Magereza, Jimboni kwangu kuna Gereza la Singa. Hili gereza liko Jimboni lakini liko chini ya Mkoa linaangaliwa na Mkoa wa Singida. Tulishaomba kwa nini liangaliwe na Singida kwa nini lisiwe chini ya Iramba?

Mimi naomba nipate majibu. Halafu bado lile Gereza lina hali mbaya sana, halina vitendea kazi, hata wafungwa walioko pale na askari hali zao ni mbaya vile vile. Walikuwa na matrekta kule nyuma sasa hivi hawana trekta na lile shamba siku hizi hawalimi.

Mimi naomba sana Mkuu wa Magereza, wana shamba zuri sana hapa tunaomba wapewe vitendea kazi na lile shamba lianze kulimwa kwa faida ya Magereza na askari pamoja na raia walioko pale. Kwa kweli wamekuwa wanatoa msaada mkubwa sana. Ng'ombe wanaibiwa wanatusaidia, matatizo yanajitokeza, ni watu ambao wana ushirikiano mzuri sana na wananchi hasa wa Singa na Nkungi ambao wako jirani. Lakini mimi ninalorudia kuomba, naomba sana wapewe vitendea kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimalizie kwa kuwaomba tu pale ahadi inapotolewa basi itekelezwe na hasa vile Vituo vya Polisi vilivyoko Vijijini. Mimi najua kwa Mijini hakuna tatizo. Upande wa Iramba ya Mashariki sasa hivi yameagizwa magari mengi ya polisi, kila *OCD* atapata na wapelelezi basi yale ya zamani tutengenezeeni hata gari moja liende Nduguti ili liwe linahudumia Iramba Mashariki yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, mimi naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja hii muhimu katika usalama wa Taifa letu. Lakini kwanza kabisa nianze kwa kuwashukuru sana Waziri mwenyewe, Naibu wake, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara. Lakini pia tuwashukuru rasmi *IGP,* Makamishna wake na Mkurugenzi wa Uhamiaji kwa kazi nzuri waliyofanya. Mimi nadhani naunga mkono moja kwa moja hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ulinzi na usalama ni zito, linahitaji nafasi nzuri ya kujadili. Lakini leo tutajaribu kugusia machache kwa sababu yaliyoandikwa katika hotuba ni mambo muhimu katika maendeleo ya nchi hii.

Mimi ningependa nitumie nafasi hii, kwanza kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, wote walioungana nasi kwa msiba uliotupata Mkoa wa Rukwa, wa kumpoteza mwenzetu Mheshimiwa Margareth Bwana. Tulipata msaada sana kutoka kwenu na sisi

tunataka kuwahakikishia tulikuwa Wabunge nane, sasa tumebaki Wabunge saba. Wenzetu Mkoa wa Rukwa kwa kweli walisikitishwa sana kwa sababu walikuwa wamemchangia Mheshimiwa Margareth Bwana, fedha za kuombea kujazia fomu za kuingia Ubunge kupitia Viti Maalum na kwa kweli imekuwa ni pengo kwao. Tunachoweza kuomba ni Mwenyezi ailaze mahali pema peponi roho ya Marehemu. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya kusema hayo, mafanikio ninayoyaona ndani ya Wizara hii yametokana na juhudi za Rais wetu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kutoa msaada wa dhati kabisa kupitia kwa Mawaziri wao. Lakini mimi nilipata nafasi pia ya kufanya kazi chini ya Mwenyekiti, Mzee John Samwel Malecela, akiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama. Ningependa kwa dhati nimpongeze alivyosimamia Kamati hii na kufanya kazi yake nzuri sana mpaka Majeshi yetu ya Ulinzi na Usalama yamefika hapa yalipo. Ni kazi nzuri. Siwafichi alikuwa halali, tukitoa ushauri anakwenda kutekeleza, anafuatilia mwenyewe. Kwa kweli yote msione yakielea, yamefanyiwa kazi. Napenda kumshukuru Mzee John Malecela, kwa kazi aliyotufanyia. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, mimi nataka kwa dhati niwashukuru Makamanda wote wa Polisi na Kamati zote za Ulinzi na Usalama nchini. Jamani amani si jambo la kuchezea, ukiona tumelala na kuamka asubuhi salama, kuna watu wametufikisha hapo. Kuna watu hawalali usiku na mchana kuhakikisha tunalala na kuamka salama. Vyombo vya Polisi vimefanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mimi nataka nimpongeze pia Kamanda wangu wa Mkoa wa Rukwa kwa sababu kwa kipindi chote ukiangalia takwimu za makosa katika Mkoa wa Rukwa, yamepungua sana tangu aingie. Hivyo amefanya kazi nzuri na mimi nadhani tutaendelea katika utaratibu huo na takwimu zote pia ukiangalia katika nchi nzima kwa kweli zimepungua. Mimi nasema ni faraja kubwa waendelee na moyo huo huo na kipindi hiki cha uchaguzi tuna imani sasa watasimama kidete bila kuogopa. Tukianza kufikiria ya kwamba Askari hawa ni wa kutetea Serikali ya Chama cha Mapinduzi, bila kujua ya kwamba nao wana taratibu na sheria zinazowalinda na kuwaongoza katika kazi zao hatufiki mahali popote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, polisi yeyote mahali popote anaendeshwa kwa *Police General Orders* zao. Ukichukua mfano, maandamano yanayofanyika nchi mbalimbali. Maandamano ni haki ya mtu yeyote anaruhusiwa kufanya maandamano kwa sababu nzuri tu. Lakini *General Order* namba 41 kama mnakumbuka inasema, kama polisi atakuwa na wasiwasi ya kwamba hakutakuwa na usalama, sheria hiyo inamruhusu kuzuia maandamano hayo. Ndiyo maana wakati mwingine wanasema polisi wanaingilia, hapana ni sheria zetu wenyewe tumejitungia ili tuhakikishe tunaishi kwa usalama na amani katika nchi yetu.

Mimi nadhani wasiogope kwa sababu sheria hazijabadilika bado ziko pale pale. Mtu kama anaandamana kwa amani polisi hawatamfanya lolote tena watamsaidia kuhakikisha maandamano yanakwisha vizuri. Lakini akiandamana kwa shari

watapambana nao na mimi nadhani waendelee bila kuogopa ndiyo njia peke yake ya kusaidia kulinda nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa kipindi kirefu katika Halmashauri yetu ya mji ambao sasa umekuwa Manispaa, nimekuwa kila wakati nikiomba Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza, letu lisaidie kuangalia Mkoa wa Rukwa na hasa Mji wa Sumbawanga, Ofisi yetu ya *OCD* Sumbawanga ni ile iliyojengwa wakati wa ukoloni nu aibu. Ukiangalia mahabusu ya Sumbawanga ni ya wakati wa ukoloni ambao ilikuwa kwa ajili ya watu kama 10, 20 sasa watu mpaka 300. Hakuna jitihada inavyofanyika kupanua maeneo hayo. Hivi tumekosa nini Rukwa? Ningependa kupata maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikilalamika kila wakati ya kwamba ni vizuri tukaangalia hali ya nyumba za askari wetu, tukaangalia hali ya maslahi ya askari wetu na tukaangalia elimu na afya zao. Ningeomba sana hayo yaangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua Gereza lenyewe la Moro kwa kweli ukiangalia hali yake si nzuri hata kidogo, wamezungusha *fence* tu na mabati yamezunguka. Sehemu ile ina baridi kubwa. Kamati zetu za Ulinzi na Usalama ziliwahi kupata nafasi kutembelea baadhi ya Magereza. Tukadhani vizuri tukatembea na kuangalia baadhi ya maeneo haya ili tusionekani sisi ni wabishi tu. Lakini tunataka haki itendeke kwa sababu mfungwa anapofungwa siyo apate adhabu nyingine ya kukosa hata mahali pa kukaa. Hayo nilidhani yazingatiwe kwa sababu yamekuwa ni kero katika eneo letu. Sumbawanga sasa ni Manispaa na kama Manispaa tunadhani mazingira yake lazima yalingane na Manispaa yenyewe ya Sumbawanga. Tunaomba msaada wa Wizara hii inayohusika iangalie sasa upya namna ya kuboresha ujengaji wa ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona katika taarifa iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri, kuna baadhi ya maeneo yatajengewa Ofisi lakini Sumbawanga haimo tupate maelezo, sababu ipi wakati ndiyo Makao Makuu ya Mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo naomba nipate msaada ni suala zima ambalo linahusiana na elimu kwa polisi. Polisi mahali popote katika ulimwengu ambao tunaendelea hivi sasa lazima tujitahidi kuwapa elimu ili waweze kupambana na mazingira tunayokwenda nayo kwa hivi sasa. Nitachukua mfano mahali kama nchi ya Nigeria, hakuna mahali ambapo watu wanakimbilia kuingia kama Polisi na Majeshi. Wataalam wengi sana wenye kisomo ndiyo wanakimbilia kwenda huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini wanafuata, wanafuata kwanza maslahi yao ni mazuri zaidi. Maslahi ni mazuri kwa sababu vyombo hivi vya ulinzi na usalama lazima wahakikishe vinaishi kwa hali nzuri zaidi ama sivyo vinaweza kuwa ni sehemu ya vichaka vya wahuni. Maslahi yaangaliwe kwa undani. Tuna imani kabisa jitihada ambazo zimeanza za Jeshi la Polisi, kuwapeleka mpaka nje Marekani ziendelezwe kwa ngazi mbalimbali. Nimeona askari wengine wanasota wanakaa miaka 20 bado wanaitwa ma-*private* tu. Hivi kuna nini, tatizo ni ufinyu wa fedha au tatizo ni nini? Lazima tuwasaidie wapate elimu zaidi ili waweze kufanya kazi yao vizuri na pia kupata morari ya kuendelea kufanya kazi yao, hilo ni lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda kuishukuru Serikali kupitia Wizara hii ya kwamba sasa Mji wetu wa Sumbawanga utapata gari la zimamoto. Mimi nashukuru kwa dhati kwa sababu ni gari ambalo tulikuwa tunategemea katika mji wetu wa Sumbawanga hata Kiwanja cha Ndege hakina gari la zimamoto. Iko *Land Rover* wakati mwingine hata haifanyi kazi vizuri. Lakini huu mwanzo utakuwa ni mzuri kuhamasisha kwa sababu wakazi wa Mji Sumbawanga walikuwa wakilalamika kwa miaka yote kwamba kwa nini hatupati gari la kusaidia ili maafa yanapokuja, yanayotokana na moto yaweze kushughulikiwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia ya leo ni dunia ya kisayansi na kwa ajili ni ya kisayansi lazima tuhakikishe ya kwamba sasa polisi ambao tunawaajiri wanakwenda na mazingira ya kisayansi yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la msingi pia tuwe waangalifu, aina ya polisi tunawaangalia. Hivi wote wamekuwa *vetted* kabla ya kuingia polisi? Kwa nini tusiwe na utaratibu wa kuhakikisha kama tutakuwa na wasiwasi wa baadhi ya polisi ambao wanaingia basi sisi raia tushirikiane na polisi kutoa taarifa ya tabia ya baadhi ya polisi ambao wanaonekana hawafai kabisa kufanya kazi hizo zenye heshima katika nchi hii. Ndiyo maana polisi wanaposema kila wakati isaidie polisi ikusaidie wana maana ya kwamba wewe ukitaka usilalamike ukiwa nje, lalamika kwa kutoa taarifa sahihi kwa vyombo vinavyohusika. Hii ndiyo, itasaidia peke yake kuhakikisha kwamba polisi tuliokuwa nao ni polisi ambao kwa kweli ni wale waliochujwa, wana nidhamu nzuri na pia ni polisi ambao wanaweza wakatufanyia kazi yetu bila malalamiko yoyote. Ningependa hilo liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi hiki ni cha uchaguzi. Kipindi cha uchaguzi ni kipindi ambacho watu wanaweza kubambikizwa kesi za kila namna, kesi za namna ili akitaka kukuondoa katika uongozi anakubambikiza kesi tena karibu na kuchukua fomu. Tungeomba *RPCs, OCDs,* kwa kupitia kwa *IGP* wawe waangalifu, wasije wakafikia mahali fulani baadhi ya Wabunge, wakaanza kubambikizwa kesi ili wang'olewe katika kinyang'anyiro cha Ubunge. Kubambikizwa kesi kuna njia nyingi, mtu anaweza kukutupia hata bangi kwenye gari yako. Ukikutwa na bangi unatiwa ndani. Lakini kweli au anakufanyia makusudi mazima, anakutumia mtu ili mgombane naye anakuchokoza, unamrudishia kofi, unaingia ndani. Ni kipindi ambacho kinaandaliwa makusudi mazima na ni vizuri Waheshimiwa Wabunge mkawa waangalifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunadhani wenzetu upande wa polisi wawe waangalifu ili kesi hizi ambazo zitakuwa za kisiasa waone namna ya kuzishughulikia zisiwe kesi zikaonekana sasa ndiyo zinaanza kutumika katika hali ambayo itakuwa ngumu. *(Makofi)*

Mwisho kuna mambo mawili, la kwanza ni suala zima la kazi nzuri iliyofanyika na magereza. Mimi nadhani tuendelee kujitahidi kusaidia magereza. Magereza tunataka kiwe ni kichocheo cha uzalishaji. Lakini baadhi ya magereza mengine ambayo ni ya kilimo ukiangalia kazi inavyofanyika hivi sasa ni tofauti kabisa na makusudio kwa sababu vitendea kazi havipo na wakati mwingine wanasuasua kutokana na hali halisi ilivyo hivi sasa. Jitihada zimeanza kuonekana, lakini Serikali inaweza kufanya zaidi ili

heshima ya magereza. Magereza yetu ya Tanzania yameheshimika katika Bara la Afrika na yamekuwa ni mfano. Lakini mfano huo usije ukapotea kwa sababu ya upungufu tu wa fedha ambao umejitokeza. Tuwape nyenzo za kufanya kazi ili wafanye majukumu yao kama wanavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria zilizopo hivi sasa ziko nyingi ambazo tunadhani ni vizuri tukazingatia. Zingeweza kupunguza mlundikano ya wafungwa katika Magereza. Moja ni matumizi ya Bodi za *Parole,* ambazo tangu mwaka 1994 tulikuwa tumezianzisha. Lakini pamoja na ufinyu wa Bajeti ningeomba bodi hizi ziimarishwe. Ziimarishwe kwa sababu zitapunguzia haya matatizo makubwa sana ya msongamano wa wafungwa katika magereza yetu. Pia Mabaraza ya Kata hayajafanya kazi yake inavyokusudiwa. Mabaraza haya yangepata nafasi, yakapata msukumo na fedha kidogo na nyenzo yangepunguza pia mzigo mkubwa sana wa kesi nyingine ambazo zinakwenda Mahakama ya Mwanzo bila sababu. Mahakama za Mwanzo, wakati mwingine zinakuwa na kazi nyingi ambazo zingeweza kuhukumiwa katika Mabaraza ya Kata tukamaliza matatizo madogo madogo.

Sasa ni vizuri ikaangaliwa na Wizara tuwasaidie angalau wenzetu hawa, hizi kesi ndogo ndogo wakazimaliza. Naelewa kwamba ziko sheria nyingine hata wafungwa wanapofungwa wenye kesi ndogo ndogo au adhabu ndogo ndogo sheria bado inaruhusu ya kwamba wanaweza kuomba Mahakama wakafungwa nje, badala ya kufungwa ndani. Lakini hayo mengine hayafuatwi kwa sababu wakati mwingine wengine hawajui kinachofanyika.

Mwisho kabisa ni suala la uhamiaji. Nataka nimpongeze Mkurugenzi Mkuu wa Uhamiaji, kwa jitihada alizozifanya hasa kipindi hiki cha kutoa *passport* kimekuwa ni kipindi kigumu. Watu wamejazana sana, lakini bahati mbaya nafasi yenyewe ukiiangalia pale ni ndogo sana kufanya jambo lolote. Nina imani kabisa ni vizuri pakaangaliwa upya ili Uhamiaji wakapata nafasi kubwa. Wakapata nyumba ambayo wanaweza kufanya kazi ambalo litatujengea pia heshima. Ama sivyo tusipoangalia suala hilo tunapata matatizo. Hatujui tunaanzia wapi na tunaishia wapi. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, napenda kusema kwa dhati ya kwamba Mheshimiwa Waziri na Naibu wako mmefanya kazi nzuri. Muendelee na kipindi hiki cha uchaguzi mkae kidete kwa sababu mtatupiwa madongo ya hapa na pale, lakini fuateni sheria na kanuni za nchi. Tutafanikiwa na uchaguzi wetu utakwenda kwa raha na amani na utulivu chini ya usimamizi wenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kusema wazi ya kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie hoja ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, hoja ambayo imewasilishwa kwa ufasaha mkubwa na imetoa mwelekeo wa matumaini makubwa. Kwa hiyo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Kupitia Bunge lako Tukufu naomba tumpe Waziri huyu fedha anazoziomba ili aende akafanye yale aliyoyapanga kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza pia Wizara hasa Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri inayofanya ya kulinda usalama wa raia wa Tanzania. MheshimiwaWaziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakuu wote wa Idara pale ni watu wasikivu, wafuatiliaji wazuri ni wachapakazi. Kwa kweli wanastahili pongezi za Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Kibakwe kulikuwa na Kituo cha Polisi Mtera. Kituo hiki kiutawala kilikuwa kinasimamiwa na *RPC* wa Iringa ingawa chenyewe kiko Dodoma. Hili lilikuwa linaleta kero kubwa kwa wananchi wangu kule Jimboni na baada ya kulifikisha kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, mara moja kituo kile kilihama kutoka Iringa kuja Dodoma na sasa kero hii imekwisha kabisa. Nalipongeza sana Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa kituo hiki kimehamia Mtera pale kijijini, naiomba Wizara hasa Jeshi lenyewe liwasiliane na uongozi wa *TANESCO* waone namna ya kuwasaidia Polisi Mtera kupata jengo la Ofisi. Hivi sasa Mtera *TANESCO* inabomoa, imeacha majengo mengi na haitumii majengo yote pale. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kama *RPC* akiagizwa akawasiliane na viongozi wa Mtera kule wajue mahitaji yao, mimi nina hakika *TANESCO* watatusaidia kupata jengo au maeneo ya kufanyia kazi pale Mtera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Kibakwe kuna Kituo cha Polisi na kwa muda mrefu kituo kile hakikuwa na simu ya redio kwa ajili ya mawasiliano. Naomba kulialifu Bunge lako Tukufu kwamba sasa simu ile tumepata imekwishafungwa na inafanya kazi. Kwa hiyo, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Kibakwe, naomba nimshukuru Mkuu wa Jeshi la Polisi na Wizara kwa ujumla kwa kutimiza ahadi yake. *(Makofi)*

Lakini vile vile nikumbushie ahadi ndogo ambayo Wizara iliahidi hasa kwa kupitia Naibu Waziri ya kuweka umeme kwenye kituo kile. Naibu Waziri, aliagiza wataalam wake walikwenda mpaka Kibakwe, wakafanya tathmini ya gharama za uwekaji umeme pale kituoni Kibakwe, *OCD* akaleta makadirio yake kwa *RPC.* Sasa yalipofika kwa *RPC* nafikiri yalitoweka mitini, toka wakati huo hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naikumbusha Wizara, kwamba ahadi hiyo, ipo na kwa kweli kinachohitajika ni kiasi kidogo sana, mahali kituo kilipo na nguzo za umeme zipo karibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kupitia kwako Wizara ione namna ya kutimiza ahadi ile ili askari wetu pale kituoni wasiendelee kutumia vibatari kwa ajiri ya kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie na jambo moja ambalo linatukera pale katika Jimbo la Kibakwe na ambalo naomba sana Waziri alifanyie utafiti na ikiwezekana alipatie jawabu. Kule Jimboni kukitokea vifo vya kutatanisha yaani kama mtu amejinyonga au ameuwawa na watu wasiojulikana na vifo vya namna hiyo, mwili wa Marehemu hauzikwi mpaka polisi na daktari waitwe kutoka Mpwapwa na ni mwendo mrefu wote tunafahamu. Lakini katika hali ya sasa tunafahamu vile vile kwamba Wilayani pale *OCD* hana gari la kuaminika, kwa hiyo, anasubiri mpaka asaidiwe na

Halmashauri ya Wilaya, ndipo aende kwenye tukio. Hii mara nyingi huchukua siku mbili, hata tatu. Ikishafika siku mbili/tatu, basi mwili wa Marehemu unakuwa umekwishaharibika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu pale Chang'ombe Ikuyu, yalitokea mauaji ya namna hiyo katikati ya barabara, wakati wa masika mwili wa Marehemu pale ulinyeshewa na mvua siku tatu ukisubiri askari na daktari kutoka Mpwapwa. Kwa kweli jambo hili ni la kutisha sana na la kuhuzunisha sana na limeshakuwa ni kero kwa muda mrefu na pengine sasa ni wakati muafaka wa kulipatia jawabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema pale Kibakwe kuna Kituo cha Polisi, pale Kibakwe kuna Kituo cha Afya, kituo ambacho kinaongozwa na *Assistant Medical Officer (AMO)* na daktari. Polisi wanapokuja kutoka Mpwapwa hawaji na daktari kutoka Mpwapwa, wanamtumia daktari huyu huyu aliyoko kwenye Kituo cha Afya Kibakwe. Ninaomba Wizara ione namna ya kuiondoa kero hii, ione namna ya kuondoa urasimu huu ambao kwa kweli umekuwa umekiwasononesha wananchi wa Jimbo langu la Kibakwe. Ili kumruhusu Mkuu wa Kituo cha Polisi Kibakwe na Daktari wa Kituo cha Afya Kibakwe, baada ya kufanya ukaguzi wa yule maiti watoe kibali cha kuzika.

Kwa kuwa Kituo cha Polisi Kibakwe kinatoa huduma kwa Tarafa yote ya Kibakwe na sehemu ya Rudi na kwa kuwa Mkuu wa Kituo cha Polisi pale Kibakwe hana usafiri. Naomba jambo la pili hili Wizara ifikirie na Jeshi la Polisi ifikirie kumpatia chombo cha usafiri huyu Mkuu wa Kituo, naomba sana. Chombo hiki kitamsaidia kufanya kazi yake kwa ufanisi na mimi nasema tukianza na pikipiki ni mwazo mzuri, inatosha kwa kuanzia kwa sababu *OCD* na Afisa Upelelezi wa Wilaya watakapopatiwa magari basi naomba lile gari ambalo litakuwa pale Wilayani likarabatiwe, halina haja ya kurudishwa mahala pengine liweze likasaidia Kituo cha Polisi Kibakwe.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa na maombi, nilikuwa na maombi haya mawili, matatu, si makubwa sana kwa Wizara ambayo ina sifa nyingi katika nchi yetu. Si makubwa sana kwa Waziri na Naibu Waziri ambao ni wachapakazi. Haya mambo ni madogo, sidhani kama yanahitaji kumsumbua sana Mheshimiwa Waziri kutatua tatizo la kuruhusu maiti zizikwe na hili la pili kumpatia Mkuu wa Kituo cha Polisi chombo cha usafiri, pikipiki na baadaye uwezekano ukipatikana gari basi itakuwa tumeshawatendea haki wananchi wa Kibakwe na wataboresha huduma ya Kituo cha Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kama nilivyosema mwanzo, hoja hii haina mgogoro wowote ni hoja ya kuungwa mkono mia kwa mia na mimi naiunga mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi asubuhi hii niweze kuchangia hoja ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri, pia nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wote wa Wizara hii wakiwemo na Mkuu wa Jeshi la Polisi, Kamishna Mkuu wa Magereza, Mkurugenzi wa Uhamiaji na viongozi wengine. *(Makofi)*

Pia napenda nitumie nafasi hii kumpongeza sana Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Dodoma, kwa kazi nzuri ambayo inafanya katika Mkoa wetu kuweka utulivu na amani. Aidha, nisimsahau Kamanda wa Polisi wa Wilaya ya Kondoa kwa jitihada kubwa ambazo anafanya kuweka Wilaya yetu katika hali ya amani na utulivu mkubwa. Hawa wote nawapongeza na nawashukuru sana kwa kazi nzuri ambayo wamefanya katika suala hili la ulinzi wa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo pia niungane na wachangiaji walionitangulia kuwapongeza kwa michango yao mizuri na mimi sipendi kurudia rudia yale ambayo wamechangia. Mengi ambayo nilitaka kuchangia yamekwishachangiwa. Mimi nitajielekeza katika kero moja tu ya Wilaya ya Kondoa na inawezekana pia ni kero kwa nchi nzima. Kero hiyo ambayo napenda niizungumzie hapa kwa kina inahusu namna ya kuwashughulikia watuhumiwa na namna ya kuendesha kesi katika Mahakama zetu. Hiyo ndiyo kero ambayo nataka niizungumzie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utawala Bora ni pamoja na wananchi kupata haki zao kwa gharama nafuu pindi wanapoleka malalamiko hayo Mahakamani. Hiyo ndiyo tungetegemea kwamba Mtanzania yeyote ambaye ana malalamiko akienda Mahakamani aendeshe kesi ama malalamiko yake kwa gharama nafuu ili aweze kupata haki yake. Lakini hali ilivyo katika nchi yetu siyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania walio wengi wameshindwa kupata haki pindi wanapopeleka malalamiko yao Mahakamani katika Mahakama zetu za Tanzania kutokana na jambo moja, gharama. Gharama ambazo wanaingia walalamikaji ni kubwa na nyingi sana na wengi wa Watanzania wanashindwa kuendesha ama kuwafikisha watuhumiwa wao Mahakamani na kuendesha kesi. Sasa ningependa nizitaje hizo gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Wilaya ya Kondoa kwa kweli na hasa wapiga kura wangu walikuwa wananilalamikia mara nyingi kwamba hizo gharama ndiyo zinawafanya wasipate haki kutoka Mahakama za nchi hii kwa sababu wameshindwa kulipia hizo gharama na leo nimepata nafasi hii niweze kufikisha malalamiko hayo kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa niaba ya Serikali yetu na naomba Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ayanukuu vizuri na kuangalia namna ya kuweza kutatua gharama hizi ama kuondoa gharama hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama ambazo wapiga kura wangu wanazilalamikia hasa wakati wa kuendesha kesi na kuwashughulikia watuhumiwa ni kama zifuatavyo:-

Moja, ni gharama ya kumkamata mtuhumiwa. Hivi sasa katika nchi yetu hasa vijijini hatuna utaratibu unaofahamika wa kumkamata mtuhumiwa pindi mlalamikaji anapokwenda kwenye dola kumlalamikia mtuhumiwa anatakiwa atoe pesa ama alipie

gharama ya mgambo kwenda kumchukua mtuhumiwa wake, kama huna pesa hiyo maana yake ni kwamba huyo mtuhumiwa wako hawezi kufikishwa kwenye vyombo vya dola. Kwa hiyo, utakosa haki yako.

Gharama ya pili ambayo wapiga kura wangu wa Kondoa Kusini wanalalamikia ni suala la kulisha chakula kwenye mahabusu, endapo una uwezo wa kumkamata mtuhumiwa wako na ukamfikisha mahabusu ya Kijiji ama ya Kata ni wajibu wako wewe mlalamikaji kumlisha mpaka kesi inapokwisha. Sasa sina uhakika wangapi, Watanzania wangapi wana uwezo huo. Kwa hiyo, hii ni gharama mojawapo ambayo wapiga kura wangu wanalalamikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama ya tatu ambayo inalalamikiwa pia wakati wa kuwashughulikia watuhumiwa ni gharama ya ulinzi wa mahabusu. Kwa kuwa Serikali haina walinzi wa mahabusu katika ngazi ya kijiji na hata katika ngazi ya Kata, mlalamikaji anawajibika kutoa gharama ama kumweka mlinzi wa kuweza kumlinda mtuhumiwa wake mpaka kesi inapokwisha ama mpaka anapohamishwa kutoka mahabusu inayohusika na kwenda labda mahabusu katika Gereza la Wilaya hapo ndiyo utakuwa umepona, lakini vinginevyo kama mtuhumiwa wako ataendelea kuwekwa katika mahabusu ya Kata inabidi mlalamikaji uendelee kulipia gharama hiyo. Kwa hiyo, hiyo pia ni gharama mojawapo ambayo Watanzania wengi wanashindwa kuimudu.

Gharama nyingine ya nne ambayo wananchi wanalalamikia ni kuhusu usafiri endapo mtuhumiwa wako atatakiwa kusafirishwa kutoka Kijijini ama kutoka ngazi ya Kata kumpeleka Wilayani ni juu ya mlalamikaji kulipa gharama hiyo. Kwa hiyo, kama huna pesa ya kumlipia gharama, matokeo itakuwa ni kwamba huyu mtuhumiwa hatapelekwa katika ngazi ya Wilaya na inawezekana akaachiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama ya tano ambayo wananchi wanailalamikia hivi sasa katika jimbo langu na Wilaya ya Kondoa ni gharama ya kumsafirisha mfungwa endapo mtuhumiwa wako atapata adhabu ya kifungo na akatakiwa kusafirishwa kwenda gereza la Wilaya ama la Mkoa ni jukumu la mlalamikaji kutoa gharama hizo za kumsafirisha yeye pamoja na mtu ambaye atamsindikiza hadi kwenye gereza husika. Kwa hiyo, hiyo ni gharama nyingine.

Gharama ya sita na ya mwisho ni kuhusu gharama ya mashahidi. Hivi sasa Serikali haina utaratibu wowote wa kuwalipa mashahidi wanaokuja kutoa ushahidi kwenye Mahakama zetu zote. Kwa hiyo, jukumu hilo limeachiwa mlalamikaji peke yake na hilo jukumu ama hiyo gharama ni kubwa kiasi ambacho ni kwamba mara nyingi walalamikaji wanashindwa kumudu. Kwa uchache kabisa ukichukua hizi gharama zote haipungui shilingi moja, laki mbili kugharamia kuendesha kesi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini kabisa kwamba kwa uwezo wa Watanzania wa wastani si rahisi kuendesha kesi katika nchi yetu, kwa sababu ya hizo gharama na matokeo yake ni kwamba walalamikaji wengi wanakata tamaa njiani na matokeo ni kwamba wahalifu ama watuhumiwa wanaachiwa.

Sasa athari yake ni nini kama hatutaweza kutatua tatizo hili. Athari yake ni kama ifuatavyo, kutokana na gharama hizi nyingi kama nilivyosema hapo awali ni kwamba walalamikaji wengi wanashindwa kumudu gharama hizo na kutokana na kushindwa ni kwamba watuhumiwa wengi hata wa kesi za jinai wanaachiwa na matokeo yake ni kwamba kama nilivyosema hapo awali ni kwamba wananchi wengi hawapati haki zao na mbaya zaidi ni kwamba hawa watuhumiwa hasa wa kesi za jinai wanapoachiwa kurudi vijijini bila kuchukuliwa hatua ni kwamba wanaendelea kufanya uhalifu na uhalifu unazidi kushamiri katika vijiji vyetu.

Sasa mimi napenda nitoe maombi kwamba tusipochukua hatua za dhati na za haraka, hali hii ama kero hii nafikiri Watanzania wengi hawatendewa haki, ama hawatapata haki kupitia Mahakama zetu kwa sababu ya hizo gharama kubwa.

Kwa hiyo, mimi napenda nitoe mapendekezo ili tuwasaidie Watanzania wengi waweze kupata haki zao pindi wanapokosewa basi tuweke utaratibu nzuri zaidi wa kugharamia shughuli hizi za kutafuta haki. Napendekeza kwanza kabisa, Serikali ingeangalia na ingetenga fedha za kutosha kupitia Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili iweze kulipia gharama ambazo nimezitaja. Baadhi ya gharama hizo ni pamoja na gharama za kukamata watuhumiwa, kulisha chakula, usafiri na gharama za mashahidi. Tungeangalia kabisa tuweze kupata pesa za kutosha kugharamia gharama hizo ili tuwasaidie wananchi wetu.

Pendekezo langu la pili, linahusu Ofisi za Watendaji wa Vijiji na wa Kata. Napendekeza kwamba tuangalie ni kada ya watumishi gani wanatakiwa kwenye Ofisi hizo. Napendekeza ili waweze kufanya kazi ya kukamata watuhumiwa na kulinda mahubusu katika ngazi hizo tungefanya utaratibu wa uajiri askari ama mgambo katika kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu la tatu, naomba sana Serikali irudishe utaratibu wa zamani wa kutoa chakula katika mahubusu za ngazi ya Kijiji na Kata. Huu utaratibu ulikuwepo mpaka miaka ya 1990 lakini sijui kimetokea nini hapa katikati utaratibu huu ukaondolewa. Naomba sana turudishe mpango huu ili tuweze kusaidia wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu la nne na la mwisho ni kwamba Serikali irudishe utaratibu wa zamani wa kulipa posho na nauli kwa mashahidi ili waweze kutoa ushahidi na kuweza kupunguza gharama kwa walalamikaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa kama Serikali itatekeleza mapendekezo yangu haya, Watanzania wengi watapata haki zao kupitia Mahakama zetu bila kukwama kutokana na kupunguziwa gharama hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia haya machache, lakini pia napenda nitamke kwamba naunga mkono hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BERNARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kwamba umenipa nafasi ya kuwa msemaji wa mwisho mchana huu. Nipende kwanza nimpongeze Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa hotuba nzuri aliyoitoa asubuhi hii na ningependa kumhakikishia kwamba nitaiunga mkono jioni hii mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina matatizo kabisa na vyombo vya ulinzi na usalama hasa kwa jambo moja kubwa ambalo linatuletea sifa Watanzania, nidhamu ya vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. Napenda niwapongeze watu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Jeshi la Polisi hasa kwa nidhamu ya hali ya juu wanayoionyesha nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti,mwaka jana nilikwenda Rome nilikokutana na viongozi mbalimbali wa nchi za Afrika na hasa Afrika Mashariki. Lakini nilikutana na viongozi kadhaa wa Kenya wakawa wanatania jeshi letu la Polisi kwamba jeshi lenu la Polisi ninyi ni watakatifu na ni wema sana wanapomfukuza Musa, wanamfukuza, wakimshika, wanamsalimia kwanza, hujambo Musa, sijambo. Umekula, sijala. Naomba nafasi ya kukufunga pingu. Anasema niacheni ninywe chai kwanza. Anakunywa chai, halafu yule mhalifu anamwuliza Polisi, wewe unaitwa nani? Anasema mimi ni Koplo Musa. Haya basi nifunge. Lakini tusikimbie sana, unajua hali yangu siyo nzuri. Kwa hiyo, anampeleka mpaka *Police Station. (Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wanasema Polisi wa Kenya anapomfukuza Musa, akimkuta tu kwenye gari, pale pale anapanda juu ya mgongo wake na kuandika *statement,* anamwuliza akiwa chini na anatoka damu, unaitwa nani? Huko chini. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *joke* lakini inayo-*demonstrate* nidhamu ya vyombo hivi. Wala siku-*regret* kwa *joke* hili. Lakini nadhani ili-*demonstrate* kwamba Jeshi letu la Polisi pamoja na matatizo mengine yote wana-*demonstrate* nidhamu ya hali ya juu na ku-*exercise humility* na ubinadamu ambao ni kipaumbele cha Watanzania. *(Makofi)*

Lakini wenzangu wanasema si kweli, inaonekana kama ukikutwa unavuta bangi, mvamie tu, nadhani hiyo haina matatizo kabisa. Kitu kilichonisimamisha asubuhi hii ni suala la uhamiaji na nitalizungumza kwa uchungu hili.

Mimi Jimbo langu la Mtama lina wakazi laki mbili na nusu. Katika wale wakazi laki mbili na nusu, wakazi wasiopungua 45,000 ni wakazi wenye asili ya Msumbiji walioishi nchini kwetu kuanzia miaka 100 na wengine wamezidi zaidi ya hapo na wamefia nchini. Lakini kwa masikitiko makubwa watu hawa inapofika wakati wa uchaguzi kama mwaka huu hawatakuwa na haki ya kuchagua wala kuchaguliwa katika Jimbo la Mtama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawa wamezaa vijana wazuri kweli na wamesoma, wamesoma vizuri kweli, wamesomeshwa na Taifa hili toka darasa la kwanza mpaka wanapata Stashahada za Juu, na wengine shahada kubwa. Wanafanya kazi katika nchi hii. Eti baadaye mhuni mmoja anapita mahali anamwambia huyu babu yake na baba

yake si raia wa Tanzania na anafukuzwa kazi, *without any due process* anafukuzwa kazi na ni Amselemu Masumbuko hapa. Amselemu Masumbuko *my best mark* na ni *class mate* wangu, tumezaliwa pamoja, amezaliwa kule,amefanya kazi, kwanza kasomeshwa na Serikali, kazaliwa Tanzania alifanya kazi miaka 23, baada ya kupata Stashahada baadaye anatoka mtu anakuja anasema baba yake huyu ana asili ya Msumbiji na mama yake ana asili ya Msumbiji anafukuzwa anapata *summary dismissal* baada ya kufanya kazi katika nchi hii na kusomeshwa katika nchi hii anafukuzwa bila aibu yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *in broad day light,* nchi yetu ya Tanzania tulianzisha Umoja wa Afrika, tunayoiona Afrika ni moja, tunayoleta *liberation* na Mozambique ambayo ilikuwa chini ya koloni, hivi tunapomfukuza sisi ndiyo tumepata Uhuru kwanza, Mozambique ilikuwa koloni *it was a Portuguese colony,* wale watu walikuwa *stateless then. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Mozambique was not a nation state,* hii si nchi ambayo unamchukua mtu unamwambia rudi kwenu, arudi wapi, *it was a Portuguese colony, this was a colony, is a Paliunius Masumbuko* leo ananisikia aliko kule ana miaka 100 mzee wa watu anaishi na mama yake Amselemu ana miaka 86 amekuja akiwa ananyonya. Mtu huyu leo amefukuzwa kazi miaka mitatu iliyopita, akiwa amesomeshwa na nchi hii, akiwa ameelimishwa na nchi na tunakaa tu.

Lakini najiuliza kuna *conspiracy* gani maana yake *this an immigration issue* walipogundua kwamba wazazi wake hawakuwa Watanganyika na ni kweli hawakuwa Watanganyika. Walikuwa wametoka Muweda, Msumbiji miaka 100 iliyopita. Kabodelgado huko ndiyo miaka 100 iliyopita. Ni kweli kabisa. Lakini jamani, tumefika mahali kweli pa kumfukuza mtu kwa kosa la kutokuwa raia wa Tanzania wakati tuna wafanyakazi wengi katika nchi hii ambao si raia wa Tanzania tunawaheshimu na kuwalipa mishahara mikubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Watanzania walioko nje ya nchi tena kiharamu na wengine kwa halali Botswana na nchi zote wanavyopata heshima na nchi walikokwenda kuishi na mpaka wanapata uraia na wanaheshimika na kupata fedha na wanasaidia wadogo zetu wanasaidia wake zao, wanasaidia familia zao. Vipi leo kina cha Uhuru wa Afrika, tuliowakomboa wakimbizi wa *Mozambique* tukaishi nao, tukazaa nao na tukakaa nao hapa leo *a hundred years later* mtoto kazaliwa tumemsomesha wenyewe tunam-*punish* na familia yake kwa kumfukuza kazi na akina Membe tuwe na kazi ya kumlisha mkate mmoja, mmoja na kumpa pole kwa sababu hastahili kuishi katika Tanzania yeye eti si raia wa Tanzania. *(Makofi)*

Mimi nasema *we must review,* kuna sheria fulani zimepitwa na wakati hasa Sheria ya Uraia, hii tunayoiimba kila siku, unajua Membe wewe kama ulizaliwa Tanzania usiku mpaka kufikia tarehe 9 Desemba, 1961 ulikuwa raia isipokuwa kama baba yako au mzazi wako mmoja alikuwa ametoka kule nje basi wewe unatakiwa u-*re-nounse* uraia wako ulipofika miaka 18 u-*re-naouse.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niwaambie leo mambo mawili. Nilikuwa na Amselemu tulipokuwa miaka 18 shuleni. Sikumbuki wala mimi wala mtu yeyote wa darasa lile aliyesema jamani sasa ni miaka 18 ngoja tukawaulize baba zetu na mama zetu, hivi sisi ni Watanganyika au Watanzania. Sikumbuki, na kama kuna Mbunge mwenzangu humu na mimi nina mtoto wangu wa miaka 18 sasa ni Richard, anatimiza miaka 18 mwezi Oktoba, sina hakika kama atakuja kuniuliza hivi wewe baba asili yako wapi nataka nijaze ni-*re-anounse citizenship,* kama kuna Mbunge humu ndani aliyefikiwa hiyo na watoto wake wakamuuliza umezaliwa wapi aninyooshee kidole, mimi sijawi kuona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Amselemu angeanzia wapi tulipokuwa darasa la 11 angeanzia wapi, amnyoshee mwalimu amwambie kesho narudi maana miaka 18 nimeshafikisha. Hili ni suala la kusema *ignorance of law is no excuse,* hali-*apply* kabisa katika suala la *citizenship. That man is a Tanzanian,* hakustahili kufukuzwa uraia wake wala hakustahili kuiomba radhi nchi hii, yule ni Mtanzania. Ni suala la kubadilika, kuangalia sheria ya aina hii na kuibadilisha mara moja, inanuka na haifai na lazima tuifanyie *review. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siku zote nataniana na rafiki zangu wa Zanzibar, kama hii sheria tungei-*apply* Zanzibar nani angekuwa raia wa Zanzibar? Nani angeishi Zanzibar? Tunajua wazazi wao, tunajua na babu zao kama tunge-*apply* hii nani angeishi kwenye kisiwa kile? Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa niliongea naye anasema hata yeye asingeishi. Angerudi Comoro. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunafumba hivi, lakini niwaambie jambo la pili la kusikitisha. Nilipokuwa Canada mimi, sasa sikia, muone nchi za wenzetu wanavyoi-*apply* sheria hii kutukandamiza. Nilipokuwa Canada pale, Serikali ya Canada ikam-*depot* mtu mmoja Mtanzania kutoka Toronto mwenye asili ya Uhindi waliposoma sheria *loose* ya Tanzania kugundua kwamba wazazi wake kama wamezaliwa Tanzania ni Mtanzania na yule alikuwa na *deal* na *drug trafficking.* Kwa hiyo, wakamleta kwenye Ubalozi *and I was incharge,* wakaniambia bwana tunataka tumrudishe huyu Tanzania kwa sababu wazazi wake ni Watanzania na ninyi mna sheria inayosema mzazi wake akizaliwa Tanzania wewe ni Mtanzania. Huyu kazaliwa Canada kwa vile mna sheria Tanzania inayosema baba kama ni Mtanzania ni Mtanzania tunaomba umpe hati ya kusafiria tunataka kum-*depot* na *KLM* arudi Tanzania akafanyie u-*criminality* huko Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikataa, hakuna cha sheria pale, *I rejected,* nikamwambia sikia, amezaliwa kwenu hapa na ninyi mna sheria yenu ya kuheshimu watu hapa, huyu mtu wazazi wake wako hapa, japokuwa baba yake alizaliwa Tanzania, mimi sitatoa kibali cha kumrudisha Tanzania, simtambui kama ni Mtanzania, *this is a Canadian* na alibaki hapa na amebaki kule anaendelea na *drug* na *process* zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ningekuwa mwoga wa kuzingatia visheria vya ajabu, vya aina hii ningeleta *criminal* yule hapa, sina hakika inawezekana kwa mwanya ule ule tuna wengi waliorejea katika nchi hii kwa sababu tu baba zao ni Watanzania wanakuja huku na wanafanya vitendo vya uhalifu, lakini hawawezi kuungama kwamba

nimerudishwa nchini kwa sababu gani. Lakini ninaamini kwa mwanya huu wako *criminals* kwa kutumia *parenthood* ya wazazi wao wanarudi nchini kufanya vitendo vya uhalifu *in the name* wao ni Watanzania *by vitual* kwamba wazazi wao walikuwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria zilizopitwa na wakati lazima tuziangalie upya. Tusing'ang'anie na hasa zinazohusu makabila yanayotoka mipakani na wanaoishi visiwani. Tukianza kuchungazana baba yako alizaliwa wapi na muanze ku-*apply* suala hili Mtwara, Lindi, Ruvuma, Kigoma, wapi kwingine, Kagera na Zanzibar, Bunge hili litakuwa na Wabunge kutoka Dodoma na Singida tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeishi na akina Mzee Jamal, tumeishi na akina Mzee Dereck Bryson, tumeishi na akina Mzee Kambona, tumeishi na watu ambao wazazi wao kwa uhakika kabisa hawakuzaliwa nchi hii. Hawakufanyiwa vitendo vya aibu vya aina hii. Walikuwa *naturalized* na wakarudishwa kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa mfano huu, mtu huyu apewe uraia wake ambao hauwezi kupokonywa na usumbufu alioupata unaolingana na jina lake la Masumbuko kwa kweli arudishwe kazini na tumlipe haki zake. Tanzania haiwezi ikafika hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namsemea Amselemu, lakini naamini wako mamia ya Watanzania wanaopata msukosuko wa aina hii. Kwa maneno hayo machache na kwa busara za Waziri nina hakika wewe na timu yako nzuri, yenye nidhamu ya kukubalika katika Afrika, mtakwenda mkakae kwa uangalifu na kwa utulivu ili nisizishike bilioni 11 za rafiki yangu Kiomano humu ndani ili tuondoke kwa usalama jioni hii. Ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema huyo alikuwa msemaji wetu wa mwisho mchana huu. Tukirudi tutakuwa na Mheshimiwa Ali Machano Mussa, Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, Mheshimiwa Emmanuel Kipole na Mheshimiwa Mohamed Abdul Ally, ndiyo watakaokuwa wachangiaji mchana huu.

Baada ya kusema hivyo, naomba niahirishe kikao mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.56 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Eliachim J. Simpasa) Alikalia kiti*

**MHE. ALI MACHANO MUSSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kunipa nafasi ya mwanzo kwa kipindi hiki cha leo cha jioni na mimi kuchangia hotuba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwanza kabla sijaanza kuchangia nafikiri nisije nikasahau niseme tu kwamba sina budi kuunga mkono hotuba hii mia kwa mia. Kutokana na maelezo ambayo nimeyaona, niliyoyasikia ambayo yamewasilishwa na Mheshimiwa

Waziri, kwa sababu nina tabia ya kusahau sahau nimeona kwanza nitangulie kwanza kuiunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hilo sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Maofisa wote wa Wizara hii pamoja na watendaji bila kuwasahau Makamishina wa Magereza, Polisi na Uhamiaji ambao wameshiriki kikamilifu katika utekelezaji wa kazi za Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia kwangu pia ningependa kutoa kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Jimbo la Tumbatu Zanzibar, kumpongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani kwa ushirikiano wake ambao anautoa wa kutembelea maeneo yake ya kazi, lakini pia kudumisha uhusiano uliokuwepo baina ya majimbo na majimbo.

Kwa hiyo, naomba kwanza apokee pongezi hizi zinazotoka kwa wananchi wa Jimbo la Tumbatu, Zanzibar. Lakini pia pamoja na kumpongeza ningewaomba wananchi wa Jimbo la Manyoni Mashariki ambako Mbunge huyu ndio anakotoka niwaambie tu kwa kutumia nafasi hii wasitupige chenga wafanye linalowezekana lakini Mbunge huyu arudi tena. Kwa sababu kuna mambo bado tunayahitaji akiwa Mbunge tunahisi tunaweza tukafanikiwa, kwa hilo kwanza naomba salaam hizi ziwafikie wapiga kura wa Chama cha Mapinduzi wazipokee kwa moyo safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa pongezi hizo nikianza kuchangia na hotuba hii kama nilivyosema kwamba naiunga mkono hakuna dosari ambazo nasema kwamba nizitoe. Lakini kuna wapiga kura wetu ambao nao wanahitaji kidogo kufikishikiwa mawazo yao ni sisi ambao wametuchagua tutakuwa hatukuwatendea haki kama mawazo yao hayakufika. Hawatakiwi wananchi wote waingie hapa waje walete mawazo yao, isipokuwa wawakilishi wao ndio wafike hapa.

Mheshmiwa Mwenyekiti, sasa mimi nawakilisha mambo mengi ambayo ni ya wapiga kura wetu, lakini jumla ya hao kwa leo nataka nipewe nafasi ya kuwachangia au kutoa mawazo yao ndugu zangu askari polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, askari polisi wamekuwa na malalamiko mengi ambayo ni ya uhakika, wanatutuma kila tunapokutana nao ili tuwasaidie yafike kwa njia moja au nyingine Serikalini. Njia ambayo ni muafaka kabisa hii ambayo tunaitumia kwa hiyo, kwanza njia ambayo nataka kuitumia na neno ambalo nataka kuliomba kwao ni kutokana na madai ya madeni ambayo wanayadai Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, askari polisi wana malalamiko ya muda mrefu kitu ambacho niseme haswa wale askari wadogo wa vyeo vya chini, hatma ya matatizo yao wanapoyaeleza yatafikia wapi ufumbuzi, utaratibu mzuri ni kuyafikisha mahali panapostahili, yazungumzwe kwa njia ya busara. Askari polisi wamekuwa na madai mengi.

Kwanza, wana madai ya posho, posho za maaskari ambazo wanahamishwa kutoka sehemu moja hadi sehemu nyingine, wanadai wale askari wa *CID,* posho za

mavazi ambazo kwa kawaida wanatakiwa walipwe *allowance* zao kutokana na mavazi ambayo wanayatumia, wale askari wa *CID* hawatumii nguo zile ambazo wanatumia askari wengi. Kwa hiyo, nazo wanadai hizo, wanadai malipo ya uhamisho kutoka vituo hadi vituo, wanamadai ya kupandishwa vyeo, kuna maaskari ambao wanapandishwa vyeo nazungumzia zaidi wale maaskari wa ngazi ya chini kutoka Koplo mpaka *sergeant major,* kwa sababu kuna kawaida maaskari wakishakuwa maofisa mara nyingi kuwa kudaidai wao wanaona si kitu kizuri, lakini hawa wenzangu hawa ngazi za chini wana matatizo wana madai mengi. Pia wana madai ya malimbikizo ya mshahara ambayo wakati mwingine wanalipwa kimakosa, kinachobakia huwa hawalipwi tena sasa hili nalo linatokea tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeomba tu Kamishina wa Polisi aliwakilishe na najua kwa sababu wote wapo pale nawaona. Hebu waangalie kwa uangalifu kabisa matatizo haya ambayo waliyonayo, madai haya mengi, kwa upande wangu nakumbuka iko siku moja mara nyingi huwa najaribu kuuliza maswali kwa Wizara ya Mambo ya Ndani, tukiangalia *Hansard* ya tarehe 21 Aprili, 2005 kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ambayo niliuliza swali, nilijibiwa kwamba kuna deni ambalo wanadai maaskari kuanzia mwaka 2000/2004 shilingi bilioni tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri amesema kwamba wanafanya maarifa kwamba pesa hizi zilipwe kwa sababu ni haki yao. *Hansard* hiyo inaeleza wakati wote unapoenda kufungua utaona kwamba ipo hivyo, lakini kama mpaka leo wanadai hivyo na hawajafanikiwa kulipwa wategemee lini na madai yanaendelea kuongezeka?

Sasa watu hawa wanapokuwa wanalalamika inatuletea matatizo, hivi ninavyokuambia kuna askari wanatayarishwa kwenda kozi, wanapokwenda kozi bado madeni yao ya nyuma wanadai na leo yanaongezeka mengine, utakapowasilisha majibu ya maswali haya naomba sana kabla hatujaenda kifungu hadi kifungu nipate majibu lini askari polisi watalipwa madeni yao ya nyuma na nikisema madeni ya nyuma si kwamba yale yanayojulikana Kiswahili nasema madeni yaliyopita huko kwa sababu wengine hapa Waswahili sana wanaweza kudai kwamba madeni ya nyuma, madeni yaliyopita nyuma. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nieleweke vizuri nafikiri hili limeeleweka. Lakini wakati huo huo niende katika askari ambao wanapewa barua za kuachishwa kazi kwa muda wao ambao umefika, tatizo lipo ni haki kabisa wakati ukifika unapewa barua kwamba ujitayarishe kuacha kazi. Kwa bahati kuna maaskari ambao wamepewa barua, baada ya muda ambao tayari hajastaafu kazi anapewa tena barua kwamba unatakiwa uende kozi chuoni, wanakwenda polisi college au wanakwenda *CCP,* Moshi au anakwenda Chuo cha Polisi Zanzibar, inatokea bahati mbaya amepewa barua ya kuacha kazi, halafu anapewa barua ya kwenda kozi kwa mfano kozi ya Koplo au *sergeant course.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna askari wanapata ajali wakati huo wa kazi. Namtambua askari ambaye amepata ajali, amekatika mkono sasa hivi anayumba ni kwamba yeye tayari amepata ajali akiwa amepata barua ya kuacha kazi na pia

amepelekwa kozi chuoni, hebu niambieni mtu huyu mnamweka katika fungu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti. tuchukulie kama ninyi maofisa ambao mpo hapo imekutokea hali kama ile, umepewa barua ya kuacha kazi, umepewa tena barua ya kuendelea na kazi umefuta kozi, umepata ajali watoto wako watafanya nini hili naliomba mliangalie sana madeni kama haya, matatizo kama haya tuyatafutie ufumbuzi. Inafikia wakati kama miaka minne sisi tunakuja kudai watakuja Wabunge wengine kwa bahati nzuri wanadai hayo hayo na Wabunge wengine wadai hayo hayo wananchi wetu huweka vipi wale nao ni wapiga kura.

Mimi wapiga kura wangu wa kituo cha polisi cha Mkokotoni ambao kimo ndani ya Jimbo la Tumbatu, lakini haitoshi tuna maaskari ambao wako *Field Force* Ziwani wana matatizo kama haya, kuna maaskari ambao wako Ukerewe, kuna maaskari wako *Field Force* Dar es Salaam, kuna maaskari ambao wako Ukonga, kuna maaskari wako Himo, kuna maaskari wako Taveta, Tanzania nzima wana matatizo haya haya. Hivyo hatuoni haya, tunachotegemea kwamba huwa tunasema walinde raia na mali zao, wao watalindwa na nani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kwamba nizungumze muda mfupi lakini mambo haya yanauma kiasi ambacho kama walivyotangulia wenzangu wanasema kwamba ikishindikana unakuja Bungeni, unaambiwa bwana unakwenda Bungeni lakini muda wa bajeti bado subiri muda ufike, leo muda umefika tunataka tuelezwe madai wanayodai haswa askari ambao hawana vyeo au wenye vyeo vya chini, madai hayo yanapatikana lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri nafikiri umenielewa vizuri, lakini pia nizungumze suala la usumbufu kwa wale ambao wanaacha kazi, nitazungumza kwa ufupi kwa sababu najua kwamba wanaonisikiliza wengi huwa akili zao timamu. Tatizo la askari ambao wanaacha kazi wamefanya kazi kwa muda mrefu nataka niseme askari polisi kama anakwenda kwenye lindo amekamatwa lindoni hayupo siku ya pili akipatikana anapelekwa maktabu anachezesha ugwaride au anapewa adhabu inayostahili. Hivi mfanyakazi ambaye anafanya kazi sehemu ya fedha hakumfanyia haki askari huyu anafanywa nini yeye, yule ambaye katoroka lindoni hakulinda benki amekimbia siku ya pili anapelekwa maktabu, anapelekwa *lock up,* anapewa adhabu, lakini wale ambao hawawajibiki kuwatendea haki askari hawa maofisa ambao unashughulika na mambo ya fedha mnawapa adhabu gani? Nataka kujua hii hali, hili nafikiri nalo limeeleweka. *(Makofi)*

Suala lingine ambalo nataka kulizungumzia kuhusu pensheni na *grace duty* mpango huu tumeuzungumza sana tumeandika masuala hapa na yanajibiwa majibu yake tunaambiwa kwamba wanaulizwa wakifika miaka kumi na tatu, kumi na mbili ni sawa wanaulizwa lakini kama wale wapiga kura wetu wengi wao wanasema kwamba mpango ule hawautaki tena nimesema hapa Waziri alipochaguliwa kwamba azungumze na maaskari wa mikoa mitatu ya Zanzibar, atakapozungumza nao awasikilize wana maoni gani kitendo hicho hakikufanyika naomba tena hebu kaa na maaskari uwasikilize wana maoni gani. Maaskari wanasema kwamba wakifika umri wa kufanya kazi kwa muda wa

miaka 21 moja kwa moja waingie pensheni kama majeshi mengine yalivyo, hayo ndio maoni yao maaskari leo unawaambia kwamba umefanya kazi muda wa miaka kumi tatu, miaka kumi na mbili analipwa shilingi 150,000/= au 300,000/ pensheni analipwa shilingi 4,000,000/= au 4,000,000 au 10,000,000/= . Tatizo hii Sheria ibadilishwe na haibadilishiki basi muamue uamuzi mwingine lakini muwatendee haki askari hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kwamba hili niwapongeze maofisa wa polisi kwa utaratibu mzuri ambao wameuweka wa kuwapandisha vyeo wale maaskari ambao tayari wamefanya kazi kwa kipindi kirefu na hawana makosa wanaonekana kwamba sasa hivi wanastahili kupata vyeo, pamoja na kwamba kufanya kazi wamefanya miaka 20 wameanza kupata ukoplo basi niwapongeze pia maofisa kwamba utaratibu mlioweka sasa wa kuwataka kwamba maaskari wazee nao wapate angalu waibukie na kitu ukoplo unawagawia hili nawapongeza. Lakini pamoja na kuwapongeza niseme tu kuwa wakati wanapokwenda kozi maaskari mambo yao hawatakiwi waingiliwe hayo tunawaachia wenyewe. Lakini kuna tatizo la UKIMWI. Tatizo la UKIMWI maaskari wetu wanawake wanapokwenda kwenye kozi lichunguzeni kwa nini baada ya kurudi kule wawili, watatu, wanne, watano, wanafariki? Hapo naacha katika mabano muangalie kwa nini wanapokwenda kozi wakirudi hawa wanawake wanakufa haraka, pamoja na wanaume lakini tatizo la UKIMWI tumesema tulishughulikie Kitaifa. Sasa suala hili ningeomba Wizara ya Mambo ya Ndani mliangalie kwa sababui ninyi ni watu ambao mnaujanja mkubwa sana wa upelelezi basi fanyeni upelelezi mbona maaskari wanapokwenda kozi za vyeo wanaporudi tayari wengi wao wanaokuwa na matatizo haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kuunga mkono, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushuru kwa kunipa fursa na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, na napenda nichukue fursa hii kwanza kabisa kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wao ndani ya Wizara yao kwa jitihada na kazi ambayo wanafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo kama matatu ambayo ningependa kuyazungumzia lakini kwa bahati nzuri wenzangu wamezungumzia. Eneo la kwanza ambalo ningependa kulizungumzia ni suala zima la makazi, lakini napenda niishukuru Serikali kwamba imeweza kutenga fedha kwa miaka mitano iliyopita kuwezesha upatikanaji wa makazi bora kwa ajili ya maaskari wetu na maafisa wetu wa majeshi yetu ya Polisi, Magereza, Uhamiaji na Zimamoto. Lakini mimi nilikuwa napenda tu niombe kwamba mpango huu ungeenea kwenye nchi nzima, kwa mfano, pale kwangu Musoma nyumba ambazo wanakaa maaskari kwa kweli si nyumba, ni aina tu ya magofu ambayo yapo ili kukidhi mahitaji kwamba watu wanajificha mle ndani. Kwa hiyo, nadhani moja ya vitu vinavyomfanya binadamu anakuwa binadamu ni ustaarabu na ustaarabu ni moja ya mambo yanayomfanya binadamu anastaarabika ni kuwa na makazi bora. *(Makofi)*

Kwa hiyo, moja ya mambo ya msingi ambayo nadhani Serikali ni lazima iyasimamie ni kuwapatia makazi bora hawa askari wetu hasa ukizingatia kwamba kazi wanazofanya ni ngumu na muda mrefu wanakuwa nje wakiteseka na baridi wanafanyakazi katika mazingira magumu. Sasa ni vyema basi wanaporudi nyumbani wakawa wanakwenda kwenye makazi mazuri na wanapumzika na familia zao. Kwa hiyo, nadhani Serikali kwa hili ilisimamie kiasi cha kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasoma hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa nane, kuhusu sera ya CCM ya kuwa na jeshi dogo la usalama wa raia lakini lenye uwezo mkubwa wa kitaaluma na nyezo za kazi.

Napenda nizungumze masikitiko yangu kwamba muundo wa sasa wa Jeshi la Polisi bado hautoi nafasi kwa wasomi kuweza kuwaajiriwa katika jeshi hili na wakapewa nafasi kulingana na taaluma zao. Sasa tunapozungumzia kwamba tunataka ku-*transform* Jeshi la Polisi liwe Jeshi la kisasa, utali-*transform* vipi bila kuwa na wataalamu?

Kwa mfano, vijana waliomaliza Chuo Kikuu mwaka 2004 ambao wamejiunga na Jeshi, wamekwenda kozi pamoja na vijana wa darasa la kumi na mbili sawa wanatakiwa kujifunza uaskari. Lakini baada ya kumaliza kozi, bado wanalipwa mishahara inayolingana na wale waliomaliza *form four.* Sasa tunaposema tunataka tuvutie vijana wasomi kuingia kwenye Jeshi la Polisi, utawavutiaje kwa utaratibu huu uliopo sasa hivi ambao taaluma na sifa zao za kitaaluma hazithaminiwi ndani ya Jeshi la Polisi.

Sasa hivi wako *graduate* hapa wanalinda kwenye nyumba za Mawaziri kwenye mageti ya nyumba za Mawiziri hapa *a graduate,* hivi kwa mtindo tulio nao katika Jeshi la Polisi ni wasomi wangapi ambao watakuwa na *interest* za kujiunga jeshini, badala yake tutaishia kwamba Jeshi la Polisi ni mahali ambapo watu wanakwenda kutafuta ajira baada ya kukosa ajira kwenye sehemu zote. Watu ambao wameshakuwa *demororised,* hawana ajira wanasema hivi hata huko polisi siwezi kupata, maana mtu haendi kwa sababu ana *interest* ya kuwa askari polisi. *(Makofi)*

Sasa huu utaratibu mimi nadhani ungeangaliwa na urekebishwe, kama ni muundo wa Jeshi la Polisi ndio ufanye kwamba watu hawathaminiwi kwa sababu ya kuwa na taaluma zao katika jeshi, basi ibadilishwe na ieleweke wazi mtu anayejiunga na Jeshi la Polisi akiwa na kiwango cha elimu fulani ataingia na atakuwa nani ndani ya Jeshi la Polisi. Kama amemaliza *form four* atakwenda kuwa nani, kama amemaliza kidato cha sita atakuwa nani na kama ame-*graduate* anakwenda kuwa nani katika Jeshi la Polisi. Lakini huwezi kumdhalilisha mtu ambaye amemaliza Chuo Kikuu unamlipa mshahara mdogo wa *form four* na bado unampa kazi ya kufanya ambayo hailingani na heshima hiyo ya kisomi ambayo anayo. Lakini napenda nipongeze kwamba kwenye idara zingine kama uhamiaji, uhamiaji wanawaheshimu wasomi, ukienda kwenye idara zingine kama wakimbizi wanaheshimu wasomi. Tatizo ni polisi kwa nini sasa tunasema hili sio jeshi la kikoloni, kwamba jeshi hili ni kusimamia virungu, hapa ni jeshi tunataka liwe la kisayansi, fungueni milango wasomi waingie kwenye Jeshi kwa nia njema kwamba wanakuja kuwa wanajeshi wa polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina ugovi na Jeshi la Polisi, lakini nasema katika dunia hii ya sasa hivi ya Sayansi na Teknolojia tunataka tuwe na polisi wasomi, nashukuru wakati mmoja nimesikia viongozi wa polisi wenyewe wakubwa kabisa ndani ya Jeshi la Polisi wakisema sasa si wakati wa kuwa na jeshi la kushika virungu, tunataka kuwa na Jeshi la Polisi ambalo lina *think tank* ndani ya Jeshi la Polisi, sio vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba Waziri kwa kusaidiana na wataalamu wake ajaribu kuboresha muundo wa Jeshi la Polisi, kwamba watu wasiende kutafuta kazi polisi kama kimbilio la mwisho kwa watu waliokosa ajira maeneo mengine. Mheshimiwa Paul Kimiti, amezungumzia *vetting,* hivi hao polisi tunao waajiri ni watu wanakwenda kuajiriwa kwa sababu wana nia ya kuwa askari kulinda usalama wa raia? Au wanakwenda pale kwa sababu wamechoka hakuna ajira mtaani kwa hiyo, watu wanawaambia wazazi, baba hivi hata upolisi siwezi kupata maana ni *last option,* kwa nini tulishushe jeshi letu hapa liwe kimbilio la watu ambao wamekata tamaa?

Kwa hiyo, mimi nadhani kuna umuhimu kabisa wa kufumua hili jeshi liundwe na lieleweke kwamba sasa ni jeshi la namna gani na watu waelewe kila mtu aelewe anavyokwenda kuajiriwa na Jeshi la Polisi anajua kabisa kama ilivyo kwenye majeshi ya ulinzi kwenye majeshi aliyoyataja mengine nyumbani mtu anajua kabisa nikiingia hapa baada ya miaka miwili nitakwenda kufanya kozi fulani na nitakuwa fulani.

Mimi nina mdogo wangu, nadhani aliingia Jeshi la Polisi miaka karibuni saba, nane amemaliza *form six* ana *pass* zake nzuri, hawezi kupata hata nafasi ya kwenda kusoma, *form six* wamejaa kule ni ma-*private,* makoplo hawawezi kwenda kusoma, jamani tubadilishe hii hali kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema nizungumzie suala la utawala bora, napenda nilipongeze Jeshi la Polisi kwa hatua linazochukua kupambana na rushwa na ndani ya jeshi hili, kwa sababu na hakika Jeshi la Polisi lilikuwa moja ya idara ambazo zilikuwa zikilaumiwa sana kwamba ndio eneo limekubuhu kwa rushwa. Lakini hii haimaanishi kwamba hatuhitaji kuongeza jitihada za kupambana na rushwa ndani ya Jeshi la Polisi, maana tunapozungumzia utawala bora moja ya vitu ambavyo lazima tupambane navyo kufa na kupona ni suala la rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nizungumze kwa masikitiko makubwa sana maeneo ambayo yanalidhalilisha Jeshi la Polisi na kuweka kichefu chefu kwa raia wa nchi hii. Mnamo tarehe 17/4/2004 yalitokea mauaji ya kutisha na ya kinyama kabisa pale Mjini Musoma, kijana mmoja aliuawa na akateswa sana, sisi ni binadamu nikisema kwamba sehemu za siri zilipondwapondwa nadhani mnanielewa, akagongwa, akatobolewa na misumari yaani ilikuwa ni mateso ya ajabu sana, baada ya kijana huyu kuwa ameuawa, askari walichukua hatua wakakamata watuhumiwa ambao walikuwa wanahusika na mauaji yale.

Sasa katika maajabu machache ambayo tunakutana nayo duniani, maajabu machache ambayo yanalidhalilisha Jeshi la Polisi, watuhumiwa hao kwa sababu wana uwezo wa fedha walikaa mahabusu nadhani miezi minne halafu ukafanyika utaratibu,

baada ya kufanyika utaratibu basi wakaachiwa. Sasa baada ya kuachiwa ukawa ndio mwisho wake huo wa hili tatizo, sasa mimi nataka nimwombe Waziri, kwamba Waziri aunde Tume huru itakayokwenda kufuatilia suala hili ili haki iweze kutendeka na ili iweze kusafisha hii sifa ya Jeshi la Polisi pale Musoma Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake jeshi linafanya kazi vizuri, lakini kama wapo watu wachache ambao wanaweza kuharibu na kuchafua sifa ambayo inaanza kujengeka katika Jeshi la Polisi, hawa ni lazima washughulikiwe. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, namheshimu sana Waziri wangu wa Mambo ya Ndani, naomba nimetumwa na wapiga kura wangu, nimetumwa na familia ya marehemu huyu ambaye anaitwa Peter Kelvin Juma kwamba watendewe haki, wale ni maskini hawana pesa za kutoa ili waweza kununua haki, maana hakuna duka la kununua haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kitu kibaya zaidi nataka nizungumze wakati ndugu zake na huyu marehemu wakifuatilia matatizo aliyopata huyu kijana, alipoteza baba yake mzazi alifariki kwenye hili tatizo, mama yake mzazi alifariki, shangazi yake alifariki na ndugu zake kadha walijeruhiwawakati wakienda kutizama huyu kijana alivyokuwa amepata matatizo. Kwa hiyo, hili suala ni suala ni *serious* na mimi na hakika kwamba haki inatafutwa kwa gharama kubwa. Serikali haiwezi kukosa fedha kwa ajili ya kuunda timu ambayo itasimamia upatikanaji wa haki ili hata hawa ndugu zake na huyu kijana marehemu waweze kuamini kwamba Serikali yao inajali watu wake. Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba Mheshimiwa Waziri utalichukua hili tatizo uweze kulifanyia kazi, uunde Tume inayojitegemea ambayo itaweza kwenda kufanya uchunguzi na kuhakikisha kwamba haki inatendeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri amezungumzia kwamba kwenye kipindi cha mwaka 2004/2005 Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya upatikanaji wa gari la zimamoto kwa Mji wa Musoma. Ningependa nielewe ni fedha kiasi gani zilitengwa, kwa sababu hilo gari mimi sijaliona na kama halikupatikana je, hii bajeti imekuwa *carried forward* kwenye bajeti ya mwaka 2005/2006 ili niweze kufahamu au kama gari hilo bado liko kiwandani linashughulikiwa niweza kufahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka nilizungumzie ni suala la ucheleweshaji wa upelelezi wa kesi zetu, limezungumzwa na wenzangu unavyocheleweshwa haki ya mtu humtendei haki.

Mimi nilipata fursa ya kutembelea magereza ili niweze kuzungumza na mahabusu, watu wanakaa ndani miaka 9, miaka 8, miaka 7 hivi huu ndio utawala bora, ndio tunavyowatendea watu haki? Unamweka mtu mahabusu, upelelezi haujakamilika mwaka wa kwanza, upelelezi haujakamilika mwaka wa pili, upelelezi haujakamilika mwaka wa tatu. Hivi tunavyokuwa tunawakamata hawa watuhumiwa si tayari tuna uhakika, kuna *indicator* zinatuonyesha kwamba huyu ndio anayekaribia karibia kuwa mshtakiwa. Sasa kwa nini tusikamate watu tuwaweke mahabusu kwa miaka mitatu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani utaratibu huu unatuletea matatizo, kwanza ni gharama kwa Serikali lakini pia si utawala bora, lakini tatu tunavunja haki za binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio sifa tukizungumza hapa kwamba magereza yetu yamefurika, mahabusu yetu yamefurika sio sifa hata kidogo, ni dalili za kutokuwa na utawala bora, hatutendi haki. Maana yake mimi ningetegemea katika utawala bora mtu akishakamatwa katika muda usiokuwa mkubwa, miezi miwili, mtu amecheleshwa sana kuhukumiwa miezi mitatu. Kama upelelezi haujakamilika, ushahidi haujapatikana wa kutosha kwa nini kesi za namna hiyo zisifutwe pale ushahidi unapopatikana, basi kesi zile zirejeshwe mahakamani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nadhani sisi tunazungumzia utawala bora, Serikali ya CCM inataka kutenda haki kwa raia wake. Kwa hiyo, kama sisi tunataka kutenda haki kwa raia wetu basi tuhakikishe tunawatendea haki hao raia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina tatizo na bajeti ya Wizara baada ya kupata majibu napenda kusema naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na mimi nianze kwa kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri na Naibu Waziri, Mheshimiwa Kapteni John Chiligati. Nawapongeza kwamba kwa miaka mitano ambayo mimi nimekuwa Mbunge nimeweza kuridhika kwamba kazi wanayoifanya ni nzuri, kwa hiyo nawapongeza sana. Kwa sababu kuna wataalam wanaowasaidia ninawapongeza pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii mwanzoni kabisa kulipongeza kwa namna ya pekee Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameonyesha kabisa kwamba makosa yamepungua kwa kiasi kikubwa ukiondoa makosa ya usalama barabarani, kwa hiyo, ninawapongeza kabisa.

Pia nichukue nafasi hii kwa namna ya pekee kabisa kuwapongeza viongozi wangu wa Jeshi la Polisi kuanzia *OCD* wa Wilaya ya Kahama na *RPC* wa Mkoa wa Shinyanga, kwa kazi nzuri sana ambayo wameanza kuifanya tangu walipofika katika Mkoa na katika Wilaya ya Kahama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kwamba sisi Wabunge wa Kahama tulikuwa na malalamiko makubwa sana juu ya usalama katika maeneo yetu ya Kahama na Mkoa wa Shinyanga. Lakini tangu viongozi hawa wafike kwa kweli wamechapa kazi ile ambayo tunaridhika na hali ya usalama imekuwa nzuri sana. Nizidi kupongeza pia hata Jeshi la Polisi Makao Makuu kwa sababu bidii za hao nina hakika kwamba zimepata *support* kutoka juu kwa maana ya nyenzo na vitu vingine ikiwa ni pamoja na kufungua vituo katika maeneo ambayo tulidhani vikifunguliwa Vituo vya Polisi kazi itakuwa nzuri zaidi.

Katika Jimbo langu la Msalala tumefungua vituo vipya vinne katika kipindi cha chini ya miaka miwili, kitu ambacho ninakiona ni maendeleo makubwa na kwa sababu ya *support* ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kumpongeza *Inspector General* wa Polisi ambaye alichukua muda kufika katika maeneo yetu kuangalia vituoa na kuwatia moyo askari walioko huko kwa kazi nzuri waliyokuwa wakiifanya. Lakini vile vile namshukuru kwa sababu aliweza hata ku-*support* ujenzi wa nyumba za askari katika Kituo cha Kagongwa. Lakini vile vile akatupa ahadi kwamba atatusaidia kutoka ofisini kwake angalau kuweka umeme katika Kituo cha Kagongwa na mimi nalizungumza hili ili kuwakumbusha tu wasaidizi wake muweze kuliangalia hilo ili kituo kipate umeme. Kwa sababu kufanya kazi ya ulinzi kwa kutumia vibatari sidhani kama ni ulinzi wa uhakika sana. Kwa hiyo, nafikiri hilo mta-*take note.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nina mambo mawili mengine ya kuzungumza, moja limezungumzwa vizuri sana na Mbunge wa Musoma Mjini, Mheshimiwa Ibrahimu Marwa kuhusu tatizo la upelelezi. Nafikiri pengine hata katika mazungumzo ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri humu haionyeshi mkakati kabambe unaoweza kuleta ufumbuzi wa suala la ucheleweshwaji wa upelelezi. Pengine labda ni uchache wa askari wanaohusika na hii Idara ya Upelelezi au namna gani, lakini bado hatujajua, pengine sijui ni uhaba wa vifaa au vitendea kazi katika Idara ya Upelelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ukichukua kwa mfano mtu amekaa mahabusu miaka 10 hata hivyo vyanzo vya upelelezi wako unaanzia wapi? Hata wale aliogombana nao kama ilikuwa ni ugomvi, kama ilikuwa ni kufanya nini pengine walishahama, pengine wengine walifariki. Unapelelezaje katika mazingira ya miaka 10? Bado kuna vyanzo kweli vya habari kupata kwamba huyu mtu alilifanya hili kosa? Sidhani mimi kama bado kuna vyanzo. Nafikiri kama kuna tatizo katika eneo hili ni mrundikano wa mahabusu katika Magereza yetu ni tatizo. Kama kuna tatizo kwani Wizara haiwezi kuja na mpango kabambe na sisi tukakubali kutoa Bajeti hiyo ili tatizo la upelelezi liishe? Makosa yapelelezwe kwa haraka, upelelezi ukamilike na watu hawa waweze kutendewa haki kwa sababu kukaa mahabusu miaka 10 sijui anakuja kuhukumiwa miaka 10 mingine then utakuwa umemuadhibu miaka mingapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka tu nilizungumze hili najua limezungumzwa na wenzangu vizuri, lakini kwa maana ya uzito wake labda mimi ningependa Waziri atueleze kama kuna mkakati wowote kabambe wa kuondokana na tatizo hili la mahabusu kukaa miaka mingi namana hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zipo hapa katika ukurasa wa 60 wa hotuba yake. Kuna mahabusu waliokaa zaidi ya miaka 10, miaka 8 sasa hebu tuambie kama kuna mikakati kabambe au tumeridhika na hii hali. Nafikiri hii si nzuri kwa sababu mtu mwingine kwa kweli ametuhumiwa na hana hatia, sasa miaka 10 yuko jela? Si haki. Nilitaka nilizungumze kwa sababu limezungumzwa sana sitaki kuendelea nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina lingine moja, ulinzi wa jadi (Sungusungu). Ulinzi wa Jadi nafikiri ni ulinzi ambao umeleta au umechangia kwa kiasi kikubwa sana katika upungufu wa matukio kama ambavyo hotuba ya Waziri imesema kwamba uhalifu umepungua kwa asilimia kubwa tu, sikumbuki ni asilimia ngapi alisema. Lakini nafikiri sungusungu ni sehemu kubwa sana ya mafanikio hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu na kila mtu anafahamu askari polisi tulionao ni wachache, vijiji tulivyonavyo ni vingi mno sasa watu wamekuwa wakijitolea kuendesha shughuli za ulinzi na usalama kule vijijini katika huu mfumo wa sungusungu. Lakini niseme tu kwamba kumekuwepo na bahati mbaya, tumekuwa tukizungumzia hapa mara kwa mara ile migongano ya kiutendaji baina ya hawa walinzi wa jadi sungusungu na hawa walinzi waliosoma yaani polisi. Kumekuwepo na migongano ya mara kwa mara katika utekelezaji wa majukumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi utakuta kwamba katika shughuli ya ulinzi wa sungusungu linapokuwa limejitokeza tatizo pengine aliyedhaniwa kuwa mualifu ameadhibiwa kiasi ambacho akaleta malalamiko polisi, hawa viongozi wa sungusungu wanakuja kusombwa bila utaratibu na wanakwenda kuongezwa kwenye hii idadi ambayo tunailalamikia hapa ya kesi zisizopelelezwa kwa miaka mingi sana. Wapo sungusungu kesi zao zinapelelezwa kwa muda mrefu sana katika mgongano wa utendaji wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukizungumza na mimi katika Wizara hii jambo ambalo nimekuwa nikilizungumzia sana ni hili hili la sungusungu kwa sababu eneo langu kwa ujumla ninaloliwakilisha hapa Bungeni linalindwa zaidi na hawa sungusungu kuliko Askari wa Polisi. Askari wa Polisi walioko Jimboni kwangu takribani hawazidi 20, lakini hali ya ulinzi na usalama imekuwepo. Sasa ni wajibu wangu kulizungumza sana hili kwa sababu nimekuwa nikiliona kama mgongano, kuna sungusungu wengi wako kwenye mahabusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilidhani kwamba Wizara ingejaribu tena na kuweka mkakati kwanza, tulisema wapewe elimu sungusungu hawa, wapewe elimu na mafunzo ya mara kwa mara. Lakini pia tulishasema wafanye kazi bega kwa bega na polisi, sasa kinachotokea hapa ushirikiano uliopo ni ushirikiano wa kukomoana. Wanasubiriwa sungusungu wafanye kakosa kadogo, hata kakosa kakubwa basi wawekwe mahabusu kwa miaka chungu mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii tunawakatisha tamaa kufanya kazi na wakikata tamaa kufanya kazi sidhani kama polisi wataweza kuhudumia kwa maana ya kutoa huduma za kiusalama katika vijiji vyote, kama sungusungu wataamua kususia kazi, sidhani kama polisi wataweza kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sungusungu ilianzaje labda? Ukienda kwenye historia ilivyoanza hii sungusungu miaka ya nyuma hapakuwepo na sungusungu labda iwe ya nyuma sana lakini kuna chanzo cha sungusungu ilivyoanza. Kuna mtafiti mmoja anaitwa Dr. Brian wa Chuo Kikuu cha Califonia alisema kwamba sungusungu ilivyoanza Tanzania ilianza hivi naomba ninukuu ameandika kwa kiingereza yeye alifanya *study*

anasema kwamba *I studied two system of inform of source of control, first in Tanzania East Africa, I investigated tribal justice organizations that imaged when one tribal* ni *Wasukuma became fed up with cattle-rustlers and weak state support.* Wananchi waliona kwamba *state* haifanyi kazi inavyopaswa ndipo walipoanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile hata sasa ni matukio mangapi yanaweza yakatokea, nitaje ninayoyafahamu Jimbo langu kwenye kijiji kama cha Bulige ukampate polisi kilometa 60 Kahama Mjini tukio litakuwa limeshatokea kule na unapokwenda kumpata askari polisi kule Wilayani anakwambia gari halina mafuta, uchange shilingi 200,000 za mafuta ili ufike kwenye tukio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa nini Serikali inashindwa kutambua umuhimu wa hawa watu wanaojaribu kuisadia kuleta hali ya amani katika nchi hii? Ninavyoona mimi sababu za kuanza kwa sungusungu bado ziko hai hata leo kwa sababu uwezo wa Serikali kutoa huduma ya kiulinzi na kiusalama bado si mkubwa kiasi cha ku-*cover* maeneo yote. Sasa ni vizuri basi hawa sungusungu tuwape moyo, Serikali iwape moyo iwa-*support,* yanapotokea makosa kwa mfano mauaji yametokea katika harakati za kujilinda inatokea bahati mbaya hata kwa askari wa polisi mauaji yanatokea na uchunguzi unafanyika. Ningeomba na ninaleta ombi maalum, sikatai kwamba pengine wakifanya mauaji sungusungu pasifanyike uchunguzi, ufanyike uchunguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningeomba uchunguzi unapofanyika kwenye eneo kama la sungusungu basi lipewe umuhimu kwamba hawa walikuwa wananchi kwenye harakati za kulinda amani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani watu holela wakajikusanya kwenda kumuuwa mtu, haiwezekani, lazima kuna sababu kwa mfano jambazi ana gobole au ana bunduki. Niliwahi kuulizwa swali, naomba niulize labda nitasaidiwa majibu na wenzangu hapa. Nilikwenda kwenye mkutano mmoja kijijini, nikakutana na wananchi wakaniuliza ninyi viongozi wetu kila siku mnatuambia sisi tusichukue sheria mkononi kuwaua majambazi, mnafahamu kabisa majambazi wapo na wanakuja, lakini hatujawasikia hata siku moja mnawaambia majambazi mkienda kuiba msiwaue wananchi. *(Kicheko)*

Sasa sijui kama wenzangu Serikalini wana majibu ya hili, mimi nilikosa majibu. Sasa wananchi wanapokwenda kuuwawa wakijilinda wakamuuwa anayetaka kuwaua inakuwa nongwa kubwa wanakaa mahabusu muda mrefu kwa nini? Lakini hata Askari Polisi si wanauwa wakati mwingine inapobidi? Na wenyewe wanakaa mahabusu miaka mingapi? Au ni sisi wa vijijini tu? Sisi walinzi tusiosoma? Lakini sisi walinzi tusiosoma pamoja na kwamba hatujasoma kazi tunayoifanya kama nilivyosema ni kubwa, iheshimiwe na itambuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba sana suala la sungusungu na bahati mbaya hata kwenye hii hotuba halijazungumziwa, limezungumzwa nafikiri kidogo kwamba kwenye ukurasa wa 25 katika kipengele (l) kwamba kuna maandalizi ya awali ya kuanzisha utaratibu wa polisi jamii, sijaelewa kama ndio sungusungu hiyo au ni kitu

kingine sijaelewa. Lakini nilikuwa najaribu kubahatisha kama pengine ndio usungusungu unazungumziwa vinginevyo hapazungumziwi mahali popote sungusungu.

Nilikuwa nadhani Serikali ni muhimu ikaendelea kutambua kwamba sungusungu wanatufanyia kazi nzuri katika Taifa hili na kwa kweli tuheshimu mchango wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba nichukue nafasi hii kusema kwamba naiunga mkono hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani kwamba tuwape pesa wakaendelee kutekeleza haya. Lakini hili la sungusungu kwa kweli waliangalie kwa macho mawili. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED ABDULLY ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii, sidhani lakini nadhani mimi ndio nitakuwa wa mwisho. Kwanza na mimi naunga mkono hii hoja hatuna sababu ya kuitakaa moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawatakiwa mafanikio na yote waliyokusudia wayatende kama yalivyo, lakini nina machache naomba kuyasema.

Kwanza mimi nilikuwa Mbunge wa Maaskari wa Polisi Zanzibar kwa vile Zanzibar sasa wamegawa Majimbo sehemu ile imepelekwa Jang'ombe. Hata hivyo Jimbo la Kwahani ni la hatari, maana yake kuna jiwe ukiliangukia litakuumiza, likikuangukia wewe litakuumiza kwa hiyo, lazima ulikwepe, ukifanya mchezo utakwenda na maji katika hilo Jimbo langu la Kwahani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo nataka kulieleza polisi kwa kule Zanzibar wamefanya kazi nzuri kweli kweli katika uandishi, wamefanya kazi ya maana hasa ya ziada kwa sababu tumepata usalama mkubwa na tumeweza kuishi vizuri vyama vyote tumeishi vizuri hakuonei mtu yeyote, sote tumeishi vizuri. Kwa hivyo, ninalotaka kuliomba sasa tunakwenda katika uchaguzi, polisi wazidishe juhudi, wazidishe ulinzi kama walivyofanya ili tuwe salama. Kwa sababu Zanzibar vyama viwili ndio vikubwa, kikubwa kabisa ni CCM kinachofuatia ni *CUF.* Lakini hao wote ni ndugu, ukichukua *CUF* wana ndugu CCM, ukichukua CCM wana ndugu *CUF.* Kwa hivyo, kazi waliyoifanya naipongeza na naomba sana wazidishe juhudi, namwomba Kamishna wangu Khalid, amefanya kazi nzuri nampongeza ajitahidi. *(Makofi)*

Pili si vibaya nampongeza rafiki yangu *IGP,* Omar Mahita, kwa kweli alikuwa akinithamini sana kama Mbunge wake pale kila akija na mimi ananiita ananiuliza tufanye nini kuna tatizo gani? Kafanya hivyo mara nyingi tu kanialika mara nyingi tu tunachangiana fikra mimi na Wabunge wenzangu. Lakini mimi nilikuwa zaidi, kwa sababu mimi ndio Mbunge wa Maaskari pale na amenitendea wema wakati mzuri. Amenifanyia jambo sitalisahau, nilikuwa na kijana *Form IV* ikazidi miezi miwili akawa anakataliwa kujiunga na Jeshi la Polisi kwa sababu kazidi miezi miwili, *IGP* akasema nyie namna gani *Form IV* sisi tunatafuta sasa hivi awekwe hapa yumo, kwa hivyo, sitalisahau niseme kweli namshukuru.

Jambo lingine Polisi kule Zanzibar ndio wanaoshughulika rushwa, kwa hivyo polisi wanatuambia watusaidie, tuwasadie. Sasa kuwasadia kwangu ni kwamba kuna

kijana mmoja nina shaka anauza unga au amepewa rushwa ana gari jipya na yeye hana uwezo ni Diwani. Najua siwezi kumtaja, nikimtaja hapa yeye hawezi kunijibu, lakini ana gari jipya wanaohusika wamchunguze huyu Diwani wa Mikunguni kalipata wapi gari hilo, si rushwa hiyo au anauza unga? Siyo vibaya kusema mimi naweza, hivyo naomba hilo Polisi wa Zanzibar walitafute. Diwani wa Mikunguni ana gari jipya kalipata wapi na yeye ni Diwani tu mshahara shilingi 30,000 kapata wapi gari hilo naomba polisi mfanye hiyo kazi.

Lingine naomba kulichangia kwamba polisi wamejitahidi sana wamepata nyumba za Tunguu. Lakini haziridhishi zile nyumba za Tunguu ni muda mrefu sasa zimekaa vibaya na sasa hivi kule ndio mji uko Ofisi ya Bunge iko pale, Ofisi ya *Immigration* iko pale na watu wamepewa viwanja wajenge nyumba za kisasa, zile nyumba za polisi bado zinaonyesha sura mbaya. Naomba wazishughulikie kidogo, wazipige rangi, zitengenezwe kidogo nyingine zimeanguka mabati, ndio Mji Mkuu sasa unahamia pale. Ofisi za Serikali zinajengwa pale kwa hivyo, naomba hilo polisi mlishughulikie.

Jambo lingine ni vyeo, siku zote mimi nilikuwa nikipiga kelele hapa kuhusu vyeo na nitaendelea. Koplo katika Jeshi la Polisi haina haja ya kusoma anasoma nini, mtu kafanya kazi miaka 15 au 20 unampeleka akasomee Koplo kwa nini hapewi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi za kipolisi hajafanya kosa, kazi za polisi anazitengeneza zile zile anafanya maadili ya kazi mazuri, unamchukua mtu mzima ameshafanya kazi miaka 20 unaenda kumpa Koplo bwana si unamdanganya hivyo, angalau akirudi kule anarudi *Sub-inspector* afadhali. Kwa hivyo, polisi jamani naomba cheo cha Koplo kisitolewe kwa kusoma apewe tu mtu kutokana na utendaji wake wa kazi, naomba hilo. Miaka yangu 10 niko katika Bunge hili naomba suala hilo rafiki yangu *IGP* hujalitizama, hebu litizame.

Jambo lingine ninaloliomba kulisema ni pensheni. Nina ndugu yangu marehemu Mungu amlaze mahali pema, anaitwa Salum Omar Swallah, alikufa Tanga. Kama maofisa mnakumbuka sasa mwaka wa nne alikufa Tanga alikwishafanya kazi miaka 12 jeshini na toka kufa kwake mpaka leo miaka 14 kiinua mgongo siku moja nimekuta mzee wake juu baada ya kupiga kelele Bunge hapa nikamkuta, nikamwambia vipi anasema sijapewa pesa lakini nimeletewa shilingi 50,000. Sasa nikamuuliza 50,000 ndio kiinua mgongo? Shilingi 50,000 umepewa unyamaze? Shilingi 50,000 hii umepewa ya nini? Akasema sijui lakini nimepewa shilingi 50,000 naomba polisi mlitizame hili. Yule kijana kafanya kazi miaka 12 ana mke ana watoto tena mkewe ni polisi hivyo hivyo, halafu kakaa miaka 12 kusubiri kiinua mgongo, sasa utapewa shilingi 50,000, shilingi 50,000 ni nini? Kwa hiyo, naomba polisi hilo waliangalie.

Jambo lingine nililotaka kulizungumza kwamba hivi sasa kuna utoaji wa *passport.* Kwa kweli tuliambiwa *passport* hizi zitakwisha, ziwe zimekwisha muda wake mwezi Septemba. Kwa hivyo watu wengi wamevamia katika Vituo vya *Immigration,* wengi kabisa ili kukimbilia muda, tumesikia muda wa maongezi lakini haujulikani. Sasa itolewe kauli rasmi kwamba muda ulioongezwa ni upi? Mpaka ile *passport* yako iishe au unaweza ile ile ukaitumia kwa muda wa miaka mingine mitano au muda gani? Hatujui.

Sasa ukienda *Immigration* wanataka wakusadie, wakupe *passport* haraka, lakini wamezidiwa na watu. Kazi nyingi wanazo, watu wengi, watu wanasongamana pale kila mtu anataka *passport* sasa hii vile vile mliyoikataza nyie polisi lazima itatokea pale mtu hakusudii lakini itatokea tu kwa sababu mtu anataka *passport* na yule mwingine hana uwezo wa kutoa, itatutoa halafu inaweza kutokea takrima, siyo rushwa takrima. Kwa hiyo, naomba liangaliwe hilo ili matatizo ya takrima yaondoke, rushwa hapana sasa kuna takrima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kulisema ni kwamba mbali na kufanya kazi na Maofisa wengi wa polisi lakini nimefanya kazi karibu sana na Mheshimia rafiki yangu Kepteni John Chiligati, kwa kweli ametusaidia sana. Siyo vibaya ametusaidia sana kijana huyu sijui kama kijana au mzee kama mimi, lakini amefanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kepteni  John Chiligati, anakubali kulala kijijini kulikokuwa hakuna umeme, lakini ile aondoe dhiki za wananchi, aondoe dhiki za polisi. Usiku anatoka tu na suruali yake kipande hivi kama gangwe anapita kutembea katika kituo anatazama hali ya *environment* ya pale, anajua hapa pana tatizo fulani. Analitatua kwa uzuri kabisa na haraka kabisa kwa hivyo namshukuru Mheshimiwa Kepteni John Chiligati na Maofisa wake wote wamefanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine Askari Polisi kule kwetu Zanzibar wanakaa katika nyumba za ghorofa, siyo nyumba za mabati kama hapa Dodoma za ghorofa zina umeme, zinatiwa rangi kabisa zinaangaliwa. Lakini ukishakuwa kwenye nyumba ile polisi anajisahau maana yake ikifika saa 1 usiku wanawasha tu umeme taa wala halipi anapiga *TV* yake, anacheza *disco* lake anasahau kujenga nyumba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, naomba utolewe mkopo maalum au wito maalum kwa askari polisi wapewe, walazimishwe kila askari ajenge nyumba, lazima. Kwa sababu walipotoka wanakuwa katika hali mbaya sana kwa sababu hawana ile nyumba hakupata nafasi ya kujenga nyumba kwa sababu ya uchache wa mshahara wanaopata wa shilingi 80,000 ni kweli polisi unampa 80,000?

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi 80,000 ni pesa kidogo sana lazima tumuangalie jamani Afisa wetu wa Polisi au Askari wa Polisi kwamba apewe fedha zaidi kitu maaluma wanafanyiwa watu. Wanafanyiwa Madaktari, wanafanyiwa walimu na polisi wafanyiwe, waongezwe mshahara, waongezwe mshahara angalau askari apate shilingi 140,000 iwe hiyo ndio *take home* yake, tena yale matatizo, mauza uza yake ya kukopa wapi hii hali yake mwenyewe lakini mshahara wake kama hakukopa angalau apate shilingi 140,000.

Lingine ni kuhusu kiinua mgongo, tumepiga kelele sana wamejitahidi sana wenzetu lakini tatizo ni nini kinakwamisha mpaka polisi anamaliza kazi hapati kiinua mgongo chake ni kitu gani mimi sikijui.

Niliomba kule Zanzibar ifunguliwe *Sub-office* ya *Account.* Mtu akishamaliza tu polisi kazi anapewa taarifa zake zote pale kama miezi mitatu inafanywa mahesabu na nini anapewa mwenyewe. Lakini polisi anafika mpaka kufa hapewi kiinua mgongo chake nini tatizo, tatizo kitu gani hili sugu lisilotatuka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli polisi wako wengi tunajua na *record* zao zipo mbalimbali lakini ofisi maalum iwepo, iwe inashughulikia, kazi yake iwe kiinua mgongo tu au pensheni tu, asipate tatizo polisi huyu anafanya kazi nzito tusione sisi tunalala pale, tunalala usiku na mama umekaa hivi yeye anaranda nje anakulinda wewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yeye hana nafasi ya kulala na mama wewe umelala na mama na *TV* unatazama, unatazama *video* ya *X,* yeye anahangaika kukulinda wewe. Sasa jamani hata alipotoka asipate starehe, hata anapotoka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nawathamini wamenitunza sana katika Jimbo langu wamenifanyia kazi sana na leo nawaaga rasmi kwamba lile Jimbo siyo langu tena. Limekwenda kwa Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, limekwenda Jang'ombe isitoshe hapa nilipo pana jiwe ukiliangukia narudia tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukilianguakia umeumia, likikuangukia umeumia, sasa wewe lazima ulikwepe ndio hali yangu niliyokuwa nayo, mnionee huruma mwenzenu maana sijua nifanye nini, ukitamka ukisema, ukipingana, ukitia nguvu unamwona huyu sasa, ukubali tu bwana upeleke shingo uchinjwe ufanye nini? Naona mmenifahamu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimekaa vizuri na polisi, nimeona, nimekaa vizuri sasa mtu anakuja kunichinja kiurahisi. Hapana sababu ukiuliza sababu ni nini hata wewe uje umchinje mwenzio hapana kwa sababu unaona umenona tu akuchinje basi ndiyo hali yenyewe ilivyo katika Jimbo langu la Kwahani, mnipe pole jamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kumalizia kwa mkono wangu kwa kuunga hoja, lakini kama mkija katika Afrika Mashariki tena msiniache. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumalizia hapa kwa kuunga mkono hii hoja mia kwa mia na ninawatakia kheri Maafisa wa Polisi, viongozi wa polisi na mimi mnitakie kheri mkinikuta njiani mnigaie chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie hoja iliyo mbele yetu. Lakini kabla sijaanza kuchangia hoja, ningependa kama ilivyo ada, nitoe salamu za rambirambi kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Jimbo la Manyoni Mashariki, kwa misiba iliyotupata hivi karibuni wa mwenzetu, Marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga, aliyekuwa Mbunge wa Kilombero na wa hivi majuzi tu, wiki iliyopita, wa Marehemu

Mheshimiwa Margareth Bwana, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Rukwa. Tunaomba Mwenyezi Mungu, azilaze roho zao mahali pema peponi. *Amin.*

Baada ya salamu hizi, kwa sababu ndiyo bajeti ya mwisho katika kipindi hiki cha miaka mitano, nitoe shukrani kwanza, kwa wataalam wa Wizara hii ya Mambo ya Ndani, chini ya Katibu Mkuu, tumefanya nao kazi vizuri kwa miaka mitano, nataka niwashukuru sana. Tulifika pale Wizarani tukiwa wageni hatujui chochote kwani ile Wizara ni pana sana lakini nataka kusema kwamba, wametupokea vizuri, wametupa ushirikiano mzuri, ningependa kwa dhati kabisa kuwashukuru sana kwa yote. *(Makofi)*

Vilevile tunawashukuru kwa kutuvumilia kuna wakati mwingine tuliwakera, tuliwaghasi, lakini nia kwa kweli ilikuwa ni mambo yaende sawasawa, haikuwa nia mbaya. Kwa hiyo, nasema nawashukuru sana wataalam wote wa Polisi, Magereza, Wakuu wa Zimamoto, Uhamiaji, Wakimbizi na Idara zote. *(Makofi)*

Lakini pia napenda nimshukuru kwa dhati, Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwamba katika kipindi ambacho tumekaa naye, ametuelekeza vizuri, amekuwa mwalimu mzuri katika kutuelekeza kazi. Alitushangaza alipokuja alitukuta lakini katika muda mfupi sana, nadhani hata mwezi hakumaliza, ikawa Wizara ameshaielewa vizuri, sasa yeye ndiye alikuwa anatufundisha mengine sisi ambao tumekaa miaka mingi sana. Tunakushukuru sana. Tunaishukuru SMZ kwa kumruhusu aje kuitumikia Serikali ya Muungano. Ni hazina kubwa tunaomba SMZ iendelee kumruhusu autumikie umma mpana zaidi kuliko Zanzibar peke yake. *(Makofi)*

Lakini vilevile naishukuru Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, tumekaa nayo miaka mitano, imetuelekeza vizuri, tumeshirikiana vizuri sana, nasema ahsanteni sana chini ya Mwenyekiti, Mzee wetu, Mheshimiwa John Samwel Malecela. Tunasema ahsante sana. *(Makofi)*

Nashukuru vilevile kwa pongezi mlizonipa asubuhi, lakini kwa kweli anayestahili hizo pongezi ni Waziri wangu, kwa sababu kila jambo ninalolifanya lilikuwa ni kwa maelekezo yake, ni lazima Waziri akuelekeze, akutume fanya hili na lile, kwa hiyo, kama kuna mambo yalifanyika mazuri, kama Kamati mlivyosema, basi kwa kweli anayestahili shukrani na pongezi ni Waziri mwenyewe, kwa sababu ndiye aliyekuwa ananielekeza kufanya hayo. *(Makofi)*

Nawashukuru Wabunge wote kabisa, mmetupa ushirikiano mzuri sisi binafsi, lakini hata katika Wizara nzima. Mwaka 2000 tulianza na migogoro hadi 2001 ugomvi ulikuwa mwingi ndani ya Bunge, ulianzishwa na *Brother,* Mheshimiwa Leonard Derefa, lakini baadaye tukaelewana. Tukaelewa tatizo kumbe hawa watu tulikuwa tunawatuma kazi hatuwapi nyenzo, hatuwapi vifaa, hatuboreshi lolote. Sasa tulipoanza kuongezea bajeti ya kununua zana mbalimbali na kuboresha mazingira, ndiyo haya matokeo mazuri ambayo leo mlikuwa mnatoa sifa. Kwa hiyo, nawashukuru sana Wabunge. Mtusamehe kama katika vipindi vya maswali na majibu kuna wakati tuliwakwaza, mtusamehe sana kwa sababu hapa niliposimama, unapokuwa unajibu maswali kuna joto kali, kwa hiyo, wakati mwingine unaweza ukamjibu mtu ovyo ovyo tu kwa sababu *temperature* hapa ni

kali. Kwa hiyo, tusameheane kama katika kujibu maswali tuliwakwaza hapa na pale. *(Kicheko/Makofi)*

Baada ya shukrani hizo, nimalizie na wapiga kura wangu wa Manyoni, nao ninawashukuru sana na baadhi yao leo wako hapa wamekuja, naomba msimame. *(Makofi)*

*(Hapa wageni waliotajwa walisimama)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Hawa ni Waratibu Elimu Kata, wanasimamia kufundisha somo la uraia, sasa leo wamekuja kutazama huu mhimili wa Bunge, unafanyaje kazi ili wakafundishe vizuri kule kwenye shule zao. *(Makofi)*

Nawashukuru sana Wananchi wa Jimbo la Manyoni Mashariki, wamenivumilia, tumefanya nao kazi vizuri, nasema ahsanteni sana. Baada ya hapo sasa nianze kuchangia kwa kujibu hoja. Kwa kweli hoja ni nyingi sana, mtatusamehe sana kama hatutazigusa nyingine katika kujibu, ni hoja nyingi sana na muda ni mfupi sana. Lakini baadaye tutazijibu kama kawaida katika maandishi na mtapata wote kila hoja na jibu lake kwa maandishi.

Nikianza na wale waliochangia kwenye hoja ya Waziri Mkuu na TAMISEMI, walikuwa Wabunge watano, mmojawapo alikuwa ni Mheshimiwa Charles H. Kagonji, yeye alisema kwamba, pale Lushoto, Ofisi ya Wilaya ya Polisi ni ya siku nyingi na ni chakavu, alitaka ijengwe upya na sisi tunakubali kwamba, ofisi ile ni chakavu. Tumeshafika pale tumeona, lakini fedha za kujenga Ofisi za Wilaya zote kwa mara moja na ninyi ni mashahidi, ndiyo mnaotupa hela hizo, hazipo, tunakwenda kwa awamu, kwa hiyo na Lushoto tutafika tu, sasa hivi tunajenga Kyela, Morogoro, Hanang, Kasulu, Mpanda, Namtumbo na *ishallah* na Lushoto vilevile na Kiteto tutafika.

Mheshimiwa Mathew Taki Ole-Timan, alisema *OCD* wa Ngorongoro hana gari, tulishajibu hapa wiki iliyopita kwamba, tumenunua magari 215 kwa ajili ya *OCDs,* kwa hiyo, *OCDs* wote ambao hawana magari au magari yako juu ya mawe, kwa nchi nzima, wawe na uhakika kabisa kwamba, safari hii wote watapata, pamoja na huyu wa Ngorongoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, alitoa hoja kwamba, baadhi ya Polisi kule Zanzibar, hawajarekebishiwa mishahara tangu mwaka 2004, baada ya kupanda vyeo. Hilo tatizo kweli lilikuwepo, watu wanapanda vyeo wanapata mshahara mpya wanalipwa huu mpya lakini zile *arreas* zilikuwa hazilipwi, tatizo lilikuwa ndani ya Wizara yetu na katika Wizara nyingine lakini Hazina imetoa Waraka kwa Wizara zote, unaoweka utaratibu wa kushughulikia jambo hili, wameleta *form* za kujaza *arreas* wale wote wenye madai ya *arreas* na zimekwisha jazwa na wakati wowote sasa *arreas* zitalipwa.

Mheshimiwa Gwassa Sebabili, ametoa hoja kwamba, ulinzi umeimarishwa katika maeneo ya mpakani, hasa yale yenye wakimbizi. Ni hoja halali kabisa na ndivyo tunavyofanya katika maeneo yetu yenye wakimbizi, tunao utaratibu maalum wa kupeleka

askari wa nyongeza. *OCD* anakuwa na askari wake wa kawaida na baada ya hapo tunapeleka kikosi cha nyongeza, ambacho kinashirikiana na *UNHCR* kila baada ya miezi sita tunapeleka wengine, *UNHCR* wenyewe wanawapa zana kama vile magari, *radio calls* na kadhalika. Kwa hiyo, hawa askari wanalinda makambi na vijiji vinavyozunguka makambi ya wakimbizi. Vilevile Jeshi la Wananchi kule mpakani limekaa vizuri tu kwani upo ulinzi mzuri kabisa kuhakikisha kwamba, nchi yetu iko salama.

Mheshimiwa Job Ndugai, ametukumbusha kuhusu Kituo cha Kibaigwa kwamba, nguvu za Wananchi zimetumika, kwa hiyo, kimekamilika lakini Serikali haifungui, ameomba kifunguliwe. Ni kweli kile kituo kimekamilika, hatujakifungua tu kwa sababu tukipeleka polisi leo, mahali pa kukaa hakuna, ndiyo tatizo. Tuliwaambia kwamba hamasisheni Wananchi jinsi walivyojenga kile kituo basi waendelee kujenga na nyumba za askari na sisi tutashirikiana nao. Juzi tulikwenda mimi mwenyewe, Mheshimiwa Job Ndugai, *DC* wa Kongwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kongwa tukakaa na Wananchi wa pale Kibaigwa, kuhamasishana na nina hakika pale pale kwenye kikao, zilichangwa shilingi milioni moja na laki sita ili kuanza kukarabati nyumba iliyo jirani pale. Kwa hiyo, kwa moyo huu wa juzi, nina uhakikika mpaka kufika Septemba, walau nyumba ya kuanzia itakuwa imekamilika na sisi tutafungua kituo na kupeleka askari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Henry Shekiffu, amezungumzia tatizo la nyumba za askari wa magereza kule kwake. Ni kweli tatizo hilo lipo na kama ilivyo kwa Jeshi la Polisi, tunajenga nyumba za askari magereza kwa awamu, kwa hiyo na kule Lushoto vilevile tutafika.

Mheshimiwa Leonard Shango, amesema tufufue trekta la Gereza la Kilimo Ushora, alisema tuliahidi lakini hiyo kazi haijafanyika. Mheshimiwa Shango, Gereza la Ushora ni la Kilimo na hilo trekta limepangiwa kukarabatiwa katika bajeti hii ya 2005/2006, kwa hiyo, ukiipitisha basi unapitisha na fedha za kukarabati trekta la Ushora.

Mheshimiwa Venance Mwamoto, ameshauri Gereza la Mgagao liwe Chuo cha Magereza. Tumepokea hoja yake, lakini sasa hivi Gereza la Mgagawo ndilo Gereza rasmi la Wilaya ya Kilolo, kwa hiyo, tukifanya haraka haraka kulifanya kuwa Chuo, maana yake sasa Wilaya ya Kilolo itakuwa haina Gereza la Wilaya, itabidi sasa wale wafungwa na mahabusu tuwe tunawachukua toka Kilolo tunawapeleka katika Wilaya nyingine. Kwa hiyo, kwa sababu hiyo, kwa sasa hivi mpango wa Wizara ni kuliacha Gereza la Mgagawo liwe ndilo Gereza rasmi la Wilaya ya Kilolo.

Mheshimiwa Willbrod Slaa, ameuliza ni lini tutaanza kujenga Gereza la Mahabusu pale Karatu. Jibu ni kwamba, tumeshaomba eneo, Halmashauri ya Karatu wameshatoa eneo kwa Magereza, tunashukuru wametupa hekari 50. Kwa mwaka huu tutatoa fidia ya shilingi milioni saba ili kupata lile eneo liwe mali ya Magereza kama maandalizi ya kuanza ujenzi rasmi mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Profesa Juma Mikidadi, ametoa hoja Gereza la Kibiti lifanyiwe ukarabati. Ni kweli tunayo programu ya kufanya ukarabati wa magereza yote nchi nzima,

tunakwenda kwa awamu na huko tutafika. Lakini vilevile Mheshimiwa Profesa Mikidadi, amezungumzia suala la Kituo cha Polisi cha Kibiti kupewa gari. Sasa hivi uwezo tulionao ni kutoa magari kwa ngazi ya Wilaya kwa *OCDs,* kwa hiyo, vituo ambavyo viko nje ya Makao Makuu, mgao wao si huu wa sasa, sasa hivi tunalenga kwenye ofisi za *OCDs* na Maafisa Wapelelezi wa Wilaya, hawa wote watapata magari. Vituo ambavyo vipo nje ya Wilaya tunaomba visubiri kama hiki cha Kibiti.

Mheshimiwa Aggrey Mwanri, ananitazama kwa makini, kwa sababu na yeye ana ombi linalofanana na hili, ana kituo chake cha Sanya Juu. Sasa jibu la Mheshimiwa Mwanri ni sawa na la Mheshimiwa Profesa Mikidadi kwamba, sasa tunashughulika kwanza na *OCDs, OCD* wa Wilaya ya Hai akiishapata gari hivyo vituo vingine navyo tutafika tu. Lakini tunawapa madaraka *RPCs,* ni vema kama kituo chake kimoja kimepata gari jipya na liko lingine pale ambalo lilikuwa la zamani na linatengenezeka, tunasema yatengenezwe ili yaende kuhudumia vituo vya nje kama kile cha Mheshimiwa Mwanri na cha Mheshimiwa Profesa Mikidadi.

Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, ana hoja ya gari pale Mwanhuzi. Kama ni kituo kikubwa, nadhani hiki ni cha Wilaya, kwa hiyo, kitakuwepo katika mgawo wa haya magari 250. Anasema ujenzi wa kituo unasuasua, japo *IGP* aliahidi kuchangia, tutakaa na viongozi wa Meatu, tuone ni kwa nini kituo kinasuasua ili tuendelee kushirikiana tupate Kituo cha Polisi cha Wilaya.

Mheshimiwa Edson Halinga, amesema ujenzi wa Gereza la Wilaya ya Mbozi ambao haujakamika, je, utakamilika lini? Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Halinga kwamba, wakaguzi wametoka huko juzi tu walikuwa wanakagua majengo haya ya Magereza, juzi tu, wiki iliyokwisha, wametoka Mbozi kwa sababu wewe uko hapa tangu mwezi wa sita mwanzoni sasa kule mambo yamefanyika. Lile Gereza wametuambia sasa kwa kiasi kikubwa limekamilika, bado rangi tu, kwa hiyo, katika wiki chache zijazo, rangi itakamilika na Gereza litafunguliwa katika muda mfupi ujao.

Mheshimiwa Edson Halinga, vilevile aliomba trekta katika Gereza la Vwawa. Jibu ni kwamba, matrekta tunayopata ni machache, kwa hiyo, hayo machache tunayapeleka kwanza kwenye yale Magereza makubwa yenye kilimo kikubwa. Kwa hiyo, Gereza la Vwawa msubiri kidogo.

Mheshimiwa Edson Halinga, vilevile alikuwa na suala la Koplo Mwasinya huyu aliyejinyonga, sasa anasema familia yake ilikataliwa kulipwa haki za mirathi, anaomba kupata maelezo. Maelezo ni kwamba, hapo zamani kweli tulikuwa na sheria kwamba, mtumishi akijinyonga ilikuwa malipo ya mirathi sheria ilikuwa inakataza, sasa sheria hii imebadilika, mtumishi akijinyonga bado warithi wake watapata mirathi, kwa hiyo, suala hili linashughulikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Herbert Mntangi, alisema kuwa katika Gereza la Kilulu nyumba ni mbovu. Ni kweli mimi na yeye miezi mitatu iliyokwisha tulilitembelea Gereza hili na mimi nilishuhudia. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mntangi, naomba tu usubiri tunakwenda kwa awamu. Hela za kujenga magereza yote, kwa kweli hatuna, ndiyo ukweli wenyewe,

lakini tatizo tunalijua, tulifika na wewe ni shahidi, tumekuwa na wewe lakini tunaliweka katika kipaumbele Gereza hili la Kilulu.

Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, anasema ana mpiga kura wake Ndugu Said Al-Jabri, alitoa huduma katika Gereza, hajalipwa. Magereza wanakubali kwamba, huyu Mwananchi alikuwa ni mzabuni, alitoa huduma na hawa wako wengi waliotoa zabuni halafu hawajalipwa. Lakini huyu ni mmojawapo ambaye madeni yake yameshahakikiwa, ni sahihi na yameshapelekwa Hazina ili waweze kulipwa, kwa hiyo, asubiri wakati Hazina wanakamilisha utaratibu wa malipo.

Mheshimiwa Venance M. Mwamoto, ameulizia habari ya kurudishiana wafungwa anasema haoni kama tunaitekeleza. Ni kweli mwaka 2004, tulipitisha hapa sheria ya nchi yetu, turudishiane wafungwa na nchi nyingine. Sheria hii inafanya kazi pale nchi mbili tunapokubaliana kurudishiana wafungwa, mpaka sasa tunakamilisha utaratibu wa kurudishiana wafungwa kati ya Tanzania na Mauritius. Kwa hiyo, muda si mrefu tutaanza kupokea Watanzania ambao wamefungwa kule Mauritius, kwa sababu Mawaziri wanaohusika watakamilisha taratibu zote za kisheria na wakati wowote tunaweza kurudishiana wafungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa George M. Lubeleje, alikuwa na hoja nyingi sana, lakini nianze na hii ya kuwapatia vifaa vya kisasa Zimamoto na Uokoaji. Ndivyo tunavyofanya, kila mwaka sasa hivi tunaongeza Halmashauri za Miji kuzipatia magari ya Zimamoto. Kwa mfano, bajeti ya mwaka 2004/2005, tulitoa hela kwa ajili ya magari ya Tanga, Tabora, Kigoma, Mtwara, Mbeya, Iringa, Ruvuma, Musoma na Sumbawanga, magari haya mkishawekeana Mkataba wa Ununuzi, ndipo wanaanza kuyatengeneza, kwa hiyo, inachukua karibu miezi sita mpaka minane hadi kufika. Mheshimiwa Ibrahimu W. Marwa, alikuwa anasema sasa mbona mmesoma kwenye hotuba lakini magari hatujayaona? Haya magari ni *special,* huwezi kwenda dukani kulinunua, mnawekeana Mkataba wa kulinunua ndiyo wanaanza kukutengenezea. Kwa hiyo, magari hayo yameshanunuliwa tayari na yako njiani yanakuja. Mwaka huu kama Mheshimiwa Waziri, alivyosoma kwenye bajeti, tunanunua magari ya zimamoto kwa Miji ya Lindi, Kibaha, Singida, Morogoro, Dodoma, Bukoba na Moshi. Tutaendelea hivihivi mpaka Miji yetu yote iwe na magari ya zimamoto na vifaa vinavyoendana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Beatus Magayane, ameonesha wasiwasi kwamba, Kikosi cha Zimamoto hakina mwenyewe kwa sababu kuna Zimamoto nyingine ziko Halmashauri, vikosi vingine viko Bandari na vingine viko *Airport.* Hili ni kweli lakini linashughulikiwa, sasa hivi inaandaliwa Sera ya Zimamoto na baadaye itafuatiwa na Sheria ya Zimamoto, ambayo inalenga sasa kuondoa hii dosari kwamba, kila mtu anajifanyia kivyake vyake, walau tuwe na mratibu mwenye nguvu ya kisheria ili moto ukiwaka mahali ambao ni mkubwa, aweze kutoa amri kikosi chochote cha Zimamoto, mahali popote kilipo, kiende kwenye tukio, hili linakuja.

Mheshimiwa Beatus Magayane, vilevile alikuwa na hoja nyingine ya mzabuni aliyesha mahabusu. Sasa hili niseme kwamba, limelalamikiwa vilevile na Mheshimiwa

Paschal Degera. Zamani ilikuwa Wizara ya Mambo ya Ndani ndiyo tulikuwa tunapata *Vote* ya kulisha mahabusu walioko kwenye mahabusu za Polisi na mahabusu waliokuwa katika Mahakama za Mwanzo. Jinsi miaka ilivyokwenda, tumegundua kwamba, wale mahabusu wa Mahakama za Mwanzo, ambao wako Vijijini, udanganyifu unakuwa ni mkubwa sana, madai hewa ni mengi sana kwa sababu tuko mbali sana. Kwa hiyo, kuanzia tarehe 1 Julai, 2005, *Vote* ya kulisha mahabusu kwenye Mahakama za Mwanzo imehamia TAMISEMI, wao wana mtiririko wa utawala mpaka kwenye kijiji, yuko *VEO,* anaweza akaratibu mahabusu wangapi wamelala kwenye mahabusu ya kijiji, wamekula shilingi ngapi, wanaweza. Sisi Wizara ya Mambo ya Ndani, hatuwezi kufika mpaka Vijijini, kwa hiyo, *Vote* sasa imehamia TAMISEMI, ndiyo watakaolisha mahabusu wa Mahakama za Mwanzo.

Yale madeni ya zamani bado yatashughulikiwa na Wizara ya Mambo ya Ndani, kama hili ambalo Mheshimiwa Beatus Magayane, ametuletea, tutalishughulikia hili, ni la huyu Bwana Yusuph, tutashughulikia sisi Wizara ya Mambo ya Ndani, haliendi TAMISEMI. Kwa hiyo, yatahakikiwa na kwa kweli yale ambayo yamehakikiwa sasa hivi yameanza kulipwa, ambayo hayajahakikiwa watapelekwa watu kwenda kuhakiki yaliyo sahihi nayo yatalipwa.

Labda niunganishe na lingine la Mheshimiwa Beatus Magayane, la mzee ambaye anatudai. Sasa tume-*check* yule mzee lile jengo alitoa kwa polisi wakae bure, ilikuwa ni hiari yake na maandishi yapo kwamba tukae bure mpaka tutakapojenga Kituo cha Polisi, ndiyo maandishi tuliyoyakuta kwenye *record* kwa nia nzuri. Lakini kwa sababu sasa anatudai kwa ule wema aliotufanyia, akatupa nyumba yake na sisi tutafanya wema wa kumlipa. Kwa hiyo, kwa kweli hilo deni Mheshimiwa Magayane, tutalilipa mapema iwezekanavyo na Mheshimiwa Waziri, ameshatoa maelekezo kwa Jeshi la Polisi, walipe mapema iwezekanavyo, kwa ule wema au *goodwill* aliyotufanyia, japo kwa kweli mwanzo *documents* zinaonesha alikuwa ametoa kwa polisi wakae bure.

Mheshimiwa Mohamed Missanga, naye alikuwa na tatizo la mzabuni aliyelisha mahabusu, nadhani jibu ni hilo hilo kwamba, yale madai ya zamani, ambayo yamehakikiwa, Wizara ya Mambo ya Ndani italipa na inaendelea kulipa.

Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, ametoa ushauri kwamba, katika kupunguza msongamano, wafungwa wenye vifungo vifupi wafanye kazi nje ya Magereza. Sheria tulishaiweka tayari ya watu hawa wafungwe vifungo vya nje na kwenye Hotuba ya Bajeti asubuhi, Waziri, amefafanua kwamba, tunaanza na mikoa sita. Kwamba, wenye makosa madogo madogo watarudi vijijini kwao wakafanye kazi za kujitolea kwenye vijiji vyao bila malipo. Tunaanza na mikoa sita na ameitaja pale asubuhi Mheshimiwa Waziri kwamba,ni Dar es Salaam, Mbeya, Mtwara, Dodoma, Kilimanjaro na Mwanza. Mratibu wa mpango huo, ametuambia kwamba, kwa mwezi huu wafungwa 113 ambao walikuwa wakae ndani ya Magereza, wataanza kutumikia jamii nje ya Magereza na utaratibu unaanza kwa mikoa sita, mwaka 2006, tuna nia ya kuusambaza katika mikoa yote.

Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, yeye alitoa ushauri tu kwamba, wafungwa ambao ni raia wa nchi za nje, hasa wale ambao ni wakimbizi, waombewe msamaha wa Rais

watoke gerezani warudishwe makwao. Hili limeshafanyika, tayari tumekwisha wasafirisha karibu wafungwa 25, ambao walikuwa wamefungwa hapa. Mheshimiwa Rais alitoa msamaha na walipotoka ndani ya jela, wakarudishwa makwao na utaratibu huu utaendelea kwa wote ambao watakumbwa na hili, kwa sababu hatuna haja ya kuhangaika kuwatunza katika magereza yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Henry Shekiffu, ametoa hoja kwamba, kituo cha Polisi Lushoto kipatiwe gari na nguo za baridi za wafungwa. Kama nilivyosema kwamba, vituo vyote ambavyo havina magari *OCDs* wote watapata magari na nguo za baridi kwa wafungwa. Tunatoa hata juzi juzi tu, mwezi uliopita, Kamishna Mkuu wa Magereza, ametoa masweta 3,000 na yameshasambazwa katika ile mikoa yenye baridi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Leonard Shango, amesema pale Shelui tuweke *Road Block,* kwa sababu kuna magari mengi yanafanya fujo. Tumepokea ushauri, tutauzingatia.

Mheshimiwa Aridi Mwananche Uledi, amesema kwamba, Mangaka Kituo cha Polisi hakuna gari. Tunashughulika kwanza na *OCDs,* tukishamaliza shida za *OCDs* tutafika kwenye vituo vya nje kama kule Mangaka.

Mheshimiwa Lydia Boma, amezungumzia habari za kujengewa nyumba za askari. Kwa kweli tumeshaanza na kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ameeleza baadhi ya idadi ya nyumba ambazo tunazijenga, kwa hiyo, tunaendelea kujenga hatuwezi kufika kila mahali kwa wakati mmoja, lakini mpaka Mtwara tutafika kwa sababu kazi imekwisha anza.

Mheshimiwa Aggrey Mwanri, kuhusu gari la Siha, nimeshakujibu naomba utusamehe sana lakini ndiyo ukweli wenyewe, penye nia pana njia.

Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, kuhusu ukarabati wa nyumba za polisi Mjini Magu, ziko kwenye programu ya ukarabati mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa William Lukuvi, amesema Paroko ametoa pikipiki kwa kituo cha Mingoli kwamba, tumwandikie barua ya kumpongeza. Kwa hiyo, tunataka nimpongeze mbele ya Bunge hili, kwanza, nitoe pongezi za dhati kwa Paroko na Maparoko wengine waige mfano, wasaidie mapolisi wetu wapate usafiri. Alijenga vilevile Kituo cha Polisi, tunamshukuru sana na sasa shukrani za barua ya Waziri zitafuata. *(Makofi)*

Kuhusu pikipiki kwa kituo cha Pawaga, ombi tumelipokea, ngoja tulifanyie kazi, tutaona kama hali ya bajeti itakavyokwenda.

Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, amezungumzia suala la kuchelewa kurekebisha mishahara ya polisi, baada ya kupanda vyeo. Hili ndilo lile nililosema kwamba, sasa Hazina wanalishughulikia, wametoa Waraka Maalum wa kushughulikia suala hili, nina uhakika sasa litapatiwa ufumbuzi kwa Wizara ya Mambo ya Ndani na kwa Wizara zote.

Mheshimiwa Masoud Abdulla Salim, alisema katika jengo la Kituo cha Polisi Kengeja ukarabati mkubwa unatakiwa. Hoja tumeipokea, tunayo programu ya ukarabati, tutafika mpaka Kengeja *inshallah.* Amesema pia katika kuajiri askari wa kike, hawapewi kipaumbele. Hoja tumeipokea, ni nzuri, kwa sababu katika kila Wizara lazima tutekeleze ile Sera ya Uwiano wa Jinsia na huo ni ushauri mzuri, tumeupokea, tunaufanyia kazi, kwa kweli ndiyo Sera hasa za Chama cha Mapinduzi, kutokubagua akina mama katika kazi zote, pamoja na za majeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Semindu Pawa, anasema askari polisi wafikiriwe nyumba zao na maslahi ya familia zao, wapewe *ration allowance.* Tunaupokea ushauri na wote ambao mmesema habari za maslahi ya askari, ni kweli maslahi bado ni duni, tunayo nia ya dhati kabisa kuongeza maslahi ya askari, lakini hii inategemea jinsi uchumi unavyoongezeka, tunajitahidi kuyaongeza.

Mheshimiwa Paul Makolo, anauliza kwa nini vituo vya polisi vinafungwa usiku. Vituo vya Polisi vina *grade*, sasa vile vidogo vinaitwa *Police Post,* vile ni vya kusikilizia mchana tu, havina *amoury,* ni vya doria za mchana. Kwa hiyo, vituo vya *grade* fulani huwa kweli vinafungwa saa 12.00, lakini kuna vituo vya *grade* ya juu huwa vinafanya kazi saa 24.

Mheshimiwa Stephen Kazi, amezungumzia tatizo la wale vijana wa Bugando, ambao waliuawa mwaka 2003. Ni kweli Polisi walifanya uchunguzi wakawakamata watu wanne, wakawapeleka mahakamani, lakini *DPP* alipopitia vizuri ile kesi, akaamua iondolewe mahakamani, kwa sababu ilikuwa na sura ya *mob justice,* kwa hiyo, kwa busara ya *DPP,* aliamua ile kesi iondoke Mahakamani, ndiyo maana jambo hili sasa hivi halisikilizwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ni nyingi sana na muda umekwisha, nimalizie tu kwa kusema kwamba, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza sana Wizara hii, kwa kazi nzuri sana wanayofanya katika idara zake zote. Majedwali yaliyooneshwa kuanzia ukurasa wa 47 mpaka 69, yanaeleza kwa uwazi kabisa takwimu zinazohusiana na maeneo mbalimbali. Uwazi wa takwimu hizi unaonesha umahiri wa watendaji na ni ishara kwamba, wanajua hali halisi ilivyo na wanajua wanachotakiwa kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya kutokana na ukweli kwamba, ukijua tatizo basi umeshalitatua kwa asilimia 50. Pamoja na bajeti kuwa finyu, naamini ufanisi wao utaongezeka kufuatia ongezeko tulilolishuhudia miaka ya hivi karibuni ya ongezeko la bajeti na vitendea kazi. Nawapongeza sana Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, kwa kuiongoza Wizara vyema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Line Police* Mjini Magu wamekuwa na kilio cha muda mrefu cha nyumba zao kufanyiwa *wiring* za umeme bila mafanikio. Wamefikia hatua ya kupitisha bakuli ili kazi hii ifanyike. Fedha inayohitajika haizidi hata shilingi milioni moja. Naomba Wizara ifikirie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naiunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii, kwa kuanza kuipongeza Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote na hasa Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza na Uhamiaji, kwa kazi ngumu, lakini nzuri wanayoendelea kuifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa pekee kabisa, namshukuru na kumpongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa *Capt* John Chiligati, kwa kutembelea Wilaya ya Muheza na hasa kwa kutumia muda wake kufanya mkutano na Askari Polisi, Magereza na Uhamiaji wa Wilaya ya Muheza. Pia, kwa kutembelea kituo kidogo cha Magereza eneo la Kilulu, Muheza na kukagua makazi ya Maofisa wake, bweni la gereza na hali ya chakula katika gereza hilo dogo la Kilulu, Muheza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda kutoa mchango wangu katika maeneo yafuatayo: -

Kwanza, ni kukabidhiwa nyumba za Shirika la Reli *(TRC)* zinazotumika sasa kama Kituo cha Polisi na nyumba za Polisi Muheza kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Tarehe 23 Juni, 2005, Wizara ilipokuwa inajibu swali langu Bungeni kuhusiana na nyumba za Shirika la Reli *(TRC),* ilionesha kwamba, upo uwezekano wa nyumba hizo kukabidhiwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Hata hivyo, katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri, hakuna ukarabati wa nyumba hizo hasa nyumba za Polisi ambazo ziko katika hali mbaya kutokana na mmiliki *(TRC),* kutozifanyia ukarabati kwa miaka mingi. Je, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, haioni ipo haja ya kujiandaa kuzipokea na kuzikarabati nyumba hizi badala ya kungoja kutafuta fedha za kujenga nyumba mpya baadaye?

Pili, ni kuhusu hali mbaya ya nyumba za Maofisa wa Magereza, gereza dogo la Kilulu, Muheza. Nyumba za Maofisa wa Magereza kituo hicho ni za miti, zimekandikwa kwa udongo (tope) na zinavuja. Je, hii ndiyo hadhi ya nyumba za Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii ni ya fedheha tupu kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Jeshi la Magereza na Wilaya nzima ya Muheza, haifai kuendelea kukubalika. Hivyo, iwapo Serikali kwa ziadi ya miaka ishirini iliyopita imeshindwa kujenga na hata kuboresha hali ya kituo kidogo cha Magereza Kilulu, Muheza, ni bora ikafunga kituo hicho hadi hapo itakapopata uwezo wa kukiboresha na Wananchi ambao ardhi yao imechukuliwa kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho irejeshwe kwa wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, aliingia ndani ya nyumba hizo na aliona hali halisi na ukweli wa haya ninayosema. Kwa kuwa ndani ya bajeti ya mwaka 2005/2006, hakuna mpango wowote wa kuboresha kituo hicho kidogo cha Kululu, Muheza, uandaliwe mpango wa dharura kuwapa heshima wanayostahili Maofisa na Askari wa Magereza wanaotoa huduma katika kituo hicho, la sivyo ni bora kifungwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono hoja hii, ili fedha za kuendesha shughuli za Wizara mwaka 2005/2006 zipatikane, nashauri Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, wafuatilie kwa juhudi mpango wa kumiliki nyumba za *TRC* za Kituo cha Polisi na nyumba za Polisi Muheza na kuboresha kwa mpango maalum kituo kidogo cha Magereza Kilulu, Muheza.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa hotuba nzuri na yenye uchambuzi wa kina, ambayo ameitoa asubuhi ya leo. Ni ukweli usiopingika kwamba, hotuba yake imeweka mtazamo mzuri na ambao unatuingiza katika mwaka wa fedha 2005/2006, kwa ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya. Hongera sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa *Capt.* John Chiligati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee naomba kumshukuru Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa kukubali kulitembelea Jimbo langu la Siha, hususan Kituo cha Polisi cha Sanya Juu na kuleta changamoto ya hali ya juu kwa Wananchi wa Jimbo langu, ambapo alitutaka tuendelee kuchangia ujenzi wa nyumba ya wafanyakazi kwa kujitolea, jambo ambalo tumelitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii, kuishukuru Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa kutupatia kiasi cha Sh.2,000,000/=, ambazo zitatumika katika kukamilisha ujenzi wa jengo nililolitaja hapo juu. Naomba niendelee kukumbushia ombi letu la muda mrefu, ambalo tuliomba kupatiwa gari jipya, kwani lile lililopo lina hali mbaya na mara kwa mara liko juu ya mawe kwani limezeeka sana. Gari hili litakuwa la manufaa makubwa kwani kutokana na kukua kwa Mji Mdogo wa Sanya Juu, matukio ya uhalifu yameendelea kushamiri. Aidha, wizi wa mifugo ambayo wakati mwingine hupelekwa nchi jirani, umeendelea kukua na hivyo kuwatia hofu Wananchi wa Jimbo langu, ambao wengi wao ni wafugaji na wachungaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali sana naomba suala la gari madhubuti litazamwe kwa uzito unaostahili, vinginevyo hali ya maisha ya Wananchi itaendelea kuwa mashakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine, narudia kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa mchango wangu kwenye hoja ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba nimpongeze Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa hotuba nzuri ya Wizara hii ambayo imeandaliwa vizuri. Pia, nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Viongozi Wakuu wa Wizara hii ambao ni Katibu Mkuu wa Wizara, *Inspector General* wa Jeshi la Polisi, Makamishna wa Polisi na watumishi wengine, kwa ushirikiano wao wa kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya ya Nchi, kwa kazi nzuri ya ulinzi, ambayo nchi yetu sasa ni tulivu na ina amani tele. Pia, niipongeze Serikali kwa kuboresha utumishi ndani ya Jeshi la Polisi kwa kuwapa mafunzo zaidi, kuongeza mishahara na kuwapatia fursa Askari Polisi wetu kupata mikopo mbalimbali kwa matumizi yao ili kupunguza makali ya maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jiji la Mwanza kuna matukio mawili yaliyojitokeza, ambayo yaligusa maisha ya wakazi wa Jjiji hili. Kwanza kabisa, naomba kusema wazi kwamba, matukio yote mawili yamehusisha kupotea kwa maisha ya wakazi hao wa Jiji. Bahati nzuri matukio yote mawili yametolewa taarifa kwenye Serikali. Tukio la kwanza linahusu vijana ambao waliuawa eneo la Bugando mwishoni mwa mwaka 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukio la pili linahusu kijana shupavu Mwana-CCM *(Green Guard),* kwa jina anaitwa Ibrahim Abdallah Elibaba, ambaye wana-Mwanza walikuwa wakimwita Babangida, alipotea mwaka 2004 na ninaomba nifafanue vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukio la vijana kuuawa usiku wa kuamkia mwaka mpya eneo la Bugando, Jijini Mwanza, linajulikana. Binafsi niliuliza swali Bungeni ili kupata taarifa kamili kuhusiana na maamuzi ya Serikali juu ya suala hili. Naomba ifahamike kwamba, wana wazazi wao, pamoja na ndugu zao, wanataka kujua hatma ya suala hili. Maswali haya yote kutoka kwa ndugu na wazazi yanaletwa kwa Mbunge wao wa Mwanza Mjini. Tafadhali nieleweke kwa Serikali kwamba, mimi sasa ninayo matatizo mengi mbele ya jamii ya watoto hawa. Ninasongwa na maswali magumu kiasi kwamba, hata raha sasa sina. Tafadhali ikumbukwe kwamba, nilipewa ahadi na Serikali kupata maelezo ya suala hili na hatma yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewasiliana sana na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, juu ya majibu na maelezo ya suala hili. Sikuishia hapo tu, Waziri mwenyewe wa Mambo ya Ndani ya Nchi, nimewasiliana naye ili nipate majibu hayo, lakini mpaka sasa sijapata maelezo na majibu ambayo naweza kuyapeleka kwenye jamii za vijana hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali sana ikumbukwe kwamba, mwaka 2005 ni mwaka wa Uchaguzi Mkuu, ambao mimi sasa naelekea nitabeba msalaba wa Serikali, maana jamii, ndugu na wazazi wa vijana hao, bado wanahoji na wanafuatilia sana kwangu majibu hayo. Tafadhali nipewe majibu/maelezo haya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukio la pili linahusiana na kupotea kwa kijana Ibrahim Abdalla Elibaba, maarufu kama Babangida, Mwana-CCM *(Green Guard),* ambaye mpaka sasa familia yake, yaani mke wake, baba yake na ndugu, wanafuatilia sana juu ya kupotea kwa mtu mzima kama huyo na hali kubaki kimya namna hii! Suala la kupotea kwa kijana huyu limetolewa taarifa kwenye Vyombo vya Dola Jijini Mwanza. Mke wake amekwenda mwenyewe na kutoa taarifa juu ya tukio hili, zaidi ya hapo amekwenda mara nyingi Kituo cha Polisi kufuatilia majibu ya suala hili. Baba yake na kijana huyo, ambaye sasa amepotea zaidi ya mwaka mmoja, amekwenda kutoa taarifa Polisi Mwanza na kufuatilia ili apate maelezo ya hatma ya mwanaye. Kwa taarifa tu ni kwamba, kwenye gazeti la Tanzania Daima la tarehe 30 Juni, 2005, kuna taarifa juu ya suala hili licha ya magazeti mengine kuzungumzia suala hili. Baada ya kupata taarifa hii kutoka kwa mke wa kijana huyu, ambaye huja kwangu kutaka msaada na kuniomba nifuatilie suala hili, ili pia apate majibu, nimeongea hivi karibuni na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kutoa majibu ya suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo ni zito na si halali kwa Serikali kuendelea kubaki kimya juu ya jambo hili. Jinsi Serikali inavyozidi kuwa kimya ndivyo inavyoniingiza kwenye matatizo na wakazi wa Jiji la Mwanza. Mpaka sasa wakazi wengine wa Jiji la Mwanza, wameanza kuwa na shaka kwamba, malalamiko yao kama haya siyafikishi Serikalini na hivyo kuniona nina mapungufu na sistahili kuwawakilisha. Naomba nafasi yangu ilindwe. Wakazi wa Mwanza wakiridhika kwamba, taarifa hizi sizifikishi Serikalini, hawatanichagua tena kuwa Mbunge wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana leo nipate majibu ya kuridhisha.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na sifa nyingi na matumaini makubwa kwa Wananchi, bado ninaona kuna tatizo kubwa katika Kitengo cha Uhamiaji. Huduma ya utoaji wa *passport* imekuwa ni ya Makao Makuu tu. Hii ni kero kubwa kwa wateja na inawagharimu pesa nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni kuiomba Serikali iipe uwezo Ofisi ya Moshi iwe na uwezo wa kutoa *passport.* Ofisi hii ina jengo kubwa na la kisasa na ina uwezo wa kuhudumia kanda yote ya Kaskazini. Kwa kuwa jengo hili halitumiki kikamilifu, ingesaidia sana kupunguza msongamano uliopo Makao Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujambazi na mauaji ya kutumia bunduki imekuwa ni jambo la kawaida Mkoani Kilimanjaro hasa Mjini Moshi. Ninaiomba Serikali, iruhusu vijana wetu wanaochukua mafunzo pale Chuo cha Polisi Moshi, watumike katika kudhibiti maovu haya. Hii itawaongezea ujuzi wa ziada *practically* katika masomo yao. Hili naliomba kwa makusudi kabisa kwani kila siku mauaji yanasikika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizi wa magari limekuwa ni jambo la kila siku, lakini kila ninayejaribu kumhoji wizi huu ni vipi wakati Jeshi letu la Polisi lipo, wengi wanasema wezi wote wa magari wanajulikana na Polisi wanawajua. Kwa nini biashara hii inashamiri, sielewi! Tunaomba Polisi wakomeshe wizi wa magari kwani uwezo huo

wanao. Wanajua gereji zinazogeuza hayo magari, pia wanawajua wote wanaochinja hayo magari na kuuza kama *used spare parts.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu haitadhurika hata kidogo kama uuzaji wa *used spare parts* ungepigwa marufuku na zile zilizo ndani ya mji zirejeshwe Serikalini na utaratibu wa kuzi-*dispose* ufanyike. Kama hili litafanyika wizi wa magari utakoma kwani magari yote yanayoibiwa na hayapatikani huwa yanachinjwa na ndiyo *spare* zake zinajaa katika maduka ya *used spare parts.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipitisha hapa Bungeni, wafungwa wa vifungo vifupi vifupi wawe wakifanya kazi za jamii na kuwa nje ili kupunguza msongamano kwenye Magereza yetu. La kusitikitisha hadi leo Magereza yetu yamefurika na wale wa vifungo vodogo vidogo, hawafanyi kazi za jamii kama sheria tuliyopitisha hapa inavyotaka. Hii inaongeza msongamano katika magereza yetu. Ningeomba suala hili lifanyiwe kazi.

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kutoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote, kwa taarifa nzuri, nawatakia kila la kheri na kazi njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni muhimu sana kwa sababu inashughulika na watu wa aina mbalimbali, wakiwemo wajuaji, wakorofi, vichaa na kadhalika, hivyo ninaishauri Serikali kuwa karibu nao kwa kuwasikiliza wataalam wake wanapotoa ushauri na pia kuwapatia huduma muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya askari katika Mkoa wa Mtwara wanaishi uraiani, kitendo hiki kinalitia aibu Taifa letu. Kuacha askari waishi uraiani ni kutotambua mchango mkubwa unaotolewa na Jeshi letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni motisha gani Jeshi la Polisi linawapatia watumishi wake waishio Mikoa ya pembezoni mwa nchi? Nasema hawajaliwi kwani usafiri pia hawana. Kwa mfano, Wilaya ya Newala gari ilianguka Mlima Namaleche usiku wa saa 1.30 na mtu mmoja alifariki na wengine walijeruhiwa. Nilikimbiza gari langu maili sita kwenda kutoa taarifa na kuwasomba baadhi ya majeruhi. Jambo la kusikitisha askari walikosa gari kwani la kwao ambalo limeanza kuchoka, lilisafirisha maiti ya askari nje ya Wilaya. Kwa mfano, huu mdogo ni wazi kuwa, kipaumbele kiwepo ili kuwapatia magari tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri askari waliopo Mkoa wa Mtwara, wakopeshwe magari, pikipiki na baiskeli, ili waipende kazi yao kuliko ilivyo sasa na kwa sasa miongoni mwao wanataka kuhama. Je, kama wangepatiwa mambo niliyoyataja wangedai kuhamishwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wa Kitengo cha Upelelezi isingefaa wakae kituo kimoja kwa zaidi ya miaka mitano hadi kumi na tano, siyo vizuri kwa usalama wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kuwe na kitengo cha kuangalia afya za askari wetu kila mara na kuwapatia ushauri kiafya na mitazamo yake. Kwa mfano, askari wetu wengine wana vitambi vikubwa hata utembeaji wao si mzuri, wanafunga mikanda vifuani, hali hii siyo nzuri. Je, endapo watapaswa kukimbia wataweza? Wizara ijitahidi sana katika suala hili, naamini inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninampongeza tena Naibu Waziri, kwa jinsi anavyojitahidi kujibu maswali Bungeni na pia niwapongeze Askari wa Mkoa wa Mtwara, kwani pamoja na mazingira magumu, wanafanya kazi vizuri sana na Wananchi wanakuwa na imani nao, nikiwemo nami na ninawapenda tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari nilishaleta mchango wangu, huu ni wa nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajali za mabasi ya abiria, siku zote nimekuwa nikilizungumzia suala hili kwa nguvu zote. Mabasi haya yanapopata ajali ni abiria wanaopata majeraha au kupoteza maisha yao, wengi wanakufa kwa sababu ya kukanyagana kwa kukosa milango ya dharura katika mabasi. Kuna mabasi yana mlango mmoja tu, hata dreva anatumia mlango huo, chonde chonde namwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Watanzania ambao wamefungwa nje ya nchi, mfano Shelisheli na kadhalika. Tafadhali naomba Serikali iangalie uwezekano wa kuwarejesha Tanzania. Nitaomba ufafanuzi wakati wa majumuisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. MASOUD ABDULLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Polisi cha Kengeja kilichopo katika Jimbo la Mtambile, Wilaya ya Mkoani ni chakavu na kinavuja wakati mvua inaponyesha, ambapo jengo hilo ni ghorofa moja la tangu enzi ya ukoloni. Hivyo, ninaishauri Serikali kulifanyia matengenezo makubwa jengo hilo angalau liweze kuwa na sifa ya Jeshi lenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba za kuishi Askari wa Wilaya ya Mkoani ni chache sana, hivyo, umekuwa ni usumbufu mkubwa sana kwa jinsi askari wetu wanavyotembea masafa marefu hadi vituo vyao vya kazi. Ninaishauri Serikali, ijenge nyumba za kutosha kwa makazi ya Polisi wote wa Wilaya ya Mkoani, angalau zifanane na zile za Mfikiwa Wilaya ya Chake Chake, Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mishahara ya Jeshi la Polisi imekuwa ni midogo mno kulingana na uzito wa kazi yenyewe, hivyo, inaonesha ongezeko la mshahara kwa askari wa kawaida kwa bajeti ya 2004/2005 ni kati ya Sh.5,000/= na Sh.7,000/= tu, hali inayowafanya askari wetu wa Polisi kuwa katika hali mbaya zaidi ya maisha. Ninaishauri Serikali, iongeze mishahara kwa Polisi angalau askari wa kawaida anayeanza kazi apate Sh.150,000/= na ninamwomba Mheshimiwa Waziri, atamke bayana kima cha mshahara wa Polisi anayeanza kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, posho ya uhamisho wa askari haipatikani kwa wakati unaostahili, inacheleweshwa mno. Hivyo, ninaishauri Serikali kutoa posho za uhamisho wa askari kwa wakati muafaka ili kuepusha malalamiko mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kumekuwepo na ucheleweshwaji wa mishahara kwa askari wanapopanda daraja toka ngazi moja kwenda ngazi nyingine baada ya mafunzo yao. Hivyo, ninaishauri Serikali itoe fedha hizo kwa wakati unaostahili, pamoja na tofauti ya malimbikizo yao. Pindi mshahara ukipandishwa malimbikizo hayo huwa hayapatikani kabisa au hucheleweshwa mno. Ninaishauri Serikali, ilipatie ufumbuzi tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa suala la *passport* ni haki ya kila raia, kumekuwepo na usumbufu mkubwa sana kupata, kwani Dar es Salaam ndiyo kituo pekee kwa Tanzania Bara kinachotoa *passport* hizo. Hivyo, ninaishauri Serikali kuwa, kila Mkoa wa Tanzania Bara, upatiwe Afisa wa kukamilisha taratibu zote mpaka kupatikana kwa *passport* hizo. Vile vile, kwa kuwa upande wa Visiwani Zanzibar, *passport* zinapatikana Unguja tu, ninaishauri Serikali kuweka ofisi hiyo ya kutolea *passport* Kisiwani Pemba na ninaishauri Serikali gharama iwe Sh.15,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali, iangalie uwezekano wa kuajiri askari wa kike zaidi kuliko ilivyo sasa, ambapo uajiri wa wanaume umekuwa ni mkubwa mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. SHAIBU AHMADA AMEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naanza kwa kuungana na wenzangu, kwa kutoa mkono wa pole kwa familia na marafiki kwa vifo vya marehemu Wabunge wenzetu waliofariki hivi karibuni. Wabunge hao ni Marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga na Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana. Namwomba Mwenyezi Mungu, aziweke roho za marehemu hao peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii tena, nawapongeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa *Capt.* John Chiligati, kwa kazi kubwa wanazofanya katika kuiongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, sasa naanza kuchangia katika bajeti hii. Katika bajeti ya 2004/2005, niliomba nipatiwe simu au *radio call* kwa matumizi ya kituo kidogo cha *Maruhubi Police Post.* Nashukuru Wizara hii imenikubalia na hivi sasa kituo hiki kinatumia simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa kuhusu dawa za kulevya kuna kitengo cha kuzuia dawa hizo, lakini hata hivyo Jeshi la Polisi nalo linahusika na wahalifu wa dawa za kulevya. Nasema hivyo kwa sababu magenge au vituo vya kuuza dawa za kulevya, vinajulikana na viko mitaani na watumiaji wanaonekana, lakini biashara hii inaendelea

kushamiri mitaani. Suala hili Jeshi la Polisi inaliona, lakini hakuna hatua inayochukuliwa! Ni kwa nini Jeshi la Polisi haliangalii magenge haya na kuyasambaratisha? Naomba Jeshi la Polisi litupie macho suala hili na hatua madhubuti zichukuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa katika hotuba ya Waziri, viko vipengele vinavyohusika na ujenzi wa baadhi ya maeneo, lakini hata hivyo, iko haja ya kufanya ukarabati kwa baadhi ya vituo. Mfano, kituo cha Malindi ukipita na kukiangalia kwa nje, utaona ni kituo kizuri maana kimepakwa rangi, lakini kituo kile ukiingia katika baadhi ya sehemu, hasa kule nyuma, kuta na dari za kituo hicho zimepasuka na inaonesha ubovu ule ni wa siku nyingi. Kama Mheshimiwa Waziri, hana habari hiyo, basi mimi namweleza aelewe na katika fedha za matumizi ya maendeleo akiangalie kituo kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache na mimi naunga mkono hoja ya Wizara hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. JANET E. MASHELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba niwapongeze Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa *Capt.* John Chiligati, kwa hotuba yao nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuwapongeza Jeshi la Polisi, kwa kazi nzuri wanayoifanya, pamoja na hali ngumu waliyonayo. Kwa kweli Jeshi hili wanafanya kazi nzuri, lakini hawana vitendea kazi vya kuwawezesha kufanya kazi yao iwe nzuri zaidi. Mfano, hawana nyenzo kama magari ya kutosha, pikipiki, *radio calls* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo vya kufundishia mafunzo ya Upolisi, viongezwe katika maeneo mbalimbali kwa kuzingatia maeneo ambayo hayana vituo hivyo. Waongeze vyuo hivyo hasa katika eneo ambalo limekuwa na upungufu, nalo ni kwa upande wa matrafiki ambao wamekuwa wakihitajika sana kwani kumekuwa na ongezeko kubwa la ajali za barabarani. Kuna maeneo mengine askari huchukuliwa na kupelekwa eneo la kazi bila kupewa mafunzo yale yanayostahili ya utrafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuzungumzia suala la leseni. Kumekuwa na utoaji holela wa leseni. Naomba uwepo ule utaratibu uliokuwa unatumika wa kuwapa leseni wale wanaofaulu kwenye mtihani wa mafunzo ya kuendesha gari na utofautishwe kwa magari madogo na magari makubwa. Hii itasaidia kupunguza ajali ambazo zinatokea kwa ajili ya uzembe wa dreva na watahiniwa hao wafundishwe sheria za barabarani.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Wizara hii na vyombo vyake nchini, kwa kujipanga vizuri na kusaidia sana usalama wa raia na mali zao, pamoja na usalama wa barabarani. Hongera sana Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, Mheshimiwa *Capt.* John Chiligati, Katibu Mkuu na Wakuu wa Idara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *IGP, RPCs, OCDs* na askari wote, wanafanya kazi nzuri. Hali hii ya utulivu inatokana na juhudi za Polisi hawa nchini. *Allowance* za Polisi

zimebaki vilevile bila ya kuongezwa miaka nenda rudi. Naomba sana Waziri awafikirie askari hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Polisi wafikiriwe kuhusu nyumba zao, pamoja na maslahi ya familia zao, maana kubwa ni kwamba, familia za Polisi wa kawaida zipewe *Ration Allowance.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Uraia iangaliwe upya. Kuna matatizo makubwa nchini yanayohusu maovu mengi. Mfano alioutoa Mheshimiwa Bernard Membe ni kwamba, sheria hii ni kokolo inazoa kila mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba usafiri Kituo cha Polisi Mkuyuni na Ngerengere.

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wote walioandaa bajeti hii. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Meatu hakuna Kituo cha Polisi cha Wilaya na ujenzi umekuwa wa kusuasua na jengo bado halijakamilika. Naomba kituo hiki kiwekewe msisitizo ili kiweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Mjini Mwanhuzi kipewe gari, kama *IGP* Omari Mahita alivyoahidi mwaka 2003. Ahadi hiyo ikamilishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la ulinzi na usalama ni suala la Muungano. Vyombo vya ulinzi na usalama ni Jeshi la Polisi, JWTZ na Usalama wa Taifa. Serikali ya Mapinduzi imejiundia vikosi ambavyo vinafanya kazi ya kulinda usalama kama Polisi. Vikosi hivyo ndivyo vinavyosababisha vurugu wakati wa uchaguzi. Naomba Serikali ya Muungano ichukue tahadhari ya kuvidhibiti vikosi hivyo la sivyo hali ya usalama inaweza kuchafuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, maslahi ya askari wa ngazi za chini bado ni madogo. Huchukua muda mrefu kulipwa mafao yao, jambo ambalo huleta usumbufu mkubwa kwa askari hao wanaostaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Polisi watumiwe kwa haki bila ya upendeleo katika kipindi cha uchaguzi na bila kuegemea upande wa Chama Tawala.

Pia, upatikanaji wa *passport* bado una urasimu mkubwa. Kuna haja ya kuangalia upya utaratibu wa kupata *passport* hizo na gharama ya Sh.50,000/= ni kubwa mno kulingana na umaskini wa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uajiri wa kazi ya Polisi kwa upande wa Zanzibar bado hauko wazi. Masheha wamekuwa kikwazo kikubwa katika kupata nafasi, wao huwapa nafasi kubwa zaidi Wana-CCM. Tunaomba Waziri, aliseme hili ili Wananchi wote wapate nafasi hii bila kuangalia itikadi za kisiasa.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nampongeza Waziri, ambaye pia ni Katibu Mwenezi wa CCM, kwa kazi zake nzuri, kweli anatosha. Vilevile, nawapongeza sana Watendaji wote wa Wizara, lakini hasa nampongeza Naibu Waziri, kwani yuko mstari wa mbele katika kusimamia majukumu ya Wizara. Mwaka 2004, tulikuwa naye Ruvuma katika wiki nzima ya Usalama Barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usalama barabarani, kwa mujibu wa sheria, unahusiana na Baraza la Usalama Barabarani la Taifa lenye Kamati za Usalama barabarani katika kila Mkoa na kila Wilaya. Baraza linaongozwa na Mwenyekiti wa Taifa na Kamati zinaongozwa na Wenyeviti wa Kamati. Makamanda wa Usalama Barabarani katika kila Mkoa na Wilaya na Mikoa ni Makatibu wa Taifa pia. Naomba niwapongeze sana Makamanda hao na hasa Kamanda wangu wa Mkoa wa Ruvuma, kama Mwenyekiti wake wa Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi za Baraza la Kamati hizo ni za muhimu sana na ni njema. Tatizo kubwa ni kwamba, Serikali haitengi fedha kwa ajili ya kuendesha shughuli za Baraza japo kwa Wiki ya Usalama Barabarani Kitaifa. Ingawa tunaishaukuru sana Serikali kwa mwaka huu kuanza kutenga fedha za Wiki hiyo ya Usalama Barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Baraza la Taifa ndiyo Msimamizi Mkuu, tunashauri fungu la maadhimisho ya wiki hiyo, lizingatie Mkoa husika ambao unakuwa mwenyeji wa maadhimisho hayo. Wiki ya Usalama Barabarani ni muhimu sana kwa kuwa huielimisha jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Watendaji wote wa Wizara, kwa kazi zao njema. Ninawaomba wazidi kusimamia vizuri udhibiti wa trafiki, kuhakikisha kazi zao zinaenda vizuri hasa kuangalia suala la ujazaji abiria katika mabasi na kwenda kasi. Mara nyingine askari hao wa Usalama Barabarani huyaachia mabasi kupita wakati abiria wamezidi kiasi halali cha ujazo ndani ya basi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nawakaribisha Ruvuma Siku ya Usalama Barabarani, kwani Kitaifa inafanyika huko tena.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa utendaji mzuri wa kuigwa mfano katika ngazi zote, pamoja na Jeshi la Polisi, Magereza na Uhamiaji. Mambo muhimu ya kuzingatia ni haya yafuatayo:-

Kwanza, kuondoa kero ya rushwa inayolalamikiwa na Wananchi hasa askari wa usalama barabarani.

Pili, kujitahidi kuongeza ujenzi wa nidhamu kwa askari. Askari wengi hasa wa kawaida, nidhamu au ufualitiaji wa maadili yao umepungua sana.

Tatu, Chuo cha Mafunzo ya Uongozi wa Polisi, kizingatie zaidi taaluma ya maadili ya askari polisi. Hii ina shabaha ya kujenga imani ya Wananchi kwa polisi

Nne, katika Jimbo langu la Uchaguzi la Lushoto, tatizo la nyumba za askari Magereza ni sugu sana. Naishukuru Wizara, kwa matengenezo ya Gereza la Mahabusu Lushoto. Naomba jitihada zifanyike ili gereza katika eneo la Yoghoi na nyumba za askari magereza zijengwe.

Tano, vurugu za utoaji *passport* zidhibitiwe. Tahadhari za rushwa na kutapakaa *passport fake* budi zichukuliwe. Kwa sasa vurugu ni kubwa sana pale Makao Makuu ya Idara ya Uhamiaji. Wizara ibuni mbinu za kupunguza vurugu hizo, vianzishwe vituo vipya zaidi vya kutolea *passport* ili kupunguza msangamano Makao Makao Makuu.

Sita, Polisi Wilaya ya Lushoto, wapatiwe nyenzo za kufanyia kazi kama magari na nguo za kujikinga na baridi.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kumtakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri, kwa hoja yake ya leo. Pongezi sana kwa Wizara, kwa kujitahidi kufanya kazi nzuri, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na *IGP,* kwani Polisi wameonesha umahiri wa kupambana na maovu kwa sehemu kubwa.

Pili, ombi la muda mrefu, Wilaya ya Mbozi, haina kituo cha maana cha Wilaya, yaani Makao Makuu. Ofisi zinazotumika ni zile zilizokuwa za kuorodheshea manamba waliokuwa wakienda Tanga kwenye Mkonge *(1950s),* kiwanja kipo miaka mingi lakini hakuna hata msingi.

Tatu, askari wa usalama barabarani wamekuwa wengi mno barabarani, hatudhani kama huo ndiyo ufanisi mzuri. Uombaji wa rushwa umeonekana kuzidi na usumbufu ni mkubwa. Nashauri tuwe na vizuizi vichache lakini vyenye uratibu mzuri na ufanisi.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kukupongeza sana, kwa hotuba nzuri, yenye ufafanuzi wa kina kuhusu Wizara yako. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia. Pamoja na kuunga mkono hoja hii naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Kwa kuwa Serikali ilikuwa na mpango wa kujenga Chuo cha Upelelezi hapa Dodoma, je, ujenzi huo utaanza lini na utagharimu shilingi ngapi, hivi sasa kuna upungufu mkubwa wa polisi wapelelezi ndiyo maana kesi nyingi huchelewa kusikilizwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Jeshi la Polisi na Magereza wanafanya kazi nzuri sana na kwa kuwa maslahi yao ni duni, je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha maslahi ya maaskari hao? Je, Serikali haioni kwamba, maaskari hawa wanafanya kazi

katika mazingira magumu na ipo haja ya kuwalipa posho ya mazingira magumu na pia kuwajengea nyumba za kuishi kuliko hali ilivyo sasa askari polisi wengi wanaishi uraiani.?

Nawapongeza askari magereza wa Gereza la Mpwapwa, kwa kujenga nyumba kumi za maaskari. Pia namshukuru sana Kamishna Mkuu wa Magereza, kwa kupeleka vifaa vyote vya nyumba hizo 10. Namwomba Kamishna Mkuu wa Magereza, atembelee Gereza la Mpwapwa na kuona ujenzi wa nyumba hizo baada ya kupitisha Bajeti hii na kabla ya kurudi Dar es Salaam. Gereza la Mpwapwa sasa lina umeme wa gridi ya Taifa, simu na usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kupanda vyeo ni haki ya mtumishi, je, ni sababu zipi zinazofanya askari polisi na magereza kuchelewa kupanda vyeo mwaka 2004/2005 ni askari wangapi wamepanda vyeo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa uhamisho kwa mtumishi/askari ni jambo la kawaida na malipo ya uhamisho ni suala muhimu, je, ni askari polisi na magereza wangapi wamehamishwa bila kulipwa malipo/mafao yao ya uhamisho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ningependa kufahamu je, hayo magari 215 yatanunuliwa lini? Kwa kuwa Bajeti ya Wizara inapitishwa Bungeni leo, nashauri magari hayo yanunuliwe haraka, Serikali isingoje mpaka wakati wa kampeni ya uchaguzi au siku ya uchaguzi, *OCDs* wana shida kubwa ya usafiri, magari yanunuliwe pia litengwe fungu la matengenezo na mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jeshi la zima moto lipatiwe vifaa vya kisasa hasa magari yenye uwezo kuzima moto katika jengo la ghorofa 10 na kuendelea, kuliko hali ilivyo sasa, wana vifaa duni na pia maslahi yao yaboreshwe. Miji yote iwe na magari ya zimamoto na viwanja vya ndege vipewe magari ya zimamoto.

Kwa kuwa, Serikali inajenga nyumba 600 za Serikali Dodoma, je, kwa nini Serikali isitenge nyumba 100 kwa ajili ya maaskari polisi wa Dodoma?

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naunga mkono hoja ya Wizara ya Mambo ya Ndani na pia nachukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Jeshi la Polisi na vitengo vyake, kwa kazi nzuri sana ya kulinda amani na utulivu wanayoiendeleza kwa umakini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu kuhusu hii hoja, ninaleta maombi mawili kutoka kwa Wananchi wa Jimbo la Iramba Magharibi. Ombi la kwanza, Wananchi wa Mji Mdogo wa Shelui, wanaiomba Serikali kuona umuhimu wa kuweka *Road Block* ya polisi (ya usalama) kabla hujaingia Mji Mdogo wa Shelui, ukitokea upande wa Mashariki. Tarehe 4 Julai, 2005 saa moja usiku, nilishuhudia kitendo cha gari moja *(semi-trailer lorry),* ambalo lilikuwa linasimamishwa na polisi wa usalama kwa ukaguzi. Dreva wa lori hilo alifanya kitendo cha hatari kwa kuzima taa na kupita kwa

kasi sana. Yule polisi alijinusuru kwa kuruka kando ya barabara na aliteguka mguu wa kulia na kuburuza vibaya mkono wa kushoto. Baada ya hapo, niliongea na Mkuu wa Kituo cha Polisi cha Shelui na aliniambia kuwa, matukio haya ya kuhatarisha maisha ya polisi katika barabara hii ni ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumai Serikali itaona umuhimu wa haraka wa kuweka kizuizi katika barabara hii ya Shelui ili kunusuru maisha ya polisi wa usalama na Wananchi wa Mji Mdogo wa Shelui. Mimi binafsi, nitawataarifu Wananchi wa Shelui kuwa, ombi lao nimewafikishia Serikalini wakati wa Kikao cha Bunge cha Bajeti 2005/2006.

Ombi la pili, wakati wa Kikao cha Bajeti cha mwaka 2004/2005, nilileta ombi kutoka kwa *OCD* Kiomboi kuwa, wanaomba kusaidiwa kufufua trekta la Gereza la Ushora, ambalo ni la kilimo. Trekta hili ni muhimu sana kwa shamba la Gereza na kwa miaka mingi shamba hili limekuwa kama Taasisi ya kufundishia kilimo na linatoa au linazalisha kiwango kikubwa cha chakula kwa Wananchi wa Wilaya ya Iramba na pia Gereza hili linalisha Magereza na Taasisi mbalimbali zilizopo Wilayani Iramba kama shule na hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mwaka 2004 Wizara iliahidi kulifufua trekta hili na mpaka leo bado hawajalifufua, basi Wananchi wa Wilaya ya Iramba, wanaomba sasa mwaka huu wa 2005/2006, Wizara itenge fedha za kutosha kulifufua trekta hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kurudia kuunga mkono hoja ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Bajeti ya mwaka 2005/2006.

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa hotuba ya Waziri, ni nzuri na yenye matumaini mazuri kwa Watanzania na naunga mkono hoja hiyo kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningelipenda kupata maelezo kuhusu vyombo *(gun-boat)* vya *marine police,* ambavyo vilikuwa vikitumika katika Bahari ya Hindi. Bajeti iliyopita Mheshimiwa Waziri, alituahidi ya kwamba, vyombo hivyo vitakarabatiwa mwaka huu kwani bajeti iliyopita ilielekeza nguvu zake kwa hili katika kuboresha vyombo ambavyo vinatumika katika maziwa yetu. Ninahisi ya kwamba, kwa hivi sasa hatuna hata kimoja katika bahari yetu ya Hindi na kama hisia hizi zina ukweli, basi kiulinzi katika maeneo hayo ya bahari yetu tuko uchi kabisa.

Ni vema kwa Jeshi letu la *Police Marine* lishirikiane kwa karibu na K.M.K.M. katika kukabiliana na hali hii, angalau kwa kuchangia mafuta, ili kuhakikisha usalama wa raia katika Bahari ya Hindi, angalau kwa muda huu, wakati tukisubiri kwa kukarabatiwa kwa vyombo vya *police marine.*

Lingine ambalo ningependa kuchangia ni kwamba, askari wengi wa Jeshi la Polisi, walipandishwa vyeo lakini hawajapewa mishahara yao mipya ikilinganishwa kwa vyeo vyao hivyo vipya, pamoja na maslahi yao ya posho. Naomba na hili liangaliwe kwa haraka na kwa jicho la huruma, kwani tatizo hili linaendelea kukua siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo ningependa kuchangia ni kuhusu askari wetu wanapofanya doria ni muhimu sana kuvaa namba zao za *force,* kwani itasaidia sana pindi yanapotokea matatizo ya askari kwenda kinyume na maadili. Liwe ni kosa kwa askari kutokuvaa namba zao pindi wanapokuwa wamevaa sare zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huu, naomba kuunga mkono hoja kwa mara nyingine. Ahsante.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala yanakera Mtwara, naomba yafikiriwe kwanza, kuna taratibu wanazotumia vijana wanajiunga katika *group* zaidi ya vijana 30 au 40 na kuvamia nyumba fulani usiku wakiwa na nondo, mashoka, mapanga, wanafanya uhalifu wa kupora nyumba husika. Hao vijana ni maarufu kwa jina la "tukale wapi". Naomba polisi waimarishe ulinzi tena wa nguvu Mtwara Mjini na muda mwingine wanafika Vijijini.

Kuna kitongoji/mtaa Mtwara Mjini, kinaitwa Mdenga huko ni makazi na hifadhi ya hawa tukale wapi. Ukiporwa kitu na watu hawa zaidi ya 40, ukienda Mdenga na fedha utapewa vitu vyako vilevile Mdenga ikifika saa moja jioni, huthubutu kukatisha hata taxi haziendi, vinginevyo utafanyiwa kitu kibaya na kusiwe na la kufanya; hivi kweli polisi hawawezi kulikomesha suala hili?

Umeanza mtindo wa kupora fedha vituo vya mafuta Mtwara, Newala, Masasi na kadhalika. Watu wenye silaha na hawana wasiwasi, wakishapora hutembea na fedha zao bila usafiri, polisi wanachukua muda kufika sehemu ya tukio na hili limeleta hofu na limesababisha vituo kufungwa mapema.

**MHE. AZIZA S. ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwa maandishi. Nawaunga mkono Waziri na Naibu Waziri, kwa ufanisi wa kazi zao kwa muda wa miaka mitano tuliyoshirikiana nao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia suala moja tu, ambalo naomba majibu na ufafanuzi wa kina kabisa. kuhusu suala la madai ya Bwana Said Aljabri, anayeidai Magereza.

Namshukuru Naibu Waziri, kwa barua yake aliyoniandikia kumfahamisha Katibu Mkuu kuhusu madai hayo, lakini mpaka sasa Katibu Mkuu hajajibu ni tofauti ni Waziri alipopata lalamiko hilo kutoka kwangu, alilijibu kwa haraka na kunipa moyo wa kuamini utendaji wake. Je, kuna nini huko alikowaandikia na kutoa hukumu kama kumlipa au la?

Kutokana na lalamiko hilo, mimi sitakuwa na uhalali wa kuunga mkono hoja, maana hata malalamiko ya wapiga kura wangu hayajajibiwa, naomba sana jibu nilipate leo wakati wa majumuisho ya Wizara hii.

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa ujumla, kwa kazi nzuri hasa katika kudhibiti uhalifu nchini. Nina ushauri mdogo ufuatao:-

Wizara kwa makusudi itoe vifaa vya usafiri Vituo vya Polisi vya Nyabibuye, Muhange na Kakonko, kwa sababu ya kuwa mpakani na kushughulikia eneo kubwa na kuwa mpakani mwa nchi iliyokuwa katika vita. Inachukua muda mrefu gari kutoka Kibondo kuja kwenye tukio hasa patokeapo mauaji. Wizara iangalie uwezekano wa kujenga kituo eneo la Bukiliro, kwani kuna matukio mengi ya kuvamiwa na askari toka Burundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara ilipe haraka deni la shilingi 240,000/= kwa Mzee Abdallah Sambino, ikiwa ni pango la nyumba yake, iliyotumika kama Ofisi na hifadhi ya silaha kabla ya kuhamia Ofisi yao ya sasa. Ieleweke kuwa, madai haya si kwa ajili ya pango kwa maaskari binafsi, ni Ofisi ya Jeshi hilo na hivyo Wizara inawajibika kulilipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba, huduma kwa mahabusu sasa inasemekana iko TAMISEMI, Wizara ilipe haraka shilingi 135,000/= kwa Mzee Yusuf Bwitonde, aliyetoa huduma kwa mahabusu waliokuwa katika *selo* ya Mahakama ya Mwanzo Kakonko, kabla ya utaratibu mpya. Alikuwa akilipwa na Wizara ya Mambo ya Ndani kupitia kwa *RPO,* sioni kwa nini sasa Wizara inataka kujivua kuhusika na malipo yaliyobaki. Nyaraka zote ikiwemo Mikataba na *Delivery Notes* ziko Wizarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la kutoa vyeti vya uraia hasa kwa Vijiji vya mipakani, lipewe kipaumbele hasa wakati huu ambapo uchambuzi wa uhakika umefanywa wakati wa zoezi la kuandikishwa wapiga kura katika Daftari la Kudumu. Vyeti hivyo viaminiwe sasa na vitumike kutoa vitambulisho vya raia wa Tanzania. Uhamiaji ifanye zoezi la mara kwa mara la kupita kwenye pfisi na viwanda hasa vya nguo, kudhibiti Wafanyakazi wasio na vibali vya kufanya kazi na wale wanaofanya kazi ambazo zinaweza kufanywa na Wazalendo.

Wizara ichunguze kwa makini, makampuni ya ulinzi na zimamoto, yaliyozuka kwa wingi hapa nchini, kwani mengine yana *agenda* tofauti na ulinzi na baadhi ya Wafanyakazi wao licha ya kutokuwa na sifa zinazotakiwa, wana historia ya uhalifu. Tabia ya baadhi ya makampuni ya zimamoto kutoshiriki katika majanga ya moto, kwa sababu tu eti hawana Mikataba na wahusika, liangaliwe upya ili wanyimwe leseni, kwani haja ni kuokoa maisha kwanza na si fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali, imekwishatoa tamko hapa Bungeni mwaka 2002 kuwa, Wizara hii itashirikiana na Wizara ya Sheria na Katiba, Wizara ya Afya na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kuangalia vipengele vilivyoko kwenye *PF 3,* ili ikidhi haja ya kimahakama. Kuna tatizo gani la kuketi na kulitafutia ufumbuzi suala hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zimamoto inaonesha haina mwenyewe, kwani inaonekana wanafanyakazi chini na kwa maelekezo ya Halmashauri za Wilaya na Jiji. Hata walioko viwanja vya ndege, wanaonekana kuwa chini ya *TAA* zaidi kuliko Wizara hii. Jambo hili linakatisha tamaa watumishi na ni vema liangaliwe kwa umakini ili kuboresha maslahi ya watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naitumia nafasi hii, kutoa pongezi zangu nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini, Mkurugenzi wa Makosa ya Jina Nchini, pamoja na maafisa na watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi yao nzuri, iliyopelekea kuwasilisha Hotuba yao hii nzuri, yenye maendeleo makubwa na yenye mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayazungumza haya pia nikiwa na ushahidi mkubwa, kwani mimi ni mmoja kati ya Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge letu Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nimehudhuria karibu vikao vyote vya Kamati yetu ya Ulinzi na Usalama, ambavyo vilitukutanisha na Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi, pamoja na idara na sekta zake na kupata taarifa mbalimbali za kiutendaji na za kimaendeleo, zinazofanywa na kusimamiwa na Wizara hii. Pia nimeshiriki ziara zote zilizofanywa na Kamati yetu ya Ulinzi na Usalama katika kutembelea maeneo mbalimbali ya nchi yetu, kukagua utendaji na usimamizi wa majukumu ya Wizara hii na vyombo vyake vyote na kwa kweli tumeona ufanisi mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaipongeza Wizara yetu hii na ninaunga mkono hotuba hii ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa asilimia mia moja.

Vile vile, sina budi kuitumia nafasi hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, pamoja na Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuviwezesha vyombo vyetu vya ulinzi na usalama, kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na mafanikio yaliyo mazuri sana na ya kiwango cha juu na Kimataifa. Kama tunavyojua kuwa, majukumu ya msingi ya Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kupitia Jeshi letu la Polisi na Taasisi nyingine za Wizara hii ni kulinda usalama wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia jukumu hili kubwa na la msingi kwa Taifa letu, linadhihirisha kuwa nchi yetu haiwezi kuendelea kama usalama wa raia na mali zao, hauko katika hali ya amani na usalama. Jambo ambalo linaweza kurudisha nyuma mipango na mikakati ya Serikali yetu ya kupambana na umaskini katika nchi yetu. Bila ya kuwa na amani na utulivu katika nchi yetu, hatuwezi kujenga na kuimarisha uchumi na maendeleo ya nchi yetu na Wananchi kwa ujumla. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali yetu, iendelee kutoa fedha nyingi zaidi kwa vyombo vyetu hivi vya ulinzi na usalama ili tuweze kujenga nguvu na maendeleo ya Taifa letu hili zuri na lenye mwelekeo wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara hii ipo Idara ya Uhamiaji, ni muhimu sana kwa amani, utulivu na maendeleo ya nchi yetu. Kutokana na hali ya dunia ya sasa kutokuwa salama, hatuna budi kuimarisha Idara yetu hii, kwa kuipatia fedha za kutosha, pamoja na vifaa ili iweze kufanya kazi zake vizuri na kwa mafanikio makubwa katika kutekeleza majukumu yao ya kiutendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa dunia haiko salama kwa hiyo, hata nchi moja moja kama nchi yetu, haiwezi kuwa salama kama hatutaweza kuimarisha Idara hii ya Uhamiaji kwa nchi nzima. Ni lazima tuiimarishe Idara hii Makao Makuu, Mikoani, Wilayani na Vijijini, hususan katika mipango yote ya nchi yetu ambayo ni moja ya njia kuu zinazoingiza wahalifu wa aina mbalimbali wakiwemo wale wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nchi yetu imekuwa ni moja ya nchi inayopokea wakimbizi wengi kutoka sehemu mbalimbali za nchi jirani na nchi nyingine za Bara la Afrika na kadhalika. Wakimbizi hawa wamekuwa ni kero kubwa kwa nchi yetu, kwani wanawasumbua sana Wananchi wetu na hata kusababisha uhalifu mkubwa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia miongoni mwa wakimbizi hawa, wapo ambao wamefungwa katika Magereza yetu hapa nchini, jambo ambalo linasababisha pia Magereza yetu kuwa na msongamano wa wafungwa wengi sana. Kwa kuwa siku za nyuma wapo wafungwa wakimbizi ambao walirudishwa makwao kwa msamaha wa Mheshimiwa Rais, ni vizuri utaratibu huo ukafanyika tena ili wafungwa wote ambao ni wakimbizi waweze kurudishwa makwao haraka iwezekanavyo ili Serikali yetu iweze kutoa huduma zaidi kwa wafungwa wetu ambao ni Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali ilishughulikie suala hili ipasavyo. Vile vile, ninaiomba Serikali yetu iangalie kwa undani, kwa nini nchi yetu inakuwa na wakimbizi wengi ambao kimtazamo kama tutaliachia hivi hivi tu, kwa kweli linaweza kuja kuleta athari kubwa kwa nchi yetu kwa siku zijazo. Suala hili lisipuuzwe hata kidogo hasa tukiangalia ubora na thamani ya Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya ubora na thamani ya nchi yetu ni kuwa nchi ya amani na utulivu na pia kuwa nchi yenye rasilimali nyingi sana, ambazo zinahitaji kutunzwa na kusimamiwa vizuri sana. Pia rasilimali hizo tulizonazo ni ardhi, watu, madini na maji mengi sana, yakiwa katika maporomoko mbalimbali, maziwa, mito na bahari. Kwa kweli rasilimali hizi zinahitaji kutunzwa na kulindwa kwa hali na mali na kwa ufanisi mkubwa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuchangia haya niliyoyaandika, ninarudia kuipongeza Wizara na Serikali yetu kwa ujumla, narudia kusema kuwa, ninaiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia. Ahsante.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja hii. Kazi zilizofanywa na Wizara hii ni nzuri na kubwa. Nichukue

nafasi hii nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watalaam wake wote. Nianze kwa kuwaombea Mheshimiwa Waziri na Naibu wake katika uchaguzi ujao ili wapate ushindi mzuri na kurudi tena Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pongezi za pekee, kwa Ndugu Muganga, *RPC* Iringa, pamoja na askari wake hasa wa usalama barabarani, kwa kazi nzuri ambazo wamezifanya. Pia nichukue nafasi hii nitoe pongezi ya pekee, kwa Mwenyekiti wa Mamlaka ya Utoaji Leseni, Ndugu Abeid Kiponza, ambaye amekuwa akishirikiana vizuri na polisi, kuhakikisha ajali zinapungua na vurugu za mabasi. Kutokana na kazi ambazo amekuwa akizifanya, ningeiomba Wizara yako impongeze rasmi ili iwe changamoto kwa mikoa mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Wizara hii inipatie maelezo kwa nini wamechelewa kuhamia Kilolo, Wilaya mpya wakati sasa hivi Idara zote zimehamia huko? Mwaka 2004, Wizara hii ilisema imetenga fedha kwa ajili ya magari Kilolo lakini cha kushangaza magari hakuna. Nisingependa kutoa shilingi kwenye Wizara hii, nipewe maelezo. Ninaomba Wizara hii itoe mipango yake kwa Wilaya mpya. Vipi Wilaya kama Namtumbo (mpya) ijengwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la msamaha wa wafungwa liangaliwe upya, kwani walio wengi wanaachiwa baada ya muda mfupi wanafanya makosa. Ninashauri wale ambao Serikali inataka kuwasamehe, itolewe orodha yao magazetini, wapate wadhamini ambao watakuwa tayari kufuatilia mabadiliko ya tabia zao, kwani walio wengi wanapoachiwa tu, huanza tena uhalifu kwa sababu hawana kitu cha kufanya na ndipo Wananchi huchukua sheria mkononi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naiomba Wizara yako, ibadilishe Gereza la Mgagao kuwa Chuo cha Magereza, hii itasaidia zaidi kutokana na eneo lenyewe. Ninamwomba sana Kamishna Mkuu wa Magereza, Ndugu Banzi, aliangalie hili. Ahsante.

**MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii, kucnagia hoja ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Nampongeza sana Waziri wa Mambo ya Ndani Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa *Capt.* John Chiligati na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wanaifanya katika Wizara hiyo. Naunga mkono hoja.

Mimi binafsi nimepata ushirikiano mzuri sana pale tatizo linalohusu Wizara hii lilipojitokeza. Nakumbuka kero kubwa ya ujambazi katika Mkoa wangu na hususan Wilaya ya Kasulu na jinsi ambavyo Naibu Waziri, siku moja nilimpigia simu saa sita usiku, alinijibu kwa utulivu na kesho yake alifuatilia akanipa jibu sahihi. Nampongeza sana Mheshimiwa *Capt.* John Chiligati, kwa umakini wake na mimi naamini amefanya hivyo hata kwa Wabunge wenzangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Vijiji vya Funda, Bukuba, Songa na Kitongoji cha Tambabisiga, kumekuwa kunatokea utekaji wa mabasi ya abiria yatokayo Munanila kwenda Kasulu Mjini. Sehemu zote hizi hazina msitu na ujambazi hufanywa peupe bila wasiwasi. Tafadhari naomba ujambazi wa aina hii uchunguzwe na ikiwezekana *operation* maalum, ifanyike kwa kushirikisha Jeshi la Polisi na Jeshi la Ulinzi. Hii itapunguza ujambazi huo. Naupongeza msako wa silaha unaofanywa Mkoa wa Kigoma.

Pia napenda kumpongeza Kamanda wa Jeshi la Polisi katika Mkoa wa Kigoma, Bwana Mgongolwa, kwa kazi nzuri anayoifanya. Anasifika kwa kuwa msikivu na mfuatiliaji mzuri wa matatizo ya Wananchi na kuyashughulikia bila usumbufu kwa raia. Wananchi wengi toka Mkoa wa Kigoma, wamekuwa wakihangaishwa sana na polisi eti wao si raia. Tatizo hili ni kubwa, maana ukihisiwa tu unakamatwa. Jambo hili linasikitisha kwa sababu wengi wao hukamatwa bila uchunguzi wowote na hupoteza muda mwingi mahabusu, jambo ambalo linakuza umaskini miongoni mwa Wananchi wa Mkoa wa Kigoma. Mbona Wananchi wengine waishio mpakani kama vile Tarime, Kagera, Kilimanjaro, Arusha, Lindi, Mtwara, Ruvuma au Rukwa, hatusikii wakikamatwa ovyo ovyo, kulikoni katika Mkoa wa Kigoma? Naomba Jeshi la Polisi lifanye uchunguzi kabla ya kuchukua hatua ya kuwakamata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninawapongeza tena kwa kazi nzuri na ninaunga mkono hoja.

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, malalamiko mengi yanatolewa na Wananchi vijijini kwamba, askari huwababambikiza kesi na huwaweka mahabusu bila makosa, naomba Wizara ifanye ufuatiliaji katika Wilaya ya Mbozi kwa vituo vidogo vya Mlowo, Tunduma na Kamsamba.

Kituo cha Polisi Makao Makuu ya Wilaya Mbozi ni cha zamani sana, kilianza katika majengo ya *SLABU.* Hali ya kituo hiki inaondoa hadhi ya Wilaya. Wananchi waliwahi kutoa uamuzi wa kukijenga kituo kwa hadhi yake, lakini Wizara haikuonesha ushirikiano na hali, imebaki kama ilivyo. Eneo lililotengwa kujengwa liko wazi hadi hivi leo. Halmashauri ya Wilaya imeamua kuliendeleza kwa kujenga stendi ya mabasi. Je Wizara inalifahamu hili na inatoa maelezo gani?

Ujenzi wa Magereza ya Wilaya, umechangiwa na Wananchi kwa kiwango kikubwa. Naibu Waziri na Kamishna, walitembelea ujenzi huo na kuahidi kuharakisha ujenzi wake na kulikamilisha. Nimejaribu kuwasiliana na Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Kamishna, lakini bado utekelezaji wake ni mdogo. Naomba Waziri anipatie maelezo ni lini litakamilika na kuanza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna huyu *Capt.* Mwashinga aliyejinyonga na familia yeke walikataliwa kulipwa haki za mirathi yao. Ilinilazimu niulize swali kwa Waziri wa Fedha, haki ya kuwanyima mirathi wahusika. Jibu lilikuwa, familia ya *Capt.* Mwashinga

ilikuwa na haki ya kulipwa kisheria. Aidha, Naibu Waziri alimwandikia Kamishna ili atayarishe malipo yake, lakini mpaka leo hakuna matokeo, pamoja na kwamba, nimekuwa namkumbusha Naibu Waziri, mara kwa mara. Naomba maelezo kama kuna badiliko la kisheria, kwani mjane na watoto wa marehemu, wana hali mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba zijengwe nyumba za Polisi Makao Makuu ya Wilaya ili askari wawe na amani na usalama wao. Hali ilivyo ni aibu kwa Serikali wakati hata mahabusu haistahili na kituo kiko barabarani njia kuu ya Zambia. Nakuomba Mheshimiwa Waziri, wewe ambaye hujafika, ufike ukajionee mwenyewe. Nimekuwa nikisema kila mwaka kuhusu Gereza la Vwawa kupewa trekta ili waweze kuzalisha chakula chao na kupunguza gharama kwa Serikali. Napenda kuishukuru Wizara kwa kukubali kutoa gari mpya kwa *OCD* Mbozi, kwani ni vugumu sana kwa *OCD* kukagua vituo vidogo bila usafiri wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa mategemeo kuwa, maombi yangu yataangaliwa kwa jicho na moyo wa huruma.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Naibu wake, Mheshimiwa *Capt.* John Chiligati, kwa kazi kubwa na nzuri, hali ya ulinzi ni nzuri ikilinganishwa na huko nyuma.

Jitihada zaidi ziongezwe ili kupambana na wahalifu. Bado wapo baadhi ya askari wa usalama barabarani, wanaharibu heshima ya Wizara ya Mambo ya Ndani, hasa katika Barabara ya Morogoro - Iringa hadi Mbeya na Kyela. Wanasumbua sana watu kwa kuomba rushwa. Suala la malipo ya Wananchi wanaolisha mahabusu nalo lipewe ufumbuzi. Pamoja na pongezi hizo, naomba yafuatayo yarekebishwe:-

Ahadi ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kuhusu kusaidia ujenzi wa Kituo cha Polisi Puma, Singida Kusini, itekelezwe. Hivi sasa wanahitaji zaidi *cement,* mawe, milango na madirisha. Wapo Polisi kadhaa ambao hawajalipwa madai yao *(arreas)* tokea mwaka 2001 - 2004 na malimbikizo mbalimbali ya askari hao ili kuweka bayana nani anastahili kuwalipa kati ya Wizara ya Mambo ya Ndani au TAMISEMI. Hivi sasa wapiga kura wangu wa Ikungi na Makungu/Mungora, wanasumbuka sana. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Idara ya Uhamiaji, lakini bado watu wanaingia nchini kinyume na utaratibu hasa Wasomali, Wazambia na Wakongomani. Hoteli ya Alurba Dar es Salaam, wapo wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri.

Pamoja na pongezi hizi napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya Karatu ilishatenga ardhi kwa ajili ya ujenzi wa Gereza la Manyola liko mbali sana kutoka Mji wa Karatu, ambako ndiyo Mahakama zipo na kwa kuwa mahabusu yaliyoko Karatu hayako katika hadhi ya kutumika na binadamu na kwa sasa mahabusu wengi wanapaswa kupelekwa Arusha, umbaki wa km 150 toka Karatu; je, Wizara imetenga sasa fedha kiasi gani katika mwaka huu wa fedha kwa ajili ya fidia ya eneo na ujenzi wa Magereza ya Wilaya ya Karatu?

Ieleweke kuwa fidia hii ni muhimu kwa vile ardhi iliyotengwa ni sehemu ya *Lease Land,* ambayo Mheshimiwa Rais, amefanya *revocation* na hivyo mmiliki wa awali ni lazima afidiwe.

(ii) Kwa kuwa mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi na kwa kuwa matamshi mengi na mazito yametolewa kuhusiana na vurugu wakati wa uchaguzi na kwa kuwa vurugu nyingi zinatokea Wananchi wanapoanza kusukumwa sukumwa, kufukuzwa ovyo na kwa kuwa nchi nyingi za *SADC* zimewataka askari wakae umbali wa mita 300 kutoka kituo cha kupigia kura na wasijihusishe na kamapeni:-

(a) Je, Serikali inafanya mpango gani wa makusudi kuwaelimisha askari wetu wafahamu wajibu wao wakati wa mchakato mzima wa uchaguzi tangu kampeni hadi siku ya kutangaza matokeo?

(b) Je, Serikali inafahamu kuwa kutoa vitisho kwa peke yake haiwezi kuleta amani na utulivu, bali amani ya kweli na utulivu wa kweli unaletwa na elimu ya wapiga kura inayojikita katika kufafanua majukumu ya kila mchezaji katika zoezi zima la uchaguzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kuwa Mheshimiwa Waziri, atatoa maelekezo na maelezo ya kina kuhusu jinsi Jeshi letu la Polisi linavyoandaliwa kikamilifu katika zoezi zima la uchaguzi ili kulinda heshima na hadhi ya nchi yetu, ambayo dunia nzima inatutambua kama kisiwa cha amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natanguliza shukrani za dhati.

**MHE. PAULO MAKOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua ni kwa nini vituo vya polisi vidogo hufungwa usiku na wakati matukio mengi mabaya hufanyika na wakati huo huo asubuhi mpaka jioni vituo hufunguliwa?

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naunga mkono hoja asilimia 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tatizo la gari kwa kituo cha Polisi cha Kibiti, nimelizungumza muda mrefu humu Bungeni tangu 1996 na kuahidiwa kila mara kuwa Kituo hicho kitapatiwa gari, lakini mpaka hivi leo hakijapatiwa gari hilo. Pamoja na kuahidiwa kwa mkazo mkubwa na aliyekuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Mrehemu Mheshimiwa John Mgeja, lakini pia niliambulia patupu. Pia nimezungumza na

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani wa sasa, Mheshimiwa *Capt.* John Chiligati, lakini mpaka sasa bado suala hilo halijashughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuifahamisha Wizara kwamba, gari moja linapokuwa kule katika Makoa Makuu ya Wilaya ya Utete, ambako ni ng'ambo ya Mto Rufiji, inakuwa vigumu kwa Kituo cha Kibiti kulitumia gari hilo na kwa hiyo, usalama wa raia na mali zao hauwezi kupatikana katika eneo lote la Jimbo la Kibiti. Vile vile upande huo wa Wilaya ya Rufiji, yaani Kibiti, kuna uhalifu mkubwa unaotendeka katika kambi ndogo za wavuvi, hasa kutokana na wahalifu wanaotoka katika maeneo mengine kama vile Dar es Salaam.

Je, Serikali haioni kuwa kwa kuchelewesha kupeleka gari Kibiti kunachochea kukua kwa uhalifu, pamoja na kuwaacha Wananchi wake bila ya ulinzi na usalama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Kituo Kidogo Nyamisati, kutokana na umbali mkubwa kutoka Kibiti hadi katika eneo la *Delta* ya Mto Rufiji, ambako uhalifu mkubwa unatendeka katika kambi za Wavuvi za Bunduki, Kibanjo, Vikacha, Bercelona na kadharika. Wananchi wameonelea wawe na Kituo Kidogo cha Polisi Nyamisati karibu na eneo la *delta* ili kuweka ulinzi na usalama katika eneo hili, kwani uhalifu unapotokea Polisi hufika kwa tabu sana katika eneo hilo kutokana na ukosefu wa usafiri.

Hivyo basi, naomba Serikali iwasaidie na kuwapa nyenzo Wananchi hao ili kituo hicho kidogo kijengwe haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Gereza la Ng'aru - Kibiti, inaonesha kuwa Wizara ya Mambo ya Ndani, imelisahau kabisa gereza hilo kwa kutolifanyia ukarabati wala kuwaangalia watumishi wake. Gereza hilo halina gari la kubebea wafungwa wala zana za kilimo, kwani gereza lina mashamba makubwa lakini hivi sasa yamegeuka kuwa mapori tu.

Mahabusu au wahalifu wanapokuwa Kibiti kuwapeleka gerezani askari hupata taabu sana au hutumia gari la Mbunge kupeleka mahabusu hao, kwani kuna umbali wa kilometa sita baina ya Kituo cha Polisi na gereza. Tatizo la ukarabati pia linahusu Gereza la Utete, Makao Makuu ya Wilaya, halijafanyiwa ukarabati kwa muda mrefu. Je, Serikali inasema nini katika hilo?

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namapongeza Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, kwa hotuba yake nzuri ya bajeti. Naomba nichangie katika maeneo machache.

Katika Jimbo la Nanyumbu, Wananchi wamejitahidi kujenga vituo vidogo vya Polisi katika Kata za Mikangaula na Nanyumbu. Vituo hivyo vyote vimesimama ujenzi wake baada ya Wananchi kuishiwa nguvu za kuweza kumalizia kazi hiyo. Naomba Serikali basi iunge mkono juhudi za Wananchi hao katika kumalizia ujenzi wa vituo hivyo vidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Polisi cha Mangaka ni muhimu sana kwa ulinzi katika Jimbo la Nanyumbu na eneo lote la barabara ya kutoka Masasi kwenda Tunduru. Aidha kituo hicho ni muhimu sana kwa ulinzi katika eneo lote la mpaka kati ya Tanzania na Msumbiji kuanzia Mto Mbangara upande wa Mashariki na Mto Lumesule upande wa Magharibi. Eneo lote hilo liko mbali sana na Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Masasi.

Licha ya umuhimu wa kituo hicho cha Polisi Mangaka, nasikitika kusema kuwa, kituo hakina nyenzo za kutendea kazi kama magari, pikipiki na hata baiskeli. Kulingana na ukubwa wa eneo la Jimbo la Nanyumbu, Kituo cha Polisi Mangaka kilistahili kupewa nyenzo za kutendea kazi kama za kituo cha Wilaya.

Kulingana na ukubwa wa Wilaya ya Masasi, ambayo inachukua asilimia 53 ya eneo lote la Mkoa wa Mtwara, ni wazi kuwa Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Masasi, hakina uwezo wa kufika katika maeneo yote ya Wilaya kwa urahisi, hivyo, kutegemea vituo kama vya Mangaka katika kutimiza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu kwa Kituo cha Polisi Mangaka kupatiwa nyenzo za kufanyia kazi ili kutoa mchango wake katika ulinzi wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huo, niseme tu kuwa naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nijaribu kufanya majumuisho ya hoja nyingi sana zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, kwenye hotuba yangu ya bajeti. Nianze kwa kuwatambua waliochangia jumla yao ni 52. Kati yao wanne, walianza kuchangia kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambao ni Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Mathew Ole-Timan, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis na Mheshimiwa Gwassa Sebabili. Mmoja alichangia kupitia Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naye ni Mheshimiwa Job Ndugai na leo tena amechangia vilevile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa kuzungumza hivi leo ni Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, kwa niaba ya Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Frank Maghoba, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani na wengine ni Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Bernard Membe, Mheshimiwa Ali Machano Mussa, Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, Mheshimiwa Emmanuel Kipole, Mheshimiwa Mohamed Abdully Ally na mwisho Mheshimiwa *Capt.* John Chiligati, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa maandishi jumla yao ni 32, nao ni Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mheshimiwa George

Lubeleje, Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Paul Makolo, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Profesa Juma Mikidadi, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Stephen Masaba Kazi, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Lydia Boma, Mheshimiwa Masoud Abdulla Salim, Mheshimiwa Shaibu Ahmada Ameir, Mheshimiwa Janet Mashele, Mheshimiwa William Lukuvi, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Ali Said Salim na Mheshimiwa Talala Mbise. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na shukrani. Naanza kwa kumshukuru kwa dhati kabisa, Mheshimiwa Frank Maghoba, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, ambaye tumekuwa wote katika Kamati ya Ulinzi na Usalama, ambapo tumefanya kazi kwa ushirikiano mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemweka ajitokeze peke yake, maana ningeweza kumworodhesha asubuhi hapa, lakini nimesema nianze sasa hivi wakati wa majumuisho ili ajitokeze peke yake, ni mfano wa Mbunge wa Upinzani, anayejua kufanya kazi vizuri na Serikali. Nadhani faida ameziona kwenye Jimbo lake kutokana na ushirikiano mkubwa na kufanya kazi kwa karibu na Serikali, kwenye Jimbo lake amefanya mengi na makubwa. Lakini pia katika Bunge hili hasa katika Kamati ya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge ni Kamati yenye vyombo nyeti vya dola na katika mazingira hayo ambapo ndiyo kwanza tunajifunza mambo ya Upinzani na Chama Tawala, maana tulikuwa hatuyajui huko nyuma wakati wa mfumo wa Chama kimoja, basi mnaingia kwanza mnawatazama Wapinzani haya mengine wakiyajua. Lakini Mheshimiwa Frank Maghoba, toka tulikuwa na wasiwasi naye mpaka tumekuwa *open* kabisa kwa kila jambo na sifa hizi anazigawa yeye na mwenzake Mheshimiwa Meja Jesse Makundi, ambao tulikuwa wote pamoja. Namshukuru sana na ndiyo maana hata ushauri wingi ambao amekuwa akiutoa kwenye Wizara yetu, tumeutekeleza na leo hapa amekiri mwenyewe kwamba, mengi ambayo amekuwa akitushauri tumeyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru na kuwapongeza Makamanda wa Polisi na Askari wote kwa ujumla, tumeingia katika kipindi cha miaka 10 tunayomaliza cha majaribu mengi na cha kujifunza mazingira mapya ya uendeshaji wa nchi katika mazingira ya Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa. Nchi nyingi hazikuweza kufanikiwa kuupitia mitihani huo, pengine mwaka wa kwanza tu zilijikuta na matatizo. Lakini miaka 10 hii inakamilika katika hali ya usalama na amani, Jeshi la Polisi lina mchango mkubwa katika hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepitia misukosuko mingi, wakati mwingine Jeshi la Polisi halikueleweka, bila shaka kulikuwa na kuteleza. Lakini pia na sisi wanasiasa

kulikuwa na maeneo tuliteleza kwa sababu wote tulikuwa tunajifunza. Kambi ya Upinzani na upande wa utawala wote tulikuwa tunajifunza. Kwa hiyo, ilibidi kwa kweli mahali pa kutumia busara tulitumia busara na mahali pa kutumia nguvu, tulitumia nguvu, lakini mwisho wa yote nadhani sasa hivi tunaweza kujivuna kwamba, jahazi la mabadiliko makubwa tumelifikia. Sasa lililobaki tuendelee kushirikiana. Kwa hiyo, pongezi maalum kabisa kwa *IGP,* Omar Iddi Mahita na Jeshi lake lote la Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani kwa Mheshimiwa *Capt.* John Chiligati, nilimsifu asubuhi na sasa hivi narejea hasa baada ya kila Mheshimiwa Mbunge, aliyesimama hapa amemsifum ni pongezi anazostahili, kuna usemi unaosema kwamba: "Mzigo mzito mpe Mnyamwezi abebe." Mimi nimekuwa Mnyamwezi kwa kubebeshwa mizigo mingi mizito, lakini pale Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na mimi nilipata Mnyamwezi wangu, Mheshimiwa *Capt.* John Chiligati. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mambo mengi ya kushughulika na watu na Waheshimiwa Wabunge na nyingine, nilimwachia yeye. Wakati mwingine pale Wizarani huwa tunapokea barua si chini ya 100 kila siku ambazo inabidi uzisome za malalamiko tu. Kwa hiyo, zile barua nilipokuwa naona zinafikia *page* 10, namwachia Naibu Waziri, ama alishughulikie mwenyewe au aniandikie muhtasari, lakini yote hayo ameyabeba na bado alipata muda wa kushughulikia Wananchi wa Jimbo lake, pamoja na Waheshimiwa Wabunge. Nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalishukuru Bunge na Waheshimiwa Wabunge wote, kwa sababu haya niliyoyaeleza yote tumeyafanya kwa pamoja. Wote kabisa tumeshirikiana kwa kukumbushana kuwajibika. Maana wakati mwingine walipotukumbusha, pengine tulikereka lakini tulipolitekeleza mkapata matokeo wote tunayafurahia na ndiyo maana hata bajeti yetu ya leo inaonekana kidogo afadhali kuliko za miaka ya nyuma. Nawashukuruni sana na ninawaombea kila la kheri Waheshimiwa Wabunge wote, tuliomo humu Bungeni, Mungu atujalie turejee tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, bila shaka tulifundishwa na Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya hapa kuzikumbuka familia zetu ambazo kwa kweli katika mazingira haya ya kazi nyingi, muda mwingi tumekuwa hatukuwa nazo na wametuvumilia. Kwa hiyo, nichukue fursa hii kumshukuru kwa dhati kabisa bi Amina Mapuri pamoja na watoto wetu wote pamoja na wajukuu wetu kwa jinsi ambavyo wamenivumilia katika kipindi kigumu cha kazi. Lakini uvumilivu wao ndiyo ulionipa nguvu za kutekeleza majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ni nyingi sana zilizozungumzwa, si rahisi kuzipitia zote, lakini tutajitahidi tutakazoziweza. Kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba, hatimaye tutazijibu kwa maandishi zote hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini napenda nianze na mambo ya jumla mawili, matatu. Kwanza, hili la kuchelewa kwa mafao na stahili mbalimbali za watumishi wetu hasa Askari wa Polisi na wengineo. Ni kero ambayo tumekuwa tukipambana nayo kwa muda mrefu sana, ipo na tunaijua na sisi inatukera kweli kweli. Kwanza, ni tatizo la

kihistoria la ufinyu wa bajeti tulipokuwa na matatizo ya kiuchumi, kwa hiyo, mara nyingi watumishi walitudai tulishindwa kuwalipa, siyo watumishi tu na watu wengine. Lakini pia kulikuwa na tatizo la utunzaji mzuri wa kumbukumbu, ambalo nalo imebidi tukabiliane nalo kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa dalili zimeshaanza kuonekana za kupungua kwa tatizo, angalau utunzaji wa kumbukumbu umeanza kuwa bora. Hazina mara nyingi wamekuwa wakiturejeshea madai ya mafao ili kuweka kumbukumbu ziwe vizuri zaidi na hili lilitokana na mara nyingine askari kwa mwaka mmoja, wanaweza kuhamishwa kwenda katika vituo vitatu mara nyingine. Sasa mkitaka kumfuatilia hasa Hazina walipotaka kwamba lazima waone *latest information* yake, yuko wapi, siyo tuwaambie yuko mahali fulani, lakini kumbukumbu zake zinaonesha yuko katika kituo kingine. Kwa hiyo, hilo lilichangia katika kuongeza muda wa kuyafuatilia hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hatimaye mengi sasa hivi tumeshayakamilisha na fomu zote ambazo zimekuwa zikirejeshwa na Hazina hatimaye tumefikia mahali tumekubaliana kwamba, sasa ziko tayari kwa malipo. Kwa hiyo, ni matarajio yetu kwamba, katika kipindi hiki cha mwaka wa fedha ulioanza mwezi huu, wataweza kulipwa kwa wale ambao wameshahakikiwa na fomu zao ziko tayari. Kwa siku za mbele, tunatarajia kwamba, usumbufu utapungua kwa sababu kutokana na uwekaji mzuri wa kumbukumbu, sasa haitachukua muda mrefu kufuatilia ya nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nyumba za askari, kwa lengo la kuhakikisha kwamba, askari wanakaa makambini kama lilivyoelezwa kwamba ili nidhamu iwe nzuri Jeshini ni lazima askari wakae makambini. Hili nalo ni tatizo la kihistoria kwa karibu miaka 10 hatukuwa na mradi wa maendeleo katika majeshi yetu, nadhani si majeshi tu hata katika sekta nyingi. Kwa hiyo, ujenzi wa majengo ya aina yoyote ya vituo vya polisi, nyumba za askari, yote yalisimama kwa karibu miaka 10. Lakini katika kipindi hicho tunaendelea kuajiri askari, kwa hiyo, matokeo yake ni kwamba, tumefika mahali mahitaji ni makubwa sana na nyumba zilizokuwepo zimechakaa kwa sababu nazo zilikuwa hazifanyiwi ukarabati. Kwa hiyo, ni lazima tuvumiliane kwamba, wakati tunalikabili hili tatizo, tuelewe vilevile kwamba, halitaweza kukamilika kwa muda mfupi, kutokana na muda mrefu ambapo limelimbikizana hili tatizo, kwa hiyo, litachukua muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili linakwenda sambamba na ujenzi wa nyumba mpya, lakini pamoja na ukarabati wa nyumba za zamani. Hivi sasa tuko katika hatua ya ukarabati. Mheshimiwa Mbunge mmoja alizungumzia *regular maintenance,* hiyo ni *policy* nzuri na tunahimizana kuhakikisha kwamba, matengenezo ya kawaida yanaendelea kila mwaka. Lakini katika hali ya sasa hivi, inabidi kwanza tukabili uchakavu mkubwa. Kwa hiyo, hivi sasa ni ukarabati, tunatarajia tena baadaye itafika mahali fedha za bajeti zitakuwa zinapatikana kikawaida na ukarabati utakuwa ukiendelea kwa kawaida. Kwa hiyo, tuendelee kuvumiliana katika hilo na kuhimizana na inapobidi kusaidiana tusaidiane hasa katika kuhamasisha Wananchi na wao kuchangia nguvu zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mafunzo kwa askari, haya tunayafanya nayo yalisimama kidogo kwa kipindi kirefu na yakaathiri upandishaji vyeo wa askari na Waheshimiwa Wabunge wamelalamikia hilo. Lakini hivi sasa napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, vyuo vyetu sasa wakati wote vina wanafunzi, wakitoa hao wanaingia wengine na wakitoka hao wanaingia wengine. Tunatarajia baada ya muda hizi *crash progamme* zitamalizika, uendelee utaratibu wa kawaida. Lakini wakati huo huo tunaendelea kutoa mafunzo kwa fani maalum hasa ya upelelezi. Tunapeleka Maofisa wetu wengi sana nchi za nje katika kipindi hiki kwa ajili ya mafunzo ya upelelezi ili waongeze uwezo wao wa kukabili upelelezi na kupunguza hili tatizo linalochangia katika mlundikano wa mahabusu katika magereza yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia napokea ushauri uliotolewa na Kambi ya Upinzani kwamba, tuongeze Vyuo kwa ajili ya mafunzo ya askari na hasa mafunzo maalum, kwa mfano, trafiki lakini pia na upelelezi, hili tunalipokea na kama tulivyosema kwenye hotuba yetu, maandalizi ya ujenzi ya Chuo cha Upelelezi hapa Dodoma tayari yameanza na mwaka huu tunatarajia kazi itaanza kuonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nieleze kwamba, mfululizo wa mafunzo ambayo tumekuwa tukiyatoa kwenye njia mbalimbali kwa semina na warsha, hasa kwa Maofisa wetu wa Jeshi la Polisi, kuhusiana na mtazamo mpya katika mazingira ya vyama vingi, mazingira ya utandawazi na mwamko wa haki za binadamu, hizi ni kozi ambazo tumekuwa tukizitoa na hivi karibuni tu Makamanda wakubwa wa Jeshi letu la Polisi, walikuwa Moshi wakipewa dozi hizo za masuala hayo na Tume ya Haki za Binadamu ilishiriki, *Legal and Human Centre* walishiriki kuwapatia mafunzo askari wetu. Nataka niwahakikishie kwamba, pamoja na matatizo ambayo bado tunaendelea kuyaona ya hapa na pale, lakini Jeshi letu la Polisi liko kwenye mwelekeo wa mabadiliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitawapeni mifano miwili tu; hivi karibuni ilitokea mizozo katika Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam na mgomo wa Madaktari katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili. Askari Polisi walikaribishwa kule kwenda kuwaondoa wale wanafunzi *DIT,* lakini pia na Hospitali ya Muhimbili, jambo ambalo si la kawaida, wakanijia Mheshimiwa Waziri, tumepata hii amri na maelekezo, lakini sisi hatujaona vurugu yoyote inayofanyika pale tunakwenda kufanya nini? Ingekuwa zamani pengine wangekwenda tu na virungu vyao. Kwa hiyo, kwa kweli wameanza kubadilika na tuendelee kuwasaidia kwa sababu na wao wanahitaji msaada wetu. Mtu ukimsifu anapofanya vizuri, naye anapata moyo na tunapowakosoa tuwakosoe kwa lugha stahili, siyo wakati mwingine kuwakosoa kwa kuwachokoza, inakuwa hatuwasaidii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa nilizungumzie kwa ujumla ni suala la *passport.* Suala la bei za *passport,* nalo limekuwa likizungumziwa mara nyingi. Kimsingi tunakiri kwamba, bei ya *passport* ni aghali, hiyo ni kweli, nikisema ni rahisi nitakuwa najidanganya mwenyewe. Lakini tukitazama upande huo, tutazame pia na upande wa pili, katika suala hili tunawahudumia wangapi kwa hali halisi ilivyo hivi sasa. Mpaka sasa hivi Watanzania wenye *passport* ni karibu milioni moja tu, kati ya Watanzania milioni 34 na ni huduma ambayo unaihitaji pale unapotaka kusafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika mazingira hayo, kwa vile ni wachache, kwa kweli inabidi wagharamike na walipe gharama kamili. Tutakuja kutazama ama kutoa fidia kwa kutoa bei nafuu kwa wote au hata bure ikiwezekana, tutakapotoa vitambulisho, kwa sababu vitambulisho ni haki ya raia ambayo anaihitaji wakati wote na vitakapotolewa itakuwa ni kwa wote. Kwa hiyo, pale hapakuwa na suala la kwamba, labda walipa kodi wengi wanawafidia wachache, kila mmoja atafaidika nalo. Lakini kwa sasa hivi, kuwataka walipa kodi wengi wawafidie wachache, kwa kweli inakuwa hatuwatendei haki na ndiyo maana inabidi ibaki hivyo hivyo, wazibebe gharama karibu zote za utengenezaji wa *passport*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama alivyoeleza Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, nadhani kwa kuzingatia Wananchi wa kawaida hasa na ujirani mwema wa Afrika Mashariki, *passport* yetu ya Afrika Mashariki itaendelea kuwa ya bei nafuu ya shilingi 10,000/=. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa nilizungumzie ni suala la uraia, niwahi kujibu swali hapa Bungeni na nikafafanua masharti ya uraia wa nchi yetu. Uraia ni jambo adhimu kwa nchi na ni kitu cha thamani kubwa kwa sababu huwezi ukawa na nchi, halafu kuna haki maalumu azifaidi kila mtu kwa sababu yumo nchini. Kuna haki maalum hasa hizi za kisiasa ni za raia tu. Kwa hiyo, ni muhimu kabisa kuwa na utaratibu wa kuwatambua raia na kuweka masharti ya mtu kuweza kuwa raia wa nchi na hii si kwetu tu, masharti tuliyonayo ni *standard* kwa nchi nyingi duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kurudia kama nilivyosema siku ile, kwanza, hatujawa na uraia wa nchi mbili, hili ni jambo ambalo tunaendelea kulifanyia kazi na linaendelea kutafitiwa. Kwa hiyo, Mtanzania anatakiwa awe na uraia mmoja tu wa Tanzania. Uraia huo anaupata kwanza kwa kuzaliwa nchini lakini pia na wazazi Watanzania. Inapokuwa mmoja kati ya wazazi wake ni Mtanzania na mzazi mwingine ni wa nchi za nje, atakuwa na uraia wa nchi mbili, yaani wa baba na wa mama hadi atakapokuwa mtu mzima, kwa sheria zetu mtu mzima ni miaka 18, atakapotimiza umri wa miaka 18 ni lazima sasa aamue mwenyewe anataka uraia upi, anataka Utanzania au uraia wa yule mzazi ambaye si Mtanzania. Kuna uraia wa kurithi, ambao unaweza ukazaliwa nchi ya nje lakini wazazi wote ni Watanzania na uraia wa kuandikishwa, huu unaomba na masharti yake yapo ukikubaliwa unapewa. Hivyo ndivyo unavyopata uraia wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo la kweli ambalo nililizungumza siku ile nilipokuwa nikijibu swali hapa Bungeni, hasa wale ambao mmoja wa wazazi wao si raia wa Tanzania. Lakini wako wengine hata wazazi wote si raia, lakini kwa sababu wameingia ndani ya nchi kwa muda mrefu, tuko pamoja nao, hatujui kama si raia, halafu mtu anazaliwa naye anajiona ni raia moja kwa moja. Haya matatizo yapo ama kwa kujua au kwa kutokujua. Kwa bahati mbaya sheria zetu zinasema kwamba, kutojua sheria si kinga, bahati mbaya sana. Kwa hiyo, unapogundulika kwamba, si raia ndiyo inabidi lazima uchukuliwe hatua ama za kufanyiwa marekebisho yapasayo au uvuliwe uraia uanze kuomba upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda kuchukua fursa hii, kutoa wito wa ujumla kabisa, kwa wote ambao wana wasiwasi na uraia wao, wajitokeze na kujihakiki, ina faida kubwa ukijitokeza mwenyewe na kujihakiki kwa muda, usisubiri mpaka uje ubainike, maana ukibainika tu utanyang'anywa uraia. Lakini katika uhakiki, una wasiwasi tu mwenyewe na ikibainika kwamba, bwana kwa sifa hizi wewe si raia, upo utaratibu wa kukupa uraia kwa uharaka bila kupitia ule usumbufu wa kujitangaza magazetini na kufanya nini na wengi tunawarekebishia *status* yao ya uraia kwa njia hiyo. Kwa hiyo, napenda kutoa wito kwa wote ambao wana wasiwasi huo wa uraia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda kuchukua fursa hii, kwa sababu muda ni mfupi naweza nisimalize yote, nigusie kabisa suala la Mheshimiwa Bernard Membe, kuhusu *classmate* wake, Ansel Masumbuko. Ndugu Masumbuko ni kama alivyokiri Mheshimiwa Bernard Membe mwenyewe kwamba, wazazi wake wote walikuja kutoka Msumbiji, kwa hiyo, siyo raia na yeye siyo raia, pamoja na kwamba, amezaliwa hapa nchini, tumemsomesha, tumempa kazi na yote hayo yaliyotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimwarifu rasmi Mheshimiwa Bernard Membe kwamba, tayari Ndugu Masumbuko, tumeshampa uraia. Lakini kama angejitokeza mapema au Wizara ya TAMISEMI walipotuletea wakatwambia hebu tazameni uraia wa huyu, tukawaambia kwamba, huyu si raia na kweli tuliwaambia kwamba huyo si raia, kuna *alternative* ambayo wangeweza kuifanya. Wangeweza kumwacha aendelee na utumishi kwa sababu si nafasi ya kisiasa, hapo angetoka tu, kama Mbunge anatoka tu. Lakini kazi za utendaji anaruhusiwa kufanya hata kama ni raia wa nchi za nje, nadhani angeweza kupewa muda akaendelea na kazi, halafu marekebisho ya uraia yakafanyika. Sasa hilo lingeweza kufanyika, lakini waliamua kufanya vingine ambayo pia wana haki vilevile kwa sababu alikuwa mtu ambaye katika hali ya kawaida, angepaswa kujua, hasa *Senior Officer* wa ngazi ile aliyofikia, angepaswa kujua kwamba, hana uraia wa Tanzania, angetuarifu mapema akasawazisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndiyo maana nimetoa wito wa jumla kwamba, wengine wote wa aina hiyo, waanze kujitokeza ili tuyarekebishe. Matatizo kama hayo tunayo hata Zanzibar kama alivyosema, tunao raia wengi wa Msumbiji, ambao hawataki kuukana uraia wao, wanautaka uraia wao wa Msumbiji, lakini pia wanataka waendelee kuishi Tanzania.

Tuna Wangazinja kule Zanzibar vile vile ni aina hiyo. Sasa kule Wizarani, miongoni mwa marekebisho ambayo tunayapendekeza Serikalini ya kufanyiwa kazi ni kuwa na *category* ya kitu tutakachokiita kama *permanent residence* au ukazi wa kudumu nao uwe na aina ya haki zake. Ukazi wa kawaida na ukazi wa kudumu kwa sababu kwa vyovyote vile ni ndugu zetu na tunaishi nao na wanachangia katika maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka nilizungumzie kidogo linahusiana na kuwaandaa wafungwa kwa maisha baada ya kifungo. Dhana ya urekebishaji wa tabia sasa hivi ndiyo tunayoendelea nayo badala ya kifungo kuwa ni

adhabu peke yake na ndiyo maana baada ya miaka karibu 10, ambapo miradi ya maendeleo ya uzalishaji mali ilikufa katika magereza zetu, hivi sasa tunaifufua.

Kwa hiyo, tunafufua kilimo kidogo kidogo, Waheshimiwa Wabunge wengi, wamelalamika hapa, wanaomba matrekta kwenye magereza fulani, wanaomba kilimo kifufuliwe, hivi ndivyo tunavyofanya, lakini na miradi ya aina nyingine yote. Hii tunaitumia vilevile kama mafunzo kwa ajili ya wafungwa ili na wao wakitoka gerezani, wawe na amali fulani itakayowasaidia watakaporejea uraiani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii vilevile kulipokea lile wazo lililotolewa na Mheshimiwa Mbunge mmoja, nadhani ni Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa kwamba, hata kuwe na utaratibu wa motisha, wanapofanya kazi wale wafungwa kama Gereza lina *contract* mahali fulani, wanafanya kazi zinapatikana fedha na wao wafikiriwe kuwa na kitu ambacho watawekewa ili watakapotoka gerezani waondoke na kitu. Hilo wazo tunalichukua tutaenda kulifanyia kazi.

Hii nadhani itakuwa ni sera nzuri tu, ambayo inatekelezwa na nchi nyingine kwamba, mfungwa akitoka gerezani, angalau awe na kitu cha kuanzia maisha kuliko ilivyo hivi sasa anaweza kukaa gerezani kwa muda wa miaka 10, akitoka hana mbele wala nyuma, atafanya kosa kwa makusudi ili arudi tena gerezani. Nadhani ni wazo zuri ambalo tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kengele ya kwanza imeshalia na kama nilivyosema, michango ilikuwa mingi na hoja ni nyingi sana. Niseme tu kwamba, zote kwa kweli tumezipokea na tutazifanyia kazi kama ilivyo kawaida. Nyingi tumezipokea kutoka Kamati ya Ulinzi na Usalama, tumezipokea kutoka Kambi ya Upinzani, tutazifanyia kazi kwa ajili ya bajeti zinazofuata ili kuendelea kuboresha huduma katika vyombo vyetu vya usalama wa raia hapa nchini kama vile Polisi, Magereza, Uhamiaji, Zimamoto na vyombo vingine. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, tulipofika hapa imetuchukua muda lakini safari inaendelea vizuri na maendeleo kadri tunavyobadilisha mambo yataendelea kuwa mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, sasa kwa heshima kubwa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 28 - Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

Kifungu 2201 - *Police Mainforce* ... ... .... Sh. 65,544,880,900/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mmewahi kusimama kabla sijauliza, mketi kwanza, nikisema kifungu kimekubaliwa ndio msimame haraka haraka. Wapo Wabunge wawili; Mheshimiwa Ibrahimu Marwa na Mheshimiwa Stephen Kazi, tunaanza na Mheshimiwa Kazi.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko katika *Vote 28 Sub-vote 200,1* kifungu 250100, Mshahara wa Waziri. Nimechangia kwa maandishi na nimetoa maelezo kuhusiana na matatizo ambayo yamejitokeza Mwanza na sehemu ya majibu nimepewa na Waziri kuhusiana na tatizo hili la vijana waliouawa kwa kupigwa, ambapo kuna utata bado kwenye suala hili na Wananchi wa Mwanza bado wananiuliza sana mimi kwa sababu hoja zao wanazileta kwangu na malalamiko yao wanayaleta kwangu na mimi lazima niyalete mbele ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kazi, nimekupata, naomba unisikilize kwanza mimi. Kwa sababu tunakwenda na muda, habari iliyoko hapa ni mambo ya Polisi, usubiri Wizara, hakuna mshahara wa Waziri hapa, usubiri Wizara yenyewe Mheshimiwa Mbunge. Wizara yenyewe ikifika basi utasema mambo ya kukamata mshahara baadaye, hapa hakuna mshahara wa Waziri katika eneo hili.

Kwa hiyo, tunaendelea lakini kamata kwenye Wizara tu.

Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, kama na wewe ni hivyo hivyo basi tusubiri wakati huo. Sawa?

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Sawa sawa kabisa. Ahsante sana.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 - *Police Marine* ... ... .... .... ... ..... Sh. 3,840,633,700/=
Kif. 2003 - *Railway Police Division* ... .... .... .... Sh. 226, 105,100/=
Kif. 2004 - *Police Signals Branch* ... ... .... Sh.3,553,470,600/=
Kif. 2005 - *Police Zanzibar* ..... ..... ... .... .... Sh.5,165,665,400/=
Kif. 2006 - *Police Airwing* ... ..... ..... ..... ..... Sh.1,129,779,800/=
Kif 2007 - *Tazara Police* ... .... ... ..... .... Sh. 252,273,000/=
Kif. 2008 - *Field Force Unit* ..... ... ..... .... Sh.2,244,179,000/=
Kif. 2009 - *Traffic Police* ... .... ... ...... .... Sh. 888,207,000/=
Kif. 2010 - *Police Airport* ... .... ... ..... .... Sh. 229,426,100/=
Kif. 2011 - *Police Dog and Horses* ... ..... .... Sh. 632,303,900/=
Kif. 3001 - *Police College Moshi* ... ..... .... Sh. 2,696,587,100/=
Kif. 3002 - *Police College* ..... ..... ... .... ..... Sh. 804,177,000/=
Kif. 4001 - *Police Vehicles Maintenance Unit* ... Sh. 169,924,100/=
Kif. 5001 - *Police Medical Unit* ..... ... ...... .... Sh.1,467,519,000/=

Kif. 6001 - *Police Building Brigade* ..... .... ... Sh. 1,448,226,000/=
Kif. 7001 - *Criminal Investigation Division* ... . Sh.6,709,677,600/=
Kif. 7002 - *Stock Theft Prevention Unit* ..... ... Sh. 314,837,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 29 - Jeshi la Magereza**

Kif. 1001 - *Prisons Headquaters* ... Sh. 7,080,272,400/=
Kif. 2001 - *Parole Department* ...Sh. 385,381,100/=
Kif. 2002 - *Prisons Welfare and Rehabilitation* Sh.38,966,907,800/=
Kif. 2003 - *Resettlement of Offenders* ... Sh. 424,582,000/=
Kif. 3001 - *Prisons Staff College* ... ... Sh. 702,001,300/=
Kif. 3002 - *Prisons Driving School* ... ... Sh. 126,760,900/=
Kif. 3003 - *Prisons Trade School* ... ... Sh. 236,262,800/=
Kif. 3004 - *Prisons College Kiwira* ... ... Sh. 625,730,000/=
Kif. 4001 - *Prison Building Brigade*... ... Sh. 1,132,018,100/=
Kif. 4002 - *Prison Industries* ... ... Sh. 134,759,600/=
Kif. 4003 - *Prison Farms* ... ... ... Sh. 413,031,800/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 51 - Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

Kif. 1001 - *Administration and General* ... ...Sh. 1,786,937,800/=

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *Vote* 51, programu ya 10, *Sub-vote* 1001, sehemu ya 250100, Mshahara wa Waziri. Nimechangia kwa maandishi na nimetoa malalamiko mawili hapo; moja ni kuhusiana na hawa vijana waliouawa na majibu nimepata kwamba, palikuwa na *mob justice,* lakini malalamiko bado ni makubwa na maelezo yanatofautiana. Sasa ningependa Bunge lako Tukufu lijaribu kutoa maelekezo, tuunde Tume Maalum kwenye jambo hili, ambayo ningeomba ihusishe pia na Wabunge, ili jambo hili liangaliwe kwa undani na tuweze kupata majibu ambayo yatairidhisha jamii na watu wa Mwanza.

Pili, nilijaribu kuulizia suala la kijana mmoja, ambaye amepotea na kupotea kwake ni kuna utata sana. Hatujapata majibu mpaka sasa na mwisho inaweza ikaleta hata lawama kwa watu wengine kwamba, labda wanahusika. Kwa sababu jambo hili nilikuwa naomba nipate majibu yake kwamba, hali ikoje. Kwa sababu ni mtu mzima, ana familia na mke wake anakuja kwangu mara kwa mara na hata barua zile nimempa Waziri akiomba msaada. Baba yake pia amekuja kwangu kunieleza matatizo haya. Sasa nimeshindwa na taarifa imeshapelekwa Polisi. Ningeomba majibu kwa hilo. Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakiri kwamba, Mheshimiwa Stephen Kazi, amekuwa akiyafuatilia masuala yote mawili, hata kabla ya kuchangia kwa maandishi, amekuwa akiliwasilisha kwetu toka kwa Naibu wangu, pamoja na mimi mwenyewe. Niliwasilisha kwa kufuatilia barua tuliyoletewa na wazazi wa vijana wale waliouawa kwenye *mob justice* na kwamba, walikuwa wazazi wakimfuatilia yeye Mheshimiwa Mbunge, wakimwambia kwamba, tumepeleka barua kwa Mheshimiwa Waziri, hatujajibiwa. Tumetafuta kwenye majalada yetu hatimaye tukaipata barua yenyewe, tulikwishawajibu kitambo kidogo. Labda tulichelewa kumwarifu rasmi Mheshimiwa Kazi, kimaandishi kwamba, ile barua tulikwishaijibu na hivi sasa tumemwandikia pamoja na kiambatanisho cha barua ya majibu tuliyowapelekea wale wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu yenyewe kimsingi ni kwamba, sisi upande wetu Jeshi la Polisi, tulipokamilisha uchunguzi, kwa upande wetu kwa kesi kubwa kama zile hupeleki Mahakamani mpaka upate maelekezo ya *DPP*. Kwa hiyo, baada ya kukamilisha uchunguzi, jalada lilipelekwa kwa *DPP,* naye akalichunguza kwa mujibu wa sheria zake, akatoa maelekezo kwamba, kwa kesi ilivyo kwa ushahidi uliopo kwa sasa hivi hata ikipelekwa mahakamani, haitoweza kupatiwa ufumbuzi huu wa kumtia mtu hatiani kwa maana ushahidi ulikuwa haujatosheleza. Kwa hiyo, hili ndilo jawabu ambalo tumemjibu na ndiyo linasimama hivyo. Sisi kwa upande wetu kama Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, tulifika hapo tulipofikia, nadhani hatuna uwezo zaidi wa kufanya zaidi ya hapo.

Kuhusu suala la pili la huyu kijana nadhani akiitwa kwa jina la utani la Babangida, nalo ameniarifu hivi karibuni, amenipatia *cuttings* za magazeti jinsi lilivyoripotiwa magazetini. Kwa hiyo na mimi nimetumia chanzo kile cha *cuttings* za magazeti kuwakabidhi Polisi ili na wao walifanyie uchunguzi kama kuna jipya, lakini mpaka hatua ile kwa kadri tunavyoelewa, Polisi kwa kule Mkoani Mwanza bado wanaendelea kulifuatilia na kutafuta. Hawajapata ufumbuzi wa kuweza kukamatwa au kupatikana kwa mhusika. Lakini naliwasilisha Makao Makuu ili na wao waongeze nguvu zao.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na nashukuru maelezo ya Waziri kuhusiana na masuala yote mawili. Naridhika na maelezo ya pili kwamba, kwa vile wanaendelea na lile jambo, nashukuru sana kwamba linafanyiwa kazi. Ila hili la kwanza kuhusiana na vijana waliouawa, lazima niseme wazi kwamba, wanaotuhumiwa kwenye jambo hili ni Polisi na ndio Wananchi wanasema wamefanya haya mauaji. Sasa ili kulisafisha Jeshi letu la Polisi, nilikuwa na mawazo kwamba, pawe na Tume Huru ya jambo hili. Iingie iangalie au tutumie mpelelezi mwingine, ambaye si Polisi, ili maelezo yakitolewa yaridhishe watu wote kwamba, hayo ndiyo majibu. Kwa sababu hali ilivyo mpaka sasa malalamiko ni makubwa na inaonekana kwamba, labda Polisi hawawezi kujifunga kengele wenyewe. Naomba Waziri aliangalie hili tena mara ya pili.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali, sisi tumeshafikia hatua yetu na Mheshimiwa Mbunge, pamoja na Wananchi wanayo haki ya kutoridhika, labda kwa kuhisi kwamba, Polisi wanalindana.

Ingawa nimekwishasema kwamba, Polisi hawakulimaliza wenyewe, limetokea mikononi mwa Polisi, Wizara Mambo ya Ndani ya Nchi, limekwenda mpaka kwa *DPP,* ni nje ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Sasa nadhani naye angeweza kubaini kama kuna kulindana kwa Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nadhani tuna utaratibu wetu mzuri sana katika nchi yetu, tuna vyombo vingi tu vya kuweza kutafuta shufaa. Nadhani bado kuna chombo kimoja Mheshimiwa Mbunge angewashauri hawa ambao hawajaridhika na mwenendo unavyokwenda wakitumie kwanza kabla ya kuingia kwingine. Kuna chombo cha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Nadhani nayo wengi tu wamepeleka kule malalamiko yao na wakapata majibu yakawaridhisha. Pengine nimshauri kwamba, wafikirie kutumia njia hiyo.

**MWENYEKIITI:** Naona ni ushauri mzuri. Mheshimiwa Stephen Kazi, ameridhika sasa twende kwa Mheshimiwa Ibrahimu Marwa.

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, pamoja na jitihada za kutuzimisha zimisha, niko kwenye *Vote* 51 *Sub-vote* 1001. Wakati nikichangia hapa nilikuwa nimeleta ombi na kilio cha wapiga kura wa Jimbo la Musoma Mjini kwamba, Waziri aangalie ikiwezekana aweze kuteua timu yake, iweze kufuatilia suala hili la mauaji ya kutisha, ambayo yalifanyika pale Musoma ili haki iweze kutendeka. Kwa sababu inaonekana kuna mazingira ambayo yana utata utata kidogo. Kwa hiyo, nilikuwa napenda tu nipate kauli ya Waziri, ni jinsi gani atalishughulikia hili ili angalau haki iweze kutendeka?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukiri kwamba, Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, amewahi kuniletea kesi, sikumbuki kama ni hii hii au ni nyingine, labda atanisahihisha baadaye. Lakini kama ni hii hii, amewahi kuniletea na mimi nikalifuatilia kwa kadri nilivyoweza na baadaye nikampatia majibu. Katika majibu yale nilimwarifu maelezo si tofauti sana na kesi ya Mheshimiwa Stephen Kazi kwamba, ni suala la ushahidi, haujaweza kupatikana wa kuweza kumtia mtu hatiani.

Polisi walipofanya upelelezi wao, walipokamilisha na walikamilisha upelelezi wakawasilisha jalada kwa *DPP,* yeye ndiyo akatoa maelekezo kwamba, kesi ile haiwezi kupelekwa Mahakamani kwa sababu haina ushahidi wa kutosha. Leo nadhani kabla sijasoma bajeti, aliniletea ki-*note* kunikumbushia hilo. Ila akaniarifu bado waathirika wameandika barua kwa Mheshimiwa Rais Mkapa na nadhani nakala kwangu, wakaniuliza je, barua hiyo imeshakufikia na nikamjibu kwamba, haijanifikia. Sasa nikachukulia kwamba, labda wameona watafute shufaa kwa Mheshimiwa Rais, ambayo pia wanayo haki hiyo na inafaa tu kuiendeleza.

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nielezee masikitiko yangu kwamba sioni tatizo ni nini? Sijui ndiyo kauli kama ya Mheshimiwa Stephen Kazi kwamba, labda ni suala la kulindana. Kwa sababu sijaona tatizo kwamba,

kama Mbunge anaomba Serikali ichukue hatua kufuatilia jambo fulani ambalo lina utata, sidhani kama hilo ni tatizo kubwa la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nataka nizungumzie kwa kifupi sana kwamba, pale nimezungumzia suala la mahabusu ambao wamekaa katika mahabusu kwa tuhuma za mauaji zaidi ya mwaka mmoja, miwili, mitatu, minne na mpaka miaka kumi. Hao watuhumiwa kulikuwa na uharaka gani kwamba, walikamatwa na wakaachiwa baada ya miezi minne; ni nini kilipelekea kwamba wao walikuwa wana umuhimu fulani wakapewa upendeleo kwamba suala lao lifanyiwe upelelezi katika muda mfupi kiasi cha miezi minne na ikaonekana kwamba hawakuwa na suala la kujibu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa utaratibu huu ndio tunasema tunakuwa na wasi wasi na *integrity* ya baadhi ya Maafisa wa Polisi. Hatutaki kuondoa imani yetu kwa Jeshi lote, lakini kama tunakuwa na wasiwasi ni lazima tueleze kwamba, hatua zichukuliwe. Kama inaundwa Tume Huru kutoka labda Makao Makuu ya Polisi kwenda kushughulikia suala hili, kuna tatizo gani, kwa sababu majibu hawawezi kuyapata kwa watu waliohusika wenyewe pale Musoma?

Lakini la pili, kwa majibu aliyotoa kwa Mheshimiwa Kazi, juzi hapa Tume ya Haki ya Binadamu, imetoa maamuzi kuhusu tatizo la Serengeti huko Nyamuma. Serikali imeamua nini hapa? Namheshimu sana kaka yangu Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, kazi nzuri. Lakini angetulinda sisi kama Wabunge wenzake kwamba, tunapofikia mahali tunaleta masuala haya ambayo kwa kweli yanahusu haki ya watu maskini ambao hawana fedha, hawatakuwa na imani na Serikali ya CCM, kama utaratibu sio wa kuwasaidia, kama sisi hapa ndani tunapeana majibu ambayo ni ya kusema jaribu kwenye chombo kingine, bado hili linaweza kufanywa na Jeshi la Polisi peke yake. Ninakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kuna lolote la kuongezea, yeye ametoa mawazo mazuri tu sasa?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Ni wazo zuri. Nimefurahi kwamba, hajafikia mahali pa kukata tamaa mpaka kufikia kutoliamini Jeshi la Polisi. Kwa msingi huo, nakubaliana naye kwamba, tuwatume Polisi Makao Makuu, waende wakafanye huo uchunguzi.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. *Vote* 51, Programu namba 10, *Sub-vote* 250100, Mshahara wa Waziri. Nilichotaka kujua Wilaya ya Kilolo ni mpya na Idara zote tayari zimeshahamia pale Makao Makuu isipokuwa Idara ya Polisi. Sasa sikuona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kama kuna hata mpango wowote. Kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Waziri, ajaribu kunieleza mipango yake na mimi binafsi kwa kweli kama kuna tatizo, kwa kuanzia ningeweza kutoa nyumba kwa muda wa miezi mitatu kwa Wizara yake ili angalau waanzie pale wakati wanaangalia mipango mingine. Kwa sababu tukiwaeleza Wananchi kwamba, Polisi pekee hawajahamia, hawaelewi. Wanajua wao kabisa kwamba, Polisi wanaweza kukaa hata kwenye mahema wakaweza kufanya ile kazi. Tusisubiri yakatokea mambo mabaya. Ninashukuru na naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mwamoto kwamba, si Wilaya yake pekee iliyo katika hali hiyo aliyoieleza. Wilaya nyingi mpya tena sio zilizotangazwa mwisho tu, nyingine hata zilizotangazwa mapema sana, najua Wilaya ya Mkuranga mpaka sasa hivi nao wana tatizo hilo nayo ni Wilaya zamani. *Police as such,* bado hawajapata Makao ya Wilaya. Kwa hiyo, kwa hilo kwanza asiwe na unyonge wa kujihisi ni peke yake.

Pili, tatizo la ukosefu wa Makazi ya Wilaya au majengo yanayostahili kwa Wilaya ni la Kitaifa na ni la nchi nzima. Ndiyo maana kwenye bajeti zetu tokea mwaka 2003, mkitazama pale mtaona kila mwaka tunafanya Wilaya mbili au tatu. Kwa sababu uwezo wa kufika Wilaya zote hatujawa nao. Nataka nifuatilie hii *offer* aliyoitoa ya kusaidiana kupata majengo ya kuanzia kazi. Tulikuwa na tatizo kama hilo ulipoanzishwa Mkoa wa Manyara ule, nako tulichukua muda mrefu *RPC* hajaenda kule. Lakini na wao wakahangaika wakapata jengo wakatukabidhi, tukashirikiana kulikarabati mwisho tumehamia. Sasa nimwombe tugawane hii changamoto atutafutie jengo, la miezi mitatu halitatosha. Ni hakika kwa sababu kwa miezi mitatu tutakuwa hatujapata *alternative* ya kuweza kuweka Polisi. Kwa hiyo, tusaidiane tupate jengo au majengo ambayo tutakuwepo kwa muda kidogo halafu tushirikiane kidogo kidogo katika maandalizi ya kituo rasmi.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba angalau atupe jina la *OCD* halafu yeye ndio tutakuwa naye jirani kule kuhangaika naye kuona kwamba, haya mambo yanakwenda vizuri. Kwa sababu yeye itakuwa tatizo kumpata, kwa hiyo, atutajie japo jina la *OCD* ili nikitoka niwaambie tumeshapata *OCD*. Kwa hiyo, yeye ndiyo tutakuwa tunashughulika naye kuhakikisha haya mambo yanakwenda vizuri. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Lakini sidhani, labda Mheshimiwa Waziri kama una majibu unaweza ukataja mtu ndani ya Bunge, umeteua hapa hapa. Sidhani kama ni utaratibu kweli?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Inanikumbusha yale mashindano watu wanaposhindana wanasema kipi kinakuja mwanzo yai au kuku? Kwa sababu *OCD* huwa tunateua tukishapata makao rasmi, pawe pana jengo stahili, pawe pana amari za kutosha na *infrastructure* ya kufanyia kazi, ndiyo *OCD* anateuliwa. Kwa hiyo, haitowezekana kumpatia *OCD* sasa hivi, naomba tushirikiane hilo ambalo amelianza mwanzo na sisi tulifuatilie kwa pamoja. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Asante sana Mheshimiwa Waziri, naona ameelewa Mheshimiwa Venance Mwamoto, wataleta tu *OCD.* Waheshimiwa Wabunge, mjue zikishaisha dakika kumi, kutakuwa hakuna maswali, tutakwenda moja kwa moja na *guillotine.*

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi tu, tulipokuwa tunapitisha ile Sheria ya Huduma kwa Jamii mwaka 2002, pamoja na mambo mengine na sababu za msingi ambazo ziliwasilishwa na Serikali katika Muswada ule na baadaye ikawa Sheria, lakini tulizingatia zana suala la msongamano katika magereza na nina hakika Mikoa yote Magereza yana msongamano mkubwa. Kwa kiasi kikubwa kuna athari za namna mbalimbali kutokana na msongamano ule. Sasa katika ukurasa wa 39 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri na kama alivyoeleza mwenyewe ni Mikoa sita tu ndiyo ambayo imeteuliwa kwa majaribio kuhusu utekelezaji wa Sheria ile, sasa napata wasiwasi kwamba, maadam Sheria ilishapitishwa kwa Tanzania nzima, sasa inakuwaje tena kuna majaribio ya Sheria ambayo tayari ipo? Nilifikiri kama kutekeleza itekelezwe nchi nzima kwa sababu ni Sheria tayari, sio suala la majaribio. Labda ningependa kusaidiwa hapa kwamba, ni vipi Sheria ambayo tayari imeshapitishwa na Bunge na Mheshimiwa Rais ameshaidhinisha, inakuwa tena kwenye majaribio kwa mikoa sita, tukizingatia kwamba, Mikoa mingine nayo ina misongamano kama hii ya mikoa ambayo imetajwa katika ukurasa wa 39 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Nakushukuru sana.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuanza na Mikoa ya majaribio ni ushauri ambao tulipatiwa na Wataalam baada ya kupata uzoefu katika nchi nyingi zilizoanza utaratibu huu. Wengi walianza kwa utaratibu wa majaribio kwanza kwa sababu jambo lenyewe si dogo ni kubwa, ni jipya na linahitaji mabadiliko ya fikra *(Change of Attitude)*. Katika jamii ambayo tumezoea adhabu ya mharifu ni kupelekwa gerezani, halafu kesho mtu amamdhuru au amemwibia amepelekwa Mahakamani halafu kaadhibiwa halafu kisha anamwona tena anarandaranda pale kijijini, kwa kweli itachukua muda kuweza kuyafahamu. Kwa hiyo, ni mambo kama hayo ambayo inabidi yapate muda wa kuzingatiwa na kuona aina ya matatizo yanayoweza kujitokeza ili tutakapokwenda nayo moja kwa moja yaweze kupatiwa ufumbuzi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* ... ... ... ... .... ... Sh. 310,195,300/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning* ... ... ... ... ... ..... ..... Sh. 182,238,100/=
Kif. 1004 - *Community Service Secretariat* ... ...... Sh. 563,585,100/=
Kif. 3001- *Fire and Rescue Services* ... ... ... ...... ..... Sh. 549,312,700/=
Kif. 3002 - *Fire and Resare Services Training Institute* Sh.392,985,200/=
Kif. 4001 - *Refugees Unit* ... ... ... ... ... ... ... ..... ...... ..... Sh. 484,975,100/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Idara ya Uhamiaji**

Kif. 2001 - *Immigration Zanzibar* ... ... ... ... ... ... Sh. 559,618,500/=
Kif. 2002 - *Immigration Mainland* ... ... ... ... .... ... Sh.11,167,680,300/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 28 - Jeshi la Polisi**

Kif. 2001 - *Police Main Force* ... ... ... ... ... ... Sh. 5,300,000,000/= Kif. 5001 - *Police Medical Unit* ... ... ... ... ... Sh. 100,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 29 - Jeshi la Magereza**

Kif. 2002- *Prisons Welfare and Rehabilitation* ... ... Sh. 1,000,000,000/=
Kif. 4001 - *Prison Building Brigade* ... ... ... ... .... Sh. 2,000,000,000/=
Kif. 4002 - *Prison Industries* ... ... ... ... ... ... .... Sh. 500,000,000/=
Kif. 4003 - *Prison Farms* ... ... ... ... ... ... ... ..... Sh. 400,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 51 - Wizara ya Mambo ya Ndani**

Kif. 1001 - *Administration and General* ... ... ... Sh. 169,000,000/=
Kif. 4001 - *Refugees Unit* ... ... ... ... ... ... ... Sh. 86,500,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji**

Kif. 2002 - *Immigration Mainland* ... ... ... ... ... Sh. 100,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi ya Bunge Zima, imepitia kifungu kwa kifungu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa

mwaka wa fedha 2005/2006 na kuyapitisha, hivyo, naomba kutoa hoja kwamba, taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Makadirio ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi yamepitishwa rasmi leo. Baada ya hapo mmeshajulishwa Waheshimiwa Wabunge kwamba, kesho kuna semina, saa tatu asubuhi, napenda tu kuwakumbusha. Sasa naahirisha Bunge mpaka Jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.39 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu Tarehe 11Julai, 2005 Saa Tatu Asubuhi)*